*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 18 DESEMBA, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

Mwenyekiti (*Mhe. Mussa Zungu Azzan*) Alisoma Dua

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani:-

**MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:-**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli Zake kwa Mwaka 2013.

**MHE. ANNE K. MALECELA (K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI):**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli Zake kwa Mwaka 2013.

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kutokana na udharura uliojitokeza kwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha ana majukumu ya kitaifa ambayo amepangiwa. Nitampa fursa maswali yake yaanze kujibiwa kwanza halafu tutaendelea na utaratibu wetu wa kawaida.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Na. 140

**Mabadiliko ya Mzunguko wa Bajeti (Budget Cycle)**

**MHE. KABWE Z. ZITTO (K.n.y. MHE. CHRISTINA M. LISSU)** aliuliza:-

Serikali na Bunge walikubaliana kubadili Mzunguko wa Bajeti ya Serikali ili uwe unakamilika tarehe 30 Juni:-

(a) Je, hadi kufikia mwisho wa Robo ya Kwanza ya Mwaka wa Fedha 2013/2014 ni kiasi gani cha fedha za Maendeleo za ndani na nje zilikwishatolewa ukilinganisha na Bajeti iliyoidhinishwa?

(b) Je, ni miradi ipi ya kipaumbele ilipokea fedha hizo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA(MHE. SAADA MKUYA SALUM):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali namba 140 la Mheshimiwa Christina Mughwai Lissu lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Bunge lilidhinisha jumla yashilingi trilioni 5.64 fedha za Matumizi ya Maendeleo kati ya hizo shilingi trilioni 2.95 ni fedha za ndani na shilingi trilioni 2.69 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwisho wa Robo ya Kwanza ya Mwaka wa Fedha 2013/2014 jumla ya shilingi bilioni 766.28 sawa na asilimia 26.37 ya Bajeti iliyotengwa zilikwishatolewa. Kati ya hizo shilingi bilioni 636.94 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 129.34 ni fedha za nje.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali imeipa kipaumbele miradi ya matokeo makubwa sasa *(BRN)* ambapo jumla ya wizara

zipatazo saba (7) zinatekeleza miradi hiyo. Wizara hizo na fedha zilizotolewa katika Robo ya kwanza kwenye mabano ni pamoja na Wizara ya kilimo, Chakula na Ushirika (shilingi bilioni 16.01); Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (shilingi bilioni 20.49); Wizara ya Maji (shilingi bilioni 79.44); Wizara ya Nishati na Madini (Shilingi Bilioni 155.20); Wizara ya Uchukuzi (shilingi bilioni 73.29); Wizara ya Fedha (shilingi bilioni 7.54) na Wizara ya Ujenzi (shilingi bilioni 100). Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na swali moja tu dogo la nyongeza. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba miradi ambayo imetekelezwa na kipaumbele ni ile ya matokeo makubwa sasa, lakini hakuitaja. Nilikuwa naomba miradi hiyo kwa mfano katika Wizara ya Kilimo ni miradi ipi ya matokeo makubwa sasa ambayo imetekelezwa? Kwa Wizara ya Elimu ni miradi ipi ya matokeo makubwa sasa ambayo imetekelezwa? Kwa Wizara ya Nishati na Madini ni miradi ipi ya matokeo makubwa sasa ambayo imetekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Zitto kama ifuatavyo:-

Kwa sasa kwa sababu Wizara ya Fedha inatekeleza *BRN concentration* yetu kutokana na swali lililoulizwa ni kwenye fedha ambazo zimetolewa. Miradi *specific* ipo katika sehemu za Wizara ambapo miradi hii inatekelezwa. Kwa upande wetu kama sisi Wizara ya Fedha tunayo miradi yetu tunatekeleza ikiwa ni pamoja na yaani kazi hapa iliyopewa Wizara ya Fedha katika *BRN* ni pamoja na kufanya *Resource Mobilization* katika maeneo mbalimbali ambayo itatekeleza hii miradi ya *BRN.* Kwa hiyo, *specific* miradi ipo katika Mawizara, sisi *concentration* yetu ni ku-*mobilize resources* ambazo zitakwenda kutekeleza miradi hiyo. Lakini hata hivyo kama hiyo *list* ipo na italetwa tu na ninadhani kila Mbunge ana nafasi ya kupata hiyo list kutoka katika specific wizara. Ahsante sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MWENYEKITI:** nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, umejibu vizuri sana. Tunaendelea na wizara hiyo, namwita Mheshimiwa Ntukamazina.

Na. 141

**Kuboresha Bajeti ya Serikali Katika Sekta za Elimu na Afya**

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Bajeti ya Serikali itaboreka na kuwezesha utoaji mzuri wa huduma muhimu za elimu na afya?

(b) Hali ya vyuo vikuu Kibajeti ni mbaya sana hususani Chuo Kikuu cha Muhimbili chenye jukumu la kuzalisha asilimia sabini (70) ya Madaktari, je ni lini Serikali itaweka vipaumbele katika uwekezaji wa rasilimali watu *(investment in human capital)?*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deogratius Aloys Ntukamazina, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya sekta ya afya na elimu zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka sambamba na ukuaji wa uchumi. Katika mwaka wa fedha 2013/2014 sekta ya elimu imetengewa jumla ya shilingi trilioni 3.1 ukilinganisha na shilingi trilioni 2.89 za mwaka 2011/2012. Aidha, kwa upande wa sekta ya Afya kiasi cha shilingi bilioni 1,498 zimetengwa katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 ukilinganisha na shilingi bilioni 1,289 zilizotengwa mwaka 2012/2013 hii ikiwa ni nyongeza ya shilingi bilioni 79.9. Serikali

itaendelea kuongeza Bajeti za sekta hizi kadri mapato yake yanavyoimarika.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili *(MUHAS)* ni miongoni wa Vyuo Vikuu vitano (5) vya Umma vilivyoendelea kupata ufadhili wa Serikali katika kugharamia wataalam wake.

Katika kipindi hicho jumla ya wataalam 295 walipata mafunzo mbalimbali, ambapo kati yao 195 waliendelezwa kwa kiwango cha Shahada ya Uzamili *(Masters Degree)* na 100 Uzamivu *(Ph.D.).* Aidha ni miongoni mwa Vyuo vikuu 6 vilivyofaidika na ufadhili wa Tume ya Sayansi na Teknolojia katika kugharamia mafunzo ya jumla ya wataalam 184 katika ngazi ya Shahada ya Uzamili na 84 katika ngazi ya Uzamivu. Aidha, Serikali imekuwa ikitoa udhamini kwa wanafunzi wa kozi za udaktari walioko katika vyuo binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi hizo, Serikali ilikwisharidhia mpango wa ujenzi wa Kampasi ya Mlonganzila Jijini Dar es Salaam ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili. Ni matarajio yetu kuwa mradi huu utakuwa kwa manufaa kwa Taifa pindi utakapokamilika. *(Makofi)*

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa taarifa za kuaminika nilizo nazo, *TRA* inakusanya bilioni 800 kwa mwezi, lakini kwa muda mrefu Wizara, Idara, Mashirika yanaomba fedha au Serikali ina-*approval* fedha lakini zinazokuwa *disbursement* zinazotolewa ni kidogo sana. Ni lini Serikali ita-*improve* hiyo *disbursement*?

(ii) Labda ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mwenyekiti wa *Council* ya Chuo Kikuu cha Muhimbili. Kuna vyuo vinne vinavyozalisha madaktari, vyuo vya binafsi kama

Bugando, *KCMC,* Kairuki na *IMTU.* Lakini bado *MUHAS* inazalisha 70% ya Madaktari wote nchini. Lakini kila tunapoomba *OC* tunapata 4% ya mahitaji halisi na juzi juzi tumepata 10% ya fedha ambazo zilikuwa zimeidhinishwa na Serikali. Sasa kwenye mambo ya *Capital Development* tunapata 30% kwa miaka mingi tu. Ni lini Serikali itakiona Chuo cha *MUHAS* kama chuo muhimu sana kinachozalisha 70% ya Madaktari na kukipa Bajeti inayostahili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza *TRA* inakusanya Bilioni 800 *average* ya Bilioni 800 lakini fedha inayotoka ni kidogo. Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili limekuwa likiulizwa sana na Wabunge na kwa bahati nzuri tulipata pamoja na Kamati ya Uchumi na Biashara. Tulipata kutembelea *TRA* na tulipata elimu kubwa sana. Labda niseme hivi Bajeti ya Serikali ina vyanzo mbalimbali vya mapato. Mojawapo likiwemo haya mapato ya ndani ambayo yanakusanywa na *TRA.* Lakini Bajeti ya Serikali vilevile inategemea misaada na mikopo kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Serikali vilevile inategemea fedha ambazo zinakusanywa kutoka kwa Halmashauri. Lakini Bajeti ya Serikali vilevile inategemea sana Maduhuli ambayo yanatokana na taasisi mbalimbali. Sasa tukisema *TRA* imekusanya zaidi ya 100% maana ni chanzo kimoja tu cha mapato ya Serikali. Maana yake nini? Kila Wizara na taasisi mbali ya mapato ya ndani inategemea vilevile mapato ya nje. Kwa hiyo, tukiona kwamba *TRA* inakusanya zaidi lakini tunachokipata kidogo maana yake zile *source* nyingine zinakuwa bado hazijaingizwa kwenye Bajeti ya Serikali.

Kwa hiyo, tunachokipata kutoka *TRA* ndicho ambacho tunagawana sote. Ukipata 3% maana yake fedha

yetu ya ndani imetokana na *TRA.* Kwa hiyo, *once* hizi fedha zikiwa zinakuja kama ambavyo tunatarajia kwenye *Budget Circle* basi kila mtu atakuwa *at least* anapata vile si lazima 100% lakini kwa asilimia kubwa tutakuwa tunapata.

Kwa hiyo, tujue kwamba hapa tunachogawana ni kile ambacho kinakusanywa na *TRA*, kwa sababu ni kidogo ukilinganisha na *the total Budget* ndipo tunapopata kidogo kidogo. Lakini tutaendelea ku-*improve.* Tunapata mawazo mengi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba *how real to improve the Budget* na sisi kama Serikali tunachukua tutakuwa tunafanyia kazi. *(Makofi)*

Swali lake la pili kuhusiana, nadhani lina-*relate* la kwanza vilevile. Lakini hata hivyo *MUHAS* katika vyuo vyote, nadhani *MUHAS* inapata kipaumbele. Tushukuru sana angalau inapata 4% *percent* ninaamini hao wengine hata hii watakuwa hawapati. Tunaweka kipaumbele sana na tuko pamoja sote kwa sababu *MUHAS* ni chuo chetu na wanaozalishwa tunatarajia kwamba watakuja kufanya kazi katika hospitali zetu kuwasaidia wananchi. Kwa hivyo tutaendelea na tutajitahidi sana kwa hilo Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, tunaendelea na Wizara ya Kazi na Ajira. Mheshimiwa Catherine Valentine Magige.

Na. 135

**Kuongezeka kwa Ajira za Wageni**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE** aliuliza:-

Yamekuwepo malalamiko mengi sana juu ya raia wa kigeni kupewa fursa za kufanya kazi hapa nchini kwenye fani ambazo wapo Watanzania wengine wenye sifa za kufanya kazi hizo:-

(a) Je, Serikali inaweza kutoa takwimu za raia wa kigeni ambao wameajiriwa na kufanya kazi ambazo wapo Watanzania wenye sifa za kufanya kazi hizo?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa fursa hizo zinatolewa kwa Watanzania na raia wa kigeni waajiriwe kwenye fani ambazo hatuna ujuzi nazo?

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentino Magige, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali haitoi vibali vya kazi kwa raia wa kigeni kwa kazi ambazo wapo watalaam wa kutosha katika soko la ajira la Tanzania na kwa namna hiyo Wizara haina takwimu za raia wa kigeni ambao wameajiriwa na kufanya kazi ambazo wapo Watanzania wenye sifa za kufanya kazi hiyo. Kwa taarifa tu ni kwamba, Wizara yangu inapendekeza wageni kupewa vibali vya kazi kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:-

(i) Mwombaji kuwa na taaluma na ujuzi adimu ambao haupatikani au hautoshelezi katika soko la ajira la ndani. Mfano Madaktari bingwa wa binadamu, Wachambuzi wa madini na kadhalika.

(ii) Kampuni zenye mikataba na Serikali inayotambulika Kitaifa kama vile, kampuni za ujenzi wa barabara na nyumba za taasisi mbalimbali.

(iii) Kampuni/Taasisi zilizopata leseni/ vibali vya kumtumia mtaaalam husika, mfano shule zilizopata leseni za wataalam wao kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Bodi ya Makandarasi, Benki Kuu na kadhalika.

(iv) Wataalam wanaowakilisha nchi zao katika kampuni husika.

(v) Makampuni yenye utaratibu wa kutoa mafunzo ya ujuzi wa kazi kwa wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vigezo hivyo, kwa mfano mwaka 2012/2013 jumla ya wageni 7,037 walipatiwa vibali vya kazi kutokana na kuwa na sifa stahiki. Kwa ujumla wageni hawa ni 4% ya wafanyakazi wote kwenye makampuni na mashirika haya, huku Watanzania wakichukuwa 96% ya nafasi zote za kazi katika Makampuni hayo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ambayo Wizara yangu inachukuwa kusimamia Sheria za ajira kwa wageni ni pamoja na kufanya kaguzi za mara kwa mara kwa lengo la kuhakiki na kubaini ukiukwaji wa taratibu za ajira kwa wageni. Kampuni zinazoonekana kukiuka taratibu kama vile kutotekeleza mpango wa kurithisha ujuzi kwa wazalendo *(Succession Plan)* huchukuliwa hatua ikiwa ni pamoja kusitishiwa vibali vya ajira zao. Kwa mfano katika mwaka 2012/2013, jumla ya makampuni 148 yalikaguliwa.

Aidha, kutokana na maswala ya vibali vya ajira za wageni nchini kushughulikiwa na taasisi kadhaa za Serikali, na hii inaleta mkanganyiko katika suala hili. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau imeandaa mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya Vibali vya ajira kwa Wageni. Lengo ni kuwa na sheria ambayo itasimamia masuala ya vibali vya ajira za wageni hivyo kuwa na mamlaka moja inayosimamia vibali vya ajira za wageni nchini kinyume na utaratibu wa sasa ambapo kuna mamlaka na Sheria tofauti zinazoshughulikia suala hili.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa mwaka 2012/2013 makampuni 148 yalikaguliwa na kubaini kuwa makampuni haya yamevunja utaratibu wa ajira kwa wageni. Ili kubaini kama makampuni

haya yamevunja utaratibu wa ajira kwa wageni. Je, ni Makampuni mangapi kati ya haya 148 yalibainika kuwa yamevunja utaratibu wa ajira kwa wageni?

(ii) Ni wageni wangapi waliofutiwa vibali vyao vya ajira kutokana na kukiuka masharti hayo ya ajira kwa wageni?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Catherine Magige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ukaguzi uliofanyika wa makampuni 148 ulikuwa ni ukaguzi wa kawaida ambao tunapitia kwenye makampuni hasa ya watu binafsi waliotoka nje ya nchi kuangalia kama taratibu za ajira za wageni zimekiukwa.

Katika ukaguzi huu wa kawaida tunaweza tukakuta kwamba kuna wengine ambao wameajiriwa bila vibali vyao ama vimeshakwisha hawajaomba tena na pale huwa tunawaambia waombe. Pale ambapo tunaona kwamba wanafanya kazi bila kuwa na vibali huwaondoa. Kwa sasa sina takwimu hapa nilipo kuangalia kwamba ni wangapi kati ya hawa 148 waliokaguliwa walikutwa na kasoro mbalimbali.

Lakini kwa ujumla tunachofanya ni kuwaambia wale ambao hawana au vibali vimekwisha waombe upya. Mara nyingi wakiomba mara ya pili mara nyingi tunawauliza kama hawakuwa na utaratibu wa kurithisha wa kufundisha wazawa ili waweze kuwa na ujuzi huo ambao walikuwa nao hatuwapi kibali cha mara ya pili na tunawaambia waondoke ili Watanzania waingie.

Kwa hiyo, wakipewa mara ya kwanza wanatakiwa vile vile wawe wanawafundisha Watanzania kushika nafasi zao baada ya kumaliza miaka yao miwili ya mwanzo.

*[NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA]*

Kuhusu wageni kufutiwa vibali, hii imefanyika na vilevile tutatafuta takwimu kuonyesha kwamba wangapi ambao wamefutiwa. Mara nyingi kama nilivyosema mwanzoni ni wale hasa ambao wamefanya mara ya kwanza hawajawafundisha Watanzania, kwa hiyo inakuwa ni vigumu kupewa kwa mara ya pili na mara nyingi tunawaambia hutapewa. Kwa hiyo ondoka nchini hatuwezi kurudia kuwapa kibali cha mara ya pili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, leo tuna Kamati mbili nzito sana, naomba tumalize kwa muda ili tupate wachangiaji wengi. Tunaendelea na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Thuwayba Mohamed.

Na. 135

**Kuwasaidia Kielimu Watoto Wenye Maradhi ya Saratani**

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED** aliuliza:-

Kuna idadi kubwa ya watoto ambao wameathirika na saratani na wengi wao hulazwa hospitali kwa matibabu na kukosa kwenda shule kwa wale wanaosoma na hata kwa wengine ambao wamefikia umri wa kwenda shule hukosa nafasi kuanza shule.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia watoto hao ili wapate nafasi yao ya matibabu na ile ya elimu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Thuwayba Idris Muhammed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa kushirikiana na Mashirika yasiyokuwa

ya kiserikali kama Tumaini la Maisha Tanzania yaani *Caring for Children with Cancer in Tanzania* na wafadhili wengine bado wanaendelea kuwasaidia watoto walio na saratani kielimu ambao wamelazwa katika hospitali ya Muhimbili kutoka mikoani. Jumla ya watoto 400 hutibiwa saratini kwa mwaka. Kati ya hawa wote hufaidika na elimu inayotolewa pamoja na watoto wote kutoka wadi za watoto ambao hawana saratani. Jumla ya watoto wanaofundishwa kwa mwaka ni 560.

Huduma ya elimu imegawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni elimu ya taaluma *(Academic Studies)* na sehemu ya pili ni elimu ya michezo *(Play Therapy).* Elimu ya taaluma na michezo wanasoma watoto wa shule ya msingi ambao wamelazwa, watoto wale ambao wako chini ya miaka mitano wanasoma masomo ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto ambao wako sekondari waliolazwa wanasoma stadi za maisha ili kuweza kujitambua na kujiamini. Lakini hawasomi masomo ya taaluma kwa sababu ya ukosefu wa walimu wa sekondari. Wengine watoto wa shule ya msingi na ya awali (chekechea) walimu wao wanatoka Manispaa ya Ilala na wanalipwa na Serikali kupitia MEMKWA na wengine wanatoka nje ya nchi na wanalipwa na Tumaini la Maisha Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. THUWAYBA IDRIS MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Pia ninatoa ahsante sana kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa, kulikuwa na Mwalimu ambaye alikuwa anakwenda hospitali kuwafundisha wanafunzi somo la uchoraji. Kwa bahati siku moja Mwalimu huyo aliwaambia wanafunzi wachore chochote kile wanachokihitaji na kwa kuwa watoto hawa walipewa nafasi hiyo, wote kwa umoja wao waliweza kuchora watoto wamelala kwenye vitanda hospitali na Manesi wanawatia *drip* wengine wakiwadunga sindano. Hili ni jambo la kusikitisha.

Je, Serikali hamwoni kwamba watoto hao wameathirika kisaikolojia na wanahitaji kupata mazingira mazuri zaidi?

Swali la pili, kutokana na jibu lako la msingi umesema kwamba watoto ambao wako Sekondari waliolazwa wanasoma stadi za maisha ili kuweza kujitambua na kujiamini lakini hawasomi masomo ya taaluma kwa sababu ya ukosefu wa walimu wa sekondari.

Je, sasa hivi hamwoni kwamba ni wakati muafaka Wizara ya Afya mkashirikiana na Wizara ya Elimu mkatafuta Walimu wa Sekondari ili watoto hawa wakapata taaluma yao na wakapata haki yao ya kielimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto walipotakiwa kuchora picha na wakachora picha ya wagonjwa wamelala kwenye vitanda na wamewekewa *drip* ni kutokana na mtazamo wa kwamba wao wapo wodini na wamelazwa na wapo watoto wanawaona wenzi wao na kwa hiyo wamechukulia picha ya uhalisia wapi walipo na ndiyo wana display kile ambacho wao wamekiona.

Kuhusu kuathirika kisaikolojia, siyo tu watoto waliolazwa wenye ugonjwa wa saratani, mtu yeyote ambaye amelazwa wodini anaweza kuwa ameathirika kisaikolojia katika maana ya kushindwa kutokuwa sehemu ambayo yeye angeweza kuwa kama afya yake ingekuwa nzuri. Sasa katika tafsiri hii maana yake kipindi cha mtoto anaugua au mtu yeyote anaugua kinaweza kikapelekea mtu huyu akapata nafuu mapema. Kwa mfano, akaweza kutoka mapema kipindi hicho cha saikolojia au kuathirika kwa saikolojia kikawa kimepita.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Lakini uchoraji wa picha peke yake hautoshelezi peke yake kusema kwamba huyo mtoto ameathirika kisaikolojia.

Kwenye eneo la pili, Wizara yangu iko tayari na tumekuwa tayari toka mwanzo kushirikiana na Wizara ya Elimu na ndiyo sababu Walimu kutoka Manispaa ya Ilala wanafika wodini kuja kuwafundisha watoto. Tatizo lililopo ni kwamba Elimu ya Sekondari inatolewa kwa kipindi vilevile ni kirefu na tutaangalia miongoni mwao kutakuwa na watoto wangapi ambao watakuwa katika umri huo wakihitaji elimu hiyo ya sekondari na magonjwa waliyokuwa nayo na kipindi ambacho huyo mtoto anabaki wodini ili angalau tuweze kuona uwezekano wa kuweza kupata elimu hiyo ya sekondari. *(Makofi)*

Na. 136

**Madhara Yatokanayo na Ulaji Wapipi**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR (K.n.y. MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI** aliuliza:-

(a) Ni madhara gani yanayoweza kuwapata watu wenye uzito mkubwa, kisukari na matatizo ya meno wanapokula pipi hasa Wabunge ambao baadhi yao wana matatizo ya kiafya kama yalivyaainishwa kwenye hili wanapotafuna pipi wakati wa vikao vya Bunge?

(b) Kama ulaji unawaathiri, je, serikali haiwezi kutoa ushauri wa kitaalam kwa Bunge ili kutafuta kitu kingine mbadala kwa pipi ili kunusuru afya za Wabunge na watu wote wenye tabia ya kutafuna pipi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la msingi la Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari, Viti Maalumu, lenye

sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo ya awali yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, viashiria hatarishi ambayo ni ulaji usiofaa, matumizi ya pombe kupitia kiasi, matumizi ya Tumbaku na bidhaa zake na kutofanya mazoezi husababisha magonwa yasiyo ya kuambukiza na magojwa ya kinywa na meno. Magonjwa hayo ni kama vile magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, saratani, kisukai, magonjwa sugu ya njia ya hewa, kuoza meno na magonjwa ya fizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ulaji wa pipi na vyakula au vinywaji yenye sukari ni kiashiria hatarishi cha ulaji usiofaa na husababisha madhara mbalimbali katika mwili kama vile unene ulikithiri, magonjwa ya moyo, ugonjwa wa kisukari na kuoza meno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo haya sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa baadhi ya watu wenye unene uliokithiri, uzito wake utazidi kuongezeka kwani ulaji usifaa utaendelea kufanywa hata nje ya ukumbi wa Bunge. Kwa mgonjwa wa kisukari, anapokula pipi anaongeza sukari zaidi mwilini ambayo tayari mwili unashindwa kutumia sukari iliyopo. Hivyo anaongeza uwezekano wa kupata matatizo (*Complications*) yatokanayo na sukari kama figo kishindwa kufanya kazi, magonjwa ya moyo, mishipa fahamu na macho. Vivyo hivyo kwa mgonjwa mwenye kuoza meno, ulaji wa pipi huongeza uwezekano wa kuoza meno mengine.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri ufuatao:-

Kwa kuwa, ulaji wa pipi unaleta athari nilizotaja hapo juu, inashauriwa kupiga mswaki kwa kutumia dawa za meno zenye *Fluoride* baada ya kutumia vyakula vyenye sukari, pamoja na kutumia *Chewing gum* ambazo hazina sukari.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri ametushauri au amewashauri wananchi kutumia *chewing gum* ambazo hazina sukari, lakini pia mimi naona kuna soda ambazo zimeandikwa hazina sukari, biskuti hazina sukari na pipi pia zipo ambazo tunanunua madukani hazina sukari. Lakini tukiwa tunazila au tukiwa tunazitumia tunaona kuna ladha ya sukari. Sasa kitaalamu naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atoe tamko hapa Bungeni kwamba je tunaweza kuendelea na zile? Lakini tunaona kama zina sukari. Tunaomba kauli yako Mheshimiwa Naibu Waziri.

Pia, kuna suala ambalo wataalamu huwa wanatushauri kwa upande wa mafuta ya kula kwamba tutumie mafuta yanayoitwa *Olive Oil*. Lakini kuna watu wengi ambao hawana uwezo wa kutumia mafuta ya *Olive Oil* kwa sababu ni ghali sana.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anatoa ushauri gani kwa watu ambao wanatumia mafuta ambayo si ya *Olive Oil* kwa kula?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi na nikisema kwa kifupi iwe kwa kifupi kwa sababu muda wetu ni mdogo sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kama ifuatavyo.

Vitu vyote ambavyo vimeandikwa kwa uhalisia vikiwa kweli kama ilivyoandikwa kwamba havina sukari lakini ni vitamu basi vitu hivyo maana yake vimewekewa *sweetener* au utamu wa kuweza kusikia hiyo ladha ya kama kuna sukari

wakati ikiwa haina uhalisia sukari na hizo ni kama biskuti, pipi na vitu vinginevyo.

Katika eneo la mafuta, tunachoshauri sisi ni kwamba ni vema kutumia mafuta yanayotokana na mimea badala ya kutumia mafuta yanayotokana na wanyama. Sasa mafuta yanayotokana na mimea ni pamoja na *Palm Oil* inatokana na mimea na Alizeti. Kwa hiyo, kwenye mafuta yoyote ambayo ukitumia ambayo yanatokana na mimea tatizo la kupata matatizo yanayotokana na kuwa na aina ya mafuta ambayo siyo mazuri na hasa yale yanayotokana na wanyama yanapungua.

Na. 137

**Kukabiliana na Wanyama Waharibifu wa Mazao Kilwa Kaskazini**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali katika kukabiliana na wanyama waharibifu wa mazao?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Serikali imeweka mikakati ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu wa mazao kama ifuatavyo;

(i) Kuendesha doria za msako na kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwa kushirikiana na Halmashauri zetu za Wilaya.

(iii) Kuelimisha wananchi wanaoishi kandokando ya Pori la Akiba Selous ikiwa ni pamoja na maeneo ya Kilwa Kaskazini. Elimu hiyo inahusu kutumia uzio wa kamba

iliyopakwa mchanganyiko wa *oil* chafu na pilipili, kuchoma moto matofali ya kinyesi cha Tembo kilichochanganywa na pilipili, ambapo moshi wake unapovutwa, husababisha Tembo kukimbilia mbali na mashamba.

(iv) Tafiti mbalimbali za kutumia njia mbadala za kudhibiti Tembo waharibifu wa mazao zinaendelea kufanywa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania *(TAWIRI)* kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

(v) Kuhamasisha Halmashauri za Wilaya kuandaa mipango bora ya matumizi ya ardhi ili kujumuisha shughuli za uhifadhi katika mipango yao ya vijiji.

(vi) Kuwezesha utoaji wa kifuta jasho kwa mujibu wa Sheria ya kuhifadhi wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 (Kanuni Na. 146 ya Kanuni za Kifuta Jasho na kifuta machozi za mwaka 2011).

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, lakini ninapenda kumwuliza maswali matano ya nyongeza.

Kwanza, hivi ni kweli mpaka leo Serikali inahamasisha teknolojia hii iliyopitwa na wakati na hakuna teknolojia nyingine inayoweza kutumika kudhibiti wanyama waharibifu ambao imekuwa ni kero kwa wananchi?

Pili, kifuta jasho ambacho kinatolewa ni adhabu na inachukua mara nyingine zaidi ya miaka kumi wananchi kuweza kulipwa fidia hiyo. Ni kwanini sasa Serikali isitumie mfumo wa kuwawekea Bima wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo yanapakana na mbuga za *Selous* na mbuga nyingine za wanyama maana kwa tafsiri iliyokuwepo wanyama wana thamani zaidi ya wanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni nini kauli ya Serikali katika kutekeleza mpango huu?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu kama ifuatavyo.

Swali la kwanza, kuhusu teknolojia iliyopitwa na wakati naomba nikiri kwamba ni kweli hii teknolojia ni ya muda mrefu sana lakini sasa hivi Serikali iko katika utaratibu na tumeanza mazungumzo pamoja na kampuni mbalimbali ambazo zina teknolojia ya kisasa. Ni teknolojia ambayo itabidi kuhusisha jamii ambazo zinazunguka hifadhi zetu kwa maana ya kusema kwamba kuwepo na ushirikiano kati ya sehemu hizo mbili ambazo kwa kweli nikiri kwamba na nitakapojibu swali lake la pili ni kwamba kidogo ushirikiano umekuwa si mzurikatika maeneo mbalimbali. Hii ni teknolojia ambayo kampuni sasa hivi zimekwishakuja na tuko katika mazungumzo nazo. Wizara inazungumza nazo pamoja na hifadhi zetu wanazungumza nazo kwa maana ya kusema kwamba tuone kama tunaweza tukatumia teknolojia ya kisasa ambayo inaweza ikasaidia kupunguza uharibifu huu na kuwaweka wanyama kutoingia katika mashamba ya wananchi.

Kuhusu suala la pili la kifuta jasho nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli ilikuwa inachukua muda lakini nafikiri atakiri kwamba jitihada zinaonyesha kwamba sasa hivi kwa kweli imepungua, ule urasimu ambao ambao ulikuwapo siku za nyuma sana katika kutoa ama kuweka hizo unaweza kusema kwamba kuwalipa wananchi kifuta jasho kwa kweli niseme kwamba utaratibu huu umepungua.

Lakini hili suala la Bima na sisi wenyewe tumekuwa tunalitazama lakini lina ugumu wake kwa sababu yapo makampuni fulanifulani ambayo yana tatizo na niseme kwamba ni mapema sana kusema kwamba Serikali kwa kweli inaweza ikachukua hatua hizo kwa sababu ni suala ambalo linahusu mapesa yaliyokuwa mengi na ni jambo la hatari Serikali kusema kwamba itatimiza hilo na isije ikatimiza, litakuwa siyo jambo jema.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Lakini nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo ni wazo jema tutalichukua na tutajaribu kulitazama katika utaratibu mzima ambao tunaufanya katika kuboresha mahusiano kati yetu sisi na wananchi ambao wanazunguka hifadhi zetu.

**MWENYEKITI:** Nakushuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, kama nilivyosema muda wetu ni mdogo sana. Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa.

Na. 138

**Kuundwa kwa Bodi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro**

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA** aliuliza**:-**

Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro *(NCAA)* imekuwa na migogoro na matatizo kwa muda mrefu ikiwemo kukosekana kwa Bodi kama inavyobainishwa kwenye Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro *(NCAA).*

(a) Je, ni kwa nini Bodi hiyo haijaundwa mpaka sasa?

(b) Je, ni lini sasa Bodi hiyo itaundwa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja na kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imekwishaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Sura Na. 284. Bodi hii inatarajiwa kutangazwa ndani ya wiki mbili kuanzia hivi sasa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ngorongoro ni moja ya *heritage* duniani tulizonazo na ni moja ya maajabu saba (7) ya Afrika. Ngorongoro ni moja ya raslimali ambayo inaleta pesa nyingi katika nchi yetu.

Bodi iliyomaliza muda wake ilimaliza toka mwezi Oktoba, 2012. Kwa hiyo, ni mwaka mzima umepita Bodi haijaundwa.

Waziri anaweza akatumbia ni sababu gani zilizopelekea Bodi kutokuundwa takribani zaidi ya mwaka mmoja na kwa kutokuundwa Bodi hiyo kumesababisha Bodi ikose mwelekeo na ifanye kazi bila utaratibu pamoja na kukosekana kwa Mhifadhi yaani  Mhifadhi amekuwa akikaimu. Waziri anaweza akatuambia kwa nini haikuundwa?

Swali la pili, ni madhara gani ambayo hifadhi ya Ngorongoro imeyapata kwa kukosekana kwa Bodi ambayo kimsingi ndiyo inasababisha hifadhi ifanye kazi vizuri?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu masuala mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa kama ifuatavyo:-

Nikiri kwamba alivyosema maana yake kwamba ni ukweli usiopingika kwamba Ngorongoro ni *heritage* ya Dunia na ni katika maajabu saba (7) katika Afrika. Bodi haijakuwepo kwa mwaka mmoja kama anavyosema, lakini mimi ninasema hivi kuna tofauti Mheshimiwa Mwenyekiti kati ya kuunda Bodi na kutangaza Bodi.

Nililolisema hapa ni kwamba Bodi tayari imekwishaundwa na ziko taratibu ambazo tunazipitia. Bodi ya Ngorongoro kama Bodi nyingine ina sehemu mbili au niseme sehemu tatu, hasa sehemu ya pili.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Sehemu ya kwanza katika Bodi ile ni sehemu ambayo inamhusu Waziri na sehemu ya pili ya Bonde lile ni sehemu ambayo inahusu Mamlaka tofauti na Waziri na niseme kwamba ni katika utaratibu huo kwamba huo umekamilikana upo utaratibu wa tatu ambao niweze kuusema kwamba wa kujaribu kuwatizama wale watu ambao wamependekezwa kama kweli wataweza kuendana na kazi husika, inaitwa *vetting* na niseme kwamba taratibu hizi zimekamilika ndio maana nikasema kwamba Bodi tayari imekwisha undwa lililosalia ni suala la kuitangaza Bodi na nimemhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika wiki mbili zijazo tutakuwa na Bodi ambayo imetangazwa hadharani.

Kuhusu madhara mimi niseme kwamba hakuna madhara yoyote Ngorongoro kumekuwa kunaendelea na hata ilipokuwepo Bodi kama atakumbuka Mheshimiwa Mbunge yalikuwepo matatizo na changamoto za hapa na pale na hakuna kitu kisichokuwa na changamoto.

Changamoto hizi zinakuwepo lakini kwamba kumekuwa na madhara kwa sababu kumekuwa hakuna Bodi katika mwaka mmoja nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kumekuwa hakuna madhara katika kipindi hicho cha mwaka mmoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika Mheshimiwa Badwel.

Na. 139

**Kuimarishwa kwa Skimu za Umwagiliaji Wilaya ya Bahi**

**MHE. OMARY A. BADWEL** aliuliza:-

Skimu za umwagiliaji za Bahi, Chipanga, Chikopele, Chali, Makulu Uhelela, Mtazamo na Mtitaa ni skimu za muda mrefu lakini hadi sasa hazijakamilika na zimeanza kuchakaa.

*[MHE. OMARY A. BADWELI]*

Je,ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha kumalizia na kukarabati skimu hizo ili zizalishe mazao ya kutosha hasa ikizingatiwa kuwa Bahi ni Wiaya yenye ukame na uhaba wa chakula?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Ahmed Badwel, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu za Umwagiliaji zilizopo Wilaya ya Bahi zipo kwenye mpango wa kuendelezwa kwa awamu tofauti kwa muda mrefu sasa. Skimu hizi zimejengwa kwa vipindi tofauti chini ya *program* za *Freedom from Hunger (FAO), SDPMA* na *IFAD (PIDP)* kuanzia miaka ya1980 - 2000 katika kipindi hicho skimu za umwagiliaji za Mtitaa, Chikopelo, Chali, Bahi Sokoni, Bahi Makulu, Mtazamo, Chipanga na Uhelela zilijengwa na kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Skimu hizo haukukamilka kutokana na usimamizi dhaifu wa hatua za ujenzi na baadaye kazi za kurekebisha udhaifu uliojitokeza kwenye hatua za awali hazikukamilka kutokana ufinyu wa Bajeti. Aidha upembuzi yakinifu uliofanyika mwaka 2008/2009 ilibainika mahitaji ya ujumla ya shilingi bilioni 12 kwa ajili ya kuboresha mifumo ya umwagiliaji mbalimbali ya skimu za mitaa, Chipanga, Chikopelo, Chali, Bahi Sokoni Bahi Makulu, Mtazamo, Uhelela, Nagulo Bahi Matajirana Kongogo. Serikali katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 ilitoa jumla ya shilingi bilioni 3.2 kwa ajili ya ujenzi wa skimu hizo.

Mheshimwa Mwenyekiti, kiasi hicho cha fedha hakikutosha kukamilisha ujenzi wa skimu zote, hivyo Wizara yangu itaendelea kutenga fedha ili kukamilisha miradi ya ukarabati wa skimu zote ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kwa kuzingatia misingi ya Sheria mpya ya Umwagiliaji ya mwaka 2013 ambayo imepitishwa hapa Bungeni inayokusudia

kuweka utaratibu wa usimamizi unaozingatia taaluma za uhandisi na umwagiliaji kwenye skimu zinazoendelezwa kwa matarajio ya kupata matumizi bora ya skimu hizo za umwagiliaji kwa manufaa ya wakulima na sekta ya kilimo.

Mheshimwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na ukame uliopo Wilayani Bahi Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, inaendelea na ujenzi wa Bwawa la Kongogo ambalo litatumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Aidha, kupitia Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Kati, kazi ya upembuzi yakinifu kwenye Bwawa tarajiwa la Chikopelo itaanza katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 ambalo litatumika kumwagilia eneo lote la skimu la Chikopelo na Chipanga na litapunguza mafuriko yanayopelekea kusababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu kwenye skimu hizo.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba miradi ile ya Bahi ili iweze kukamilika na ili iweze kufanyiwa ukarabati inahitaji jumla ya shilingi bilini 12 na Serikali tayari imeshatoa billioni 3.2 na millioni 200 lakini Mheshimiwa Mwenyekiti fedha hizi zimetolewa mara ya mwisho mwaka 2006 katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 na sasa ni miaka sita imepita hakuna tena fedha zilizotolewa katika miradi hii ya Bahi na kwa maana hiyo hizo fedha sasa zinaonekana kama hazina maana yoyote kwa sababu miradi imeshachakaa.

Je, Serikali sasa iko tayari kuwahakikishia Wananchi wa Bahi kwamba itatenga fedha katika Bajeti inayokuja ya mwaka 2014/2015 ili kazi ya ukarabati na umaliziaji wa miradi ile iendelee?

Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri alipata fursa ya kutembelea miradi hii yote ya kupata fedha katika Wilaya ya Bahi takribani miezi sita iliyopita na kwa bahati

*[MHE. OMARY A. BADWEL]*
mbaya sana yeye mwenyewe alijionea namna ambavyo fedha hizo hazikutumika vizuri na kwa bahati mbaya zaidi miradi yote iliyopata fedha ilikuwa inafanya kazi kabla ya kupata fedha lakini baada ya kupata fedha hizi za Serikali na kuanza kukarabatiwa miradi ile yote sasa haifanyi kazi. Mheshimiwa Naibu Waziri alisikitika sana na mimi baadaye nilimwandikia barua kumwomba atume timu yake ya Wataalamu ifanye uchunguzi.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, amefikia wapi juu suala la kuja kufanya uchunguzi wa matumizi mabovu ya fedha hizo za ukarabati?

**NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, naomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Badwel, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema kwamba kuanzia mwaka 2006/2007 pesa zilizotoka ni bilioni 3.2 ni kweli kwamba kwa makadirio ya *estimates* zilizofanywa pesa hizo ni ndogo lakini Mheshimiwa Mwenyekiti tatizo la miradi ya umwagiliaji sio tu upatikanaji wa fedha hata kwa kiasi kidogo kinachopatikana kwa sababu kuna miradi ya umwagiliaji ambayo inaweza ikaanza uzalishaji hata ikianza ikiwa na asilimia 50/60 ya *completion* mengine mpaka ifike asilimia 100 kutegemeana na mazingira ya mradi huo.

Kwa hiyo, tunachosema Mheshimiwa Mwenyekiti na bahati nzuri kama alivyosema mwenyewe tumekwenda kule, tatizo la miradi ya Bahi ni kwamba pamoja na ile pesa iliyokwenda pale matatizo makubwa yalikuwa kwenye usimamizi kwanza Maafisa wetu wa Kilimo lakini pia kwenye Idara ya Umwagiliaji.

Kwa hiyo, Mheshimwa Mwenyekiti kama nilivyosema kwenye sheria hii mpya tuliyoweka ambayo tumepitisha Bungeni kuna dhamana na wajibu ambao tumeweka kwa Watendaji wote hawa na tutasimamia kwa karibu zaidi miradi hii ili iwe na ufanisi zaidi kuliko ilivyokuwa. Kwa hiyo,

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nimhakikishie Mheshimiwa Badwel kwamba kama tulivyosema tutaifanyia tathmini miradi hii ya Bahi sio yote lakini kwa ile ambayo inahitaji pesa kiasi fulani ili iweze kuanza utekelezaji pamoja na mtazamo na ile miradi mingine ambayo tulikwenda kuiona.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, swali Namba 142 la Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo.

Na. 142

**Sheria ya Umiliki wa Ardhi Katika Vijiji**

**MHE. KOMBO. K. KOMBO** aliuliza:-

Uwepo wa Sheria ya Umiliki wa Ardhi katika vijiji vilivyokwisha anzishwa kunaonyesha nia njema ya Serikali:-

(a) Je, Serikali itasimamia vipi sheria hii yenye migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji?

(b) Je, umiliki huo utaambatana na Hati zilizotolewa kisheria kumilikishwa kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Magogoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inasimamia ardhi ya vijiji kupitia Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999. Sheria hii inaipa Halmashauri ya Kijiji mamlaka kusimamia ardhi ya Kijiji chao baada ya mipaka yao kubainishwa na hatimaye kijiji husika kupatiwa cheti cha ardhi ya Kijijij.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Kijiji inalo jukumu na Mamlaka ya kusimamia ardhi yake na kutoa Hati

za Hatimiliki za kimila kwa mwananchi mmoja mmoja. Utoaji wa Hati hizo hutanguliwa na Mpango shirikishi wa matumizi bora ya ardhi ya Kijiji. Mpango wa matumizi bora ya ardhi ndilo suluhisho la kudumu litakaloondoa migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu mara kadhaa nimekuwa nikitoa taarifa kwamba Hatimiliki za kimila zina hadhi sawa na Hati zitolewazo kwenye ardhi ya ujumla chini ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999. Naendelea kuzihimiza benki zote kuzipokea na kuzitambua ili wananchi waweze kuzitumia kukopea mikopo kwa lengo la kuboresha maisha yao.

**MHE. KOMBO. K. KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana, baada ya majibu naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mpango shirikishi katika vijiji vyote haupo kutokana na vijiji kuwa havina fedha ya kutekeleza mpango huo.

Je, ni lini Serikali itaandaa mpango kazi wa kuviwezesha vijiji kifedha kupitia Halmashauri zao ili viweze kutekeleza mpango huo?

(2) Kwa kuwa migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji ni jambo linaloshamiri siku hadi siku kutokana na wafugaji kuingilia maeneo ya wakulima na wakulima kuingilia maeneo ya wafugaji. Mfano ni Kiteto na Kongwa. Je, ni lini Serikali itapima na kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wakulima na kwa ajili ya wafugaji na taarifa hiyo iweze kuletwa katika Bunge hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Magogoni, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ningependa tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba jukumu la kuandaa mpango kazi ni la kila kijiji husika chini ya uongozi na usimamizi wa Halmashauri ya Wilaya, hivyo wito wangu ni kwamba kila Halmashauri ihamasishe na kuhimiza vijiji vilivyo katika eneo lake kuandaa mpango kazi utakaowezesha wao kupatiwa rasilimali zitakazowawezesha kupanga matumizi pamoja na kupima na kumilikisha wananchi.

Kwa upande wa Serikali niseme tu kwamba hivi sasa tengeo la fedha ambazo sekta ya Ardhi inapewa ni kidogo mno kuweza kuweka ahadi hapa kwamba ni lini tutafanya hiyo kazi kama Serikali Kuu, vipaumbele ni vingi chini ya *BRN* tunazo sekta sita (6) kwa sasa hivi nina uhakika kwamba pato la Taifa litakapoongezeka basi Sekta hii itapatiwa fedha za kutosha ili kuweza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni lini Serikali itapima ardhi kwenye maeneo yenye mgogoro ya Ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tunao mpango tunaouandaa hivi sasa ambao chini ya makubaliano tuliyoingia na Nchi za *G8* Benki ya Dunia pamoja na Sweden huenda tukapata fedha kidogo ambazo zitasaidia kupanga matumzi ya ardhi pamoja na kupima na kumilikisha kwa sehemu kubwa kadiri ya fedha tutakazokuwa tumepangiwa. *(Makofi)*

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro mingi ya ardhi imekuwa ikijitokeza na imekuwa ikitolewa taarifa lakini Mamlaka husika zimekuwa hazifanyi kazi yake inavyostahili.

*[MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA]*
Suala la ardhi ni suala la mbadala Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, niliishamletea suala la mpaka wetu wa Nyantimba. Niliishamweleza suala la Wananchi wa Kata ya Kaninha ambao leo hii wamewekewa mabango kwamba wahame.

Je, Naibu Waziri ni lini utafika kutatua mgogoro wa ardhi katika Kata ile ya Kaninha?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, jibu fupi tu lini, ni lini kama unakwenda kama una nafasi.

**NAIBU WAZIRI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mbassa, kama ifuatavyo:-

Nitaandaa ratiba kwa sababu kama ambavyo tunajua mimi ninalo Jimbo na Jimbo hilo nalo linanisubiri, ninayo Tanzania nzima inanisubiri sasa hivi nilifuatwa na Mbunge wa Mkoa wa Lindi akitaka niende huko:-

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri basi kama unampangia ratiba imekwisha rudi kapumzike....

**NAIBU WAZIRI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nitumie fursa hii kuelezea........

**MWENYEKITI**: naona unachukua muda wangu Mheshimiwa Naibu Waziri watapanga ratiba Mheshimiwa Naibu Waziri nenda kapumzike nakuomba.

**NAIBU WAZIRI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** nitapanga ratiba kisha nitamjulisha Mheshimiwa Mbunge nitaenda kule. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Inatosha nakushukuru sana kwa majibu mazuri. Tunaendelea Wizara ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Ndugulile.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Na. 143

**Vigezo vya kuanzisha Mahakama ya Wilaya**

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED (K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE)** aliuliza**:-**

Katika Jimbo la Kigamboni kuna huduma nyingi za Kiwilaya kama vile Polisi, *TRA, TANESCO* na kadhalika. Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Temeke inawahudumia wakazi wapatao million moja na laki nne (1,400,000/=):-

(i) Je, ni vigezo gani vinavyotumika kuanzisha Mahakama ya Wilaya?

(ii) Je, ni lini Serikali itaanzisha Mahakama ya Wilaya katika Jimbo la Kigamboni?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria na kwa ridhaa yako naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vinavyotumika kuanzisha Mahakama ya Wilaya ni kuanzishwa kwa Wilaya Kiserikali. Pindi Wilaya inapoanzishwa Kiserikali, Mheshimiwa Jaji Mkuu hutangaza katika Gazeti la Serikali kuanzishwa kwa Mahakama ya Wilaya katika Wilaya iliyotangazwa na Serikali. Kwa mfano Wilaya 19 zilizoanzishwa na Serikali hivi karibuni, tayari zimekwishatangazwa na Mheshimiwa Jaji Mkuu kuwa Mahakama za Wilaya na kupewa Mamlaka kama Wilaya Kimahakama.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu nilizozitaja hapo juu, katika kipengele (a) Jimbo la Kigamboni haliwezi kupewa hadhi ya Mahakama ya Wilaya hadi hapo litakapotangazwa na Serikali kuwa Wilaya.

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kutokana na idadi kubwa ya wakazi wa Kigamboni, idadi yao zaidi ya milion 1,400,000 inazidi baadhi ya Nchi kama vile Zanzibar na Pemba. Kwa nini Serikali isifanye upendeleo maalum wa kuunda Mahakama za Kanda kama vile Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, iliunda Kanda maalum ya kule Tarime, Kanda maalum Temeke, Ilala na Kindondoni. Kwa nini Mahakama isifanye upendeleo kutokana na uhalifu unaozidi Kigamboni na idadi ya watu kuongezeka. Kwa nini mahakama isifanye upendeleo maalum kwa kuunda Kanda Maalum za Mahakama?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa Kanda maalum ambazo wameunda lakini kwa sasa kwa mfumo wa Mahakama ulivyo tunafuata mfumo wa Kiserikali. Lakini hata hivyo tumeanza hatua kwa hatua tumeanza na Mahakama Kuu kwa upande wa Dar es salaam tumeshaunda Mahakama Kuu Ilala na tunatarajia kuunda Mahakama Kuu Temeke na baadaye Mahakama Kuu Kinondoni.

**MHE. SAID J. NKUMBA**: Mheshimiwa Mwenyekiti ninamba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema pindi Wilaya mpya zinapoanzishwa baada ya hapo zinapewa hadhi ya Mahakama.

Je, zile Wilaya ambazo ziliishaanzishwa miaka mingi iliyopita na hazijapewa hadhi ya Mahakama mpaka sasa, Waziri anasema nini juu ya hili ikiwamo Sikonge?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri jibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa nilizonazo hadi hivi sasa tunazo Mahakama za Wilaya 133 na Mahakama za Wilaya zinazofanya kazi ni 113. Kwa upande wa Mahakama ya Wilaya ya Sikonge unaweza ukaanzisha lakini taratibu za kuanzisha majengo na mambo mengineyo zinachukua muda.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, swali linalofuata.

Na. 144

**Ujenzi wa Soko la Kimataifa – Segera, Tanga**

**MHE. OMARI RASHID NUNDU (K.n.y. HERBERT JAMES MNTANGI)** aliuliza:-

Kulikuwa na mpango wa kujenga Soko la Kitaifa la Matunda eneo la Segera, Mkoani Tanga.

(a) Je, mpango huo umefikia wapi?

(b) Mheshimwa Rais aliahidi kusaidia Muheza kupata kiwanda cha kusindika Matunda. Je, Serikali imefikia hatua gani juu ya ujenzi wa soko hilo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua iliyofikiwa kuhusu Ujenzi wa Soko la Kimataifa la Matunda na Mboga mboga la Segera, Tanga ni kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



(i) Eneo la hekta tano (5) limeisha pimwa na taratibu za umiliki wa eneo hilo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni upo katika hatua za mwisho.

(ii) Upembuzi yakinifu *(Feasibility Study)* umeisha fanyika na mpango kabambe *(Master Plan)* umeishakamilika.

(iii) Tathmini ya Mazingira *(EIA)* kutoa *(NEMC)* imeishafanyika na Hati yake imepatikana.

(iv) Tathmini ya mazao na vitu vingine vitakavyoathirika imefanyika upya na taarifa ipo tayari.

Aidha, Wizara imewaunganisha Halmashauri ya Wilaya ya Handeni na Benki ya Uwekezaji Tanzania *(TIB)* na tayari *MoU* kati ya Halmashauri ya Handeni na *TIB* imeandaliwa kuona ni jinsi gani wataanza ujenzi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Rais kusaidia Muheza kupata kiwanda cha kusindika matunda tunafuatilia naitatekelezwa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Muheza. Tayari hivi sasa, Halmashauri ya Muheza imeshaanza kutekeleza mkakati wa kuwa na mbegu bora za miche ya michungwa inayofaa kwa ajili ya usindikaji wa juisi na bidhaa zingine kama ilivyoshauriwa na wataalam wa kilimo.

**MHE. OMARI RASHID NUNDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazurl yanayotia moyo na pia naipongeza Serikali kwa kuchukua hatua hizi mbili za kuanzisha soko hili na kiwanda hicho. Wananchi wa Tanga tulikuwa tunajiuliza sasa lini! Sasa nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yanayotajwa hapa ni vitu ambavyo vinaharibika upesi na lengo hapa ni Soko la Kimataifa kwa maana ya kupeleka nje. Sasa Serikali ina mpango gani kuhakikisha kuwa bidhaa hizi zitasafirishwa kwa haraka na kwa unafuu ili zifike katika soko hilo kwa wakati muafaka?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Pili, eneo lote linalotajwa, si Muheza tu ambako kuna machungwa. Lakini kuna matunda ya aina mbalimbali kama mafenesi, matokokwa, makomamanga, mazaituni na kadhalika. Serikali ina mipango gani ya kuwasaidia wakulima wote wa bidhaa hizi, siyo wakulima wa Muheza tu bali na wale wa Korogwe na wale wa Lushoto, ili bidhaa zao ziwe na ubora unaokubalika katika ngazi ya Kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwanza kabisa nataka nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba kama endapo Soko la Segera litakamilika na kuzalisha matunda na mboga mboga kwa wingi, usafiri ambao utatumika kwa kuuza bidhaa kama hizo ni wazi kwamba tutatumia usafiri wa anga kwa kutumia Kiwanja chetu cha Kilimanjaro *(KIA)* kilichopo karibu na Tanga pamoja na usafiri wa barabara ambao ni ya lami ambayo inafika Tanga na mpaka sehemu nyingine mbalimbali hapa nchini mpaka Uwanja wa Ndege wa *Kilimanjaro International Airport (KIA).*

Sehemu kubwa ya matunda ambayo yanaweza kuwa yanaweza kusaidia ni machungwa ambayo Mheshimiwa Mbunge ambaye ameuliza swali ameshapata fursa ya kwenda Afrika ya Kusini na Ujerumani kujifunza jinsi ya kuendesha soko hili, mbegu bora ambazo zitakuwa zinazalishwa sehemu za Wilaya ambazo zinahusika ili kuboresha mbegu bora za machungwa ambayo yanaweza kutoa juisi.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kufungwa Kiwanda cha *TANGOLD* katika Wilaya ya Korogwe, wakulima wa matunda katika Mkoa wa Tanga hawana kiwanda cha uhakika. Je, Serikali iko tayari sasa kuidhamini Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ili iweze kupata mkopo rahisi na kuweza kujenga kiwanda kitakachowaondolea tatizo wakulima wa Mkoa wa Tanga?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika jibu la msingi sehemu ya (b) ni kwamba iko ahadi ya Rais ya kuweza kuisaidia Muheza kupata Kiwanda cha Kusindika Matunda.

Halmashauri ya Muheza imeshaanza kutekeleza mkakati wa kuwa na mbegu bora za miche ya michungwa inayofaa kwa ajili ya usindikaji wa juisi na bidhaa zingine kama ilivyoshauriwa na Wataalam wa Kilimo. Vile vile Kiwanda cha *TANGOLD* ambacho kimekufa kule Korogwe, ni kwa sababu ya Menejimenti mbovu iliyokuwepo.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Segera Mkoani Tanga, linalingana kabisa na eneo la Makambaku ambapo Serikali kwa muda mrefu ilitangaza kujenga Soko la Kimataifa katika Mji wetu wa Makambaku. Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi huo na kuwalipa fidia wananchi wangu wa Mji wa Makambaku?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Kimataifa la Mkakati la Makambaku, mradi wa ujenzi wa soko la Mkakati hili unatekelezwa kwa mfumo wa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi *(BBP).* Hekta 62 zimepatikana na hatua za upimaji wa maandalizi ya upimaji na fidia, unaendelea chini ya Halmashauri husika. *(Makofi)*

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Na. 145

**Uuzaji wa Pamba Ghafi Nje**

**MHE. AUGUSTINO MANYANDA MASELE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvutia Wawekezaji wa Viwanda vya Nguo na Nyuzi ili kuepusha kuuza pamba ghafi nje:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NABIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inatambua kuwa kuongeza thamani *(Value Addition)* ya mazao ya kilimo hapa hapa nchini ndiyo njia pekee ya kuzalisha ajira zenye uhakika, kuongeza kipato na kuinua hali za maisha za wananchi wake. Kuongeza thamani ya pamba yetu kwa kuzalisha nyuzi, nguo na mavazi hapa hapa nchini kunategemewa kuzalisha ajira kushinda sekta nyingine zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika sekta yoyote inavutiwa na mambo mbalimbali. Hivyo Serikali ina mpango wa kuvutia wawekezaji kwa umeme wa uhakika na kutoa unafuu wa kodi *(Tax remission)* kwa wawekezaji wa viwanda vya nguo, mavazi na nyuzi wanaoingiza mashine na mitambo kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa viwanda vyote vikiwemo viwanda vya nguo kama *MWATEX (Mwanza), MUTEX (Musoma), Sunflag (Arusha)* na kadhalika.

Unafuu huo wa kodi unatoa fursa kwa wawekezaji wenye kuweza kutumia teknolojia ya kisasa, kuzalisha kwa ubora kwa ajili ya mauzo ya ndani na nje ya nchi pamoja na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa viwanda vya nguo nchini, Serikali kupitia Mamlaka ya Kutenga Maeneo Huru ya Uzalishaji kwa Mafunzo nje *(EPZA)*, imetenga maeneo ya kipaumbele ambapo hadi hivi sasa jumla ya viwanda 17 kutengeneza nguo *(EPZA Textile Factories)* vimejengwa.

**MHE. AUGUSTINO MANYANDA MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, maswali mawili ya nyongeza.

(1) Kwa kuwa Serikali imesema kwamba kuna viwanda 17 vimejengwa na kwa kuwa Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya *PPP.*

Je, ni viwanda vingapi ambavyo vimejengwa kwa mtindo huu wa *Public Private Partnership (PPP)?*

(2) Kwa kuwa nchini Ethiopia na India, wakulima wa Zao la Pamba wamewezeshwa kuwa wana Viwanda Vidogo Vidogo vya Kufuma Nguo.

Je, Serikali yetu ina utaratibu gani wa kuwawezesha wananchi kuwa na Viwanda Vidogo Vidogo vya kutengeneza nguo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba uko utaratibu wa kuweza kujenga Viwanda vya Nguo hapa nchini, kama nilivyosema kwamba mpaka sasa hivi chini ya utaratibu wa Mamlaka ya Kuwekeza maeneo mbalimbali ya kuweza kutengeneza nguo, viko viwanda 17 ambavyo sasa hivi vimeshajengwa kwa utaratibu wa *EPZ,* yaani *Textile Factories* 17 hapa nchini zimeshajengwa. Kwa hiyo, hiyo inasaidia katika kuonyesha kwamba Viwanda vya Nguo vinapewa uzito mkubwa hapa nchini.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba uongezaji wa thamani katika mazao ndiyo njia kuu ya kuleta maendeleo ya viwanda: Je, Wizara ya Viwanda na Biashara ina mpango gani wa kushirikiana na Halmashauri ya Mbinga kuhakikisha kwamba Kahawa ya Mbinga sasa inatengenezwa hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kama alivyosema kwamba tuna Viwanda vya Kahawa hapa nchini, Viwanda vya Kahawa kama mazao mengine ambayo yanapewa kipaumbele hapa nchini, navyo vitaangaliwa; na kama ushauri ambao umeshatolewa kwamba Serikali inavipa viwanda vyote nchini vipaumbele sawasawa ikiwemo na Viwanda vya Kahawa kujengwa hapa nchini.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuuliza swali moja la nyongeza:-

Je, kwa kuwa nchi yetu ilichelewa sana kuingia katika Soko la Agoa ambalo tulipewa ili kuweza kupeleka nguo nchini Marekani, ningependa kujua bado fursa ya Agoa ipo kwa Tanzania? Je, viwanda gani ambavyo mpaka sasa hivi vinapeleka nguo nje kwa kupitia mfumo wa Agoa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Suala la Mheshimiwa Mbunge kwa sababu linahitaji takwimu, naomba kwamba nitashirikiana naye niweze kutafuta, halafu niweze kumjibu yeye mwenyewe binafsi kwa baadaye.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Na. 146

**Mafanikio ya MMEM na MMES Awamu ya Kwanza**

**MHE. MARGARETH AGNES MKANGA** aliuliza:-

Mpango wa MMEM na MMES awamu ya kwanza umefanikiwa kutatua baadhi ya changamoto katika elimu ngazi ya Msingi na Sekondari:-

(a) Je, mpano wa MMEM na MMES awamu ya pili umeisha anza au bado?

(b) Je, Serikali imeandaa mikakati gani ya kuwezesha mpango huo kuwa endelevu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi Awamu ya Pili (MMEM II) umetekelezwa katika kipindi cha 2007 - 2011. Baada ya kukamilika kwa Awamu ya pili ya MMEM, tathimini ilifanyika na Andiko la MMEM III (2012 - 2016) liliandaliwa na hatimaye kupitishwa na Kamati ya Kisekta ya Maendeleo ya Elimu *(ESDC).* Aidha, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili (MMES II) unaendelea kutekelezwa kuanzia mwaka 2010 - 2015.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha Mipango hii inakuwa endelevu, Serikali ina utaratibu wa kuwashirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo katika ugharamiaji wa Mipango hiyo. Aidha, MMEM na MMES itakapomaliza muda wake, shughuli za mipango hiyo zitaingizwa katika mipango ya kawaida ya Serikali. Serikali kupitia Wizara yangu

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



itaendelea kushirikiana na Washirika mbalimbali wa Maendeleo wa Ndani na Nje ya nchi ili kuhakikisha kuwa Mipango ya Elimu inakuwa endelevu na kuwezesha kufikia azma ya utoaji wa elimu bora nchini. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu ambayo hayajaniridhisha sawasawa na kwa sababu nilikuwa nimeomba mikakati:-

Je, sasa Serikali itanieleza wazi wazi hiyo mikakati kwa mifano kwamba ni kitu gani ili wananchi tuweze kujiandaa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Margareth Mkanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge aliuliza kama mpango huu wa MMEM II uliishaanza? Sisi Wizarani swali hili tumelijibu kwamba mpango tayari ulishaanza na baadhi ya mafanikio kama uandikishaji wa wanafunzi katika kipindi hicho umeongezeka sana kwa kufikia mpaka wanafunzi laki moja na kitu. Lakini vile vile Walimu wameongezeka sana kwa kipindi chote cha miaka hiyo mitano ya mpango. Lakini vile vile hata kiwango cha ufaulu kwa Elimu ya Msingi uliongezeka kwa kipindi hicho, madawati na vitabu kama ambavyo kila siku tumekuwa tukijibu maswali haya ya Mipango ya MMES na MMEM na mafanikio yake. Japokuwa bado baadhi ya changamoto zinaendelea kutolewa.

Na. 147

**Azma ya Utoaji wa Elimu Nchini**

**MHE. PAULINE P. GEKUL (K.n.y. MHE. JOSEPH R. SELASINI)** aliuliza:-

Enzi ya Baba wa Taifa, nchi yetu iliwaandaa wanafunzi ili wajitegemee wakati wote kupitia Stadi mbalimbali za kimaendeleo, usafi ubunifu, upishi, ushonaji na kadhalika.

(a) Je, Serikali yetu kwa sana inalenga kwenye jambo gani ili kufuta ujinga au kuwapatia elimu ya ubunifu wa kujitafutia ajira?

(b) Je, kama ni elimu na ubunifu, tutatambuaje kama azma hiyo imetimia?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 pamoja na malengo mengine, inasisitiza kuandaa wanafunzi wa Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ufundi Stadi na Ualimu pamoja na Vyuo Vikuu kujiunga na Ulimwengu wa Kazi.

Aidha, sera hii inalenga kuwapatia wanafunzi maarifa na ujuzi utakaowawezesha wajitegemee baada ya kuhitimu masomo yao. Mwaka 2005, Serikali ilianzisha Masomo Mapya ya TEHAMA, HAIBA na MICHEZO na STADI ZA KAZI katika Ngazi ya Elimu ya Msingi. Aidha, mada ya Ujasiriamali imechopekwa katika mihtasari ama *syllabus* ya masomo hayo pamoja ile ya *Civics* na *General Studies* katika Elimu ya Sekondari mwaka 2012 na kufundishwa kwa majaribio katika Mikoa nane. Vivyo hivyo, ujasiriamali hufundishwa kama mada katika Taaluma ya Maendeleo katika ngazi ya Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kutekeleza malengo ya kuwapatia vijana wengi Elimu ya Ubunifu ya kujipatia ajira, Serikali inaendelea kuongeza upatikanaji wa

fursa ya Elimu ya Ufundi kwa kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi kwa kila Wilaya.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itawatambua wahitimu wenye elimu na ubunifu kutokana na uwepo wa wahitimu wa vyuo hivyo katika Sekta za Umma na Binafsi, wakifanya kazi au biashara kwa ubunifu na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa wadau wote kushirikiana na Wizara yangu kuhamasisha na kushawishi wahitimu wa Elimu ya Msingi na Sekondari kujiunga na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* ili waweze kujiajiri na kuajiriwa baada ya kuhitimu mafunzo hayo.

**MHE. PAULINE P. GDEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(1) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa haya Masomo ya *VETA* yanasaidia sana katika kupunguza tatizo la ajira na kwa kuwa Ujenzi wa Vyuo vya *VETA* unakuwa unachukua muda mrefu sana kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri.

Je, Serikali iko tayari sasa kuchukua mitaala ya *VETA* na kuweka katika Masomo ya Sekondari ili wahitimu hao wajiajiri moja kwa moja pale wanapomaliza masomo yao?

(2) Mheshimiwa Waziri, kuna wabunifu wengi sana katika nchi yetu na katika majibu yako umesema Serikali itaendelea kuwatambua. Naomba nifahamu, kuna wale wabunifu ambao wanabuni vyombo vya kilimo, kutengeneza umeme, wengine wamebuni hata bunduki na nina mfano wa mwananchi katika Mkoa wangu wa Manyara, katika Jimbo la Hanang, amebuni vifaa vya kupandia vya Trekta. Amebuni vifaa vya kulima, vya kilimo na Mheshimiwa Rais alipotembelea aliona.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline uliza swali.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifahamu. Je, Serikali iko tayari kuwapatia sasa mtaji hao wananchi ambao wameonyesha uwezo wao, ili kuliondolea Taifa letu aibu ya kuendelea kuingiza vifaa kutoka nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Gekul, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mitaala ya *VETA,* kwa sababu Ujenzi wa *VETA* unakwenda polepole kwamba tuipeleke kwenye Elimu ya Sekondari. Mheshimiwa Gekul anajua kabisa kwamba hata kabla ya *VETA* kuna Mitaala hiyo ya Ufundi kwenye Shule za Sekondari kama Shule za Iyunga *Technical,* Shule za Ifunda na shule zingine *(Arusha Technical)*. Kwa hiyo, mitaala hii huwa inawiana kwa upande wa Sekondari na hata upande wa Vyuo vile vile tuna mitaalam hiyo.

Lakini kwamba wananchi hawa wanaokuwa wamepata ubunifu na wanatengeneza vifaa kama bunduki na vifaa vingine vya kilimo, kwamba Serikali sasa iweze kuwapatia mitaji. Swali hili kidogo mimi inakuwa vigumu kulijibu kwa sababu kuna Wizara zake ambazo zinaweza zikatekeleza hili, hasa Wizara ya Kazi na Ajira. Lakini bado kama hawa wanakuwa wabunifu, bado wanaweza wakaenda Benki wakaunda *SACCOS,* wakaenda kwenye vikundi wakaweza kukopa fedha kama Benki za *NMB* wakawa kama kikundi, bado wakaendelea kujifanyia shughuli zao. *(Makofi)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Kwa kuwa changamoto ya dunia ya leo, ya mabadiliko ya kasi ya Sayansi na Teknolojia yanahitaji taifa la watu wabunifu, yaani wenye kuweza kufikiri yakinifu. Swali la Msingi lilikuwa linauliza enzi ya Mwalimu Nyerere Itikadi yetu ilikuwa ni Ujamaa, yenye lengo la Kujitegemea. Leo hii tuko kwenye soko huria. Kasi ya mabadiliko ya Sayansi na

Teknolojia. Itikadi yetu leo hii ni ipi na Elimu yetu inatolewa namna gani ili tuwe na Taifa lenye kufikiri yakinifu. Kuwa na *power of reasoning* inayofanana?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa James Francis Mbatia, kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa James Francis Mbatia ni swali zuri sana. Lakini ninaomba tu anipatie muda nitalijibu vizuri, nije niweke kwenye swali langu la msingi.

Na. 148

**Kuiwezesha Sekta ya Uvuvi Mkoa wa Rukwa**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO (K.n.y. MHE. ABIA M. NYABAKARI)** aluliza:-

Wananchi wa Mkoa wa Rukwa licha ya kujishughulisha na masuala ya kilimo lakini pia hujishughulisha na masuala ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika.

Je, Serikali inawawezeshaje wavuvi katika kuwapatia nyenzo bora za uvuvi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika Swali Na. 8 lililoulizwa na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, tarehe 3 Desemba, 2013 kuhusiana na kuwawezesha wavuvi katika Ziwa Tanganyika, Serikali imeandaa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi mwaka (2012/2013 – 2016/2017) ambayo imeainisha maeneo ya utekelezaji yanayolenga kuwa na uvuvi wenye tija na endelevu. Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi; kuboresha

miundombinu ya uvuvi ikiwemo mialo na masoko, kutoa elimu ya uvuvi endelevu, ukuzaji viumbe kwenye maji, matumizi ya teknolojia sahihi ya kuhifadhi mazao ya uvuvi na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Serikali imeanzisha mfumo wa kutoa ruzuku kwa wavuvi wadogo utakaotolewa kwa utaratibu wa Mfuko wa Mzunguko yaani *(Revolving Fund).* Jumla ya Shilingi bilioni 1.9 zimetengwa kwa ajili ya kununua Boti za uvuvi na viambata vyake yaani (injini, kasia, kamba na vinginevyo) na zana za uvuvi yaani (nyavu za uvuvi na ndoana).

Chini ya ya utaratibu huu maboti 50 (na viambata vyake) na zana za uvuvi (nyavu pamoja na ndoana) zipatazo 15,562 zinatarajiwa kununuliwa. Ruzuku hii itatolewa kwa wavuvi wakiwemo wavuvi wa Ziwa Tanganyika ambapo watatakiwa kupitisha maombi yao kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya husika kwa ajili ya uhakiki na kuona kama yanakidhi vigezo kabla hayajapitishwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mradi huu Shirikishi wa Kikanda wa Usimamizi wa Ziwa Tanganyika *(PRODAP)* uliotekelezwa kuanzia mwaka 2008 hadi Desemba 2013, mialo minne (4) ya kupokelea samaki yaani ya Kibirizi kule (Kigoma Ujiji), Muyowozi (Kigoma), Ikola (Mpanda) na Kirando (Nkasi) imejengwa. Aidha, chanja za mfano za kuanika dagaa kwenye mialo zitawekwa na wavuvi wapatao 3,713 watanufaika.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kwa kuwa Serikali iliahidi kununua Boti na mpaka sasa hizo Boti hazijanunuliwa katika maeneo ya Kirando, Kasanga, Karema, Ikola, na kwingineko katika maeneo ya Mkoa wa Kigoma. Ni lini Serikali itanunua hizo Boti na kuzipeleka kwa wavuvi ili ziweze kuwasaidia, ukilinganisha na maeneo wanayofanyia kazi wavuvi ni hatarishi?

*[MHE. MOSHI S. KAKOSO]*

Swali la pili, Serikali kupitia Mradi wa kuboresha Mazingira, iliahidi kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo katika maeneo ya Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma. Mpaka sasa maeneo hayo bado hawajawezeshwa ipasavyo kupitia vikundi vyao.

Je, Serikali ni lini itasimamia mradi huo na kuhakikisha unawanufaisha wavuvi hao katika Ziwa Tanganyika? *(Makofil)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Moshi Kakoso, maswali yake mawili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwanza, ninampongeza kwa jinsi anavyoshughulikia wavuvi wake. Ninamwahidi kwamba, mipango yote ambayo imewekwa na Serikali inasubiri upatikanaji wa fedha. Hapo fedha zitakapopatikana basi mipango hiyo itatekelezwa.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa mujibu wa majibu ya Serikali ni kwamba Wavuvi watapatiwa ruzuku hiyo kwa kutimiza vigezo. Wakati nikijibiwa swali langu kunako tarehe 3 Desemba, 2013, vilitajwa tu hivyo vigezo.

Je, ni vigezo gani hivyo ili wavuvi waweze kusikia na wajiandae kwa ajili ya kupata ruzuku hiyo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo hivyo ni pamoja na kuwa na Ankara kifani. Kuwa na mahesabu ya biasara na kuwa na *SACOS* ama umoja ambao umeishakuwa *registered.*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na

yeye mwenyewe anajua kwamba siyo sahihi kwamba wavuvi watakuwa tayari wameisha anzisha vikundi.

Je, haoni kwamba hayo masharti ambayo yanayowekwa kwa vyovyote vile hatutaweza kuwafaidisha wananchi kwa sababu vigezo hivyo hakika hawatakuwa wamevitimiza?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Josephat Kengege, kama hivi ifuatavyo. Ni jukumu letu sisi viongozi kuwahamasisha Wavuvi wetu na wananchi wetu waweze kujiunga kwenye vikundi. Lakini hata hivyo kwa wale ambao wanafahamika ni wavuvi hata mmoja mmoja anaweza kupewa ruzuku hii, kwa sababu ameonekana kwamba anafaa na *document* zake zinajionyesha vizuri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba radhi sana. Hapa punde Mheshimiwa James F. Mbatia ameuliza swali la nyongeza ninaona limeairishwa halikupata majibu. Naomba kwa ruhusa yako nimjibu Mheshimiwa James Mbatia, hili swali ambalo limeulizwa kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Ameuliza habari ya Itikadi yetu, bado ni ya Ujamaa na Kujitegemea na uchumi wetu ni vipi. Ninafikiri ndivyo nilivyomwelewa. Lakini kama ndivyo nilivyomwelewa na ndivyo tulivyosikia.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Waziri, Siyo Mheshimiwa James Mbatia, aliyeuliza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE:** Siyo Mheshimiwa James Mbatia! Mimi nilifikiri ni Mheshimiwa James Mbatia, amemwuliza Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri unaweza ukalijibu tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yeyote aliyeuliza, sasa ninataka nimjibu. Ni hiyo hiyo Ujamaa na Kujitegemea kama ilivyo sasa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Uchumi ni wa Soko ambalo linaambatana na tunu za Kijamaa. Uchumi wa Soko unaoambatana na Tunu za Kijamaa. Kama unavyouona mfumo wa uendeshaji wa nchi yetu. Ruzuku, elimu bure na mambo mengine mengi. Hizo zote ni tunu za Ujamaa na Kujitegemea, kama Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimwia Mwenyekiti, kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo mpaka sasa. Uchumi wa Soko kwa kuzingatia sera ya Ujamaa Kujitegemea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

**MHE. MWIGULU M. L. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

*(Hapa Mheshimiwa Mwigulu M. L. Madelu alisimama akiomba nafasi ya kuongea)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu Madelu, ninakuomba upumzike kwanza nisome matangazo.

WaheshimiWa Wabunge, muda wetu umekwisha na umekwisha kwa muda unaotakiwa, ninawashukuru sana kwa umahiri wenu na uwezo wenu mkubwa sana kwenye Bunge hili. Sasa ninatangaza Wageni ambao wako katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Omari Rashid Nundu, anaomba kutangaza kuwa anao wageni wake kutoka Tanga ambao

*[MWENYEKITI]*

ni Timu ya Mpira ya *Costal Union,* hii ni Timu ambayo inacheza *Premium League* na imeshinda Kombe la Uhai, ninawapongeza sana karibuni sana katika Bunge letu. Hongereni sana, tatizo moja tu kubwa ni kwamba hamkuvaa jezi nyekundu. *(Kicheko/Makofi)*

Kuna wanafunzi 113 kutoka katika Chuo Kikuu cha Mipango Dodoma, karibuni sana Bungeni Dodoma. Kuna watoto 40 wanaoishi kwenye mazingira duni, kutoka Baraza la Watoto Mkoa wa Mwanza, karibuni sana. Watoto 6 (sita) kutoka Dar es Salaam, wamekuja kwa ajili ya kujifunza masuala ya Kibunge, wakiongozwa na Adelina Kulaga, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimwia Wabunge ni wageni 27 timu ya *Coastal Union,* nimeishawatangaza hao. Mgeni wa Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria, ambaye ni Ndugu Mohamed Dungele, karibu sana Bungeni. Wageni wa Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mbunge wa Nyamagana, ambaye ni Bi. Flora Wenje – Mke wake. Ndugu Hope Vivian Wenje, mtoto wake na Ndugu Vanesa Faith Wenje, mtoto wake mwingine. Karibuni sana. Mheshimiwa Ezekia Wenje, chunga mzigo wako. *(Kicheko/Makofi)*

Wabunge Wanawake wa CCM, wanatangaziwa kuwa kutakuwepo na kikao leo tarehe 18 Desemba, 2013 baada ya kipindi cha Maswali asubuhi hii. Tafadhalini msikose. Hili tangazo limeletwa na Mheshimiwa Mary Chatanda na baadaye mtamwuliza ni katika ukumbi gani ambako mtafanya mkutano huo. Itakuwa ni baada ya kusitisha Bunge mchana kunako saa saba (7.00) mchana.

Mheshimiwa Amour Chomboh, Katibu wa Umoja wa Wabunge kutoka Zanzibar, anawatangazia Waheshimiwa wote kutoka Zanzibar, kuwa kutakuwa na kikao leo hii saa saba mchana. Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi wa *basement* saa saba (7.00) mchana.

Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa – Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biasahara,

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MWENYEKITI]*
anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake kuwa leo, kutakuwa na kikao saa saba (7.00) mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa (B).

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasimama hapa, kwa Kanuni ya 68(7), kwa ajili ya muda ninaomba nisiisome. Leo hii asubuhi, vyombo vingi vya habari viliondoka na vichwa vya habari vinavyoliongelea Bunge na kwa kutoa taswira hasi kwa Bunge zima kuhusiana kwamba kuna baadhi ya Wabunge walipangiwa safari za kiofisi na Bunge hili Tukufu, wakalipwa fedha za safari, lakini hawakwenda kwenye safari hizo na jambo hili limechukua taswira kama ni Bunge zima liko vile na jambo hili limevunja heshima ya Bunge.

Jambo hili linatuvunjia heshima hata watu ambao tuna maadili ya uongozi na tunaheshimu taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo ninaotaka kuuomba ni kwamba kiti chako kinachukua hatua gani stahiki ya kupambanua kwamba mambo yaliyofanywa na Mbunge binafsi, ni ya Mbunge binafsi na yashughulikiwe kwa Mbunge binafsi mwenyewe kuliko kupaka taswira nzima tuonekane ni Wabunge wa hovyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo tu, magazeti mengine yameandika kwamba kuna Kigogo mmoja amemzuia hawara yake kusafiri na yameandika kwamba alikuwa ameishalipwa kila kitu na hajasafiri. Jambo hili ni jambo la binafsi. Lakini vile vile kwenye Magazeti mengine wameandika na kuna ujumbe nimeupata.

Kiongozi wa Kambi ya Upinzani amemzuia Mbunge wake na Magazeti yakaandika kwamba wana mahusiano. Mimi sipendi kwenda kwenye mahusiano. Ninataka kwenye taswira ya Bunge na kwenye taswira ya taifa kwamba mnapopanga Wabuge, mnapanga wa Chama Tawala na wa Upinzani, ili kuweka uwakilishi. Lakini wameenda

Wabunge wa CCM wengine wamezuiwa. Hapa niombe Mwongozo pia, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani akiwa amemwandikia Mtumishi wa Bunge, kwamba rejea mazungumzo yetu Bwana Kabunju, kuhusu Mheshimiwa Joyce J. Mukya, ambaye yuko safarini, nitashukuru kama utambadilishia *booking* yake ili aweze kurudi aondoke *New York* tarehe 1 Desemba, 2013, na kurejea Dubai. Ili baadaye ataunganisha kuelekea Dar es Salaam. *By Freeman Mbowe – Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Nakala kwa Joyce Mukya).*

Mheshimiwa Mwenyekiti haya ni mambo binafsi. Lakini pia Ofisi yako inasemaje kwa Mbunge aliyetumwa kuwakilisha taifa. Halafu mtu binafsi kwa kutumia nafasi yake anamrudisha mtu ambaye ameishatumia fedha za Serikali, ameishakatiwa *ticket.* Ameishaziba nafasi ya kwenda kuliwakilisha taifa kule. Anamwita arudi Dubai, kwa kazi maalum. Hii ni zaidi ya Ubunge wa Viti Maalum. Ni Ubunge wa kazi maalum. Je, hii kwa Taifa ina taswira gani na kiti chako kinatoa kauli gani. Watu wanaenda kutumia fedha za Serikali kwa mambo binafsi Dubai. Taifa langu lina bahati mbaya kiasi gani. Watu waliotakiwa watoe *check and balance* wanaitana kwa fedha za Serikali kwa burudani Dubai. Puuuuuuu! *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, umemaliza?

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba utoe mwongozo wa hatua stahiki, kupambanua Wabunge wa aina hii. Ili Bunge hili lisionekane ni Bunge zima na hatua stahiki kwa Mbunge anapoingilia kazi za Kiti na hatua stahiki kwa watumishi wanapoingiliwa na kubadilisha kazi waliyotumwa kwa ajili ya Serikali. Puu! *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, ninakushukuru! Ninakushukuru! Ninakushukuru!

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge alikatizwa na Kiti asiendelee tena kuongea)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi ninaomba mwongozo wako kwa kupitia Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaliyosemwa na Magazeti na mwombaji wa mwisho alipokuwa anatoa mwongozo amejaribu kuwaelezea Wabunge wa Upande mmoja wa Upinzani. Lakini taarifa za Wabunge wengi ambao wanachukua fedha bila kwenda safari, siyo tu ni kwa upande wa Upinzani peke yake, ni pamoja na Wabunge wa CCM, akiwemo na Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Mbeya, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi. Amechukua fedha za *PAC,* hakwenda safari na Kamati ya *PAC* na wenzake, akawa anazunguka katika ziara na Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzai (CCM), Ndugu Abdulrahaman Kinana, Katika Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magazeti yameainisha kinachotakiwa kifanyike ni Bunge lako Tukufu lichukue hatua stahiki na wala siyo kuainisha Wabunge wa upande mmoja. Wapo pia Wabunge wengine wengi tu ambao Wajumbe wanawafahamu na wataendelea kuwataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mwongozo wako ni kwa namna gani hili suala litachukuliwa hatua na wala siyo kufanya *propaganda* za kisiasa ndani ya Bunge lako Tukufu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru. Mheshimiwa Maryam S. Msabaha.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawahi kusimama katika Bunge hili Tukufu tangu nimeingia kwenye Bunge hili. Ni mtu ambaye nina *discipline* ndani ya Bunge hili, lakini kwa hili imebidi nisimame. Kuna watu wameandikwa ndani ya Magazeti, wanaiba vidani, lakini hilo halijasemwa. Inaonekanika huku, Mambo ya mapenzi ni mtu na mpenzi wake. Huku kila mtu ana mpenzi wake. Kuna mambo chungu nzima yanafanyika ndani ya Bunge hili, mbona hayasemwi? *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uwaambie Wabunge watulie.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaomba utulivu tafadhali. Tunaomba utulivu. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la aibu sana, kwamba Bunge linaingia katika *dispute* ya namna hii, kwa sababu tunachora taswira mbaya sana kwa wananchi, kuhusiana na matumizi ya fedha za Umma, na kadhalika. Bunge lina taratibu zake za namna gani ya kushughulikia masuala kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya *PAC,* ambayo inahusika na matumizi ya fedha za Umma tayari imeishamwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG),* afanye uchunguzi kuhusiana na safari zote, ili jambo hili liweze kufika mwisho na taarifa tutaileta kwa Mheshimiwa Spika na kama Spika, atapendezwa nayo itakuja Bungeni, ili mambo hayo tuweze kuyamaliza.

Ni aibu kubwa sana kujadili mambo kama haya kwenye Bunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba mkae. Mheshimiwa Peter Msigwa ninaomba ukae. Nimepokea miongozo yote na Kiti kinasema. Kiti hakina ulazima wa kujibu sasa hivi. Nitatoa majibu ya miongozo hiyo baada ya kuyafikiria na kuyatafakari hapo nitakapopata nafasi. Ninawashukuru wote na tuendele. Katibu kwa hatua inayofuata. *(Makofi)*

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu Pamoja na Mapendekezo na Maoni yaliyomo Katika Taarifa Hiyo

**MHE. PETER JOSEPH SERUKAMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mwenyekiti, kwa sababu ya muda ripoti yangu sitoisoma yote, lakini naomba ripoti itakayogawiwa hiyo ndiyo itakuwa ripoti, naomba ichukuliwe kwenye *Hansard* kama ilivyo.

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti, subiri, Waheshimiwa Wabunge mnaotoka nje, naomba mtoke kwa utulivu, tuna Kamati mbili ambazo ni nzito sana. Tunaomba utulivu mkubwa sana.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU**: Mheshimiwa Mwenyekiti , kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2013 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kazi za Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuanzia mwezi Machi, 2013 mpaka Desemba 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati hii kwa umoja na ushirikiano mkubwa waliouonyesha katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Naomba kuwatambua wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, usiwataje waruke tu.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mwenyekiti na Mheshimiwa Prof. Juma Athuman Kapuya, Makamu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Mwenyekiti. Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Saidi Ramadhani Bwanamdogo, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mheshimiwa Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mheshimiwa Suleman Masoud Nchambi, Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Majukumu ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu yameainishwa kwenye Kanuni za Bunge Toleo la Mwaka 2007, Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 8 (9) na 9 (1) kama ifuatavyo:-

Kusimamia Serikali kupitia Wizara tatu (3) ambazo ni Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Aidha, Katika jukumu la kusimamia Wizara hizo, Kamati ilifanya yafuatayo:-

(a) Kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia;

(b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

(d) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kazi zilizofanywa na kamati, katika kipindi cha Mwezi Machi hadi Novemba 2013, Kamati ilifanya kazi zifuatazo:-

(i) Kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara zote husika kwa mwaka 2013/2014;

(ii) (Ziara ya Mafunzo nchini Malaysia; na

(iii) Kupokea taarifa mbalimbali zilizohusu utendaji wa Wizara pamoja na ziara za kukagua miradi mbalimbali iliyo chini ya Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Kamati ilipata fursa ya kupitia mapendekezo ya makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 kwa Wizara zote inazozisimamia. Wizara hizo ni:-

(i) Wizara ya Uchukuzi;

(ii) Wizara Ujenzi; na

(iii) Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Maoni na mapendekezo ya makadirio ya Bajeti yaliwasilishwa mbele ya Bunge lako tukufu. Hata hivyo, changamoto kubwa ambayo Kamati imekuwa ikishauri mara kwa mara, ni kutokupatikana kwa Fedha zilizotengwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu kwa wakati jambo linalosababisha miradi mingi kutokukamilika kwa wakati na kuchelewesha maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Ziara ya Mafunzo ya Miundombinu nchini Malaysia. Kamati ilipata fursa ya kwenda kujifunza masuala mbalimbali yanayohusiana na miundombinu nchini Malaysia. Katika ziara hiyo, Kamati ilijifunza kuwa sasa wakati umefika, Serikali itambue kuwa ni muhimu kubadili mfumo wa utendaji kazi katika kutatua kero za wananchi na hasa katika kusimamia na kuhakikisha kunakuwa na matokeo makubwa ya maendeleo nchini (*Big Result Now*).

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** Kamati ilienda Malaysia kwa lengo la kujifunza namna ambavyo wameweza kuleta maendeleo yao ya haraka hasa katika Sekta nzima ya Miundombinu. Malaysia kwa kutambua kuwa Serikali haina uwezo wa kifedha wa kuleta mapinduzi ya haraka ya maendeleo ya nchi waliamua kwa dhati, na kwa nia na kwa vitendo kuipa nafasi sekta binafsi kwa asilimia 90 kuwekeza katika kubuni na kutekeleza miradi inayotokana na dira ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta binafsi nchini Malaysia imegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni:-

(i) Sekta binafsi ya ndani; na

(ii) (Sekta binafsi ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta binafsi ya ndani, inaundwa na wazawa. Kwa kutambua umuhimu wa kuwajengea uwezo zaidi, Serikali kwa makusudi imetengeneza sera, Sheria na mazingira yanayowawezesha wazawa kukopa fedha kununua vifaa na teknolojia ili kuwawezesha kuungana na makampuni ya kigeni. Makampuni yote makubwa ya wageni yanatakiwa chini ya Sheria kutenga asilimia 30 ya hisa kwa wazawa ambao nao wanaingia na mtaji unaotokana na mtaji wa Serikali kupitia dhamana na mikopo ya moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera na Sheria za Fedha za nchi yetu pamoja na mfumo mzima wa fedha haumsaidii kabisa mzawa wa Tanzania. Kwa kuwa tumeamua kuifanya Malaysia kama mfano kwa nchi yetu, iko haja ya kwenda kujifunza kwa wenzetu ili nasi tuweze kuimarisha sekta binafsi ya wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta binafsi ya nje, hii inatekeleza asilimia 10 mpaka 15 ya miradi yote ya kiuchumi ya Malaysia. Hii ni miradi inayohitaji fedha nyingi sana na teknolojia ya hali ya juu. Serikali inachofanya ni kusimamia utoaji wa huduma ya miradi hii ili tozo zake zisije zikawa za

juu sana kiasi cha kuwafanya wananchi waone zinawaumiza na hazina maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya hivi ndiko kulikoiwezesha Malaysia kufanya mabadiliko makubwa katika Sekta ya Miundombinu na hivyo kuiletea nchi yao maendeleo makubwa ndani ya miaka 20 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** ni dhahiri kuwa katika miradi ya miundombinu, kuna haja ya Serikali kujipanga, kuamua na kutoa nafasi kwa sekta binafsi kwani mafanikio haya ya Malaysia yanaonekana kama miujiza lakini yanawezekana pia kwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Uchukuzi, Kamati katika kutekeleza majukumu yake ilipokea taarifa mbalimbali za utendaji wa Taasisi zilizo ndani ya Wizara ya Uchukuzi .

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Bandari Tanzania, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea bandari mbalimbali nchini zikiwemo bandari ya Dar es Salaam, Bagamoyo, Mwambani, Kemondo, Musoma, Itungi. Bandari hizi zinakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Mabadiliko ya teknolojia ya ujenzi wa meli ambapo nyingi zinajengwa kubwa bila kuwa na krini za kupakia mizigo ambazo haziwezi kuhudumiwa katika bandari zetu kwa sasa;

(ii) Kupungua kwa shehena toka Uganda; kutokana na utendaji hafifu wa Kampuni ya Reli *(TRL)* katika reli ya kati kiasi cha shehena ya kahawa kutoka Uganda kimepungua sana kutoka wastani wa tani 250,000 kwa mwaka hadi chini ya tani 100,000 mwaka 2009/2010;

(iii) Kupungua kwa idadi ya abiria na shehena kutokana na uchakavu wa meli za abiria na mizigo pamoja na kutokuwepo kwa meli ziendazo kasi;

[MHE. PETER J. SERUKAMBA]

(iv) Bandari ya Mwanza, Bukoba na Kemondo kuendelea kutoa huduma bure kwa Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL);* kutokana na Sheria ya Bandari Namba 17 ya Mwaka 2004 kifungu Namba Saba (7). Mamlaka imeendelea kukosa mapato ya wastani wa shilingi 225.00 milioni kwa mwaka kutokana na kutoa huduma bure kwa *MSCL.* Huduma zinazotolewa bure ni kuegesha meli bandarini, matumizi ya ofisi, matumizi ya karakana pamoja na matumizi ya chelezo *(Floating Docks);*

(v) Uchakavu wa Miundombinu ya bandari zote ndogo nchini;

(vi) Tatizo la kujaa mchanga bandarini pamoja na kupungua kwa kina cha maji kutokana na sababu mbalimbali hasa katika bandari ya Mwanza, Bukoba na Itungi Mbeya;

(vii) *Tanzania Building Agency (TBA)* kuendelea kumiliki na kutoza pango la nyumba 24 katika kiwanja kinachomilikiwa na Bandari ya *Kemondo Bay;*

(viii) Kukosekana kwa umeme wa uhakika katika baadhi ya bandari hivyo kutegemea umeme wa jenereta ambao ni ghali;

(ix) Kukosekana kwa gati za kuhudumia mizigo na abiria katika bandari zote isipokuwa Mbamba Bay; na

(x) Gharama kubwa za kuendeleza Bandari za maziwa ambazo nyingi ni za huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati.

(1) Bandari bila reli haziwezi kufanya kazi kwa ufanisi hivyo Serikali iamue na itekeleze haraka ujenzi wa reli ya kisasa; na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*[MHE. PETER J. SERUKAMBA]*

(2) Serikali sasa iamue kutekeleza mkataba wa makubaliano *(MOU)* na Serikali ya Uganda ya kuanza ujenzi wa Bandari ya Mwambani kwani kucheleweshwa huku kunaifanya Uganda kuhamisha matarajio yake na kuyapeleka nchi jirani kwani kama kusema tumeshasema sana sasa ni wakati wa kuyatekeleza kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Dar es Salaam. Kamati iliitembelea Bandari Dar es Salaa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza, lengo lilikuwa ni kutaka kujifunza zaidi namna bandari yetu inavyofanya kazi zake na kuweza kushauri namna bora zaidi ya kuongeza ufanisi bandarini. Kamati iliezwa kuwa Bandari ya Dar es Salaam ndio bandari kubwa kuliko zote Tanzania yenye uwezo wa kuhudumia shehena tani milioni 10.1 kwa mwaka.

Bandari hii ina magati 12 ambayo ni gati namba 1-7 inayohudumia shehena mchanganyiko yenye uwezo wa kupakuwa tani milioni 3.1 kwa mwaka na gati namba 8-12 inayohudumia shehena ya kontena-kampuni ya *TICTS.* Bandari ya Dar es Salaam pia hutegemewa na nchi jirani za Burundi, Rwanda, Congo, Uganda, Zambia na Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya pili, Kamati ilitembelea Bandari ya Dar es Salaam ili kupata taarifa za athari za mgomo wa Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania *(TATOA)* uliofanyika tarehe 5 mpaka tarehe 9 Oktoba, 2013. Mgomo ambao ulisababisha kupungua kwa shehena iliyopakuliwa kutoka wastani wa tani 450 hadi tani 150 pamoja na kupungua kwa makusanyo ya fedha. Kabla ya mgomo mapato yalikuwa shilingi milioni 868.309 kwa siku ambapo yalipungua hadi shilingi milioni 595 kwa siku ikiwa ni upungufu wa 31.4%. Hali hii inatishia kutokufikiwa kwa malengo ya miradi inayotekelezwa chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa *(Big Results Now)* kwa kipindi hiki.

Aidha, ukiachilia mbali changamoto ya mgomo wa malori nchini, bandari ya Dar es Salaam bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



(i) Kina kifupi cha lango la bandari kisichoweza kuhudumia meli kubwa.

(ii) Utegemezi wa barabara kwaajili ya usafiri wa shehena kutoka na kuingia bandarini ambapo barabara inasafirisha asilimia 99 ya shehena bandarini.

(iii) Uhaba wa ardhi kwaajili ya upanuzi wa Bandari; na

(iv) Mtaji mdogo wa kuendeleza miradi ya ujenzi na upanuzi wa bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati.

(1) Kamati inaamini Bandari ya Dar es Salaam ndio roho ya uchumi wa nchi yetu. Gati zilizopo sasa Namba 8 hadi Namba 12 zikiwa chini ya *TICTS* karibu zinafikia ukomo wake hivyo kuna haja ya kujenga Gati Namba 13 na 14 inazidi kujitokeza zaidi na *dredging* ndio zinazotakiwa zifanye kazi ya Gati Namba 13 na 14 nazo pia zitahitaji *dredging* hivyo hivyo.

(2) Ili kuepuka migomo ikiwemo ya *TATOA* ni vizuri serikali iwe inaitisha vikao vya pamoja na wadau wa usafirishaji mara kwa mara hasa kunapokuwa kunahitaji mabadiliko. Hii itaepusha migogoro inayosababisha migomo ambayo mwisho wa siku Taifa ndilo linalopata hasara kubwa.

(3) Iligundulika kuwa moja ya sababu za kupungua kwa ufanisi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania ni kuwepo kwa maofisa wengi wanaokaimu kwani wanakuwa hawajiamini katika maamuzi na mambo wanayoyafanya ikiwemo kutojua hatma ya utumishi wao. Kamati inashauri nafasi hizo zijazwe haraka ili kuleta ufanisi katika kazi.

(4) Ili kuongeza ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam na kuiweka katika nafasi ya ushindani na nchi za jirani ni vyema Bandari kuweza kufanya kazi kwa saa 24, ikishirikiana na wadau wote muhimu kama vile Wizara ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Fedha , Wizara ya Ujenzi, Mamlaka ya Mapato Tanzania, na Wakala wa Upakiaji na Upakuaji mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hizo, Mamlaka ya Bandari Tanzania imefanikiwa kuongeza upakuaji magari kutoka magari 343 kwa shifti mwaka 2011/2012 hadi magari 672 kwa shifti mwaka 2012/2013 sababu zikiwa ni uboreshaji wa *TEHAMA* katika kupakua na utoaji wa magari bandarini, ununuzi wa vifaa vya kuhudumia magari mabovu na ongezeko la madereva na makarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tanzania and Zambia Railway Authority (TAZARA).* Kamati pia ilipokea taarifa ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA),* ambapo ilijulishwa kuwa *TAZARA* ilianzishwa kwa mujibu na Sheria Na. 23 ya mwaka 1975 na inamilikiwa na Serikali ya Tanzania na Zambia kwa asilimia 50 kwa 50. Mwaka 2005 hadi 2009/2010, Serikali ya Tanzania ilitoa jumla ya shilingi milioni 400 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya reli nakuendelea kutoa msamaha kwa malighafi na vifaa vyote.

Mwaka 2012, jumla ya Shilingi bilioni 5.0 zilitolewa kwa ajili ya malimbikizo ya staili za wastaafu wa *TAZARA.* Kwa mwaka 2013/2014 Serikali ilitenga shilingi bilioni 8.3 za mtaji wa uwekezaji na shilingi 12.0 bilioni kwa ajili ya malipo ya malimbikizo ya pensheni kwa wastaafu wa *TAZARA.* Shilingi milioni 400 za mtaji wa uwekezaji na shilingi 2,437,270,521.98 za malipo ya pensheni ya wastaafu wa *TAZARA* ambazo zimetolewa mwezi Julai na Agosti, 2013.

Aidha, mapato ya *TAZARA* ya usafirishaji wa mizigo na abiria yameendelea kushuka kutoka shilingi bilioni 62.77 mwaka 2009/2010 hadi shilingi blioni 34.40 mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinazoikabili *TAZARA.*

(i) Kupungua kwa shehena ya shaba kutoka Zambia pamoja na bidhaa nyingine za madini zinazosafirishwa kupitia *TAZARA.* Kwa mfano, kuanzia mwaka

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



2011, shehena zimepungua kwa asilimia 80 na bado zinaendelea kupungua.

(ii) Mizigo kuchukuwa muda mrefu kuifikia bandari ya Dar es Salaam na kuchelewa ratiba ya meli hali iliyopelekea makampuni mengi kuacha kutumia reli hii.

(iii) Kukosekana kwa mtaji wa uendeshaji ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mafuta ya kutosheleza uendeshaji wa treni, mishahara kwa wakati, vipuli vya mashine na mitambo ya uendeshaji.

(iv) Kupungua kwa uwezo wa utendaji wa vichwa vya treni kutokana na kutofanyiwa matengenezo yanayostaili na kuharibika mara kwa mara.

(v) Uchakavu wa miundombinu, njia kuu ya reli imekuwa katika hali isiyoridhisha kutokana na kukosekana kwa matengenezo ya njia mara kwa mara. Pia kumekuwa na vizuizi kwenye maeneo korofi ambayo yakijumuishwa ni urefu wa zaidi ya Km 100 za njia kuu ya reli.

(vi) Kupungua kwa ari ya utendaji wa wafanyakazi, kutokana na kutokupata haki zao kwa wakati ikiwa ni pamoja na mishahara; na

vii) Kuongezeka kwa uhalifu ndani ya shirika unaofanywa na wafanyakazi wasio waaminifu. Kwa mfano kuiba vipuri, vitendea kazi na mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na ushauri wa Kamati.

(1) Liko tatizo la msingi la kisheria linaloathiri tija ya *TAZARA* ambalo ni muundo wake, sheria inatamka wazi kuwa mtendaji mkuu wa *TAZARA* atoke Zambia. Kamati inashauri viongozi wetu wakuu wa nchi wakae na kutoa dira ya muundo wa *TAZARA.* Kwani kwa sasa *TAZARA* inaonekana haina mwenyewe, ni yatima. Kamati inasema hivyo kwa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



kuona kuwa Serikali ya Zambia haitoi tena kipaumbele kwa reli hii kama viongozi wetu waasisi walivyokubaliana wakati reli hii inajengwa;

(2) Madeni yote *TAZARA* inayodai yafwatiliwe na kuhakikishwa yanalipwa haraka na baada ya kuyapata asilimia kubwa itumike kulipa madeni *TAZARA* inayodaiwa hasa kwa wafanyakazi na wastaafu ili kusaidia kupunguza migogoro ya wafanyakazi inayoibuka mara kwa mara; na

(3) Kamati inashauri, Mkurugenzi Mkuu ahamie kwenye nyumba ya *TAZARA* ili kuondoa mzigo wa gharama kubwa kwa Kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Reli ya Kati. Katika vikao mbalimbali Kamati imekuwa ikiendelea kuishauri Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi kuhusu umuhimu wa kuifufua reli ya kati. Ni dhahiri kuwa nchi nyingi duniani usafiri wa reli ndio wa gharama nafuu na pia unaowezesha kuchochea ukuaji wa uchumi kwa haraka. Kwa kutegemea usafiri wa barabara kusafirisha mizigo mizito kunachangia barabara zetu kuharibika haraka na kugharimu matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa muda mrefu sana imekuwa na mipango mbalimbali ya kujenga mitandao ya usafiri wa reli hapa nchini. Kati ya mipango hiyo ni kuikarabati reli ya kati iwe ya *Standard Gauge*. Kujenga reli ya Mtwara - *Mbamba Bay,* Mchuchuma - Liganga, reli ya kuunganisha bandari ya Mwambani jijini Tanga na Bandari ya Musoma Mkoani Mara pamoja na ukarabati wa reli ya Manyoni Singida na Kaliua Mpanda, kujenga.

Mheshimiwa Mwemyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati.

(1) Kamati inaisisitiza Serikali umuhimu wa kuwa na reli ya kati ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa hasa kuelekea mikoa ya pembezoni na kubwa zaidi kuokoa fedha

*[MHE. PETER J. SERUKAMBA]*
za Serikali zinazotengwa kila mwaka kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa barabara.

(2) Reli ya kati ilikuwa na injini zaidi ya mia moja mpya, nzuri na zenye uwezo wa kufanya kazi ambapo hivi sasa hizi zote zimekufa. Serikali inashirikiana na Malaysia kukarabati injini 8 ambapo inasemekana zitakuwa tayari ndani ya miezi sita. Serikali pia inaundisha injini 13 mpya nchini Marekani ambazo zinatarajiwa kuwa tayari baada ya miaka miwili na nusu. Kwa ujumla tutakuwa na injini 21. Mahitaji ya sasa hivi ni angalau injini 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kwa nguvu zote kuwa, kwa kuwa bado tunahitaji injini nyingi na mabehewa zaidi ya 2000, ni vema tuingie mkataba mpya wa ukarabati wa injini nyingi zaidi, ili wakati tunasubiri hizo za Marekani, angalau tuwe na injini 50 au 60. Ikumbukwe kuwa gharama ya kukarabati injini moja ni asilimia 60 ya bei ya injini mpya ambayo inauwezo wa kutumika kwa miaka 30 bila matatizo kuliko ilivyo hivi sasa ambapo hali yetu ni mbaya sana. Kamati inaamini Serikali isipokuwa na kigugumizi katika hili reli itarudisha tija yake haraka sana, kinachotakiwa tu ni kuamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri pia kutokana na mabadiliko makubwa ya teknolojia katika sekta hii ya uchukuzi, ni vema Serikali sasa iamue kukopa Fedha kwa makusudi ili ijenge reli ya *Standard Gauge* katika maeneo yote yaliyokusudiwa kwani kuendelea kuzungumzia juu ya umuhimu wa reli ya *Standard Gauge* bila vitendo kutaifanya Tanzania ibaki kuwa ni kisiwa, na kwa hiyo kuendelea kunyang'anywa biashara. Inasemekana reli yetu ya sasa uwezo wake wa juu wa ubebaji ni tani 13 kwa yadi wakati reli ya *Standard Gauge* uwezo wake unaanzia tani 16 yadi na kwenda juu. Tofauti hii inaathiri tija ya reli yetu na kuifanya isiwe na wateja hasa kwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Reli ya Kusafirisha Abiria Jijini Dar es Salaam *(City Train).* Kamati ilifanya ziara kutembelea mradi wa Reli ya kusafirisha abiria Jijini Dar es

Salaam kwa lengo la kuona namna usafiri huu unavyopunguza adha ya usafiri Jjini Dar es Salaam. Kamati inaipongeza serikali kwa kuamua kuanzisha usafiri huu kwani sasa kutoka Ubungo hadi Stesheni abiria anatumia dakika arobaini tu badala ya saa mbili mpaka saa tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa katika mradi huu ni gharama za uendeshaji kuwa juu sana zaidi ya mapato yatokananyo na tozo la nauli. Gharama hizi zinahusisha mafuta, mafuta mazito kwa ajili ya injini, mishahara na gharama za Bima *(Premium)* kwa abiria.

Aidha, ili kufanikisha uwepo wa usafiri huu, Kampuni ya Reli Tanzania inatumia injini zilizokuwa za treni za safari ndefu ambazo zinatumia mafuta mengi sana na wakati mwingine sehemu zenye muinuko mdogo tu hulazimika kutumia injini mbili ili kusukuma mabehewa. Inakadiriwa kuwa kila siku Serikali inapoteza takriban shilingi milioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati**,** ili kuboresha usafiri wa treni Jijini Dar es Salaam, Serikali inunue treni ya kisasa itakayotumia mafuta kidogo na nguvu zaidi ambayo inakadiriwa kugharimu Dola za Kimarekani milioni 6. Hata hivyo tatizo la msongamano katika Jiji la Dar es Salaam haliwezi kutatuliwa na treni moja tu.

Kamati inashauri Serikali iamue kwa dhati kushirikisha Sekta binafsi ili iweze kurahisisha usafiri katika Jiji la Dar es Salaam. Serikali ikiamua haitakuwa na haja ya kutoa fedha. Kazi ya Serikali iwe kutangaza tenda kwani yapo makampuni yanayozihitaji fursa hizi. Baada ya hapo Serikali isimamie Sera za tozo na ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** ikumbukwe kuwa kazi hii ikifanywa na sekta binafsi itachukuwa muda mfupi sana na pia itazingatia teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usafiri wa Malori**.** changamoto kubwa ni taratibu na urasimu mkubwa uliopo katika biashara ya kusafirisha mizigo kwenda nje ya nchi

(*Transit Goods).* Taratibu zilizopo hapa nchini siyo rafiki kwa biashara na hivyo kuwalazimu wafanyabiashara wengine kuamua kusafirisha mizigo yao kupitia bandari ya Mombasa badala ya Dar es salaam. Sababu zipo nyingi zikiwemo vituo vingi vya mizani ambavyo vinapoteza muda mwingi njiani. Upimaji huu unachukuwa muda mrefu ikizingatiwa kuwa katika vituo hivi kuna foleni kubwa ya malori, magari ya mafuta na mabasi jambo ambalo ni hatari sana endapo kutatokea mlipuko.

Vituo vingine njiani vinavyosimamiwa na mamlaka nyingine kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na askari wa usalama barabarani ambavyo pia pamoja na kazi nzuri wanazofanya wanachangia kuchelewesha muda wa malori haya na hivyo kukatisha tamaa wafanyabiashara kutumia Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati.

(i) Adhabu kali zitolewe kwa wanaozidisha uzito wa mizigo ili iwe fundisho kwa wengine;

(ii) Serikali kufanya vikao vya mara kwa mara na wadau muhimu wa usafirishaji mizigo ili kuweka mazingira ya utendaji kazi wa pamoja na ushirikishwaji wa kutoa mawazo pamoja nakujulishwa mabadiliko mbalimbali yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usafiri wa Anga, katika miaka miwili yanyuma kulitokea mabadiliko makubwa ya uongozi wa kampuni ya *Air Tanzania.* Mabadiliko haya yaliashiria kuimarisha uongozi, kuimarisha mtaji ili kurejesha tija katika sekta hii. Chakushangaza hadi leo biashara hii inaendelea kudorora tena kwa kasi kubwa zaidi. Tatizo ni Wizara kutotoa ushirikiano na wawekezaji ili kulikwamua shirika hili.

Wamekuja wawekezaji wengi sana wakiwemo Wachina, Waarabu, Wazungu na kadhalika. Wawekezaji

hawa hawakupewa ushirikiano, kwani utashangaa kuona Kampuni inayofanya kazi zenye tija Angola au Kenya hapa kwetu unaambiwa uchunguzi umefanyika na kugundua Kampuni hiyo ni ya kitapeli. Wakati mwingine utaambiwa ya Benki Dunia au Marekani ndio waliosema, Kamati inajiuliza je Benki ya Dunia na Marekani vinavyofanywa Angola au Kenya hawavioni? Mbona hawaweki vipingamizi kama ilivyo hapa kwetu?

Kukataa kwa Wizara kufanya maamuzi ya kukaribisha mwekezaji mwenye nia thabiti kama yule mchina aliyetaka kuleta ndege tisa, kunatoa mwanya kwa viongozi kuendelea kufanya ubadhirifu kwa kukodisha ndege na mara nyingi ndege hizi huwa ni mbovu. Matokeo yake ni kuongezeka kwa deni hadi kufikia zaidi ya bilioni 40 kama ilivyogunduliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege**.** Kamati pia ilipata wasaa wa kufanya ziara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere Dar es salaam ambacho ndicho kinachotumiwa na wageni na watalii wengi ukiachia mbali kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro. Hata hivyo, majengo na miundombinu ya uwanja huu vimechakaa na vinahitaji ukarabati mkubwa.

Changamoto kubwa ni kutokutolewa kwa fedha zilizotengwa kwaajili ya uwanja huu kwa wakati. Fedha zinapochelewa zikitolewa hufanya kazi kwa namna ya mipango ya dharura yaani *(Crash Program)* ambayo mara nyingi huwa haileti tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na mpango wa ujenzi wa jengo la abiria katika kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere. Mpango huu ni muhimu kwani inakadiriwa kuwa kukamilika kwa awamu ya kwanza ya mradi kutaongeza abiria kutoka abiria milioni 1.2 kwa mwaka hadi abiria milioni 4.7 kwa mwaka. Hii itakuwa fursa nzuri ya kukuza uchumi wa nchi yetu hasa kwa kutoa ajira kwa watu wengi zaidi.

*[MHE. PETER J. SERUKAMBA]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati.

(1) Kwakuwa tayari kunamazungumzo ya kukopa ili kujenga *Terminal III,* Kamati inashauri makubaliano ya mkataba wa mkopo yasainiwe haraka ili mradi wa ujenzi wa kiwanja hiki ufanyike haraka na mapema kwani kwa sasa wawekezaji wamekata tamaa.

(2) Kamati inashauri miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege kama vile Mwanza, Bukoba, Songwe, ikamilishwe na kukabidhiwa kwa wakati.

(3) Vilvile, fidia zilipwe kwa wananchi waliochukuliwa viwanja na kupisha upanuzi wa viwanja vya ndege.

(4) Mipaka ya viwanja vya ndege ipimwe na kuwekwa alama za kudumu ili kuzuia uvamizi wa maeneo ya viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanja cha Ndege cha Songwe-Mbeya. Uwanja wa kimataifa wa Songwe ni kati ya viwanja vikubwa viwili kujengwa baada ya uhuru ukitanguliwa na uwanja wa Mkoa wa Kilimanjaro. Uwanja huu unatoa fursa muhimu kwa wakazi wa mkoa wa Mbeya na mikoa ya jirani kwani utaweza kuwasaidia kukuza uchumi kutokana na shughuli mbali mbali za kiuchumi zitakazofanyika kutokana uwepo wa uwanja huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali iendelee kukamilisha maeneo yaliyobaki ili ndege kubwa za kimataifa zianze kutumia kiwanja hicho na kuvutia mashirika makubwa ya ndege kukitumia kiwanja hiki.

Pia kuhakikisha kunakuwepo mafuta ya ndege katika kiwanja cha Songwe Mbeya, kwani kwakuwepo kwa mafuta ya ndege kutaweza kutoa uhakikika kwa ndege kubwa na za kimaifa kutua kiwanjani hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Udhibiti Usalama wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA).* Mamlaka hii ilianzishwa kwa lengo la kudhibiti usalama wa usafiri wa nchi kavu na majini. Kamati ilielezwa kuwa kutokana na mabadiliko ya sheria, mamlaka ilipewa jukumu la udhibiti wa pikipiki. Hata hivyo Mamlaka imezipa halmashauri za jiji na miji jukumu hili kama wakala kwani ndizo zilizokaribu zaidi na wananchi. Halmashauri 130 tayari zimehusishwa kati ya 135 zinazotegemewa kuingia mkataba.

Aidha, Mamlaka imefungua ofisi 21 mikoani na inategemewa ifikapo mwisho wa mwaka huu wa Fedha mamlaka itakuwa imefungua ofisi zake katika mikoa iliyobaki ya Simiyu, Geita na Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto zinazoikabili *SUMATRA.* Mamlaka hii inakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa Bajeti unaosababisha yafuatayo:-

(i) Jengo la Ofisi ya Makao Makuu linalotumika ni dogo na halikidhi mahitaji ya Mamlaka ukilinganisha na ongezeko la wafanyakazi na shughuli. Jengo linalotumika na Mamlaka kwa sasa limekodishwa kwa *TICRA*. Katika kupambana na changamoto hii Mamlaka imenunua eneo mtaa wa Nkrumah Jijini Dar es Salaam. Ujenzi unategemea kuanza katika mwaka huu wa fedha 2013/2014.

Aidha, Mamlaka inahitaji kufungua Ofisi katika Mikoa iliyosalia ili kusogeza huduma za Mamlaka karibu zaidi na wananchi. Mikoa hiyo ni Simiyu, Katavi na Manyara;

(ii) Idadi ya ajali hasa katika usafiri wa njia ya barabara, changamoto kubwa ipo katika kuwafanya watoa huduma na umma kwa ujumla kujenga utamaduni wa kujali usalama; na

(iii) Uharamia katika bahari ya Hindi- pamoja kuwa na kituo cha kisasa cha mawasiliano, uokoaji na utafutaji lakini uwezo mdogo wa kutoa msaada pindi taarifa za majanga zitolewapo.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizo, Kamati inashauri yafuatayo:-

(1) Utaratibu wa utoaji stika za zima moto (fire) uangaliwe upya na kwa makini kwani malipo haya hujumuishwa moja kwa moja kwenye malipo ya TRA na hivyo stika kupatikana bila ukaguzi wa magari kufanyika;

(2) Sumatra wajiridhishe na usimamizi wa vyombo vya majini na nchi kavu kwa kukagua na kuhakikisha vyombo hivyo ni salama kwa kubeba abiria;

(3) Sumatra iendelee kusimamia ubora wa huduma na kuendana na mabadiliko ya technolojia ili kuweza kukabiliana na ulimwengu wa kisasa; na

(4) Sumatra iongeze kasi ya utekelezaji wa upatikani kwa jingo lake;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi, Wakala Wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* , kumekuwa na ongezeko la ajali na uharibifu wa magari unaosababishwa na matuta na rasta za barabarani. Kamati ilielezwa kuwa matuta yaliyopo nchi nzima ni 114 ambayo kati yake 60 yameshaondolewa, ila kutokana na wananchi kutokujali sheria za barabarani inalazimu kuendelea na matuta hadi hapo sheria ya usalama barabarani itakapoletwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto zinazokabili Wakala wa Barabara. Wakala wa Barabara Tanzania unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Baadhi ya wahandisi washauri kushindwa kusimamia miradi kikamilifu. Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kuongeza katika mikataba vipengele vya kutoa adhabu au kuzuiwa kushiriki zabuni kwa siku za usoni;

(ii) Baadhi ya makandarasi kushindwa kutekeleza miradi kulingana na mikataba;

*[MHE. PETER J. SERUKAMBA]*

(iii) Baadhi ya wasafirishaji kuendelea kuzidisha uzito wa mizigo kwenye magari na kusababisha uharibifu wa barabara. Tatizo hili limeongezeka kwa asilimia 6 mwaka 2005/2006 hadi takribani asilimia 26 kufikia Juni 2013; na

(iv) Idadi ya watumishi ni ndogo ukilinganisha na ongezeko la mitandao ya barabara mfano kwa sasa TANROADS inawatumishi 710 wakati mahitaji ni 829.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati.

(1) Kamati inarudia kushauri, matuta na rasta za barabarani zinazosababisha uharibifu wa magari na ajali ziondolewe kwani duniani kote hakuna barabara kuu zenye matuta na rasta kama ilivyo hapa Tanzania. Wananchi kutokujua sheria za barabara isiwe ndio kigezo cha kuendelea kusababisha maafa makubwa zaidi na uharibifu wa mali. Elimu zaidi itolewe kwa wananchi; na

(2) Kamati inashauri Serikali ianze kuajiri wahandisi wengi zaidi kwani kwa Wizara ya Uchukuzi asilimia kubwa ya wahandisi watastastaafu muda si mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara katika Jiji la Dar es salaam. Jiji la Dar es Salaam limekuwa likikabiliwa na msongamano mkubwa wa magari unaotokana na sababu mbalimbali zikiwemo ofisi nyingi za umma kujengwa sehemu moja na kupelekea wakazi wa Jiji kuwa na uelekeo mmoja, ubovu wa barabara za mlisho *(Feeder Roads),* utegemezi usafiri wa barabara kwa kiasi kikubwa, uduni wa huduma za usafiri wa umma na ongezeko kubwa la idadi ya magari ikilinganishwa na uwezo wa barabara. Msongamano huu wa magari unaathari nyingi za kiuchumi, kijamii na kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara ya kuangalia ujenzi wa miundombinu ya kupunguza msongamano Jijini Dar es Salaam, hii ikihusisha barabara za kupunguza msongamano wa magari kama vile barabara

ya Kawawa - *Msimbazi Valley - Jangwani/Twiga Junction (2.7 Km)* na ujenzi wa miundombinu ya mfumo wa usafiri wa haraka wa mabasi *(BRT)* awamu ya kwanza haraka.

Kamati inapongeza juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kuhakikisha Jiji la Dar es Salaam linakuwa halina msongamano mkubwa wa magari. Hata hivyo mara kwa mara, Kamati imekuwa ikishauri kuwa Serikali itafute Fungu Maalum *(Special Fund)* kwa ajili ya kuendeleza na kuboresha miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam. Nchi mbalimbali Duniani, Mfano Kenya - Nairobi, Adis Ababa, Angola na Afrika Kusini wamefanikiwa kujenga miundombinu mizuri ya barabara za juu (*Fly Overs)* na kupunguza msongamano mkubwa wa magari katika miji miji yao.

Aidha, njia nyingine ingekuwa Serikali kuruhusu Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam kukopa kwa kutumia (*Municipal Bonds*) na kuweza kujenga barabara nyingi kwa kiwango cha lami.

Vilevile, Kamati inasisitiza kujenga barabara za juu maarufu kama (*Fly Overs*) hasa katika makutano ya barabara kuu zote zenye msongamano mkubwa wa magari kama Ubungo, Magomeni, *TAZARA, Morocco,* Mwenge, *Kilwa Road,* Makutano ya Kenyata, Kinondoni, Ali Hassan Mwinyi road hususani Salenda Brigde na Kamata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri pamoja na kuwa na mpango wa kujenga barabara za juu na za mabasi yaendayo kasi, kama barabara unganishi *(ring roads)* na za mitaani hazitaboreshwa, ujenzi wa barabara za *DART* na barabara za juu *(Fly Overs)* haziwezi kumaliza tatizo la msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Kamati inarudia na kusisitiza kuwa si lazima kila kitu kikafanywa na Serikali. Sekta binafsi ingeweza kufanya kazi hii kwa tija na haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya ujenzi wa Barabara, uvamizi wa maeneo ya hifadhi za barabara

*[MHE. PETER J. SERUKAMBA]*

umeongezeka kwa kiasi kikubwa, wananchi wengi wamekuwa wakijenga katika maeneo ya hifadhi za barabara bila kujali Sheria ya barabara Na.13 ya Mwaka 2007. Hii inaleta usumbufu na gharama kubwa katika ujenzi wa barabara.

Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi isimamie Sheria za barabarai kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vya habari kama runinga, magazeti radio na mikutano. Pia kuweka alama zitakazoonesha mwisho wa eneo la barabara.

Vilevile vyombo vya usimamizi wa Sheria ya barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu anajenga ndani ya hifadhi ya barabara kuzuiwa na kubomolewa mapema kuliko kuacha na baadae huleta msuguano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na migogoro na mvutano kutoka kwa wananchi mbalimbali unaotokana na wasiwasi wa kutolipwa fidia au kulipwa fidia kwa kiasi kidogo ambacho hakiendani na hali ya uchumi wa sasa jambo linalopelekea wananchi kugoma kuondoka katika maeneo ya miradi na kusababisha kuchelewa kuanza kwa miradi.

Kamati inashauri Sheria ya fidia itazamwe upya kwani fomula inayotumika katika kukokotoa fidia haikidhi viwango vya sasa.

Aidha, Kamati inashauri itungwe Sheria ya kudhibiti uuzaji wa chuma chakavu ili kunusuru miundombinu yetu iliyogharimu fedha nyingi na kwa usalama wa watumiaji wa barabara zetu**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mizani za Barabarani. Moja kati ya majukumu ya *TANROADS* ni ujenzi na utunzaji wa barabara, kudhibiti uzito wa magari ili kuhakikisha barabara zinadumu kwa muda mrefu. Mizani ndicho chombo muhimu sana katika udhibiti uzito wa magari ambao hupelekea uharibifu wa barabara.

Pamoja na kuwepo kwa vituo vingi vya mizani bado barabara zimekuwa zikiendelea kuharibika. Tatizo hili lisipotafutiwa ufumbuzi wa kudumu mapema, Taifa hili litakuwa linaendelea kutenga Fedha nyingi kwaajili ya ukarabati na ujenzi wa barabara zilezile kila mwaka. Kamati inashauri *TANROADS* itekeleze majukumu yake ya kusimamia barabara kwa umakini mkubwa.

Aidha, Kumekuwa na changamoto ya wafanya biashara wengi kutokujali uharibifu wa barabara. Magari mengi ya aina ya fuso kwa wastani yanatakiwa kubeba mzigo usizidi tani 3.5 lakini mengi yanazidisha na kubeba mizigo hadi tani 8, hii ni hatari sana kwani mara nyingi yamekuwa yakisababisha ajali na pia kuharibu barabara kwani matairi yake ni membamba na huchimba barabara na kusababisha mabonde.

Kamati inashauri upimaji wa uzito katika Mizani uendane na ukaguzi wa Kadi za magari, kwani katika kadi ya gari huonesha gari linatakiwa kubeba mzigo wa kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika juhudi za kupunguza msongamano wa magari katika vituo vya mizani, ni vyema Serikali kununua mizani ya kisasa ambayo inauwezo wa kupima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo (*Weight in Motion*).

Kamati inakubaliana na wazo hili na kuendelea kushauri mizani hizi za kisasa zifungwe pia katika maeneo mengine yanye kusababisha msongamano mkubwa wa kupima magari Mfano, Himo - Moshi, Mizani ya Mikese - Morogoro, Kihonda - Morogoro na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Kigamboni. Kamati ilitembelea mradi wa ujenzi wa daraja la Kigamoboni nakuelezwa kuwa eneo la ujenzi lilikabidhiwa rasmi kwa mkandarasi 1 Februari 2012 na daraja linatarajiwa katika kipindi cha miezi 36. Mradi huu wa ujenzi wa daraja la kigamboni unahusisha yafuatayo.

*[MHE. PETER J. SERUKAMBA]*

- Ujenzi wa njia sita (6) za lami umbali wa Km 1.0 kwa upande wa kurasini.

- Ujenzi wa mita 680 ya daraja *(cable stayed bridge).*

- Ujenzi wa njia sita (6) za lami urefu wa Km 1.5 kwa upande wa Kigamboni.

Changamoto zinazoukabili mradi wa ujenzi wa daraja la Kigamboni:-

- Uhamishaji wa miundombinu mbalimbali katika eneo la ujenzi.

- Kutopatikana haraka kwa eneo la ujenzi wa barabara unganishi katika pande zote mbili za Kurasini na Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri ujenzi wa daraja uendane na upanuzi wa barabara ya Kilwa mpaka Kamata na kwa upande wa Kigamboni ili kutoruhusu msongamano karibu na daraja.

Aidha, Kamati inasisitiza kuwa kwenye makutano ya barabara ya Kilwa Road na Mandela Road pia pakawekwa barabara za juu (*Fly-Over)* vinginevyo katika eneo hili kutatokea msongamano na kulifanya daraja la kigamboni kutokuwa na tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Kamati ilifanya ziara ya kutembelea Mamlaka ya MawasilianoTanzania.

Katika ziara hiyo Kamati ilijulishwa kuwa mchakato mabadiliko ya Mfumo wa Utangazajia (analojia kwenda digitali) ulianza Mwaka 2001. Chimbuko la mabadiliko hayo ni makubaliano ya nchi wanachama wa Umoja wa Mawasiliano Duniani *(ITU)* kusitisha mfumo wa utangazaji wa tekinojia ya analojia ifikapo tarehe 17 Juni, 2015 na kuanza kutumia rasmi mfumo wa digitali. Sababu ya uamuzi huu ni kuzingatia faida mbalimbali zinazoweza kupatikana kwa kutumia mfumo wa utangazaji wa digitali ambazo ni:-

(i) Matumizi bora ya Masafa (*radio frequency*) ya utangazaji;

(ii) Ubora wa picha na sauti;

(iii) Matumizi bora ya nishati na umeme;

(iv) Huduma za ziada kama intanenti; na

(v) Uwezekano wa matumizi ya runinga za mkononi na kwenye magari.

Hivyo, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikubaliana kusitisha Mfumo wa analojia tarehe 31 Desemba 2012. Ili kutoa muda wa kutosha kwa nchi wanachama kufanya tathmini ya kiufundi ili kuweza kurekebisha kasoro ziatakazojitokeza, Kufupisha kipindi cha mpito (*simulcast*) ambacho kina gharama kubwa za uendeshaji. Kutoruhusu nchi zetu kuwa soko la vifaa vya analojia vilivyopitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati.

(i) Changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika mfumo huu mpya wa digital zitafutiwe ufumbuzi

mapema Mfano, ubora wa ving'amuzi, picha kukwama kwama, rangi kubadilika badilika na kadhalika.

(ii) Katika maeneo mengi sana hizi chaneli tano za Kitaifa ambazo zinapaswa zionekane bure *(TBC, ITV, CHANEL TEN* (10), *STAR TV, EAST AFRICA TV)* hazionekani, Kamati inashauri ili kuondoa malalamiko na wasiwasi kwa katika jamii Mamlaka ya Mawasiliano itoe matangazo na elimu ya kutosha kwani itapunguza malalamiko na hofu kubwa iliyopo kwa wananchi;

(iii) Mamlaka iwasimamie kikamilifu mawakala wanaosambaza ving' amuzi kwani inaonekana wanaenda kinyume na makubaliano napengine ndio maana chaneli tano za bure hazionekani kwa wananchi na wanapopiga simu kwa maajenti wa vingamuzi huwataka kuongeza fedha ya vocha; na

(iv) Zoezi la uzimaji mitambo ya analojia katika mikoa iliyobaki lisimamishwe kwa mda ili tathmini ifanywe katika maeneo yaliyokwisha ingizwa katika mfumo huo.

Vile vile kuundwe kikundi kazi kitakachohusisha wadau wote muhimu ili lifanye tathmini na kuleta mapendekezo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Simu Tanzania *–TTCL.* Kampuni ya simu Tanzania inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 65 na asilimia 35 inamilikiwa na mmiliki mwenza *Bharti Airtel.*

Mazungumzo na majadiliano ya Serikali (*Government Negotiation Team (GNT)* na mbia mwenza *Bharti Airtel* kuhusu ununuzi wa asilimia 35 za hisa yalianza rasmi mwezi Aprili 2013 na vikao viwili vimeshafanyika ambapo pande zote mbili zimekubaliana kufanya udhamini wa hisa hizo upya na kupeana miezi miwili kukamilisha zoezi hilo.

Kufuatia makubaliano *Bharti Airtel* alikamilisha zoezi na kuwasilisha taarifa yake ndani ya muda uliopangwa. Mnamo tarehe 21 Oktoba, 2013 Kamati ya watalaam (*Diverstiture Technical Committee (DTC)* imefanya kikao cha maandalizi kwa ajili ya kuendelea na majadiliano na mbia mwenza ambapo mchakato upo kwenye hatua za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Changamoto zinazoikabili Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* ni:-

(i) Uhaba wa Fedha- tangu *TTCL* ibinafsishwe 2001 hakuna uwekezaji mkubwa uliofanyika jambo lililopelekea kushindwa kukabiliana na ushindani wa kibiashara, baadhi ya (asilimia 50) miundombinu kuchakaa bila kufanyiwa ukarabati;

(ii) Taasisi za Fedha zimeweka masharti ya kuikopesha *TTCL* kwa sharti la Serikali kutoa dhamana kwa Kampuni kwa asilimia 100. Serikali imeonesha nia ya kuidhamini *TTCL* ili mradi mbia mwenza *Bharti Airtel* aondoke;

(iii) Masafa ya Mawasiliano. Ili kukabiliana na ushindani wa kibiashara katika soko Kampuni haina budi kuacha kutumia teknolojia ya *CDMA* ambayo haitumiki na wateja wengi wa simu ukilinganisha na teknolojia ya *GSM* inayotumika na makampuni mengi ya simu. Kampuni imeshapeleka maombi hayo kwa *TCRA* lakini bado hayajaridhiwa;

(iv) Mizania ya Mahesabu. Hesabu za kampuni zilizokaguliwa kipindi cha 31 Desemba 2012 inaonesha kampuni ina uhaba wa mtaji *(Deficit in Shareholders Equity)* ya Shilingi milioni 72,975 hali inayosababisha vyombo vya fedha na mitaji kusita kushirikiana na kampuni kwa kuwa haina mtaji;

(v) Kuendesha mkongo wa Taifa. Serikali ifikie makubaliano ya jinsi *TTCL* inavyoweza kufaidika kifedha katika jukumu lake ili kukidhi mahitaji ya uendeshaji wa Mkongo wa Taifa. Aidha inailazimu kampuni kuwa na vifaa

vya kutosha hususan magari, wafanyakazi makini na vifaa vya kazi ambavyo vyote vinahitaji fedha nyingi;

(vi) Gharama kubwa za uendeshaji ikilinganishwa na mapato. Hili linasababishwa pamoja na mambo mengine idadi kubwa ya wafanyakazi wasiokuwa na tija hasa kutokana namabadiliko ya teknolojia;

(vii) Wizi na hujuma wa ukataji wa nyaya za simu aina ya *copper cables* na *optic fibre cables*; na

(viii) Soko la simu za mezani. Soko la simu ya mezani limeshuka kote duniani ukilinganisha na simu za mkononi. Mfano *TTCL* inamili asilimia 1 ya soko la simu (kwa idadi ya wateja).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na ushauri wa Kamati.

(1) Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)*, Wizara ya fedha na *Consolidated Holding Corporation (TTCL)* kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia vishirikiane kwa karibu na kuhakikisha madeni yote yanakusanywa katika kipindi cha miezi mitatu ijayo na ikishindikana taasisi hizo zikatiwe huduma kwani ni aibu kubwa kuona wadaiwa wote wa *TTCL* ni wizara na mashirika ya Serikali;

(2) Usimamizi wa Mkongo wa Taifa uwe chini ya Kampuni ya Simu ya *TTCL* na Serikali isaidie ili *TTCL* iimarike zaidi; na

(3) Wizara kwa kushirikiana na *TTCL* ifwatilie na kuhakikisha *TTCL* inaingia kwenye masafa ya *GSM.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Mapendekezo Mahsusi ya Kamati ni kama yafuatayo:-

(1) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa Serikali ikae kufikiria upya sekta nzima ya miundombinu kama

[MHE. PETER J. SERUKAMBA]
vile bandari, reli, viwanja vya ndege na barabara na kuamua kwa makusudi kuiruhusu Sekta binafsi kuwekeza. Serikali ijikite zaidi katika kukusanya kodi na suala zima la ajira;

(2) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka minane watanzania tumewaambia sana, tumesema sana kuhusu ukarabati wa gati namba 1-7 na ujenzi wa gati namba 13-14 . Serikali imekuwa ikisema itajenga, ipo mbioni, ipo kwenye mchakato na maneno mengi ya kufariji.

Kamati kwa msisitizo inasema muda wa maneno bila vitendo sasa umeisha na watanzania wamechoka na wanahitaji tija katika bandari yao. Naomba nirudie Kamati kwa msisitizo inasema muda wa maneno bila vitendo sasa umeisha na watanzania wamechoka na wanahitaji tija katika bandari yao.

Kamati inaona pamoja na sababu zote zilizopo na zinazosemwa na Serikali kwa miaka nane sasa bado Wizara haijawa na nia thabiti ya kulitekeleza hili. Serikali ikiamua inauwezo wa kujenga gati hizi, na kama inashindwa kupata fedha hata za mkopo, ni vyema sasa Mamlaka ya Bandari *(TPA)* iingie ubia na Sekta Binafsi na mradi huu uanze mara moja. *(Makofi)*

(3) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashangazwa na kigugumizi ambacho Serikali inapata na kushindwa kutekeleza miradi ambayo ni mikubwa na muhimu kwa Taifa letu. Imefika wakati Serikali iliambie Bunge lako Tukufu kinachoendelea *ATC* kwani mpaka leo imebaki ndege moja tu na ukiuliza unaambiwa Serikali ina mipango. Je, mipango hii itakamilika lini?

Kamati inazidi kusisitiza ushauri wake kuwa ili biashara iweze kufanikiwa inahitaji ujasiri na kuacha kuchanganya biashara, siasa na ubinafsi. Tubadilike na kuwa watendaji zaidi na sio kuwa waongeaji na walalamikaji. Narudia, tubadilike na kuwa watendaji zaidi na sio kuwa waongeaji na walalamikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya kati ilikuwa na injini zaidi ya 100 mpya, nzuri na zenye uwezo wa kufanya kazi ambapo hivi sasa hizi zote zimekufa. Serikali inashirikiana na Kampuni ya Malaysia kukarabati injini nane ambapo inasemekana zitakuwa tayari ndani ya miezi sita. Serikali pia inaundisha injini 13 mpya nchini Marekani ambazo zinatarajiwa kuwa tayari baada ya miaka miwili na nusu. Kwa ujumla tutakuwa na injini 21. Mahitaji ya hivi sasa hivi sasa ni angalau injini 70 na mabehewa zaidi ya 2000. Kamati inashauri kwa nguvu zote, kwa kuwa bado tunahitaji injini nyingi na mabehewa mengi, ni vema tuingie mkataba mpya wa ukarabati wa injini nyingi zaidi, ili wakati tunasubiri injini toka Marekani, angalau tuwe na injini 50 hadi 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa gharama ya kukarabati injini moja ni asilimia 60 ya bei ya injini mpya ambayo ina uwezo wa kutumika kwa miaka 30 bila matatizo, kuliko ilivyo hivi sasa ambapo hali yetu ni mbaya sana. Kamati inashauri pia kutokana na mabadiliko makubwa ya teknolojia katika Sekta hii ya Uchukuzi, ni vema Serikali sasa iamue kutafuta Fedha ama kwa kukopa au kushirikisha sekta binafsi ili ijenge reli ya kisasa ya "*standard gauge*". Kamati inaamini Serikali isipokuwa na kigugumizi katika hili reli yetu itarudisha tija yake haraka sana, kinachotakiwa tu ni kuamua. Kwani tusipofanya hivi tutaendelea kunyang'anywa biashara na kuonekana tunatengwa na majirani zetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la msingi linaloathiri tija ya *TAZARA* ni muundo wake ambao umeainishwa katika Sheria iliyoanzisha *TARAZA*, Sheria Na. 4 mwaka 1975. Kamati inashauri Sheria iliyoianzisha *TAZARA* irekebishwe ili iweze kuondoa upungufu uliopo ambao ni vikwazo kwa uhai wa reli hii na Viongozi wetu Wakuu wa Nchi wakae na kutoa dira ya muundo wa *TAZARA* katika hali ya sasa *TAZARA* inaonekana haina mwenyewe. Ni yatima. Kamati inasema hivyo kwa kuwa Serikali ya Zambia haitoi tena kipaumbele kwa reli hii kama Viongozi wetu waasisi walivyokubaliana wakati reli hii inajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwakuwa tayari kunamazungumzo ya kukopa ili kujenga jengo la abiria *(Terminal III)* katika Uwanja *wa* Kimataifa wa Julius Nyerere, Kamati inashauri makubaliano ya mkataba wa mkopo yasainiwe haraka ili mradi wa ujenzi wa kiwanja hiki uanze haraka na mapema kwani kwa sasa wawekezaji wamekata tamaa. Aidha, Wizara ya Fedha itoe vivutio *(incentive)* na dhamana *(guarantee)* ili mkataba uweze kusainiwa na kazi ianze haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafute fedha za kulipa madeni ya barabara hata kwa kukopa nje ya bajeti ya Serikali. Vile vile, Wizara ya Fedha ihakiki madeni yote ya Wizara ya Ujenzi, iyachukue na kuyafanyia utaratibu wa kuyalipa hata kwa kukopa nje ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Kamati inasisitiza kuwekwa kwa mizani bandarini kwani itasaidia kupunguza uharibifu wa barabara na usumbufu wa kutumia malori wakati yameshaharibu kiasi kikubwa cha barabara. Kuwekwa mizani hii bandarini kutarahisisha ukaguzi, urahisi na usalama wa zoezi la kupunguza mizigo endapo itakuwa imezidi uzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msongamano katika Jiji la Dar es Salaam ni kati ya matatizo makubwa yanayonyonya uchumi wetu na kuwakosesha raha wafanyakazi na wananchi wanaoishi Dar es Salaam. Kamati imekuwa ikishauri mara kwa mara kuwa ni wakati sasa Serikali kutafuta fedha hata ikibidi nje ya bajeti kuondoa tatizo la msongamano katika jiji la Dara es Salaam.

Vile vile ni maoni ya Kamati kuwa, Wizara ya Ardhi, TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi, wakutane na kutafuta fedha na kuona namna ambavyo wataweza kuondoa kero hii katika Jiji la Dar es Salaam kwani ni dhahiri kuwa hatuwezi kuondoa msongamano wa magari kwa kujenga barabara ya juu *(fly over)* moja tu ya *TAZARA* na usafiri wa mabasi yaendayo kasi "*rapid transport*". Jiji la Dar Salaam linahitaji fedha na kuangaliwa kwa jicho la pekee.

Kamati inarudia kusisitiza kuwa si lazima kila kitu kikafanywa na Serikali pekee, Sekta binafsi zinaweza kuleta maendeleo kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kuliambia Bunge lako Tukufu hatua zilizofikiwa hadi sasa za ujenzi wa barabara kuu ya Dar es Salaam - Chalinze iliyokuwa ijengwe chini ya *Public Private Partinership (PPP).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Simu ya Tanzania *(TTCL)* inamilikiwa na Serikali kwa hisa asilimia 65 na mmiliki mwenza *Bharti Airtel Tanzania* asilimia 35. Kwa hivi sasa Kampuni ya *(TTCL)* inakabiliwa na hali ngumu ya kifedha na uwezo mdogo wa kukabiliana na ushindani katika soko. Hii imetokana na mbia mwenza *Bharti Airtel* kushindwa kuwekeza katika Kampuni kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliridhia pendekezo la kununua hisa asilimia 35 zinazomilikiwa na *Bharti Airtel* baada ya *Bharti Airtel* kuonesha nia ya kujitoa katika ubia huu na Serikali kubaki kuwa mmiliki wa pekee wa *TTCL.* Kamati inashauri kuwa ni vyema sasa mmiliki mwenza wa *TTCL Bharti Airtel Tanzania* akaondolewa ili Serikali iweze kuidhamini *TTCL* kwa asilimia 100 jambo litakalowezesha taasisi nyingine za fedha kuweza kuidhamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria na aliyewahi kuwa Gavana wa *New York, Eliot Spitzer* aliwahi kusema "*delay is the enemy of progress*", *kwa* tafsiri isiyo rasmi alisema kuchelewa ni adui wa maendeleo. Kamati inasema ili kuweza kupambana na adui wa maendeleo, sasa wakati umefika wa kutekeleza yale yote ambayo ni ya msingi katika kuleta maendeleo ya nchi yetu hususan kuipa sekta binafsi nafasi inayostahili katika kuendeleza miundombinu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu. Nawashukuru pia Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu, Maofisa wote na Taasisi zilizo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Bunge ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


Miundombinu kwa ushirikiano. Ushauri na utaalam wao kwa kiwango kikubwa umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashililah, kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Vile vile shukurani ziwaendee makatibu wa Kamati hii Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi na Hosiana John kwa kuihudumia Kamati muda wote. Nawashukuru pia Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa kusoma kwa umakini sana. Sasa namwita Mheshimiwa Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA – MWENYEKITI WA KAMATI NA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana ili nitoe taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kipindi cha kuanzia Machi hadi Novemba mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013, na kwa niaba ya Wajumbe wenzangu naomba kuwasilisha taarifa kuhusu shughuli ambazo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imezifanya katika kipindi cha kuanzia Machi hadi Novemba, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini uliowateua Mwezi Machi, 2013

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



kwa mujibu wa kanuni ya 116 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Dismas Jerome Bwanausi – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Charles Jonh Paul Mwijage, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagulla, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118, nyongeza ya nane (7) (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Nishati na Madini imepewa majukumu yafuatayo:-

(i) Kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini;

(ii) Kushughulikia Miswaada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara;

(iii) Kufuatilia utendaji wa Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara;

(iv) Kushughulikia Taarifa za kila mwaka za utendaji wa Wizara; na

(v) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara kwa mujibu wa ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu ya Kamati Miongozo ifuatayo ilitumika:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



(i) Taarifa ya Wizaya ya Nishati na Madini;

(ii) Taarifa za Taasisi zilizo chini ya Wizara;

(iv) Ziara za ukaguzi wa ufanisi wa Miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa; na

(iv) Ziara za mafunzo, Semina na mikutano inayohusu sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati katika kipindi cha Machi hadi Novemba, 2013 imetekeleza kazi zifuatazo ambazo tunazitolea taarifa na mapendekezo yake kama ifuatavyo:-

(i) Kupitia Bajeti ya Wizara;

(ii) Utendaji wa Wizara;

(iii) Utendaji katika sekta ya Nishati; na

(iv) Utendaji katika sekta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kuchambua na kujadili kwa kina taarifa za Wizara na Taasisi zake kuhusu utekelezaji wa shughuli na bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha, Kamati ilichambua na kujadili taarifa ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ongezeko la bajeti kwa asilimia 58.1 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013, kuna maeneo ambayo Kamati iliyatolea ushauri, maoni na mapendekezo kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara kama ilivyowasilishwa kwenye taarifa yetu ya Bajeti ya mwezi Mei, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 ambapo katika kipindi cha Julai - Oktoba 2013,

Wizara ilizingatia maeneo ya kipaumbele yafuatayo katika kutekeleza mpango na bajeti kwa mwaka 2013/2014: Sekta ya Nishati, kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali za nishati, kukamilisha ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam, kuongeza njia za usafirishaji umeme, kuongeza uzalishaji wa umeme nchini na kuendelea na juhudi za kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Wizara iliendelea kusimamia udhibiti wa biashara ya mafuta na kuweka misingi ya kisheria kusimamia sekta ndogo ya gesi ikiwa ni pamoja na kutengeza Sera ya Gesi ya mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Madini Wizara iliendelea kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokananyo na rasilimali za madini ambapo Shilingi bilioni 64.0 zilikusanywa sawa na asilimia 29.1% ya lengo la makusanyo ya Shilingi bilioni 220, kukuza ushiriki wa Serikali katika kuvutia wawekezaji, kuendeleza wachimbaji wadogo kwa kuwatengea fedha za mikopo kiasi cha Shililngi bilioni 2.3 ambazo dirisha maalum la mikopo limeanzishwa Benki ya *TIB*, kuimarisha usimamizi wa utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nchini ambapo mfumo wa utoaji wa leseni za madini umeimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho, pia Wizara iliendelea kujenga uwezo wa watumishi wake na kuboresha vitendea kazi kwa watumishi wakiwemo wale wa Wizara, Ofisi za za Madini za Kanda na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai - Oktoba, 2013 Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha Shilingi bilioni 37.2 kati ya Shilingi bilioni 110.2 ya bajeti ya matumizi ya kawaida, ikiwa ni asilimia 34% ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha za maendeleo, Wizara ilipangiwa kiasi cha Shililngi bilioni 745.2 na katika kipindi hicho cha utekelezaji wizara ilishapokea kiasi

cha Shilingi bilioni 311.7 ya fedha za ndani sawa na asilimia 42% ya bajeti ya fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha hizo za ndani Shilingi bilioni 95.35 sawa na asilimia (12.8%) ya fedha zote za ndani zilipelekwa Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* kwa ajili ya kutekeleza miradi ya umeme vijijini. Aidha, kiasi cha Shilingi bilioni 63.0 sawa na asilimia (8.5%) ya fedha zote za ndani zilipelekwa kwa ajili ya mradi wa kujenga bomba la gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za nje Wizara ilitoa taarifa kuwa Wizara ilishapokea kiasi cha Shilingi bilioni 19.0 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo *(SIDA),* hii ikiwa ni asilimia 4.4% ya bajeti ya fedha za nje ya kiasi cha Shilingi bilioni 433.8 zilizotengwa katika mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ilionesha kuwa Wizara katika Sekta ya Nishati, miradi 29 iliainishwa na kuwekwa chini ya mpango wa Matokeo Makubwa Sasa *(Big Results Now - BRN).* Katika kutekeleza mpango huo, Wizara ilishaanzisha Kitengo Maalum cha ufuatiliaji wa *BRN* kiitwacho *Ministerial Delivery Unit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya miradi 28 chini ya Matokeo Makubwa Sasa yameelezewa vizuri katika utendaji wa Sekta ya Nishati kwenye taarifa hii kwa upande wa kazi zilizotekelezwa na *TANESCO* na pia mradi mmoja wa bomba la gesi umeelezewa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pamoja na kuridhishwa na kiasi cha fedha kilichopangwa kwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake, ilishauri kasi ya upelekaji fedha kwenye miradi na kwa watekelezaji iongezeke ili tupate matokeo makubwa. Mfano, kwa upande wa fedha za nje, Wizara imepokea kiasi cha Shilingi bilioni 19.0 ikiwa ni asilimia 4.4% tu ya bajeti ya fedha za nje. Hali hii siyo nzuri kwani itakwamisha miradi ya maendeleo na kuifanya Serikali isifikie malengo yake ya mpango na bajeti ya mwaka wa 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa *TANESCO* imepewa miradi 28 lengo ikiwa ni kuwezesha Taifa kupata nishati ya umeme ya kutosha. Kuna miradi saba ya uzalishaji, saba ya usafirishaji na 14 ya usambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii imeelezwa vizuri kwenye kiambatisho Na. 1 mwishoni mwa taarifa ambapo jedwali linaonyesha mradi ulipo, gharama, mwezeshaji, ukubwa wake, utamalizika lini na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa. Kwa kiasi kikubwa mpango huu umeanza vizuri ambapo Mmradi wa Mwanza (Nyakato) *MW 60* tayari umekamilika na unazalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko juhudi dhahiri zinazoendelea za kukamilisha miradi mikubwa ya umeme itakayolifanya Taifa kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme wa uhakika hadi ifikapo mwaka 2015. Kwenye uzalishaji umeme, utekelezaji wa miradi minne ya Kinyerezi unaendelea vizuri katika hatua mbalimbali. Pamoja na miradi hii, ni miradi ya *PPP* ya Kinyerezi Namba III na IV, Kinyerezi Namba I utakaozalisha *Megawatt* 150 uko katika hatua nzuri ya ujenzi na utakamilika mwezi Agosti mwakani. Mradi huu wa Kinyerezi I na Kinyerezi II (240 MW) itamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 kupitia *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miradi ya usafirishaji umeme, Kamati inafarijika kwamba utekelezaji wa miradi muhimu ya Makambako - Songea, na Iringa - Shinyanga umeanza na Makandarasi wanaendelea na kazi. Vivyo hivyo miradi muhimu ya Namanga - Singida, Iringa - Mbeya, Mbeya - Sumbawanga - Mpanda - Kigoma - Nyakanazi, Dar es Salaam - Chalinze - Arusha, Somangafunga - Dar es Salaam iko katika hatua nzuri za kukamilisha mikataba ya kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye usambazaji umeme, *TANESCO* inaendelea na miradi muhimu nchi nzima yenye lengo la kuimarisha usambazaji umeme nchini. Hii ni pamoja na kujenga na kupanua vituo vilivyopo vya kupoza umeme na kujenga njia mpya za kuufikisha umeme kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa juhudi na miradi inayoendelea kutekelezwa inatupa matumaini makubwa kwamba hali ya umeme nchini katika miaka michache ijayo itaimarika na kuifanya nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi zenye umeme wa uhakika katika eneo la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine inayoendelea kutekelezwa kupitia *PPP* ni mradi wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi III. Mradi huu unatarajiwa kuzalisha umeme wa kufikia *MW 600,* mazungumzo kati ya *TANESCO* na Mwekezaji kutoka China *(China Power Investment Corporation (CPI))* yanaendelea. Mwingine ni wa Kinyerezi IV. Awamu ya kwanza ya Mradi huu itajumuisha kujenga mitambo ya *MW* 300 ambayo itagharimu Dola za Marekani milioni 400. Kwa sasa *TANESCO* inajadiliana na mwekezaji kutoka China *(Poly Group)* kuhusu mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na mafanikio hayo, miradi hiyo imekuwa na changamoto kama vile kutokupatikana kwa fedha za kutekeleza miradi yenye kipaumbele kwa wakati; upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuwezesha miradi ya usafirishaji na usambazaji na ucheleweshwaji wa vibali vya msamaha wa Kodi kwa vifaa kwa ajili ya miradi ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara nchini Kenya kwa ajili ya kujifunza juu ya uzalishaji umeme kwa kutumia Joto Ardhi *(Geothemal).* Teknolojia hii ni endelevu, rafiki wa mazingira na yenye gharama nafuu katika uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu wa Serikali kuanza kujifunza juu ya uzalishaji na utumiaji wa umeme Joto Ardhi *(Geothermal Power).* Serikali ya Kenya kupitia Wizara yake ya Nishati wamewekeza katika kuendeleza sekta hii, ikiwa ni pamoja na kuwezesha tafiti mbalimbali, uchimbaji wa visima *(Drilling of wells)* na uzalishaji wa umeme huu. Kwa Kenya, mradi huu unasimamiwa na Kampuni maalumu ya Serikali inayojulikana kama *Geothermal Development Company (GDC).* Kuna haja ya kuiga mfano huo mzuri.

*[MHE. VICTOR K. MWAMBALAZWA - MWENYEKITI WA NISHATI NA MADINI]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Nishatyi Vijijini *(REA).* Katika utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijni, Wakala ulitoa taarifa juu ya miradi inayotekelezwa na Wakandarasi wa ndani, rejea kiambatisho namba mbili kama ilivyowasilishwa Mezani. Chini ya miradi hiyo, wateja 400 wameunganishwa. Miradi yote itakapokamilika mwezi Desemba, 2013 itagharimu Shilingi bilioni 23.4 na hadi sasa Shilingi bilioni 7.2 zimekwishalipwa kama malipo ya awali. Kwa upande wa Mradi Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijijini awamu ya kwanza, na jumla ya miradi 41 yenye thamani ya Shilingi bilioni 129 ilitekelezwa na Wakandarasi wa nje na ndani katika Mikoa 16. Utekelezaji ulianza Desemba, 2011 na inategemewa kukamilika mwezi Desemba, 2013 na jumla ya Shilingi bilioni 104.7 zimekwishalipwa na wateja 15,000 wa awali wameunganishwa kwenye miundombinu ya usambazaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi midogo ya kusambaza umeme vijijini chini ya *REA* inayotekelezwa na *TANESCO* katika Mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara, iko katika hatua za mwisho za utekelezaji na hadi sasa wateja wa awali 1,200 wamekwishaunganishwa kwenye miundombinu ya usambazaji wa umeme. Miradi hii inagharimu Shilingi bilioni 7.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mradi kabambe wa awamu ya pili, kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi hivi sasa, Wakala umekamilisha mchakato wa manunuzi na kuingia mikataba ya utekelezaji wa miradi 15 kati ya 25 ambayo utekelezaji wake umeshaanza. Pia Wakala unategemea kukamilisha mchakato wa manunuzi kwa miradi 10 iliyosalia mwezi Januari 2014. Miradi hii inategemea kukamilika ifikapo Juni, 2015. Miradi hii itagharimu Shilingi bilioni 881 na wateja wa awali 250,000 wanatarajiwa kuunganishwa. Hadi sasa Shilingi bilioni 38.7 zilikwishalipwa kama malipo ya awali asilimia 10 kwa baadhi ya Wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyojionyesha hapo juu, *REA* inakabiliwa na changamoto kubwa ya kutopatiwa fedha za kutosha za utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



na hii inaathiri utekelezaji wa miradi kwa wakati na pia inapunguza kasi ya utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao kuhusu Wakala wa Nishati Vijijini *(REA):-*

(i) Ili kuleta ufanisi *REA* iimarishwe na kupewa mamlaka ya kutafuta rasilimali fedha, kubuni miradi, kuitekeleza na kuiendesha kama ilivyo katika nchi ya Thailand. Mfumo huu utawezesha taifa kunufaika na rasilimali rasilimali zilizowekezwa katika sekta hii. *(Makofi)*

(ii) Katika miradi inayofuatia (mfano mradi kabambe Na. III) *REA* na *TANESCO* wajiandae kutumia nguzo za zege badala ya miti kwani nguzo za zege hudumu kwa muda mrefu, na itasaidia katika utunzaji wa mazingira. *(Makofi)*

(iii) *REA* na Wizara waandae utaratibu wa kuhakiki na kufuatilia tozo zote kwa ajili ya kuzikusanya kwa haraka ili utekelezaji wa miradi uende kwa kasi kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

(iv) Serikali itafute vyanzo vya pesa hata nje ya Bajeti ya Wizara kwa ajili ya kuhakikisha miradi yote ya *REA* inafanikiwa na kukamilika kwa wakati kwani kila Mbunge anataka kupata huduma ya umeme wa *REA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilihudhuria uzinduzi wa zabuni ya kunadi vitalu vya utafutaji mafuta kwenye kina kirefu cha maji marefu baharini na kaskazini mwa Ziwa Tanganyika. Uzinduzi ulifanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete katika ukumbi wa Mikutano wa Mwalimu Nyerere Dar es Salaam tarehe 25 Oktoba 2013. Zabuni inategemea kufungwa tarehe 15 Mei, 2014. Zabuni imefanyika nchini Tanzania kwa mara ya kwanza na hii inatoa fursa nzuri kwa ushiriki wa Watanzania katika Zabuni hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zabuni imetoa upendeleo maalum kwa Kampuni za Kitanzania au kwa zile ambazo zitashirikisha Watanzania kwa kutoa alama za upendeleo kwa kufuata misingi ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004. Aidha, wakati wa uzinduzi wa Zabuni, Mheshimiwa Rais alisisitiza kuwa ushiriki wa Watanzania wote utakuwa kwa kupitia Shirika la Maendeleo ya *Petroli Tanzania (TPDC)* ambapo ushiriki wake upo zaidi ya asilimia 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhakikisha kuwa vitalu vitatolewa kwa Kampuni zenye uwezo za ndani na nje ya nchi. Aidha, makosa tuliyoyafanya kwenye utoaji wa vitalu vya madini usirudiwe kwenye vitalu vya utafutaji gesi na mafuta. Kwenye madini Watanzania wengi wanamiliki vitalu vya utafutaji madini maeneo makubwa sana lakini mchango wao kwenye pato la Tanzania haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati isingependa kurudia makosa ya awali ya kumilikisha watu au Kampuni vitalu na kuvihodhi bila ya kuviendeleza kama ilivyofanya kwenye Sekta ya Madini, kitendo cha kuwamilikisha watu au Kampuni mfano eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 3.886 ambazo ni sawa na 0.4% ya eneo lote la Tanzania (eneo ambalo ni sawa na ukubwa wa Mkoa wa Dar es Salaam mara nne) bila kulifanyia kazi, siyo jambo jema kwa ustawi wa nchi yetu eti kwa kisingizio cha kuwapa maeneo wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania (wazawa) katika utaratibu wa kupata vitalu vya gesi, chini ya *TPDC* upo wazi. Wazawa hawajazuiwa, hawabaguliwi ili mradi taratibu zilizowekwa na *TPDC* zikafuatwe. Lakini ijulikane kuwa uwekezaji katika uchimbaji wa gesi unahitaji fedha nyingi. Kamati inawaomba Watanzania wenye uwezo wajitokeze waache kulalamika, lakini ikumbukwe kuwa *TPDC* ni Shirika la Serikali na umiliki wake ni asilimia 65. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea Taarifa kuhusu uundwaji wa Kampuni ya Taifa ya Mafuta *(COPEC)* iliyoanzishwa na *TPDC* mnamo mwaka 1999. Pamoja na

maelekezo na maamuzi ya Bunge ambayo mara kwa mara yamekuwa yakiagiza Kampuni hii kuanza kufanya kazi iliyokusudiwa, bado Kampuni hii haijaanza kazi. Kamati kama ilivyoamuliwa kwenye vikao vya Bunge vilivyotangulia, bado inaona umuhimu wa kuwa na Kampuni ya mafuta ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena, Kamati inaishauri Serikali kulichukulia suala la kuwa na Kampuni ya Mafuta ya Taifa kama suala la kufa na kupona. Ni matumaini yetu kupitia Bunge lako Tukufu litaishinikiza Serikali kuhakikisha kampuni hii inaanza kufanya kazi au la, waeleze sababu za kukaidi maelekezo ya Bunge (tangu 1999 mpaka 2013).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata taarifa kutoka kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* ambapo pamoja na majukumu mengine inasimamia mradi wa bomba la gesi toka Mtwara hadi Dar es Salaam lenye urefu wa Kilomita 542. Bomba hilo litakuwa na uwezo wa kusafirisha gesi futi za ujazo milioni 784 kwa siku *(784 MMCFD).* Utekelezaji wa ujenzi wa bomba ambao Kamati imeushuhudia, njia ya mkuza imesafishwa kwa kilomita 491, vipande vya mabomba 24,077 kati ya 44,700 vinavyohitajika vimeishawasili nchini na shughuli za kuunganisha vipande vya mabomba zinaendelea. Hadi sasa vipande vya mabomba vyenye urefu wa kilomita 161 vimeunganishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na maelezo ya Wakandarasi kwa Kamati kufikia Januari 2014 mabomba ambayo hayajawasili nchini ambayo ni asilimia 47 yatakuwa tayari yamefikishwa kwenye eneo la mradi. Aidha, Kamati ilishuhudia zoezi la kuweka tabaka la zege zito kwenye vipande vya mabomba ambayo yanaandaliwa mahususi ili kuzamishwa baharini katika eneo la kilomita 25 ambapo bomba linapita baharini mpaka kisiwa cha Songo Songo. Katika eneo la Somanga Fungu, bomba litokalo Mtwara litaunganishwa na Bomba litokalo Songosongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mipango ya *TPDC* na Serikali kukamilisha ujenzi wa bomba na mitambo ya kusafisha

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



gesi asilia kule Madimba (Mtwara Vijijini) na Songosongo unaotegemewa kukamilika mwezi Desemba, 2014 na mara baada ya kukamilisha ujenzi wa mitambo hiyo majaribio ya kusafirisha gesi kwa bomba yatafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa mikataba ya ujenzi wa bomba na mitambo ya kusafisha gesi asilia kule Madimba na Songosongo unatamka kuwa kutakuwepo wafanyakazi Watanzania wakipata uzoefu kutoka kwa Wakandarasi na wataalamu toka China, hali sivyo ilivyo, mpaka sasa hakuna Watanzania walioajiriwa kupata uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inayo maoni yafuatayo kuhusu *TPDC*:-

(i) Ujenzi wa mitambo ya kuchakata gesi Madimba na Songosongo na nyumba za wafanyakazi uharakishwe.

(ii) Kamati kwa mara nyingine tena inaisihi na kuishauri Serikali kuharakisha utaratibu wa utoaji vibali vya ajira za vijana ili vijana wa Kitanzania wapate uzoefu pindi bomba linapokamilika.

(iii) Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* lishiriki kama mbia katika miradi ya utafutaji na uendelezaji wa miradi ya mafuta na gesi.

(iv) Matumizi ya "*Flow Meter*" yarejeshwe katika mfumo wa kupakua mafuta kutoka kwenye Meli ili kudhibiti uhakika wa viwango vya mafuta yanayopokelewa kuboresha makusanyo ya kodi.

(v) *TPDC* wapewe wataalamu wa kutosha kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji wa bomba la gesi asilia linalotegemewa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2014.

(vi) Serikali iliwezeshe Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kuanzisha Kampuni ya kitaifa ya biashara ya mafuta.

(vii) Vitalu vya utafutaji mafuta vitolewe kwa misingi ya uwazi na uwezo wa kufanya kazi ya kuongeza rasilimali kwa Taifa na siyo kwa watu, kwa zana ya Utanzania, halafu kuwa madalali. *(Makofi)*

(viii) Makampuni ya ndani hasa yanayomilikiwa na wazawa (Watanzania) kwa asilimia 50, yaliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya nchi yetu, na yaliyotimiza au kukidhi vigezo, na hata yale yaliyosajiliwa nje ya nchi yaliyotimiza vigezo yenye ubia na Watanzania (wazawa) yapate upendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na wadau mbalimbali wa Mafuta kwa ajili ya kujadili changamoto wanazokutana nazo kwenye biashara ya mafuta nchini. Wadau hao ni pamoja na Wamiliki wa Malori *(TATOA), Petroleum Importation Coordinator (PIC), Energy and Water Utility Regulatory Authority (EWURA),* Shirika la Taifa la Mafuta *(TPDC)* na *Tanzania International Petroleum Reserves Ltd (TIPER).* Changamoto wanazokutana nazo katika utekelezaji wa shughuli zao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Umoja wa Wasafirishaji na Wamiliki wa Malori ambao wanajihusisha na kusafirisha mafuta toka bandari ya Dar es Salaam kwenda Miji ya Mikoani na nchi za jirani, wana changamoto kuu nne zifuatazo zinazokwamisha shughuli zao:-

(a) Magari ya kusafirisha mizigo ikiwemo mafuta jamii ya petroli hayana eneo maalum ya kuegeshwa hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Hali hii inahatarisha usalama. Mafuta ni bidhaa inayohitaji uangalizi wa hali ya juu kutokana na tabia yake ya kulipuka. Sheria inataka magari yakishapakiwa mizigo ya *transit* hayawezi kuegeshwa kwenye maeneo nje ya barabara kuu iliyoainishwa.

(b) Sheria inayowataka wasafirishaji wa mafuta kuwa wameondoa mafuta yaendayo nchi jirani katika siku zisizozidi 30, inawalazimisha wamiliki wa magari kuwa na magari mengi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



hivyo kuongeza gharama za uendeshaji. Wadau wanaomba waongezewe siku kutoka 30 hadi 60.

(c) *TATOA* walilalamikia vikwazo vinavyowekwa na nchi jirani kwa magari toka Tanzania kwa kuwatoza gharama za maegesho hata kama hawana sababu ya kuegesha na kuwachelewesha mipakani.

(d) *TATOA* walilalamikia ongezeko la ada na tozo zinazodaiwa na mamlaka mbalimbali kama ongezeko la bima na tozo ya *SUMATRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Uratibu wa Uagizaji wa Mafuta *(Petroleum Importation Coordinator)* ilianzishwa mahsusi kuratibu uagizaji wa mafuta chini ya Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa wingi *(BPS).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifahamishwa kwamba maeneo yanayokwamisha utekekelezaji wa chombo hiki ambayo ni:-

(a) Uwezo mdogo wa kifedha wa Makampuni yanayoagiza mafuta hali inayopelekea ucheleweshaji ufunguzi wa malipo *(LCs);*

(b) Kuchelewesha kwa meli;

(c) Ushirikiano duni kwa wadau wa uagizaji wa mafuta ambao ni Mamlaka ya Bandari *(TPA), TBS, TRA, EWURA* na *PIC* yenyewe;

(d) Kutokuwepo mabomba yenye kipenyo kinachohitajika na matenki yenye uwezo mkubwa wa kuhifadhi mafuta; na

(e) Muundo wa chombo chenyewe *(PIC)* na hasa Bodi yake inao mgongano wa kimaslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa uagizaji mafuta kwa wingi ulikuwa wa busara na wenye mafanikio kwa Taifa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Kamati inaishauri Serikali ifanye tafakari ya kina juu ya chombo kitakachoratibu uagizaji mafuta kwa kuondoa upungufu wa *PIC* ya sasa, lakini kwa kuchukua uzoefu mzuri uliopatikana hasa suala la uwazi katika kuendesha tenda za ugavi wa mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Sekta ya Nishati *(EWURA)* umekuwa wenye ufanisi kwa kuweza kudhibiti ubora wa mafuta, bei na viwango vya miundombinu inayohusiana na shughuli za hifadhi, usafirishaji na vituo vya kuuzia mafuta jamii ya petroli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri na kuielekeza *EWURA* kubuni aina ya vituo vya kuuzia mafuta ambavyo vitaweza kusambaa maeneo hasa ya vijijini kufuatia wimbi la uuzaji wa mafuta ya petroli katika vifaa visivyokuwa na viwango. Vituo hivyo ni bora viwe vya gharama nafuu na vizingatie usalama na utunzaji wa mazingira. Pia Kamati inaishauri *EWURA* iziongoze mamlaka zote zinazohusika na ujenzi wa Vituo vya Mafuta ili kupunguza usumbufu kama ulivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Wafanyabiashara wa Mafuta *(TAOMAC)* ni Umoja wa Makampuni yanayojishughulisha na uagizaji, utunzaji na usambazaji wa mafuta nchini. Sekta muhimu katika uendeshaji na uendelezaji wa Sekta ya Mafuta, *TAOMAC* wanawezesha mafuta kufika kwa mlaji wa mwisho. Kamati ilikutana na *TAOMAC* kwa lengo la kujadili changamoto zinazowakabili ili kwa pamoja tutafuta suluhisho kwa ustawi wa sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PIC* waliainisha upungufu katika ujenzi wa boya la kupakulia mafuta la *SBM* kwa kuwa na bomba moja tu linalotumika kupakua dizeli wakati huagiza petroli *(Mogas)* na mafuta ya ndege *(Jet A1).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutumia fursa nzuri ya mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja, boya lililojengwa *SBM* liwekwe bomba la pili ili kuwezesha kupakua mafuta aina

mbili kwa wakati mmoja. Utaratibu huo utapunguza muda wa meli kukaa Bandarini ili kupunguza gharama *(Demurrage Charges).* Makampuni ya Mafuta pia yaongeze ukubwa wa mabomba yao ya kupokelea katika matanki yao kutoka *KOJ (Kurasini Oil Jet)* na *Tipper* na kusimamia ulinzi ili kupunguza upotevu wa mafuta ambao unaendelea kuongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau walieleza masikitiko yao kwa Serikali kupitia Sheria na Kanuni zinazowekwa na Mamlaka zake kuonyesha kutopendelea uwepo wa biashara ya mafuta na nchi jirani *(transit business)*. Hii ni pamoja na matakwa ya kuondoa mafuta kwa kipindi kifupi cha siku 30 na kanuni zinazopingana juu ya uuzaji wa mafuta hayo nchini *(localisation).* Ilipendekezwa upungufu wa biashara hii uainishwe na kuondolewa ili Taifa lifaidike na biashara ambayo faida zake ni nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabili tatizo la malipo ya mafuta yanayoagizwa na udhibiti wa fedha adimu za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta, wadau walipendekeza Serikali kupitia Benki Kuu ianzishe mfumo ambapo Muungano wa Benki za Ndani chini ya usimamizi na udhamini wa Benki Kuu watasaidia kipengele cha malipo katika uagizaji mafuta. Yaani makampuni yafanye malipo benki kwa kutumia fedha za kigeni na benki au chombo maalumu kwa shughuli hii wamlipe anayeleta mafuta kwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ililelezwa juu ya tishio la usalama katika mtandao wa mabomba na matenki ya kuhifadhi mafuta. Kuna ongezeko la wizi wa mafuta unaohusisha utoboaji wa mabomba hali inayoweza kupelekea milipuko ya moto au uvujaji wa mafuta kwenye eneo la bandari unaoweza kukimbiza meli kwenye bandari ya Dar es Salaam. Jukumu hili libebwe na mamlaka ya kiSerikali kudhibiti uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umoja wa Makampuni ya mafuta walionesha kutoridhishwa na uendeshaji wa Kampuni ya Uratibu wa Uagizaji wa Mafuta *(PIC)* ambayo wanaimiliki

na kugharamia uendeshaji wake, lakini inaonekana kuwajibika kwenye mamlaka za *EWURA* na Wizara ya Nishati na madini. Pendekezo lilitolewa kuwa kuna haja ya kuangalia upya muundo na uwajibikaji kwa chombo cha kuratibu uagizaji wa mafuta kwa wingi ili mradi chombo hicho kisiwe shirika la Umma ili kuepuka upungufu unaoendana na Mashirika ya Umma na kiazime mafanikio ya *PIC* ya kuendesha tenda kwa haraka na uwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau pia walieleza jinsi Serikali inavyopoteza mapato yake kwa waagizaji wa mafuta ya kulainisha mitambo *(lubricants & greases)* wanavyoagiza mafuta na kudai kuwa ni malighafi. Pia ilielezwa jinsi soko la Tanzania linavyolishwa vilainisha mitambo vilivyo chini ya viwango na kuwatia hasara watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ndogo ya mafuta, Kamati inaishauri Serikali na mamlaka zake kufanya kazi kwa karibu na wadau hawa na kuwaona kama washirika wenza katika ustawi wa sekta hii. Katika mjadala na wadau yaliyohusisha mamlaka za Serikali na Watendaji wa Serikali ilibainika wazi kuwa masuala mengi ambayo yanaonekana kuwa ni kikwazo yanaweza kutatuliwa kwa kukaa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuhimiza mamlaka zake, sekta binafsi na hata Serikali kuu kuwekeza katika hifadhi ya mafuta ambayo italipatia Taifa letu faida ya kuwa soko la mafuta kwa nchi zilizotuzunguka ikiwemo nchi zisizopakana na bandari. Shughuli hii ina fursa na faida kubwa ikiwemo usalama wa mafuta ya akiba bila mtaji wa kuyanunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Kamati ya Bunge ya Bajeti ifuatilie kwa karibu ukwepaji wa kodi kupitia mafuta ya kulainisha mitambo *(lubricants & greases)* ili kutoa ushauri kwa Serikali juu ya njia thabiti ya kudhibiti uvujaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Wizara na *EWURA* kuandaa kanuni na sheria zinazohusiana na Sekta ya

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Mafuta. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuwa makini katika kusimamia uendeshaji wa mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa wingi kwa kuuboresha na kuepuka kupoteza faida zilizokwisha patikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea hifadhi ya mafuta ya *TIPER* ambayo inamilikiwa kwa asilimia 50 kwa 50 baina ya Serikali na Kampuni ya *Oryx*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIPER* huhifadhi mafuta ya Makampuni ya Mafuta *(OMCs)* bila kujali makampuni hayo hayana uwezo wa kuhifadhi mafuta kwenye vituo vyao, au hawana vituo vya kuhifadhi mafuta au kutumia *"Bonded facility"* kwa mafuta yanayoenda nje ya nchi. Kwa miaka mitatu ya nyuma idadi ya wateja waliokuwa wanatumia *TIPER* imeongezeka kutoka Makampuni 18 hadi kufikia Makampuni 26 kwa mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwaka 2012 *TIPER* ilikuwa na uwezo wa kuhifadhi mafuta kiasi cha mita za ujazo 140,000 ambayo ni sawasawa na matanki 30. *TIPER* ina mpango wa kuongeza matanki ya mafuta hadi yafikie uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 220,000 ambayo ni sawa na matanki 32 na kufikia mwaka 2016 *TIPER* itakuwa na uwezo wa kuhifadhi mafuta mita za ujazo 264,000 sawa na matenki 33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo yatatekelezwa ndani ya miaka mitatu ijayo:-

(i) Kuongeza ufanisi na kutegemewa kwa kubadilisha bomba la kusafirisha mafuta kutoka Kigamboni hadi Kurasini kwa seti ya mabomba manne na kubadilisha pampu na *new manifold.*

(ii) Kuweka *flow meters* kwa uhakika zaidi wa upimaji mafuta, kipimo cha moja kwa moja kitakachowekwa kwenye matenki *(automatic tank gauging)* ili kuongeza uzalishaji wenye ufanisi utakaowezeshwa kwa vipimo vya kielekroniki kwenye matenki kwa muda muafaka (kamili).

(iii) Pia ujenzi wa kituo kipya *(LPCs)* cha kuhifadhia mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri *TPDC* na *TIPER* kujenga uwezo mkubwa zaidi wa kuhifadhi mafuta kwa wingi *(Bulk Storage)* ili mafuta yote yanayoagizwa yahifadhiwe na Serikali na kupoa baada ya hapo *"flow meters"* ziwekwe kwenye matanki hayo ili kuruhusu kwenda kwenye matenki ya Makampuni yanayouza mafuta (baada ya kupoa). Mtindo huu unapunguza upotevu *(losses)* wa mafuta kama ilivyo sasa wakati wa kushusha. Vile vile inaongeza *yield* ya kodi baada ya mafuta kupoa. Wenzetu wa Kenya wanafanya hivyo kwa sasa, na sisi tuige. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na *STAMICO* kwa lengo la kupokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Bajeti kwa kipindi cha miezi sita ya mwaka wa fedha 2013/2014. Kuanzia mwezi Julai hadi Novemba, 2013 Shirika limetekeleza na linaendelea kutekeleza shughuli nne zifuatazo:-

(i) Kukamilisha mikataba ifuatayo:-

(a) Ununuzi wa mgodi wa Tulawaka ambapo *STAMICO* imesajili kampuni tanzu itakayoendesha mgodi huo inayoitwa *STAMIGOLD Company Limited*.

(b) Ubia baina ya *STAMICO* na *Manjaro Resources* wa kuendeleza upya mgodi wa Buhemba ambapo hadi sasa Kampuni ya *Manjaro Resources* wametakiwa kuweka *Bank Guarantee* na kuwasilisha ratiba upya ya utekelezaji wa mradi ndipo mkataba utiwe saini na unatarajiwa kukamilika mwisho wa mwaka huu.

(c) Umiliki wa pamoja wa Kitalu C, eneo la Mirerani kati ya *STAMICO* na *TanzaniteOne Mining Ltd*, rasimu ya mwisho ya mkataba imekwishasainiwa baada kupata maoni na ushauri ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



(d) Urejeshaji wa mgodi wa Kiwira ambapo *STAMICO* wamekabidhiwa rasmi mgodi huo mwezi Novemba, 2013 na juhudi za kupata mkopo au mbia mwenye uwezo zitaendelezwa.

(i) Kufanikisha ajira mpya baada ya kupata kibali cha ajira mpya 78 kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambapo kufikia mwezi Desemba, 2013 usaili kwa ajira hizo utakuwa umekamilika.

(ii) Kuendelea kutafuta kazi za uchorongaji miamba ambapo kwa mwezi Agosti na Septemba, 2013 Shirika limeshiriki katika zabuni mbili za Kampuni ya *MMG Gold Limited* na *Mbeya Cement* zinazohitaji kuchorongewa na Shirika linasubiri majibu ya zabuni hizo.

(iii) Kuendelea kuratibu masuala ya wachimbaji wadogo ambapo Wizara na *STAMICO* walifanikisha kazi ya Uongozi wa mpito wa *FEMATA* na uitishaji wa Mkutano Mkuu uliofanyika Dodoma tarehe 25/08/2013 ambao ulipitisha Katiba Mpya na kuwachagua viongozi wa *FEMATA* kwa kipindi cha miaka mitano.

(iv) Uanzishwaji wa Mfuko wa *TIB* ambao umeanza mwezi Juni, 2013 kwa ajili ya kuendeleza wachimbaji wadogo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa maoni na Ushauri ufuatao kwa Serikali:-

(i) Wafanyakazi wa *STAMICO* wamefikia umri wa kustaafu hivyo kutakiwa kuajiri wafanyakazi wengine. Ili kuepuka kupoteza hazina ya historia na uelewa wa Taasisi hii nyeti *(institutional memory)*, Kamati inashauri Watendaji walioko waendelee kwa kipindi maalumu ili warithishe uzoefu wao kwa wafanyakazi watakaoajiriwa.

(ii) Serikali ilenge kujenga *STAMICO* yenye nguvu na uwezo *(autonomous)* ya kujisimamia katika ubunifu na

utekelezaji wa mipango na mikakati yake bila kusubiri maelekezo na ruksa toka Wizarani kwa kila jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, Wakala wa Ukaguzi wa Madini *(TMAA)* wana majukumu ya ukaguzi wa gharama za uwekezaji na uendeshaji wa migodi, uhakiki wa mapato, na ukaguzi wa shughuli za ukarabati na utunzaji wa mazingira Migodini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai hadi Oktoba, 2013 Wakala ilifanya ukaguzi kwenye migodi mikubwa na midogo na kufanikiwa kuifanya Serikali iweze kukusanya mrabaha wa Shilingi bilioni 41.1 kutoka kwa wamiliki wa migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa Kamati ilizozipata kutoka kwa Wakala ni kuwa, kiasi cha madini kinachochimbwa nchini mwetu na kutoroshwa nje ya nchi ni kingi mno kuliko takwimu rasmi katika Ofisi za Serikali. Kwa mfano, takriban tani 20 za dhahabu huzalishwa kila mwaka na wachimbaji wadogo lakini takwimu rasmi za Serikali za uzalishaji ni chini ya tani mbili kwa mwaka.

Vilevile Wakala huu una taarifa kuwa, katika kila kilo nne za Tanzanite inayozalishwa kwa siku, ni kilo moja pekee inayoripotiwa Serikalini kupitia kwa wenye viwanda vya ukataji vito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kwa kuanzia na *Tanzanite,* ili kudhibiti utoroshaji, eneo lote la migodi ya Mirerani liwekewe uzio. Chini ya utaratibu huo, ulinzi utawekwa kwa kutumia watu na mitambo maalum ili kuhakikisha kila kipande kinachotoka kimehakikiwa na kulipa tozo na ushuru stahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni maoni na ushauri wa Kamati kwa Wakala ambao ni muhimu kwa ustawi wa Sekta ya Madini.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



(i) Serikali isaidie Taasisi hizi *(TMAA, STAMICO na TANSORT)* kuingia ubia na hifadhi za kijamii au Taasisi nyingine za kifedha ili kujenga jengo la kuendeshea shughuli zao *(Madini House).*

(ii) *TMAA* wajitahidi kuelezea kazi na majukumu yao ili kutangaza mafanikio yanayopatikana katika kusimamia na kudhibiti Sekta ya Madini.

(iii) Ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa *TMAA* Serikali itilie mkazo utekelezaji wa Sheria ya Madini hasa katika kifungu cha 6(4) cha Sheria hiyo. Sheria hii inasema Kamishna wa Madini ata-*forfeit* yakikamatwa madini ambayo yako nje ya utaratibu wa Serikali.

(iv) Pamoja na nia ya kudhibiti wizi na utoroshaji wa madini kama ilivyoshauriwa hapo juu, maboresho katika Sheria ya Madini yafanyike ili kuwataka wachimbaji wadogo wote kuendesha shughuli zao chini ya umoja wao. Hii itasaidia Serikali kuwezesha kirahisi, kuisimamia na kuidhibiti kwa lengo kuleta ustawi sawia kwa wadau wote.

(v) Kutokana na mafanikio ya Wakala na kutokana na ukubwa na umuhimu wa Sekta ya Madini nchini, Serikali inashauriwa kuipa uwezo zaidi *TMAA* ikiwa ni pamoja na kuigeuza kuwa mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANSORT* ni Kitengo kinachojihusisha na kuthaminisha almasi na madini ya vito kwa ajili ya kukokotoa mrabaha, kutayarisha miongozo ya bei *(Price Guides)* za almasi na madini ya vito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya almasi zilizothaminiwa na kitengo kuanzia mwezi Julai hadi Novemba, 2013 kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi ni kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



| No. | Exporting Companies | Carats | Value US$ | Royalty US$ |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Williamson Diamond Ltd | 50,778 | 12,867,777 | 643,389 |
| 2. | El Hillal Minerals Ltd | 8,601 | 2,601,156 | 130,058 |
| 3. | Other Dealers | 8,939 | 671,104 | 33,555 |
| | Total | 68,318 | 16,140,038 | 807,002 |

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoonesha kwenye jedwali hapo juu, Jumla ya *Carat* 68,318 za almasi zenye thamani ya Dola za Kimarekani 16,140,038 zilithaminishwa. Aidha, mrabaha uliokusanywa ni Dola za Kimarekani 807,002 sawa na Shilingi bilioni 1.3. Katika kipindi hicho, minada miwili ya mauzo ya almasi ya *WDL* ilisimamiwa huko *Antwerp* (Ubelgiji), thamini nne zimefanyika katika Kampuni ya *El Hillal Minerals Ltd* na thamini 27 zilifanyika kwa wazalishaji wengine 12 wa almasi.

*Mauzo ya vito vya rangi nje ya nchi –*
*Hadi 30/09/2013*

| ***Month*** | ***Weight Kg*** | ***Grams*** | ***Carats*** | ***Value ($) USD*** | ***Royalty (Tshs)*** |
|---|---|---|---|---|---|
| Jul-13 | 3,625,311 | 294,781 | 27,813 | 5,196,665 | 222,446,314 |
| Aug-13 | 6,101,040 | 1,159,134 | 18,004 | 4,574,094 | 301,783,589 |
| Sep-13 | 415,863 | 6,950,881 | 24,297 | 3,087,479 | 159,076,719 |
| Total | 10,142,214 | 8,404,795 | 70,114 | 12,858,237 | 683,306,622 |

Hadi sasa tani 10 za madini ya mapambo *(Ornamental stones),* gramu milioni nane za madini ya vito visivyochongwa *(rough gemstones)* na *carat* 70,000 za madini ya vito vilivyochongwa yamethaminiwa na wataalam wa Kitengo kwa thamani ya US$ milioni 12.8. Mrabaha uliokusanywa na Serikali kutokana na shughuli hii ni Shilingi milioni 683. Zaidi ya thamini 343 kwa zaidi ya Makampuni 70 yanayozalisha au kufanya biashara ya vito yamefanyika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza kazi zake, kitengo hiki kinakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Kutokuwepo kwa kada ya wajemolojia katika muundo wa kada za Utumishi Serikalini;

(ii) Uhaba wa watumishi wenye ujuzi na utalaam kwa viwango vinavyokubalika Kimataifa;

(iii) Ukosefu wa ofisi yenye nafasi ya kutosha kwa watumishi wote wa Kitengo;

(iv) Kutokuwepo kwa kituo au mahali maalum pa kufanyia biashara ya almasi ya vito nchini (Hakuna soko la ndani);

(v) Kushamiri kwa vitendo vya wizi, udanganyifu na utoroshwaji wa madini ya almasi na vito nchini; na

(vi) Ukwepaji wa kodi na tozo za Serikali hasa miongoni wa wazalishaji na wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa juu ya miradi inayoendeshwa kwa Ubia baina ya Serikali na Watu Binafsi *(PPP)* katika Sekta ya Nishati na Madini ambayo ni pamoja na:-

(1) Mgodi wa Buckreef. Serikali kupitia *STAMICO* imeingia Ubia na Kampuni ya *TANZAM 2000* ili kuendeleza upya Mgodi huu. Katika Mgodi huu *STAMICO* inamiliki hisa asilimia 45 na *TANZAM 2000* asilimia 55. Kazi zilizokwisha fanyika ni pamoja na kuchoronga miamba, uchunguzi wa Sampuli za miamba katika maabara na *resource modelling* kwa ajili ya tathmini ya mashapo yaliyopo. Kupitia tathmini hiyo imebainika kuwepo kwa Wakia milioni 2.12 za dhahabu. Pia ukubwa wa leseni umeongezwa kutoka Kilometa za mraba 3.9 hadi kufikia 16 pamoja na kutathmini mali zilizopo kwa eneo lililoongezeka ili kulipa fidia kwa wahusika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



(2) Mgodi wa Buhemba. Serikali kupitia *STAMICO* imepata mbia ambaye ni Kampuni ya *Manjaro Resources* ambaye anamiliki asilimia 60 ya hisa na *STAMICO* asilimia 40. Hatua iliyopo sasa ni *STAMICO* kukamilisha taratibu za kuunda na kusajili Kampuni ya Ubia baina yao.

(3) Mgodi wa Tulawaka. Mgodi huu uliokuwa unamilikiwa na *African Barrick Gold* kwa sasa umekabidhiwa *STAMICO* kwa niaba ya Serikali. Kwa sasa bado hatua ya makabidhiano ya mitambo na vifaa unaendelea na mara tu baada ya kukamilika *STAMICO* itatafuta Mbia wa kushirikiana naye kuendeleza mgodi huo kwa njia ya *PPP*.

Miradi ya Mfano katika maeneo ya migodi katika kukabiliana na changamoto za wachimbaji wadogo, Serikali kupitia *PPP* imeanzisha miradi ya mfano maeneo ya Geita baina ya Mgodi wa *Anglo Gold Ashanti,* na *African Gold Barrick* pamoja na *North Mara* eneo la Tarime. Serikali kwa kushirikiana na wamiliki wa migodi wameingia makubaliano ya awali *(MOU)* kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo na wameanza kwa kuainisha na kufanya uchambuzi wa kina kuhusu matatizo yanayozikumba jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya *PPP* katika nchi yetu bado ni changa, hivyo basi, katika utekelezaji wake inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Uelewa mdogo kati ya Wadau;

(ii) Mtizamo tofauti kati ya Serikali na Sekta Binafsi;

(iii) Ukosefu wa fedha kwa kuwa uzoefu unaonesha kuwa wadau wengine hutaka dhamana ya Serikali ili kukopa;

(iv) Mazungumzo kati ya pande mbili kuchukua muda mrefu.

Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali inapoingia Mikataba ya Makubaliano *(Memorandum of Understanding)* Serikali iwe na asilimia kubwa ya hisa zaidi ya Mwekezaji. Mfano, Serikali iwe na 55% na Mwekezaji 45%.

(ii) Sheria ya uchimbaji wa madini inayomtaka mchimbaji kuchimba madini aina moja iboreshwe kwa kuruhusu mchimbaji aliyepewa leseni katika eneo husika kuchimba madini ya aina zote yatakayokutwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kutembelea migodi mikubwa ya Kanda ya Ziwa na ule ulioko Kaskazini *(Tanzanite).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea Migodi mikubwa yaani *Geita Gold Mine* na *African Barrick Gold* (Bulyanhulu, Buzwagi na North Mara (Nyamongo)) inayojihusisha na uchimbaji wa dhahabu. Migodi hiyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uvamizi unaofanywa na wachimbaji wadogo hali inayotishia usalama, matarajio makubwa miongoni mwa jamii, ukosefu wa umeme wa gridi, wizi unaofanywa na watu wa nje ya mgodi, hujuma kwenye mabomba, kushuka kwa bei ya dhahabu katika Soko la Dunia, na ukosefu wa maji kwa ajili ya shughuli za migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migodi ya Almasi *Williamson Diamonds Ltd (WDL)* na *El Hillal Minerals* (mgodi unaomilikiwa na mtanzania mzawa) ambayo ipo Mwadui Mkoani Shinyanga ilitembelewa. Mgodi wa *El Hillal Minerals* ulionekana kushirikiana kwa kiasi kikubwa na jamii kwa kutoa huduma za afya, maji na elimu na Kampuni hii inalipa kodi stahiki kwa Halmashauri.

Mgodi huu unakabiliwa na changamoto nyingi kama vile uvamizi wa wachimbaji wadogo, Wanakijiji kuingiza mifugo katika eneo la mgodi, uchomaji moto na ukataji miti ovyo maeneo ya mgodi hali inayosababisha uharibifu wa vyanzo vya maji, Wanakijiji kulima pembezoni mwa

mabwawa ya maji na pia ukosefu wa maji kwa shughuli za mgodi wakati wa kiangazi. Kubwa lililojitokeza ni mgodi kutopata *exemption* (misamaha) kama migodi mingine inavyonufaika na misamaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tanzanite One Mining Ltd* ambayo ni moja kati ya Kampuni za *Richland Resources Ltd.* inamiliki eneo la Kitalu 'C' Mirerani kwa hisa za asilimia 50 na 50, nyingine inamilikiwa na *STAMICO*. Kampuni hii katika kujishughulisha na uchimbaji wa madini aina ya *Tanzanite* imekuwa ikitoa huduma mbalimbali kwa jamii inayowazunguka ili kuboresha mahusiano na jamii. Huduma hizo ni maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na mifugo, mafunzo kwa wachimbaji wadogo kupitia mradi wa *Small Miners Association Project (SMAP),* elimu, ujenzi wa Kituo cha Polisi, Ujenzi wa Ofisi ya Kata ya Nasinyai, ukarabati wa shule na usambazaji wa vitanda na ujenzi wa barabara yenye urefu kwa Kilomita moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na kutoa huduma hizo kwa jamii, Kampuni hiyo inazo changamoto ambazo ni pamoja na uchimbaji haramu katika eneo la Kitalu 'C' *(Block C),* uharibifu wa mali yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni tano uliofanywa na wachimbaji wadogo mwaka 2012 na upotevu wa *Tanzanite* wakia milioni tatu kutokana na uchimbaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembembelea migodi ya wachimbaji wadogo ya Buziba na Lwamgasa (Geita) na ule wa Marema Mirerani (Arusha). Kamati ilibaini kuwa katika maeneo yote hayo wachimbaji wadogo wanaendesha shughuli zao kwa kutumia zana duni; hawana mitaji ya kutosha na wanaharibu mazingira kwa kukata miti na matumizi ya kemikali (zebaki na *cynide*).

Pia Kamati ilielezwa juu ya utaratibu wa ukodishaji wa migodi kati ya wenye leseni na wachimbaji, mfumo unaowanyonya wachimbaji wadogo, kwani hulazimika kulipa asilimia 40 ya dhahabu wanayopata kwa mwenye leseni. Utaratibu huu ni wa kinyonyaji kwani mwenye leseni hupata

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



hiyo asilimia 40 bila kuingia gharama zozote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kuzungumza na wachimbaji wadogo wa Marema Mirerani ambao walikumbushia ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2010 kuwa pindi Mkataba wa *Tanzanite One* unapokwisha eneo hilo watapewa wachimbaji wadogo. Pia walizungumzia Kitalu A *(Kilimanjaro Mine)* kutofanya shughuli za uchimbaji wakati wananchi hawana sehemu za kuchimba. Waliiomba Kamati inaishauri Serikali kufuta umiliki wa sasa ili wapatiwe wao. Hii inalenga kuongeza hali ya usalama eneo hilo na kupunguza hali ya kutobozana kati ya *Tanzanite One Mining Ltd* na wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutembelea migodi na kuzungumza na wamiliki, wananchi pamoja na wachimbaji wadogo, yapo mambo mengi ambayo Kamati iliyaona na kuyasikia ambapo tulitoa ushauri kwa yale ambayo yangeweza kutekelezwa huko huko kwa wakati huo bila kusubiri Serikali. Kamati ilisisitiza mahusiano mazuri kati ya wananchi na wamiliki wa migodi hasa wanaozunguka migodi ili kuepusha vurugu na purukushani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hayo, Kamati ilishauri yafuatayo:-

(i) Migodi ijitahidi kuboresha mahusiano na wachimbaji wadogo na jamii inayozunguka hasa ikizingatiwa kuwa waliachia maeneo yao kwa ajili ya kupisha uwekezaji mkubwa.

(ii) Migodi ihakikishe huduma za jamii inazotoa zinawiana na faida wanayopata kutokana na shughuli za uchimbaji. Aidha, wananchi washirikishwe kuchagua aina ya huduma ambayo wanaona ni muhimu kwao. Wasipelekewe tu! Migodi ihakikishe inasimamia vyema utunzaji wa mazingira kwani uchimbaji unaofanyika unaathiri sana mazingira.

(iii) Kutokana na migodi mingi kuonekana

kutotumia umeme wa gridi kwa sababu ya umeme huo kutokuwa wa uhakika, Kamati inashauri wenye migodi wakae na *TANESCO* na Wizara ya Nishati ili kuona jinsi ya kuboresha hali ya umeme huo kwani kwa kufanya hivyo itapunguza gharama za uzalishaji.

(iv) Migodi iboreshe mahusiano na Halmashauri kwa kuwa mdhamini *(Gurantor)* kupitia *Service Levy*. Hali hii itasadia Halmashauri kukopa na kuendeleza miradi ya jamii badala ya kusubiri wawekezaji peke yao wasaidie huduma hizo.

(v) Kamati imebaini kuwa, baadhi ya Migodi inalipa *Service Levy* nje ya maeneo ilipo kwa kudai kuwa ndiko Makao Makuu ya Makampuni yalipo. Kamati inayataka Makampuni yote kulipa kodi eneo migodi ilipo.

(vi) Kamati inawashauri wamiliki wa migodi wahakikishe wanawaajiri Watanzania na hasa waliopo kwenye maeneo ya migodi kwa kazi ambazo hazihitaji utaalamu ili kuboresha mahusiano.

(vii) Pamoja na uwepo wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura Na. 290, kifungu cha 7(1)(z) inayotaka mtu yeyote anayetoa huduma kulipa *Service Levy* ya 0.3%, Halmashauri zitunge sheria ndogo ili kutekeleza hili. (Kujirisha kwa Sheria kama iko sahihi).

(viii) Serikali isaidie kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo ili waweze kuwa na mitaji ya kununua vifaa bora pia ihakikishe inatenga maeneo ya kutosha kwa ajili ya wachimbaji wadogo ili kupunguza malalamiko yaliyopo.

(ix) Kwa kuwa wachimbaji wadogo wengi wamekuwa wakitumia kemikali ya zebaki na *cyanide* bila hofu, Serikali isaidie kutoa elimu na kudhibiti matumizi yake kwani ni kemikali hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati baada ya kupitia taarifa ya Wizara na Taasisi zilizopo chini yake, na kwa faida

na uzoefu wa ziara, Mikutano tuliyohudhuria kuhusu Sekta hii, yafuatayo ni maoni na ushauri wa Kamati kwa ujumla:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Serikali imewekeza nguvu na rasilimali nyingi katika kujenga miundombinu katika Sekta ya Nishati. Ni ushauri wa Kamati kuwa pamoja na jitihada za ujenzi mipango iandaliwe ili kuweka ulinzi wa miundombinu hii ikiongozwa na intelijensia ya kisasa na inayokwenda na wakati. Pamoja na bomba la gesi asilia ushauri huu uhusishe mtandao wa mabomba na matenki ya mafuta yaliyoko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, pamoja na majukumu mazito na yenye manufaa kwa Taifa letu iliyokabidhiwa Wizara hii, kuna tatizo la upatikanaji wa vibali vya kuajiri wafanyakazi katika sekta hizi nyeti. Kamati inashauri Idara ya Serikali inayohusika na utoaji wa vibali vya ajira itambue umuhimu wa sekta hii na kutoa vibali kwa wakati. Ni busara kwa manufaa ya Taifa letu wafanyakazi Watanzania wanaopashwa kujifunza uendeshaji wa shughuli za kusafisha na kusafirisha gesi asilia wakaajiriwa sasa. Taasisi kama *TMAA, TPDC, TANSORT, STAMICO* ambazo zimeomba kuajiri kwa manufaa yaliyo wazi nao waruhusiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za kujenga bomba la gesi kwa kasi, Kamati inashauri Serikali ijiandae kwa changamoto za kuendesha shughuli za usafirishaji wa nishati na hasa uanzishwaji wa Kampuni itayohusika na menejimenti ya bomba hilo. Sambamba na Kampuni ya Uendeshaji wa Bomba, Kamati inashauri kwa mara nyingine tena umuhimu wa *GASCO* kupata uhai upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali juu ya mafuta ya kulainishia mitambo *(lubricants& greases).* Mafuta haya yamenyoshewa kidole kuwa yanatumika kukwepa ushuru na kodi lakini pia ni kuwa soko la Tanzania limegeuzwa jalala la mafuta yaliyopitwa na wakati au yasiyokuwa na ubora unaotakiwa. Kamati inaishauri Serikali na kufuatilia suala hili kwa manufaa mapana ya Taifa hili. *(Makofi)*

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Sheria ya Madini kwa wale au yale Makampuni yaliyohodhi maeneo ya uchimbaji madini kwa muda mrefu bila kuyaendeleza kwa faida ya Watanzania maeneo hayo yatwaliwe na Serikali ili yagawiwe kwa Watanzania wengine wenye nia na uwezo wa kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa kuweka kifungu cha Bima kwenye Sheria ya Gesi Asilia cha kuyajumuisha Makampuni ya Bima yaliyopo hapa nchini ili kutimiza dhana ya ushiriki wa Watanzania katika suala la gesi. *TPDC* ishirikishe Mamlaka ya Bima *(TIRA)* katika suala zima la utaalamu wa mambo ya Bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ianze kuendeleza miradi ya jotoardhi katika kufua umeme nchini, kwani nchi ina rasilimali kubwa sana ya jotoardhi katika ukanda wa bonde la ufa. Kamati inashauri Serikali imiliki maeneo yote yenye jotoardhi na siyo kumilikisha mawakala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa Serikali iliuza mlima Kabulo kwenye mradi wa Kiwira kinyemela. Kamati inashauri mlima huo urejeshwe haraka *STAMICO* ili nao uanze kuzalisha umeme bila matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ili kuweza kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Aidha, nakupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru Mawaziri wafuatao Mheshimiwa Prof. Sospeter M. Muhongo - Waziri wa Nishati na Madini na Manaibu wake; Mheshimiwa George Simbachawene, na Mheshimiwa Stephen J. Maselle, kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kazi ya Kamati.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini Ndugu Eliakim Maswi, Naibu Katibu Mkuu Eng. Ngosi Mwihava na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kuwa tayari kutoa ushirikiano pale ulipohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Makamu Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, (namtakia Mungu amrejeshe haraka kwani yuko kwenye matibabu nje ya nchi) kwa ushirikinao anaonipa. Aidha, naomba kuwashukuru kwa dhati na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati kwa uvumilivu, busara na ushirikiano mzuri wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuipongeza Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge ndugu Thomas D. Kashililah kwa ushirikiano anaoipa Kamati. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndugu Evelyne R. Shibandiko na Ndugu Stanslaus W. Kagisa kwa kuihudumia Kamati vizuri kwa kipindi chote na kuratibu ukamilishaji wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kuyakubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza kuchangia, Mheshimiwa Anne Kilango ajiandae Mheshimiwa Kessy, Mheshimiwa Msabaha na Mheshimiwa Jafo.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kunifanya mchangiaji wa mwanzo na ningeomba nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wote wanne. Kuna Waziri wa Nishati na Madini

*[MHE. ANNE K. MALECELA]*

nampongeza kwa kazi nzuri ; Waziri wa Ujenzi, Waziri wa Uchukuzi na Waziri wa Mawasiliano Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba ku-*declare interest* mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati ya Madini. Naomba nizungumzie suala la moja tu kwa dakika zangu zote kumi. Suala la vilainisho vya mitambo *(lubricants)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tulikaliona kama hili ni suala dogo lakini hili suala ni kubwa kuliko ambavyo watu wengine wanaliangalia. Watu wengi wamezoea kuita *lubricants*. Vilainishi vya mitambo ndiyo vinavyodumisha uhai wa mitambo, vinadumisha magari yetu wote hapa nchini.

Tatizo linalojitokeza ni kwamba kumekuwa na wimbi kubwa sana la kuingiza vilainishi ambavyo havina viwango vinavyostahili *(fake lubricants).* Hizi *fake lubricants* zipo sana kwenye nchi yetu na watu wengi wanunua wakidhania ni zile *genuine*. Hazina tofauti wakati mwingine ukiziona kwa haraka haraka, tofauti ni kwenye bei. Bei za *genuine lubricants* ambazo zinatoka kama ni *Oryx*, *TOTAL, PUMA* na kadhalika zenyewe zinakuwa na bei tofauti na zile za *fake*. Unaweza kuona kama zinafanana. Hizi za *fake*, bei yake iko chini. Sasa Watanzania kwakuwa na haraka, kwa kutokuwa makini labda na kwa kupenda kununua vitu vya bei nafuu, tunakimbilia kununua *fake lubricants*. Kwasababu nipo kwenye Kamati ya Nishati ya Madini, tunamekaa na wanaohusika na vilainisho vya mitambo, tumelichambua hili kwa undani, nikaona nilizungumze hapa ndani kwa faida ya nchi yetu wenyewe na Watazania pia. Kwamba unapoviona hivi vitu unaweza usigundue. Tofauti inakuja kwenye bei. Zile *genuine lubricant* zenyewe zinakuwa na bei ya chini.

Sasa kwa kununua fake *lubricants* kwa kufuata bei ya chini hasara ni kubwa sana. Kwanza, hii ni *slow poison* kwenye magari yetu. Tunapoanza kutumia *grease* na *engine oil* hizi ambazo ni feki moja kwa moja tunahatarisha maisha ya magari yetu bila sisi wenyewe kujijua. Kina wakati utaona mtu anakwenda kupeleka gari yake kwa ajili ya *maintanance. Maintanance cost* zinakuwa ziko juu *as a result* maisha ya magari yetu yanakuwa mafupi. Lakini ni kwa

sababu ya kununua vilainisho vya mitambo ambavyo havina viwango. Hili tatizo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *fake lubricants* ni adui mkubwa wa uchumi wa nchi. *How*? Inakuwaje? Ni kwamba kwa sisi kununua vipuri kila wakati, tunatumia fedha ya kigeni kununua vipuri kwa sababu magari yanahitaji vipuri kila wakati. Kwa sababu magari yakuwa mabovu, uhai wake inakuwa mashakani, pesa ya kigeni nyingi inanunua vipuri kwa ajili ya matatizo ya kutumia vilainisho vya mitambo visivyo na viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna haya Makumpuni makubwa *Oryx*, *TOTAL, PUMA* ambayo yanauza *genuine lubricants* zao. Wao wanalinda majina yao. Sasa wao wana-*compete* na watu wanaouza *lubricants* ambazo hazina viwango. Watu kwa kutokujua wanakimbilia kule. Inakatisha tamaa sana haya Makumpuni ambayo yanauza *genuine lubricants,* kwa hiyo, unakuta Makampuni mengine kidogo kidogo yanaweza yakaondoka kwenye nchi ya Tanzania yakaenda kwenye nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina point nyingine zaidi ya hiyo ya *fake lubricants*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata taabu sana kwamba Serikali iko wapi ? Inamwachiaje *TBS* aendelee kuruhusu nchi hii iwe ni soko la vilainishi vya mitambo ambavyo havina viwango? Hapa ningependa Serikali leo itoe tamko, hebu imshike *TBS* vizuri, atuambie kwanini Tanzania inakuwa soko kubwa la *fake lubricants*? Hapana, hatutaki hiki kitu kiendelee. Watanzania ni vyema wakajua kwamba ni vyema wanunue *genuine lubricants* hata kama ni za bei ya juu kidogo, lakini wanalinda mitambo yao na magari yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado narudi kwenye Serikali yangu, hivi inakuaje *TBS* anaachia hizi bidhaa ambazo ni hatari kwa uchumi wetu, kwa mitambo yetu na magari yetu vinaingia katika nchi na kutuweka katika hali mbaya ?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naunga

mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Keissy atafuata Mheshimiwa Msabaha na Mheshimiwa Jafo ajiandae.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa fursa na mimi nichangie kidogo kuhusu hii Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Wizara ya Nishati na Madini. Kusema kweli wananchi wa Nkasi mpaka sasa vijiji kumi vimepata umeme. Tangu uhuru tulikuwa gizani, hatujui umeme ni kitu gani. Sisi tulikuwa na gharama sana. Gharama ya mawe ya tochi tu kwenye redio ni zaidi ya umeme. Mawe ya tochi tu ukifungua redio yako; watu wa kwetu kule wanapenda sana muziki; ukitumia mabetri kununua kwa siku moja ni sawa ya bili ya umeme ya mwezi mzima. Kwa hiyo, naiomba Serikali iendelee kuipa *REA* fedha ili wananchi wote tupate umeme. *(Makofi)*

Naomba Dkt. Lutongano ile Mikoa na vile vijiji ambavyo alituahidi atatupatia Wakandarasi, tuondoke na majina ya wakandarasi. Tupatiwe majina majina ya wakandarasi twende nayo. Vile vile Serikali iwape *REA* fedha za kutosha isiwe ni maneno tu. Maendeleo hayaji bila pesa. Watu wanaendelea kusema Mawaziri mizigo, Mawaziri mizigo; ndugu yangu atatoa hela za mfukoni kwake? Serikali iwape pesa waone zile pesa kama hazifanyi kazi ndiyo utamwambia fulani mzigo. Siyo mzigo mtu. Kama ana pesa, hawezi kuwa mzigo! Pesa ndiyo inafanya kazi. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iwape *REA* pesa ili vijiji vyote vilivyoorodheshwa vipate umeme jinsi tulivyoahidiwa hapa na Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Jambo linguine, *TANESCO* ni aibu kuendelea kuagiza nguzo Afrika Kusini. Tuna misitu yetu ya kutosha. Tunapoteza pesa za kigeni kwa ajili ya nguzo. Ni aibu! Ndio maana Dola inapanda bei kila siku, kwani tunaagiza kila kitu. Nywele tunaagiza, kucha tunaagiza, mpaka nguzo tunaagiza!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Itakosaje hela yetu kutokuwa na thamani? *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, naomba *TANESCO* wajidhatiti kule *Sao Hill* Iringa kupanda miti katika mashamba ili tupate nguzo hapa hapa nchini kwetu, tuokoe pesa zetu za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu reli. Ndugu zangu reli ni uti wa mgongo. Bila reli hamna maendeleo, tusidanganyane. Reli ya Kati ndiyo uti wa mgongo. Nenda leo Kigoma; Kigoma zamani ilikuwa inahudumia Burundi mpaka Zambia kwa mizigo. Leo Kigoma imekufa. Reli hamna! Ukisafiri ndani ya treni leo unafukuzana na panya. Sasa ni hatari!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza hapa mara ya kwanza, kwamba tunakimbilia viwanja vya ndege, lakini wananchi wetu hawana uwezo wa kupanda ndege. Leo mwananchi wa Kigoma muuza migebuga na mawese anaweza kupanda ndege? Mwananchi wa Shinyanga, Mwanza na Tabora ana uwezo wa kupanda ndege? Tufufue reli ya Kati na ya Mpanda kule. Mahindi yanaoza pale Mpanda kwa sababu hakuna reli. Tunapata hasara! Kwa hiyo, tufufue reli ndiyo iwe kipaumbele, ndiyo mambo yetu yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Tunduma ukifika ni aibu tupu! Msongamano wa magari Tunduma hamna nchi hii! Nimezungumza mara nyingi kuhusu Tunduma. Sisi tunatoka Sumbawanga nimezungumza mara nyingi kuhusu Tunduma, siye tunatoka Sumbawanga na mabasi pale hatupiti masaa matatu, masaa manne, magari hayaendi, yame-*jam*.

Mnasema msongamano uko Dar es Salaam? Siyo Kweli! Kaone msongamano wa malori Tunduma pale. Utakimbia! Tunapoteza hela hivi hivi kienyeji. Ni bandari ya nchi kavu Tunduma, lakini magari hayaendi. Mheshimiwa Silinde shahidi! Magari hayaendi! Waziri Mwakyembe alikwenda akasema hapo watafanya kazi masaa 24, waambiwe wafanyakazi masaa 48, na wapanue njia za kutolea magari, badala ya njia moja, hata waweke njia sita,

magari hayawezi kwisha pale Tunduma. Tunapoteza hela zetu bure! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa maziwa yetu. Ziwa Tanganyika, hakuna barabara; tunategemea meli. Tumeahidiwa meli, wanasema meli inatengenezwa Korea, sijui Korea Kaskazini au Kusini. Naishukuru sana Wizara ya Uchukizi, inajenga bandari katika Ziwa Tanganyika. Sasa baadaye itafanya kazi gani kama hatuna meli?

Nimeomba ile meli ya *MV Liyemba* iongezewe *trip* za kupita Ziwa Tanganyika. Wananchi wanapata taabu, wanakufa kwenye mitumbwi! Nimemwambia Mheshimiwa Waziri anasema hamna mapato. Siyo hamna mapato; nimemwambia siku moja avae kanga, akanicheka. Wafanyakazi ndiyo wamekuwa meli yao. Wanachukua pesa, mtu anatokea Kipili anaandikiwa kijiji cha mwisho cha kuteremka. Hamna kitu! Treni ni hivyo hivyo! Wanapanda treni Dar es Salaam, anaandikiwa kwenda Kigoma, akifika Kasulamemba anateremka, hela zote anachukua *TT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya mambo ni ya kufanyia kazi. Wananchi wanasafiri kwenda na kurudi, mnapataje hasara? Mizigo kwenda na kurudi unapataje hasara? Haiwezekani! Naomba Mheshimiwa Waziri aangalie hili jambo. Hili jambo walifuatilie kwa karibu. Watumishi wa Shirika la Reli, wameua wenyewe lile Shirika. Nilizungumza mapema sana; ni kama Shirika la Bima walivyoua, Shirika la Ndege walivyoua, ni hivi hivi. Nenda leo Kenya, ndege pale zimejazana hata hesabu hakuna. Hamna hesabu kwenye ndege za Kenya na tulikuwa pamoja. Sisi hata ndege moja hakuna. Nashangaa wanasema ile ndege inakwenda Burundi! Ukiiona hata abiria wa Burundi watakataa kupanda. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio sahihi kupeleka ndege Burundi ile! Ihudumie humu humu, ni aibu ile ndege kupelekwa Burundi. Ndege ya kizamani, imechoka! Walioingia mikataba wameachwa wanakula starehe. Nchi hii mzee ni ya kula kwa raha yake.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Umeme nimeshazungumzia sana. Nalishukuru Shirika la Umeme. Kusema kweli Shirika la *TANESCO* tuombe Mungu hii gesi, maana yake mpaka sasa tunapata hasara kubwa sana. Serikali inafidia; tunanunua umeme kwa haya Makampuni senti 35 mpaka senti 40. Sisi tunauziwa umeme senti 11 bado tunapiga kelele. Wananchi wanapiga kelele! Mheshimiwa Waziri anafanya kwa ajili ya gesi, hao wanaochimba gesi waingie mikataba na *TPDC,* lakini kuna baadhi ya watu wanasema haiwezekani.

Ndugu zangu gharama za kuchimba gesi, siyo mchezo. Benki gani itakukopesha? Aende benki, aje na hela! Mheshimiwa Waziri anasema wazi kabisa. Lakini katika vyombo vya habari kumsema kwamba hafai, sijui amekuwa ni mzigo, nani atakubali tukupe kisima wewe binafsi na familia yako wananchi wote tuteseke, wananchi wa Namanyere hawana kisima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mali ya gesi nilizungumza tangu mwanzo ni gesi ya nchi nzima. Gesi yako labda ya tumboni ile ya kwenda hospitali ndiyo ya kwako. Lakini gesi ya Mtwara, mafuta yakigunduliwa *Lake Tanganyika* ni yetu sote na *TPDC* ndiyo ishughulike, sio mtu binafsi. Mtu binafsi njoo na pesa, usiwe dalali, hatutaki udalali hapa!

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Keissy, kengele ya pili imeshalia.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Udalali hakuna nchi hii Mheshimiwa! *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Msabaha na Mheshimiwa Jafo ajiandae.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kupata fursa hii ya kuchangia Kamati hii. Kabla ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Mwenyekiti wetu na Makamu wake na Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwa uchungu mkubwa sana, sitampongeza Waziri yeyote wa Uchukuzi, siyo wa barabara, sio wa Bandari wala wa kitu gani. Kwanza Mawaziri hawa wameshiba sifa; na katika Mawaziri vibomu na hao ni vibomu. Wasiseme wenzao ni vibomu, nao vibomu. Kama Mawaziri hamsikilizi maoni ya Kamati pia na nyie ni vibomu. Waswahili wanasema hivi, "Ukimsifia mgema tembo, hulitia maji." Hatuwezi kufanya kazi kama Waziri anafanya kazi na Waandishi wa Habari na kupamba magazeti, halafu tuseme anafanya kazi. Watanzania wanataka wasikie bandari inafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari ni moyo wa Tanzania. Watanzania wanataka wasikie reli zinafanya kazi. Leo hii barabara zinatengenezwa siku mbili zimeshavimba. Tumekwenda kwa wenzetu; hawa ni wabinafsi! Sisi tunawaambia kila siku, jamani Wajumbe tunatakiwa hivi, hizi Wizara ambazo tunasimamia ni nyeti. Lakini sasa kila tukiwafahamisha hawati kuelewa. Lakini nimesema kwa makusudi kabisa, Mheshimiwa Mwakyembe namheshimu na nitazidi kumheshimu, lakini kwa hili sitamheshimu. Hatutaki kufanya kazi kwa magazeti. Tufanye kazi tuone Watanzania wanafanya nini.

Leo hii tunaomba gati, tunaambiwa tuko kwenye mchakato, tuko kwenye upembuzi, sijui tuko kwenye kitu gani, hazijengeki. Huwezi kununua kiwanja leo ukasema nyumba hujamaliza, unaenda tena kununua kiwanja kingine. Hujamaliza, kuhamia nyumba, unasema leo unaenda kujenga pahali pengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku unasikia sijui gati ya

*[MHE. MARYAM S. MSABAHA]*
wapi, sijui gati ya Mwambani! Mpaka leo nasema huyu, hata sijui kama Mheshimiwa Rais wanamsikiliza! Hawa Mawaziri wengine ndio wanachangia hata Mheshimiwa Rais wetu aonekane ni mbaya katika Afrika Mashariki. Mengine nayaacha ni ya siri sitaki kuyaweka hewani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunaangalia Kenya, Uganda na Rwanda wanajitenga; sasa sisi Tanzania wanaona hatufanyi. Kila siku tuko kwenye mchakato, tuko kwenye upembuzi yakinifu, huku kuna maslahi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie watu wanaokuja na vitabu hapa; kuna siku mimi niliwahi kusema Bungeni, hawa wataalam hawa wanajitia wamesoma, wanaiba kwa kalamu. Tupitie kwa kina mtakuta kuna mambo mengi sana yanayofanyika huko Bandarini. Mimi nasema kwa uchungu; kama mtanichukia, mtanichukia, nitabaki kuwa Msabaha tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie leo nchi za Afrika Mashariki zina ndege mpaka nyingine hazina pahala pa kwenda. Tukiangalia sisi tuna ndege moja na hii ndege moja tuliyonayo iko *mortuary*, inavuja na Watanzania msipande ndege ile msihatarishe maisha yenu, haiko katika usalama. Tumo tunajenga viwanja vya ndege mara kiwanja hiki, mara kiwanja hiki; hizo ndege ziko wapi? Shughulikieni reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ndiyo mkombozi wa Mtanzania, reli ndiyo chanzo kizima cha mapato ya Tanzania. Leo reli zetu Nyerere kama angefufuka huko aliko akaja akatazama reli, tungeenda wapi sisi? Ukienda kwenye bandari huko, wanakaimu; huyu kakaimu, yule kakaimu, huyu kakaimu. Ni Wizara gani ambayo inaendeshwa kwa mambo ya kukaimu? Huyu kakaimu, yule kakaimu, unategemea nini? Mambo ya kulindana hayapo! Tufanye kazi, tuangalie Tanzania yetu tunaifanyia nini. Tusimpe Mheshimiwa Rais wakati mgumu. Msiseme Mawaziri wengine vibomu, kuna wengine ni vibomu vya *petrol* vinangoja kulipuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje kwenye barabara. Tunasikia Dar es Salaam. Dar es Salaam leo kuna watu

*[MHE. MARYAM S. MSABAHA]*

wanashindwa kwenda kazini. Wengine mashimo tu wameachiwa, vituo vile sijui vya mwendo kasi vipo hapa, vipa hapa, yaani vimejengwa tu karibu karibu. Wangetuachia zile barabara zetu za Mheshimiwa Rais wetu wa Kwanza alizozijenga, alizijenga katika *standard* nzuri sana. Tuache siasa, tufanye kazi! Wizara hii ndiyo Wizara nyeti, ndiyo uhai wa kila Mtanzania. Hizo gati namba 13 namba 14 zitajengwa lini? Leo sijui tuende Bagamoyo, leo sijui twende Mwambani Tanga, hakuna kitu chochote kinachofanyika. Mambo ya siasa tu! Tunapiga siasa katika mambo nyeti kama haya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie, kama utamfukuza huyu utamleta huyu, mambo hayaendi; umefukuza watu wangapi? Mbona mambo hayajaenda mpaka leo? Mimi nimekwambia utabaki kunichukia, lakini leo nasema ukweli, tena nina hasira kweli kweli, mengine tu nayavumilia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo unapokuwa ni Waziri, Waziri ni Mbunge, na Waziri ni Mjumbe wa Kamati. Hawahudhurii Kamati, wananata, kusalimia kwenyewe kwa matatizo, wanatuona kama sisi ni maboya kama hatujaenda shule. Tumesoma! Kwa nini hamhudhurii kwenye Kamati? Kwa nini tukiwapa ushauri hamchukui? Mtamwona Mheshimiwa Serukamba sijui anafanya siasa, sijui anafanya kampeni za Urais; siyo mambo ya Urais, naye anachoka! *(Kicheko)*

Tena nimshukuru Mheshimiwa Spika kwa kutupeleka Malaysia, tumekwenda kwa pesa ya Ofisi ya Bunge, sisi Kamati hatujatoroka, tumekwenda tumeona mambo mengi sana kule. Tumejifunza mambo mengi tena mazuri na mengine myafanyie kazi kabla hatujaanza kuja kuyasema humu Bungeni. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalieni Wizara hii kwa makini sana, muipitie ndani kwa ndani, muichunguze ndani kwa ndani, mtabaini madudu makubwa sana kwenye Wizara hii. Msiwapambe watu sifa. Watanzania wanataka wapite kwenye reli zao, wanataka mapato yatokane na Bandari,

*[MHE. MARYAM S. MSABAHA]*
wanataka wakienda kwenye viwanja vya ndege wakute ndege. Siyo ndege ambazo ziko *mortuary* zinavuja, mseme ni Waziri bora. Waziri bora kwa kufanya kazi na magazeti! Waziri bora kwa kutokusikiliza Wajumbe wa Kamati!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe tunatakiwa tujifunze kwenye Wizara. Mimi ni Mjumbe mpya nimekwenda, tena najuta! Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Makongoro Mahanga kwa kusafiri na Wajumbe wake kwenda Malaysia. Ni Naibu Waziri gani wetu, Mawaziri hawa wanaonata? Ni nani aliyepanda ndege akaenda na Wajumbe wake hapa? Lakini Mheshimiwa Mahanga amekwenda na Wajumbe wake wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Lakini nyie mko *busy* na mambo yenu. Huo ubize utakwisha! *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, ahsante. *(Makofi)*

Sasa namwita Mheshimiwa Jafo Mheshimiwa Natse ajiandae, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Nkya.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ni kwamba ukiona hivyo Bunge kila mtu ana *stress* zake, lazima tuwekane vizuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia mchana huu wetu wa leo katika Kamati hizi nyeti. Kwanza, nawapongeza Wenyeviti wote wa Miundombinu na Kamati ya Nishati na Madini kwa kazi kubwa waliyoifanya. Lakini kwa ujumla nawapongeza Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa sababu kwa mujibu wa taarifa zao walizoziwasilisha hapa ni wazi kwamba wamefanya kazi kubwa ya kutosha kwa ajili ya kuhakikisha wanaishauri Serikali na kulisaidia Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekti, kwanza napenda kuishukuru Wizara ya Nishati na Madini kwa kazi kubwa waliyoifanya kule Jimboni kwangu katika suala zima la uwekezaji wa nishati ya

umeme. Kwa kweli nashukuru sana. Watu wanasema usipomshukuru binadamu mwenzio, basi hata Mwenyezi Mungu huwezi kumshukuru. Kwa hiyo, ndugu zangu wa Nishati na Madini napenda kuwashukuru sana kwa kazi kubwa mliyoifanya, naomba sana mwendelee kuhakikisha vijiji vyote Wilaya ya Kisarawe imepata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa zilizokuja hapa, naomba kuchangia katika suala zima la ujenzi wa miundombinu ya reli. Kwa kweli napenda kuishukuru sana Kamati, imetueleza wazi kwamba tuna changamoto kubwa sana katika reli zetu hizi mbili. Lakini nikianza katika reli ya Kati, ni wazi sasa hivi ukipita katika barabara zetu, zimeharibika sana. Wote ni mashahidi, kama unakuja Dodoma, ukianzia kutoka Morogoro kuja Dodoma hali ni mbaya zaidi. Ukitoka maeneo ya Mlandizi mpaka maeneo ya Chalinze pale katikati hali ni mbaya zaidi. Barabara zimeharibika sana na hizi barabara zimeharibika kwa sababu ya malori mazito yanayopita katika barabara zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najua wazi kwamba barabara zile zimejengwa na pesa ya Tanzania na barabara hizi zinapoharibika, maana yake lazima zirekebishwe. Ina maana muda wote kazi yetu inakuwa ni kurekebisha barabara. Kwa hiyo, naomba sana Wizara inayohusika na suala zima la *TANROAD* ione ni jinsi gani tutaweza kusimamia vizuri barabara. Napenda kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Magufuli kipindi kile alichosema kwamba lazima malori yapite kwa uzito wake unaostahili. *(Makofi)*

Ndugu zangu tusije tukabembelezana katika mambo ya kuhakikisha kwamba tunasimamia uchumi wa Taifa letu hili. Barabara zikiharibika ni kwamba tutashindwa kujenga barabara zile mpya ambazo zinatakiwa zijengwe. Kwa hiyo, kila siku tutakuwa tunarekebisha barabara zile zile za zamani. Kwa hiyo, katika hili kulifanikisha vizuri ni lazima tuhakikishe reli yetu tunaiboresha vizuri zaidi. Kwa hili napenda kuwashauri Mawaziri wanaohusika na wenye dhamana katika suala la miundombinu ya reli. Watu wamechoka historia hizi za kila kila siku za upembuzi yakinifu. Watu wanataka kuona reli

inajengwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi tumeona wenzetu kule Kenya ile reli sasa wameshaianza kwa kasi ya kutosha. Tusipofanya hivyo ni kwamba tunakwenda kuathiri uchumi kwa kiwango kikubwa. Najua kuna kazi kubwa inafanyika, lakini naomba tuongeze *speed* ya utekelezaji wa ujenzi wa reli hizi. Tutakapojenga tutasaidia uchumi wetu kwenda kwa kasi zaidi kama tunavyokusudia.

Vile vile napenda kushauri sana katika suala zima lililozungumzwa hapa na Kamati katika ujenzi wa geti namba 13 na 14. Tanzania tuna bahati kubwa ya kijiografia ya kiuchumi. Bandari yetu na suala zima kuwepo kwa bahari, tuna fursa kubwa sana kuifungua nchi yetu kwa ajili ya kuhakikisha tunapata uchumi imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshauri sana Mheshimiwa Waziri katika Wizara yake aweze kuhakikisha kwamba tunabadilisha Tanzania yetu kuhakikisha kwamba geti namba 13 na 14 iwe historia. Kwa sababu nakumbuka toka alipokuwa Mheshimiwa Mzee Nundu hapa tulikuwa tunapata habari hizi. Nilitarajia sana sasa hivi tungekuwa tunazungumza lugha nyingine tofauti. Juzi juzi nilikwenda pale Mtwara, niliona ile bandari ya Mtwara, lakini ndugu zangu lazima tuhakikishe tunawekeza vya kutosha katika hizi bandari kwa uchumi wa Tanzania. Tunaweza tukabidilisha uchumi wetu kwa kutumia bandari zetu hizi. Nami naamini kwamba kama Serikali ikijipanga vizuri tufanye maamuzi magumu katika hili, tutahakikisha watu Burundi na *Congo* bidhaa zao zote zinapita katika bandari zetu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipofanya haya maamuzi magumu, maana yake tunaenda kuathiri uchumi wa nchi yetu. Tumezungumza hapa na Waziri wa Fedha, juzi juzi alikuwa anazungumza suala zima la bajeti kwamba bajeti haitoshi, ni kwamba makusanyo yetu hayaendani na matumizi yetu. Nami nina imani kwamba kama tukijipanga vizuri katika kuhakikisha tunatengeneza bandari nzuri, tunavutia, mizigo mingi inapita, reli zetu zinaimarika, nina imani

[MHE. SELEMANI S. JAFO]
uchumi wa nchi utabadilika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri katika hili liwe ni sehemu yake ya kipaumbele. Watanzania katika hii *Big Result Now* tunatarajia katika bajeti inayokuja tuone tumefanya maamuzi magumu kuibadilisha nchi. Tukiacha historia zile zile, Watanzania sisi wengine tunaumia, tumechoka! Nami nakuamini sana Mheshimiwa Waziri Mwakyembe. Naamini kwa *speed* yako, ukiongeza na juhudi tutaweza kufanya mabadiliko makubwa sana. Lakini mabadiliko hayo lazima tuweke mipango yenye kuashiria vipaumbele kwamba Taifa tunaweza kulibadilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tupate Mawaziri kama mlivyo ili tukifika mwaka 2015 Tanzania yetu tuone imebadilika. Lakini hatutaweza kubadilika kwa kutumia maneno. Naomba Mawaziri muwe wakali; kama kuna watu wanawakwamisha muwe wakali. Hatutarajii kila siku mnazungumza historia hizo hizo. Maana yake sisi Wazaramo ndiyo maana siku zote tunasema *"zilongwa mbali, zitendwa mbali."* Mnachotuambia hapa katika makaratasi, tuone kinatekelezeka kivitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiifungua Bandari ya Mtwara, tukiweka geti namba 13 na 14 kama ile bandari ya Tanga ikiimarika, naamini Tanzania itakuwa ni nchi ambayo hata wenzetu wa Jumuiya mbalimbali wataweza kujifunza kutoka kwetu na wote watatukimbilia. Kwa hiyo, naomba sana ndugu zangu tuweze kuimarisha katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze katika suala zima la Sekta ya Nishati na Madini. Awali nimewapongeza sana, lakini naomba niwaeleze jambo moja. Sasa hivi Tanzania tumepata fursa kubwa sana ya kugundua gesi. Hii gesi tuliyogundua, naomba mjihadhari nayo kuhakikisha kwamba nchi yetu inakwenda mbele zaidi. Bahati mbaya nchi mbalimbali zinaonekana kama zimeingia katika laana kubwa baada ya kundulika kwa rasilimali, na tatizo kubwa ni suala zima la kukosa *transparency.* Kutokuwa na uwazi kunaleta matatizo makubwa sana. bahati nzuri hapa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



naona mchakato wa Sera ya Gesi unakwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka Watanzania twende mahali pazuri ambapo tutakuja kuona tunajivunia sana; nami namwamini sana *Prof.* Muhongo, juzi alikuwa anatoa *presentation* moja nzuri sana pale. Hata watu wa nchi mbalimbali walikuwa wakisema Tanzania mna Profesa kweli wa mambo ya Nishati. Sasa tuweze kujipanga vizuri, kwamba hii gesi sasa iweze kuwanufaisha Watanzania wote kwa undani wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya zaidi, tutakapokwenda kuvuna vizuri rasilimali ya gesi, kama hatutakuwa wazi katika mapato tunayoyapata kama nchi, tutakwenda kuigharimu nchi yetu kwa kiwango kikubwa sana. Kwasababu nchi inapoingia katika mikataba mikubwa na kupata fedha, kama hakutokuwa na uwazi wachache wataweza kujinufaisha katika fedha hizo. Kwa bahati mbaya sana fedha mara nyingi inaziba watu, inawapa upofu. Inawapa watu masikio wasiweze kusikia, kiasi kwamba wako tayari wachache wa kuweza kurubuniwa na suala zima la rushwa, na nchi hapo anaangamia. Nchi ikiangamia, maana yake watu wengi sana wataanza kuathirika na hasira za watu zinaanza kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Watanzania tujifunze kutokana na jinsi gani wenzetu wamepata matatizo. Mara nyingi sana haya Mapampuni yanapokuja na wingi wa fedha, kuna watu wachache wanawezeka kurubunika zaidi wakashindwa kutetea maslahi ya nchi. Nchi inaanza kuangamia mahali pabaya sana. Kwahiyo, nikuomba sana Mheshimiwa Waziri na timu yako kwa ujumla katika Sekta ya Gesi tuweze kukaa vizuri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKI:** Nakushukuru Mheshimiwa Jofo.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimwa Natse, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Nkya na Mheshimwa Mbatia ajiandae.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie katika hotuba hii ya Wenyeviti ya Kamati mbili.

Kwanza naomba kuchangia maeneo machache katika Kamati zote mbili, nikianza na Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Tanzania tutakuwa na dhamira ya kweli katika kufufua uchumi wetu, tunapaswa kuweka kipaumbele katika reli reli, zetu zote. Tuna bahati nzuri, tunao ukanda mrefu wa bahari tangu Mtwara mpaka Tanga. Kwa hiyo, tuna Bandari nyingi, tunahitaji kuzikuza, kuziimarisha Bandari zetu. Watu wamezungumza juu ya Bandari zetu, lakini dhamira ya kweli kwa Serikali yetu, mimi najiuliza na hii naomba Waziri wa Uchukuzi uangalie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini tumeua reli zetu na badala yake tumeagiza Ma-*semi treiler* mengi mno nchi hii yenye kuharibu barabara zetu? Tukaacha reli inakufa, ikabaki ni wimbo tu reli, reli; ukiangalia ndani wahusika wote wanaohusika na uchumi huu wa uchukuzi na nini, watu wamejiwekeza katika malori makubwa yanayoharibu barabara zetu? Kwa hiyo, nahitaji tuwe na uzalendo, tufufue reli zote kwa usafiri nchi hii, tupunguze hizi *semi treilers.* Nani wanamiliki hizi *semi treilers* na nani wanamiliki na nani ambao wanapaswa kuhakikisha kwamba tunaimarisha reli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ngumu kidogo kuona kwamba mimi mwenye *conflict of interest* katika usafirishaji niwe nasimamia usafiri wa reli; sina maana ya Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe; lakini ukiangalia, tunaua reli zetu, tunabaki kwenye maneno tu kila siku! Lakini *semi treilers* zinaingia kwa wingi nchi hii zenye kuharibu barabara. Jambo hili liangaliwe sana! Katika uchukuzi reli ni ukombozi wa nchi hii kwa habari

ya uchukuzi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nilitaka kusema juu ya Nishati na Madini. Naomba Wizara ya Nishati na Madini, wamefanya kazi nzuri kidogo katika Jimbo langu la Karatu. Wananchi wangu wa Karatu wamejitolea kusimamisha nguzo, kusaidia *TANESCO* kufunga nyaya Karatu Endamararie, kazi ile imesimama kwa muda mrefu na Vijiji vingi Mbulumbulu Mang'ola kule, *REA* katika Bajeti ya Wizara inayokuja iongezewe fedha za kutosha ili tuweze kupeleka umeme vijiji. Hii itaepusha sana uharibifu wa mazingira. Kwa hiyo, bajeti iongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye gesi, utajiri mkubwa ambao sasa nchi hii tunao na tunausema sana. Ni kwa jinsi gani Serikali imejiandaa? Maana najua wataalamu walio wengi katika gesi sasa sio wazawa, ni wageni. Tumejiandaa kiasi gani kuelimisha Ma-*engineer* wa Tanzania ambao baada ya muda mfupi watakaochukua gesi nchi nzima, vitalu vyote wataalamu wa Kitanzania?

Naomba Serikali ijiandae kuhakikisha kwamba inaandaa wataalamu wa kutosha Ma-*engineer* kwa ajili ya gesi, na kuwapa wazawa vitalu, ni afya njema. Lakini tumezoea tuki-*hold* vitu kwa muda tukitafuta, tunakaa kama madalali, baada ya muda tuwatafute wengine ndiyo tuwape. Hii hapana. Serikali lazima iwe makini, Watanzania wenye uwezo wamilikishwe vitalu na vitalu hivyo viendelezwe kwa manufaa ya nchi yetu! Siyo vinakaa tu halafu wajanja wachache wanasubiri watu fulani ili wakae kama madalali wayauze baadaye. Hili hapana. Tukitaka maendeleo ya nchi hii, lazima tukubali kuwa wazalendo kwa ajili ya nchi yetu na uaminifu katika kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa habari ya Uchukuzi, wengine wamesema sana kuhusu usafiri wa anga. Tanzania ni nchi kubwa sana. Mheshimiwa Waziri Mwakyembe anajitahidi sana na Viwanja vya Ndege. Hatuna Ndege; sasa ndege sijui *bird* ndio waje watue huko au ndege wapi hao! Nchi ina ndege moja halafu imelala, wamesema

iko *ICU.* Kwa kweli tubadilike! Nchi yetu haiwezi kuwa na ndege moja halafu iko *ICU.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna viwanja vizuri, kwa hiyo, mimi nafikiri suala la usafiri wa anga kupokea ndege nyingine tu, Mataifa mengine yatue huku, sisi kama nchi hatuna ndege, Mheshimiwa Waziri na Serikali, mwangalie kwa upya kabisa, nini kinatufanya Watanzania tushindwe kuwa na usafiri wa anga? Watanzania, Mtume Paulo anasema,"Enyi Wagalatia, ni nani aliyewaloga?" Nami nasema, enyi Watanzania, ni nani aliyewaloga? *(Kicheko/Makofi)*

Serikali hii ya CCM tumepewa rasilimali za kutosha nchi hii, tunazo fedha za kutosha nchi hii, tumeshindwa kupangilia na vipaumbele vyetu, tumeshindwa kuwa waaminifu katika kusimamia rasilimali hizi! Ndugu zangu, Serikali hebu hawa Watanzania tuwahudumie kwa uwezo wetu wote. Waheshimiwa Wabunge, tuna nafasi kama Wabunge ya kuisimamia Serikali. Lakini utaisimamieje Serikali wakati wewe mwenyewe unayeisimamia, hujakaa sawasawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubui imenisikitisha sana yaliosemwa hapa ndani; "*The comedy",* watu wanatuma ujumbe kwamba Bunge ni *Comedy.* Inasikitisha mno, ni aibu kwa Bunge.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mweshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Nkya, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbatia na Mweshimiwa Arfi ajiandae.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mweshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nichangie kwenye Kamati hizi mbili ambazo ni muhimu sana. Kwanza, napenda kuchukua fursa hii niwapongeze sana Wenyeviti wote wa Kamati zote mbili. Vile vile niwapongeze Mawaziri wanaohusika na

*[MHE. DKT. LUCY S. NKYA]*
Miundombinu pamoja na Nishati na Madini kwa kazi nzuri. Naomba niwaambie tu kwamba msikate tamaa. Sisi kama Wabunge, kuzungumza ni wajibu wetu. Tutakapotoa *coments* zozote ni njia moja pia ya kuwafanya muwe na mori zaidi ya kufanya kazi. Poleni sana ndugu zangu. *(Makofi)*

Mweshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nizungumze katika maeneo matatu. Eneo la kwanza ni eneo la Nishati na Madini. Naomba niseme kitu kimoja, kwamba Shirika letu la *TANESCO* kwenye umeme vijijini kuna sehemu ambazo wamejitahidi, wamepeleka nguzo za umeme, ziko zimelala chini, wamechimba mashimo. Mfano mmojawapo, huko Morogoro vijijini, katika eneo la Mikese, kule Kiloka pamoja na Mkuyuni, zile nguzo zipo, zinaoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii kuishukuru Serikali kupitia *MCC,* wametuletea umeme Morogoro vijijini. Lakini ule umeme unapita, na sio watu wengi ambao watapata umeme.

Mimi naomba ule umeme kwasababu umegharimu Serikali? Basi *TANESCO* iangalie namna ya kusambaza ule umeme kwa wananchi wote kwenye vile vijiji vinavyozunguka ile njia ya umeme wa kutoka Kuloka kwenda mpaka Matombo na ninaomba waongezee uende mpaka Mvuha Makao Mkuu ya Morogoro Vijiji. *(Makofi)*

Mweshimiwa Mwenyekiti, la pili kwenye nishati na madini, napongeza sana juhudi ambazo Serikali inafanya baada ya kujua sisi tumepata gesi. Mimi nimepata ahuweni nikasema kweli sasa mazingira ya Tanzania yatakuwa yamenusurika kwa ajili ya kuchoma mkaa na kukata kuni, kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. *(Makofi)*

Mweshimiwa Mwenyekiti, tusisahau kwamba matumizi ya kuni na mkaa yanaongezeka kwasababu ya Watanzania tumeongezeka. Ukipita hii barabara ya kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam, tunaona jinsi ambavyo kila siku miti imekatwa, tuna magunia ya mikaa barabarani nikawa najiuliza, hivi kama tunasema kwamba tunaanza kuona athari

*[MHE. DKT. LUCY S. NKYA]*

za kuwa na ukame nchi, na miti inakatwa, hii gesi inatusaidiaje? Sijasikia mpango ambao unaonesha kwamba tutachakata ile gesi, ipatikane kwa bei rahisi ili iweze kutumika majumbani hata vijijini. *(Makofi)*

Mweshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapozungumza hapa leo atuambie kwamba ni mpango gani kabambe ambao kipekee utatusaidia kupunguza matumizi ya mkaa na kukata miti? Misitu inakwisha, misitu inaondoka kama hatutachukua hatua inayostahili.

Mweshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuzungumza ni kuhusu wachimbaji wa Madini wanaotoka nje. Wanatoka Wizarani moja kwa moja wanakwenda Kijijini wanasahau kwamba kuna Serikali ya Mkoa, kuna Serikali ya Wilaya, kuna Halmashauri na wakati mwingine hata Kijiji hakipati taarifa yoyote wanaanza kuchimba. Ukiwaandea wanasema sisi tuna kibali kutoka Wizarani. Nisiende mbali, nitoe mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uchimbaji wa madini unakwenda kwa kasi kubwa sana katika eneo la Mwarazi Kata ya Mkuyuni. Kule nimemkuta Muingereza yupo mle ndani, ukiuliza hata mtu wa *immigration* hajui kwa sababu yule ameingia nchini kama mtalii. Ukimwuliza, anasema anayo leseni. Kumbe ni leseni ya Mtanzania ambaye amemuuzia, nadhani hata Wizara haijui, hata sisi wenyewe hatujui.

Mweshimiwa Mwenyekiti, kuna mwingine anaechimba madini kule karibu na Kisaki, anatua na Ndege pale, anabeba madini yake anaondoka; ukimwendea anasema, mimi nafanya *exploration*.

Mweshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara sasa ijipange vizuri itoe ushirikiano kwa Halmashauri, sisi tutasaidia sana kutuatilia kujua kwamba ni nani anayechimba madini ambayo ni halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mchina anachimba

*mable* pale Maseyu, siyo mbali zile mabo zinauzwa Dar es Salaam kwenye maduka ya *Good Oone* na maduka mengine, wanasema zinatoka Uchina. Tumetafuta wananchi wameniambia wanafika kule, majibu anayotoa anasema Serikali inamfahamu. Ni Serikali gani inamfahamu kama Kijiji hakimjui, Halmashauri na Mkoa haimjui?

Mweshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri alichukulie hilo *seriously* kwasababu mabo zile zinatoka Lugoba, nyingine analeta kwa malori usiku. Nilimjua kwasababu amevunja madaraja ya Kijijini kwetu kule. Naomba hii nchi yetu isije ikawa ni shamba la bibi kwenye madini.

Mweshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nilie na reli ya kati na reli ya *TAZARA* pia. Kuna wananchi usafiri wao waliokuwanao ni Reli ya Kati tu, hasa maeneo ya Kilosa, huku Dodoma pamoja na Tabora. *(Makofi)*

Mweshimiwa Mwenyekiti, kama hazitembei, mtu akiumwa haendi Hospitali. Waliokuwa wanalima vitunguu kule Kilosa, sasa hivi kwenye maeneo ya Dete wameacha kulima kwasababu hakuna usafiri. Naomba hiyo reli iangaliwe. Naomba na wenye malori walipe kodi *special* maana wameharibu barabara sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mhesimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mweshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Suala la miundombinu lina upana wake. Usafiri ulio rahisi kuliko usafiri wowote ni wa maji. Tanzania tumebahatika, tuna ukanda wa bahari wa kilometa 1,424. Tunautumiaje ukanda huu ambao una usafiri ulio rahisi zaidi?

Tunaweza kuwa na boti kwa ajili ya kusafiri kutoka Dar es Salaam, kwenda Mtwara, kwenda Tanga na kuepusha

[MHE. JAMES F. MBATIA]
msongamano wa Jiji la Dar es Salaam. Kwanini tusitumie boti katika kusafiri ukanda wa Dar es Salaam ambao uko katika eneo la Dar es Salaam? Uwezo huo upo, ni suala la kufanyia maamuzi. *(Makofi)*

Mweshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa pili ni usafiri wa reli. Tunazungumzia suala la reli hapa, lakini nashauri tu Serikali kusema kwamba, ni vyema tukishapitisha bajeti, Kamati ya Bajeti na Serikali wakakaa pamoja kuangalia vipaumbele ni vipi. Kwasababu ukiagiza kwa mfano kichwa cha treni, kichwa cha treni inabidi utumie miezi 12 uipate. Kuna kitu kinachoitwa *lead time* na nitatoa *definition lead time. Manufacturing lead time is the total time required to manufacture an item, including order, preparation time, fuel time, setup time, run time, move time, inspection time and put away time.* Sasa hii ni taaluma, kwasababu ukitoa fedha hizi baada ya miezi sita au saba kwisha, haziwezi zikasaidia kutokana na bajeti mliojimpangia nyie wenyewe.

Kwakuwa usafiri huu na hasa Reli ya Kati, ili uweze ukawa na ufanisi wa kutosha, kwa mfano, vichwa vya treni vinavyopita *acciology* yake haitatakiwi kuzidi zaidi ya tani 15 inatakiwa iwe kwenye tani 13.7. Sasa tusipofanya maamuzi na kupanga vipaumbele vya bajeti kujua fedha gani zinakwenda wapi na kwa wakati gani, tutakuwa tunaongea tuhapa, tunapiga kelele tu hapa badala ya kuzungumza kwa vitendo na kuisidia Wizara na kuisimamia Serikali iweze kufanya kazi yake inavyohitajika.

Mweshimiwa Mwenyekiti, tuje kwenye usafiri wa barabara. Usafiri wa barabara leo hii tunategemea mwaka 2015 tuwe na kilometa elfu 17 za lami lakini *routine maintenance,* ukarabati wa barabara ukoje? Leo hii kuanzia Dar es Salaam kuja Dodoma, barabara ile imeshafika kwenye *class A classification theory,* imekwisha ndiyo inayosababisha ajali za kila leo. Njoo barabara za kwenda Kaskazini Tanga, Kilimanjaro, mpaka Arusha, hakuna *routine maintenance.* Barabara ya kwenda Kusini hakuna routine *maintenance.*

Sasa tusipofanya usimamizi wa kufanya *maintenance*

kutokana na taaluma ya kiuhandisi ilivyo, ni kwamba tunajiongezea umasikini, kuwekeza kwenye barabara zaidi, badala ya kuwekeza kwenye reli zaidi, na kuwewekeza kwenye Bandari zaidi tunajidanganya.

Pia kwenye Bandari; kwa Mfano, Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Mtwara, tunatakiwa hata kupunguza msongamano wa Dar es Salaam kutumia *dry port* ya Kisarawe. Imekuwa tunazungumza *dry port* ya Kisarawe, Kisarawe, Kisarawe; leo hii imefikia wapi *dry port* Kisarawe kupunguza msongamano katika ya Jiji la Dar es Salaam?

Mweshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa gesi. Naomba tuangalie gesi iliyogundulika inawezaje ikatumika kwenye Bandari ya Mtwara yenye kina kirefu katika ukanda huu ukilinganisha na gesi ambayo imepatikana Msumbiji, tukawavutia watu wa Msumbiji wakatumia Bandari ya Mtwara vilevile. Japo hapa kwetu tuna *cubic metre* trioni 46,000, wenzetu wana zaidi ya *cubic metre* trioni 100, lakini wakatumia kwa maslahi ya hapa. Tunaweza tukalalamika sana, sawa, lakini tujue vilevile ukubwa wa nchi yetu ukilinganisha na wenzetu wa Africa Mashariki. Tanzania tuna Kilometa za mraba 945,203/= wakati Kenya wana 581,309, Uganda wana 236,040, ndugu zetu wa Burundi 27,000/= na Rwanda ni 26,000. Sasa Tanzania tuna zaidi ya asilimia 52 ya eneo lote la Afrika Mashariki. Kwa sababu kutokana na ukubwa tulionao, inabidi tuweke vipaumbele vyetu, mikakati yetu, tuamue ni lipi la kufanya na kwa wakati gani na tukishalimaliza, tunafanya jambo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipowekeza hivyo, tukakubaliana kwamba kipaumbele chetu kiko wapi, tutapata matatizo. Tunapopiga danadana, nirudi kwenye msongamano wa Jiji la Dar es Salaam kwa siku tunapoteza zaidi ya Shilingi bilioni tano ambapo kwa mwaka ni zaidi ya trilioni mbili tunapoteza kwa ajili ya msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Hili ni janga la Kitaifa. Lakini kuweza kuliondoa hili janga, uwezo upo. Tunaweza kuona ni namna gani tunatumia hata helikopta kwa misafara ya Viongozi wakatumia helikopta badala ya kutumia ving'ora na nini

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



kuzidi kuongeza msongamano katika Hiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Sasa wataalam wakikaa likaonekana kwamba ni janga na janga likachukuliwa hatua kama janga, uwezekano wa kupata *mitigation measures* upo, ili mradi tunafanya maamuzi kwa nia iliyo sahihi.

Ni lazima tubadilike kifikira, namna ya kuweza kusimamia uchumi wa Taifa letu na kufanya mapinduzi makubwa sana. Tunaweza tukasema bajeti haipo lakini matumizi ya Serikali ni makubwa sana na ya kutisha. Lazima tubadili, tuone ni wapi tunawekeza kwa maslahi gani, na kwa muda gani. Tukiunganisha haya yote, na tukienda kwenye kazi ya Wizara ya Nishati na Madini, tukiangalia na gesi ambayo tumeipata, tunafikiria ubunifu wa namna gani kuwekeza kwenye rasilimali watu wa kusimamia sekta hii kwa miaka 10, 20, au 30 ijayo. Yote haya yanawezekana ili mradi tu tunafanya maamuzi kwa wakati tuliokubaliana kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya ukubwa wa Taifa letu, kuna migongano ya Bunge na Serikali. Bunge kazi yake kubwa ni kuisimamia Serikali. Sasa tunaisimamia Serikali katika misingi ipi ambayo tumekubaliana kwa pamoja kwa maslahi ya Watanzania katika sekta zote hizi kwa pamoja? Tukiangalia Sekta ya Nishati ambapo umeme vijiji *REA:* Je, wamepata fedha kiasi gani? Lakini Wizara inajitahidi sana yenyewe kutafuta vyanzo vingine vya mapato. Ni vizuri tuondokane vilevile na hizi fikra kwamba tunaweza sisi wenyewe tu humu ndani, kama tuna uwezo wa kukopa, tuondokane na huu mtazamano wa kizamani labda *IMF, World Bank;* kuna mikopo mingine poa katika nchi za Asia, na katika Mataifa mengine tutanue uwezo wetu kwa maslahi yetu na rasilimali tulizonazo kwa maslahi yetu sisi sote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

nashukuru sana, lakini naona nimetumia dakika saba tu. Mimi nina *stop watch* hapa. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Mbatia. Tunafuata *time* ya Bunge. Sasa namwita Mheshimiwa Arfi, atafuatia Mheshimiwa Barwany na tutamalizia na Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati kwa taarifa nzuri walizowasilisha, lakini nitajikita katika maeneo machache, na kwanza nitaanza na Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na reli, ni-*declare interest* kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, lakini nataka kutofautiana na wenzangu katika suala la aina gani ya reli tuwe nayo. Nilikuwa nadhani kwamba reli ya *meter gauge* ambayo sasa hivi tunayo, tukiimarisha na tukaboresha madaraja na tukaongeza uzito wa reli tulizokuwa nazo, tutaweza kubeba mizigo mingi na mizito na kwa muda wa haraka zaidi na badala ya kusubiri kutafuta fedha na kuanza kujenga reli nyingine ya *standard gauge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naamini kabisa kwamba reli hizi za *meter gauge* zimebakia Tanzania peke yake, kumbe siyo kweli! Duniani reli za *meter gauge* zipo na zinafanya kazi kwa ufanisi mkubwa sana. Kama tutaimarisha reli tuliyokuwanayo, tutatoka katika ubebaji wa *extra load* wa 136 *tones* tukaenda mpaka 160 mpaka 200. Hili linawezekana, na litakuwa la gharama ndogo zaidi kuliko sasa kwa hali tuliyokuwanayo kama Taifa kuanza kufikiria kujenga *standard gauge*. Wala sitaki kuamini kabisa kwamba tutakapokuwa na *standard gauge* tutakuwa tumetokana na matatizo hayo ambayo tunayo sasa hivi.

Tunayo *standard gauge* katika reli ya *TAZARA,* lakini reli ya *TAZARA* hali kadhalika ina matatizo lukuki. Kwa hiyo, huo ulikuwa ni mtazamano wangu katika eneo la reli. Tunaweza tukajenga reli nzuri na itakayobeba mizigo mingi

*[MHE. SAID A. ARFI]*
na ya haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie bandari. Tunaulizwa kwanini Tanzania hatuendelei wakati Mungu ametupa neema ya kuwa mahali ambapo tungeweza kuendelea kutokana na nafasi hii tuliyokuwanayo kijiografia. Tuna bandari, na tuna nchi kadhaa zimetuzunguka ambazo hazina lango la bandari lakini tumeshindwa kuitumia bandari yetu ya Dar es Salaam kwa ufanisi na matokeo yake kazi zinakwenda zinapungua.

Pamoja na jitihada ambazo zinafanywa na Wizara na Mamlaka ya Bandari kwa sasa inatia moyo. Lakini naiomba Wizara kwamba ujenzi wa gati 13 na 14, ni wa muhimu kuliko kitu kingine chochote. Najua Wizara ina mtazamo wa kujenga Bandari ya Bagamoyo; sikatai kujenga Bandari ya Bagamoyo, lakini kutakuwa na maana gani kama tunajenga bandari ya Bagamoyo wakati gati namba 13 na 14 tumeshindwa kujenga? Bandari ambayo tunaimiliki Watanzania kwa asilimia 100, leo tunakubali tutafute wageni waje wajenge Bandari Bagamoyo na Bandari yetu ya Dar es Salaam ife. Jambo hili wataalam hebu waliangalie na waje na mtazamo wa kizalendo kwa maslahi mapana ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara, wenzangu wengi wamesema na fedha nyingi zimetumika kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara kwenye barabara. Lakini linalonisumbua sana ni fidia kwa wananchi. Nashangaa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, Wizara moja inapotaka kufanya miradi ya maendeleo kwa mfano upanuzi wa viwanja vya ndege, wananchi wanalipwa fidia katika maeneo ambayo wanapisha upanuzi wa viwanja vya ndege. Lakini Serikali hii hii inapotaka kujenga barabara, Watanzania masikini ambao walijenga nyumba zao, zinavunjwa kwa ujeuri, wanaambiwa hawawezi kulipwa fidia. Hamwatendei haki Watanzania hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali hii inaweza kulipa fidia kwa ajili ya upanuzi wa viwanja vya ndege ambao ni maendeleo, kwanini inashindwa kuwalipa fidia watu

*[MHE. SAID A. ARFI]*

ambao wamevunjiwa majumba yao kupisha ujenzi wa barabara? Naomba jambo hili waliangalie ili kusiwe na *double standard;* Wizara moja inalipa, Wizara nyingine jeuri, haitaki kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme, nazipongeza juhudi zinazofanywa na Wizara ya Nishati na Madini, lakini nina tatizo kubwa la umeme katika eneo langu. Nimeongea na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba hali ya Mji inakua, *engine* zilizopo pale zina zaidi ya umri wa miaka 40 toka zimetengenezwa. Zimefanya kazi Shinyanga na hatimaye zimeletwa kule Mpanda na zimechoka sana. Mahitaji ya umeme Mpanda pamoja na yale ambayo tutapeleka katika mradi wa *REA* ni zaidi ya 3.8 Megawatt, uzalishaji wa umeme sasa hivi ni 1.9. Kuna mgao wa ajabu Mpanda. Mlituahidi mtatupelekea *engine* mbili mpaka sasa hazijaenda nilikuwa napenda tu kuikumbusha Wizara, nimeongea na Naibu Waziri aangalie ni namna gani anaweza kutusaidia katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ili *TANESCO* iweze kufanya biashara ni lazima iingie katika ushindani na katika ushindani ni lazima ipate wateja wa kutosha. Wateja wapo, wapo tayari kulipa fedha na kulipa hizo gharama za ankara kila mwezi. Tatizo kubwa ambalo *TANESCO* wanalo ni vifaa. Hakuna nguzo, hakuna nyaya, hakuna vikombe, hakuna vifaa vingine vya kuunganishia, hakuna mita na kadhalika. Serikali ijaribu kuwasaidia *TANESCO* kuweza kupata vifaa ili waweze kuunganisha wateja wengi kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo nitapenda kuzungumzia ni maeneo ya madini na hasa wachimbaji wadogo wadogo. Tuna matatizo ya muda mrefu sana kule Mpanda. Maeneo mengi yamehodhiwa na Makampuni makubwa ambao wameshindwa kuendeleza maeneo yao na wamendelea kuhodhi na kubakia kuwa Mawakala wakingojea labda neema ya Mungu itashuka, watapata wawekezaji. Jambo hili halikubaliki! Wachimbaji wadogo wadogo wanahangaika, maeneo mengi yamehodhiwa na Makampuni makubwa ya matajiri, lakini

kwa bahati mbaya sana wafanyakazi wa Wizara ya Nishati na Madini sio waaminifu. Sio wote, lakini wako miongoni mwao baadhi ya watumishi katika Wizara ya Nishati na Madini na wao ni sehemu ya hii biashara ya kuhodhi maeneo ya madini. Tunaomba mwangalie kwa sababu maeneo mengi sasa hivi yameshikwa kupitia msaada mkubwa wanaopewa na watumishi walioko katika Wizara ya Nishati na Madini. Niiombe Wizara iliangalie eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisema sasa hivi, nishati mbadala ni nini? Mtu ana baiskeli moja ya mkaa anakamatwa.

Tuwaambie wananchi wetu, watatumia nishati gani badala ya mkaa? Mkaa sasa hivi ni kweli kunakuwa na uharibifu wa misitu, lakini hakuna nishati nyingine. Mafuta ya taa ni ghali, gesi haipatikani na hakuna nishati nyingine yoyote. Serikali ina mpango gani sasa kwa watu wanaoishi Mijini na watatumia nishati gani na hasa wale masikini wanaotegemea kutumia nishati ya mkaa, watatumia nini badala ya mkaa ili miti iendelee kuwepo? Vinginevyo Serikali itoe tamko hapa kwamba uchomaji wa mkaa kwa matumizi ya majumbani uweze kuendelea na wasibughuziwe, hasa wananchi hawa wadogo wadogo wenye kubeba baiskeli moja au mbili za mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni reli ya Mpanda. Najua sasa hivi jitihada inafanyika ya kuimarisha Reli ya Kati, na baadhi ya reli zenye uzito wa ratili 80 zimeng'olewa, na nilikuwa nimeambiwa kwamba reli hizo zitahamishiwa katika njia ya kutoka Kaliuwa kwenda Mpanda. Ni lini sasa kazi hiyo itafanyika? Nilikuwa nataka kuihimiza tu Serikali kwamba umuhimu wa reli ya Mpanda unafahamika, mtusaidie kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Arfi. Sasa namwita Mheshimiwa Barwany, ajiandae Mheshimiwa

Ndassa na tukipata nafasi atamalizia Mheshimiwa Said Mtanda.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nitumie nafasi hii pia kukushukuru kwa kunipa nafasi hii mchana huu wa leo. Lakini pia nizipongeze Kamati zote mbili kwa ushauri wao juu ya Serikali katika Wizara zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa tulizonazo ni kwamba nchi yetu ina utajiri mkubwa wa rasilimali hasa rasilimali za madini ambazo takriban sasa zaidi ya miaka 50 bado ni ngonjera kwa Viongozi wetu wa siasa kujisifia kwamba Tanzania ni nchi tajiri. Tunaambiwa pia kwamba Tanzania ni nchi ya tatu kwa dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu nimezaliwa, niliambiwa kwamba Tanzania tunachimba madini ya almasi Mwadui, tuna madini ya *Tanzanite* ambako hakuna kokote duniani zaidi ya Tanzania na nyingi nyinginezo. Lakini tukizungumzia suala la maendeleo ya nchi kupitia rasilimali zake, tunaambiwa kwamba kuna maeneo mawili ya umuhimu kabisa katika maendeleo. Kwanza ni maendeleo ya watu, halafu maendeleo ya vitu. Sasa tunaweza tukawa na miundombinu, tukawa na barabara nyingi, tukawa na reli, lakini: Je, watu wake wana maendeleo gani? *(Makofi)*

Hii rasilimali ambayo tunasema tunayo, imewasaidia nini Watanzania? Leo tuangalie katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, Wasukuma kule katika maeneo ya Geita, wana dhahabu ya kutosha, twende Mererani kule Arusha, kuna utajiri wa kutosha, lakini watazamane wananchi wake katika maeneo yale, wanaishi katika umaskini mkubwa, umaskini wa kutisha. Ukiangalia takwimu, watu ambao wamekosa elimu ya kutosha, huduma ya afya, ni maeneo ambako tayari kuna rasilimali kubwa za madini. Hebu tazamana ndugu zangu Wasukuma na Wanyamwezi kule, wanaishi katika umaskini mkubwa! Pamoja na utajiri uliokuwepo, bado Serikali haijaona umuhimu wa kutumia rasilimali hii kwa maslahi ya wananchi wake.

*[MHE. SALUM K. BARWANY]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie katika eneo la bandari zetu. Ni mwaka wa tatu sasa hivi tangu tuanze Bunge hili la Kumi hapa Dodoma. Nimezungumza sana suala la Bandari ya Lindi. Ni kauli tu za mara kwa mara zenye kutoa matumaini juu ya Bandari ya Lindi, lakini bado hakuna dalili zozote kwamba kuna upembuzi yakinifu, kuna hivi, kuna Wajerumani tayari wanatoa ushauri, kila siku tunapokutana, ni kauli za namna hiyo. Lakini bado wananchi wa Lindi walitoa kura nyingi kwa ahadi kwamba pindi mtakapoichagua Serikali ya Chama cha Mapinduzi tutahakikisha kwamba Bandari ya Lindi inajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokukamilika kwa Bandari ya Lindi ni utapeli wa kura za wananchi wa Lindi. Wamelaghaiwa! Walikuwa na uhuru wa kuchagua Chama wanachokitaka. Lakini kwa sababu waliona tatizo lao kubwa ni Bandari, wakasema kura zetu tutapeleka katika ilani ambayo inatuhakikisha kwamba Bandari ya Lindi itajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengi, lakini Bandari ya Mtwara ilijengwa mwaka 1950. Waingereza walijenga Bandari ile kwa sababu kubwa moja ya kiuchumi katika Mikoa ya Kusini. Walijenga reli kutoka Nachingwea ambako kulikuwa na mradi wa karanga ambapo wakajenga reli mpaka Mtwara kwa ajili ya kusafirisha karanga kupeleka nje ya nchi. Lakini pia tulitaka kuhakikishiwa kwamba Bandari ya Mtwara ingetoa huduma muhimu katika nchi ya Malawi. Kuna mashedi kule karibu manane ambayo yamejengwa katika Bandari ya Mtwara kwa kutaka kusafirisha shaba kutoka Malawi na Zambia na zoezi liliwahi kufanyika katika miaka ya nyuma. Lakini leo Bandari ya Mtwara tunaambiwa zinajengwa Bandari nyingine mpya, wakati Bandari tulizokuwanazo mpaka leo hazijakidhi mahitaji ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sababu gani ya kutumia pesa, tena kukopa mikopo katika Benki ya Dunia kwa kutoa madeni makubwa kwa nchi wakati bandari tunazo hazijafikia kiwango kinachohitajika kwa kutoa huduma ndani ya nchi yetu. Hayo ni matumizi mabaya ya Serikali yetu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala zima la gharama za uwekaji wa umeme katika nchi yetu. Tunaambiwa kwamba katika sehemu ambayo tayari mradi wa umeme unapelekwa, Serikali itagharamia gharama zote za pale ikiwepo nguzo na vitu vingine. Lakini ni kinyume chake kwa ahadi ya Serikali, kwamba mpaka pale ambako tayari mradi wa Serikali umepelekwa umeme kule, lakini wananchi wake wanaambiwa waendelee kuchangia nguzo za maeneo yale. Lakini mbaya zaidi, nguzo ile ambayo mtu wa kawaida ananunua, yake kwa fedha yake, inaambiwa kwamba siyo mali yake. Sasa akili ya kawaida ikoje hapa? Akili ya kawaida inatuambiaje? Kwamba nimenunua kwa pesa yangu, lakini wananiambia siyo ya kwangu. Kama ingekuwa ya kwako, kwanini usinunue kwa pesa yako. *(Makofi)*

Sasa hili linaleta mkanganyiko. Lakini pia elimu ya watumiaji umeme katika bili ya umeme bado haijatosheleza. *TANESCO* wanawajibika sasa kutoa elimu kwa watumiaji wa umeme juu ya bili zao. Kuna malalamiko mengi katika maeneo mbalimbali kwamba bei za umeme mpaka sasa bado hazijaeleweka katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizungumzie juu ya mikataba ya madini. Hili ni Bunge. Bunge ni jumba la kutunga sheria, Bunge jukumu lake ni kuisimamia Serikali. Yote yanayofanywa na Serikali, basi Bunge linapaswa kujua. Bunge ndiyo wananchi! Hivyo Bunge likipata taarifa ya maendeleo ya Taifa lake, wananchi wanapata taarifa zao pia kupitia Bunge lao, kupitia Wawakilisha wao. Tumedai muda mrefu tunataka mikataba ya madini ije Bungeni, tuifahamu. Serikali imekuwa kiziwi! Serikali imekuwa kipofu juu ya hoja za Wabunge, kwamba tunataka mikataba hiyo ije kuna siri gani Serikali ina hofu gani kuwasilisha mikataba katika Bunge hili, kuna nini hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tunataka mikataba, tena hili lisiwe ombi. Wabunge wenzangu mara zote

tunaiomba Serikali; haituombi Serikali, tunaitaka Serikali ilete Mikataba ya Madini Bungeni. Mgogoro wa Mtwara, ni siri ya Serikali kutowaeleza wananchi wa Mtwara mikataba gani iliyopo. Mikataba ya gesi iko wapi? Leo Mikoa ya Mtwara na Lindi shughuli za kisiasa zimefungwa, hazipo kwa sababu tu wananchi wanahoji Sera ya Gesi iko wapi? Wananchi wanahoji mikataba iko wapi?

Leo katika maeneo ya Lindi na Mtwara shughuli za kisiasa hazifanyiki, zimepigwa marufuku kwa sababu wananchi wanataka kujua haki zao za msingi kwamba, baada ya mafanikio ya gesi, wanananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara watapata maslahi gani kupitia gesi yao? Wanageuziwa bao Viongozi wa Serikali kwamba wananchi wa Kusini hawataki gesi yao itoke. Sio kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kauli ya kutaka kuwagonganisha Watanzania, kuwagawa Watanzania kwa misingi ya kisiasa, kwamba hawa wananchi wa Mtwara hawataki gesi yao iende Kaskazini, wanataka itumike Kusini. Sio kweli! Mwananchi wa Mtwara na Lindi hawajasema gesi isitoke Mtwara hata siku moja! Wanachodai wao, mikataba iko wapi tuione? Itakuwa na maslahi gani kwa Watanzania? Ndiyo hoja ya msingi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kumuua mpwa wako, basi unamtafutia jina baya, ili kesho ukimkuta katika mtaro; si mwizi yule, mpwa wake mwenyewe alishasema! Ndicho wanachofanyiwa wananchi wa Mkoa wa Kusini, waonekane wanakwenda tofauti na Serikali yao. Kumbe sivyo.

Tunataka mikataba ya madini yetu ije hapa. Tumeona mifano ya Wasukuma na Wanyamwezi kule, wameachiwa mashimo tu katika migodi yao. Tunataka pia wananchi wa Kusini sasa, tumeamka tujue tutanufaika vipi na rasilimali ya Taifa letu? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Ndassa, na Mheshimiwa Said Mtanda ajiandae.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napongeza taarifa za Kamati zote mbili. Niseme tu kwamba mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa zote mbili kwa ruhusa yako naomba Waheshimiwa Mawaziri wazichukue. Lakini nianze na mchango wangu wa kwanza, upande wa bomba la gesi kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mambo mawili. La kwanza, ni usalama wa bomba lile. Niiombe sana Serikali, kwa sababu Serikali mmewekeza sana pale. Usalama wa bomba lile kutoka mwanzo mpaka mwisho ikiwa ni pamoja na kwenye vinu vyake isimamiwe vizuri. Kama ni watu wa Usalama, wao wenyewe wanajua sitaki kuwasemea. Lakini ni vizuri ikaangalia kwa macho mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwenye bomba la gesi, ni kuhusu Wataalam. Kamati yetu imeshauri sana wataalam wazalendo, ajira zitolewe na waende wakasome, ili baada ya hawa wenzetu kuondoka Watanzania waweze kuendesha na kusimamia bomba hili. Lakini kuna bomba tayari, wataalam tunao, mambo ya usalama yapo; suala zima la bima, hili halikwepeki. Naishauri sana Serikali kupitia *TPDC* na watu wa *TIR*A wakae pamoja waangalie namna moja nzuri zaidi ya Bima zitakavyowekwa. *(Makofi)*

Mheshmiwa Mwenyekiti, la tatu, *TANESCO* na *REA* wanafanya kazi nzuri sana. Nawapongeza sana, lakini zipo changamoto ambazo kwa kweli bila kuwa pamoja, nafikiri watu wanaweza wakafika mahali wakashindwa. Niombe sana *TANESCO* na *REA*, watakapokabidhi miradi hii watu wa *REA, TANESCO* nawaomba imara sasa katika kuwasimamia kwa sababu ni mzigo mzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Mawasiliano hebu tusaidie, tuambie tu ule ukweli. Hivi tatizo la Ndege za *ATCL* ni nini? Kumekuwa na hadidhi nyingi humu ndani; itakuja kesho, kesho kutwa, bila mafanikio yoyote. Tuambie

Wabunge ukweli na Watanzania wanaopenda kutumia ndege ya Shirika la *Air* Tanzania wajue, tatizo ni nini? Ni vizuri wenzetu Mawaziri wakasema ukweli na ni tabia nzuri tu. Lakini kila mkija hapa mnatuambia inakuja, inakuja inakuja. Leo nataka utuambie kwa mara ya mwisho, tatizo ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwa nini msiwasaidie *ATCL*. Hivi hii tabia ya kukodi ndege, inatoka Dar es Salaam, inakwenda Burundi, inabeba mtu mmoja. Hivi kweli kuna faida kweli hapo! Ile tunasema dhamani ya pesa, unaiona kweli hapo? Abiria mmoja!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sana, mambo haya wenzetu na nyinyi ni wasomi, ni Wahasibu, mnajua uchumi, mtazame.

Mwanza *Airport,* Mkandarasi aliyekuwepo pale, kwanza amesuasua kuanza. Mwanza *Airport* kwetu ni uchumi. Amesuasua kuanza, lakini leo ni miezi sita ame-*raise certificate* zake Shilingi bilioni nne hajalipwa. Mwanza mnasema iwe *hub* kwa Maziwa Makuu. Lakini hamtaki kupeleka pesa pale. Uswahiliswahili tu! Unajua watu wengine hatujazoea kusema maneno makavu, hatujazoea! Siyo tabia yangu, lakini mnafika mahali mnataka kutufikisha huko. Fikeni mahali muamue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vya Shinyanga na Sumbawanga viko pale, tulikubaliana kwamba Zabuni ingelitangazwa Septemba, 2013, leo hii ni mwezi Desemba, 2013. Semeni tatizo ni nini? Waziri, tunakuamini sana, unaheshimika, unafanya kazi vizuri, lakini unakuwa na kigugumizi katika maamuzi ya kufanya mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nisisahau kuipongeza sana Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)*. Ukiona mahali pametulia, siyo bure. Kuna watu wanafanya kazi zao vizuri. Lazima nimpongeze sana *CEO* wa *TAA* kwa kazi nzuri ya usimamizi wa viwanja vyetu na *Management* nzima. Ukiona sehemu kuna migogoro kama ilivyo *TAZARA,* tatizo ni

Uongozo, wala siyo pesa. Kwa hiyo, naishukuru sana *TAA* kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho kabda kengele yangu haijalia, Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, bandari bila reli, na reli bila bandari ni kazi bure. Kila siku yanasemwa humu ndani. Hivi tatizo ni nini? Kila siku tunasema reli, reli, reli; bandari, bandari, bandari. Sasa sijui ni kitu gani, mimi sielewi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti - Mheshimiwa Mtemi Chenge juzi hapa alisema; hatuelewi ni nini? Lakini ni vizuri kwa kweli hebu tuanze na kitu kimoja kimoja. Tukisema tunakwenda kujenga Gati Na.13 na Na.14, hebu tujielekeze huko sasa tupunguze maneno, twende kwenye vitendo. Tunachelewesha kuleta uchumi na mapato kwa nchi yetu. Twende kwenye vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, na niipongeze Serikali kwa kukaribia kukamilisha ujenzi wa Daraja la Mto Simiyu.

Naipongeza sana Serikali. Daraja lile lina urefu wa kilometa 104, sasa limekamilika kwa asilimia 90. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, nakusihi sana, kwenye zile *approach* pande zote za barabara, kuna sehemu zilizobakia. Kamilisha kutoa pesa ili wananchi wangu wa Maligisu, Mahaha, Shishani, Kabila, Kadachi na maeneo mengine waweze kuvuka kwenye daraja lile bila matatizo hasa kwa kipindi hiki cha mvua. Mto ule wa Simiyu ni mkubwa sana. Kama daraja lile halitakamilika haraka iwezekanavyo katika maeneo yaliyobakia, nafikiri wananchi wangu watashindwa kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, lakini naunga mkono mapendekezo ya Kamati zote mbili. Naomba Serikali iyachukue na iyafanyie kazi ili kusudi tukija katika kipindi cha mwaka ujao, 2014, katika kujadili Taarifa za Wizara tukute baadhi ya mambo yamekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante

sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saidi Mtanda, ndio mchangiaji wetu wa mwisho mchana huu.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika mjadala huu. Nitumie fursa hii pia kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati zote mbili kwa kazi nzuri waliyoifanya, na taarifa zao zina ushauri mzuri ambao endapo Serikali itauchukua kuufanyia kazi na kuutekeleza basi tunaamini changamoto nyingi zitapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika maeneo mawili. Eneo la kwanza ni kuhusu gesi. Ninazungumza gesi, kwa sababu miongoni mwa maeneo ambayo gesi itazalishwa ni pamoja na Mkoa wangu wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ipia nitumie fursa hii, kuwahakikishia Watanzania na Waheshimiwa Wabunge, ndani ya Bunge hili kwamba, wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara hawana tatizo kabisa kuhusu gesi kusafirishwa kwenda Dar es Salaam. Wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara, wanachoihoji Serikali ni kuhusu namna gani baadhi ya ahadi ambazo zilitolewa kwao kwa muda mrefu hazijatekelezwa? Lakini mradi huu ndani ya mwaka mmoja sasa unaeldekea kukamilika, lakini ahadi hizo bado hazijafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza bomba la gesi, lifike Dar es Salaam na maeneo mengine wapate umeme, lakini bado vijiji kadhaa vya Mkoa wa Lindi havina umeme. Jimbo la Mchinga lina umeme kwenye vijiji viwili. Tunayo maeneo tuliyoahidiwa na *REA*, Umeme Vijijini toka mwaka 2010 hadi leo hii, hakuna dalili ya nguzo kwenye maeneo hayo. Vijiji vya Kikomolela, Kilangala, Kitomanga, Moka, Matimba, Makumba, mpaka Nangaru, Milola na Rutamba, havina umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumzia

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



namna ya kuwaomba wananchi wetu waweze kushiriki katika kulinda miundombinu ya bomba la gesi kwenda Dar es Salaam, jambo ambalo ni bora sana, lakini walinzi wa bomba hilo wanashudia gesi ikipita kuelekea Dar es Salaam, wao wakiwa kwenye giza. Jambo hili halikubaliki. *(Makofi)*

Tunaishauri Serikali, kwanza ahadi ambazo ilitoa kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara, ikiwemo watu wa *ATMUS*, ambao walisema wangeleta umeme kwa gharama nafuu kwenye vijiji vya Mikoa ya Lindi na Mtwara, Kampuni hiyo hatuelewi imeishia wapi. Hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile fidia kwa wananchi wale ambao wamepisha Mradi huu; unatoa shamba lako, wanatathmini miembe miwili mitatu na minazi unapewa Sh. 5,000/= kwa mnazi mmoja, bomba limepita. Sasa hivi tunafikiria namna ya kujenga viwanda vya kuchakata gesi kwenye baadhi vya maeneo ikiwemo Mkoa wa Lindi. Tunaishauri Serikali kuja na fidia mpya ambayo inakwenda na wakati, fidia inayozingatia maslahi ya wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara, wawe nao ni wabia katika mradi huo wa Kiwanda badala ya kupewa Sh. 5,000/= kwa mnazi mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Lindi wanajiuliza, iweje leo mradi wa bomba la gesi, unakwenda Dar es Salaam, zaidi ya kilometa 456 kwa kipindi cha mwaka mmoja, lakini kipande cha barabara cha kilometa 40 ya barabara pale Nangurukuru kimechukua zaidi ya miaka 10 kutokamilika? Jambo hili halikubaliki. Halikubaliki hata kidogo! *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali, kwanza, wakati tunaendelea kuishauri Serikali yetu kufikiria na kupeleka gesi katika maeneo mbalimbali ya Taifa ambalo ni jambo la msingi, ni lazima kero hizi ambazo ziko katika maeneo yetu ziweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sera ya Gesi, sera hii inawahusisha vipi Watanzania, walioko katika maeneo

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



mbalimbali? Sera hadi leo imekamilika, hatuelewi itakuja lini hapa Bungeni, lakini pia uhusishwaji wananchi ili waweze kutoa mchango wao wa mawazo katika kuwa Sera bora zaidi ya gesi, haujafanyika kikamilifu. Kwa hiyo, wakati mwingine tunalaumu wananchi, lakini hatujawapa elimu ya kutosha juu ya masuala haya. Kwa kipindi hiki ambacho Mradi huu unategemewa kuanza, nilitarajia pia Wizara ichukue hatua za makusudi kwenda katika maeneo.

Ningeliomba kuishauri Wizara ijifunze kutoka kule Msumbiji, wenzetu katika kijiji cha Palma, Serikali ya Msumbiji, ilipoamua kujenga kiwanda cha kuchakata gesi kwenye kijiji kimoja wapo pale Msumbiji, kiliamua kuwahamisha wale wananchi lakini wamejenga nyumba 500 za kisasa ili wananchi wale waweze kuwa na makazi bora yanayoenda sawasawa kabisa na maisha ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Gesi ni lazima iwashirikishe wananchi, tukusanye maoni ya wananchi kabla ya kujadili katika Bunge hili, na ni lazima iseme wazi wazi maeneo ambayo yanazalisha gesi, ni lazima kuwe na mrahaba utakaowezesha Halmashauri za maeneo hayo kunufaika na kusaidia katika kupunguza umaskini maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bandari ya Lindi, kinachohitajika ni kutoa mchanga pale. Lakini hadi leo na hata taarifa ya Kamati haielezi wala haigusi chochote kuhusu Bandari ya Lindi. Kwa hiyo, naomba wenzetu hawa waweze kuzingatia kwamba miongoni mwa bandari nzuri sana ni bandari ya Lindi, waipe kipaumbele katika taarifa zao ili tuweze kwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Lindi, tunao uwanja wa ndege mzuri sana. Lakini takriban miaka miwili sasa sijawahi kuona ndege ikitua, lakini wafanyakazi wapo, wanalipwa mishahara yao. Nilikuwa nataka kujua kutoka Wizarani: hivi uwanja wa Kimataifa wa Lindi umejengwa kwa ajili ya nani? Kwa nini ndege zinazoelekea Mtwara zisiweke kituo cha muda mfupi pale Lindi, badala yake sisi tunalazimika twende

Mtwara kilometa 70 kutoka Lindi, tushuke pale Mtwara tuanze kurejea nyuma tena kuelekea Lindi, wakati ndege hizi zingeliweza kuweka kituo cha muda pale Lindi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze pia kuhusu baadhi ya tabia mbaya zinazofanywa na Makampuni haya ya ndege kama vile *Precision Air.* Kuna ubaguzi mkubwa sana. Niliwahi kushuhudia siku moja pale uwanjani. Watu tunakwenda tumechelewa ndege, lakini kwa misingi na sababu wanazozijua wao, wanatoa upendeleo kwa baadhi ya watu, na kuwaacha watu wengine. Lakini ndege hii ya *FLY 540*, ukienda pale ukiwa na *ticket* yako unaweza kuambiwa umechelewa ndege. Wanakata *ticket* nyingi kwa abiria, wanawaacha abiria pale uwanjani hata ukichelewa dakika moja, hata ukiwa ndani ya muda pia unaweza ukaachwa, wanasema ndege imejaa, wanaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakwambia usisafiri na mzigo. Ukifika pale mzigo ukipimwa, kilo 10 unaambiwa ni Dola 50. Nauli yake ni ndogo kuliko kifurushi cha kilo tano. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri Wizara iko haja ya kuangalia sana Mashirika haya, wakae na wenzetu wawaeleze kuhusu namna bora ya uendeshaji wa ndege hizi ili ziweze kutuletea tija Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, ningefurahi sana leo endapo Mheshimiwa Waziri anayehusika na masuala ya nishati na madini, angelitueleza, hivi hawa watu wa Mamlaka ya Umeme Vijijini, ambao sisi tunaamini kwamba Umeme Vijijini, ingelikuwa ni kigezo kikubwa sana cha kuondoa umaskini vijijini; lakini toka mwaka 2010 tumepitisha bajeti, vijiji vyangu vya Kilangala, Kilolambwanin na Mipingo, vimeingia kwenye mchakato, lakini mchakato huo toka mwaka 2010, 2011 bajeti tumeipitisha, mwaka 2012, 2013 na leo tunaelekea 2014 mchakato haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa kufahamu, hivi hawa *REA* wenzetu wanayo azma ya kweli? Kila anayezungumza anasema waongezewe fedha. Hizo ambazo wanazo, na maeneo ambayo tayari walituahidi,

*[MHE. SAIDI M. MTANDA]*
mbona bado hawajaleta umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa umeme ukifika maeneo kama Milola, wananchi watajihusisha na shughuli nyingine za kiuchumi. Ile inaitwa *effect of economic multiplier.* Kutakuwa na shughuli mbalimbali za kiuchumi vijana wanaweza kufanya na kusaidia kupunguza umasikini vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina haja ya kugongewe kengele, nimalizie kwa kusema, daraja lile la Mchinga, kuunganisha wananchi, wa Mchinga I na Mchinga II, kuelekea Kilolambwani, lenye thamani ya Sh. 380,000,000/= ambalo tulipeleka ombi maalum Wizarani, kuomba wenzetu watusaidie kwa sababu fedha za barabara kwenye Halmashauri yangu ni Shilingi milioni 600 haziwezi, na tukitumia Shilingi milioni 380, hatutaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru na ninawashukuru Wabunge wote kwa michango mizuri.

Waheshimiwa Wabunge, leo hii asubuhi kulikuwa na Mwongozo uliombwa na Mheshimiwa Mwigulu na sasa niko tayari kutoa *ruling.* Suala hili ni la kiutawala, na masuala yote yanayohusu matumizi ya fedha yatatawaliwa na Sheria na Kununi za Fedha. Hivyo, kwa wale wachache ambao wamechukua fedha bila kusafiri, Sheria na Kanuni zitatumika ili waweze kuzirejesha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha Bunge mpaka saa 111.00 jioni.

*(Saa 6.57 mchana Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Murtaza Mangungu, sidhani kama yupo na kwa sababu orodha yangu ni ndefu kwa mtu ambaye...

**KATIBU:** Yupo!

**NAIBU SPIKA:** Yupo! Ahsante sana. Mheshimiwa Murtaza Mangungu, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Njwayo.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumweleza ndugu yangu, Mheshimiwa Bwana Peter Serukamba na Mzee wangu Mheshimiwa Kilasile Mwambalaswa kwamba uchumi wa nchi hii, aidha kwenda mbele, kurudi nyuma au kukwama inatokana na utendaji na utekelezaji wao. Hakuna maendeleo ya kiuchumi bila nishati, hakuna maendeleo ya kiuchumi bila kuwa na miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamechangia leo asubuhi wameeleza mambo mengi sana, lakini na mimi ningependa nichangie machache pamoja na kuwiana na mawazo ambayo wao wamekuwa wakiyatoa.

Kwanza, nastaajabu sana mpango wa ufufuaji wa reli unasuasua; lakini kuna jambo ambalo nimejitahidi sana kufikiria na kufuatilia katika nchi mbalimbali, sijapata kuona bali Tanzania peke yake; barabara za Tanzania ndiyo barabara pekee ambazo zikinyeshewa na mvua lami yote inatoka. Huu ni utafiti rahisi tu ambao unaweza ukaufanya, mvua ikinyesha barabara zetu za lami zinatoka, zinabaki kokoto tupu, kesho mashimo yanaendelea. Sijui hili wenzetu

*[MHE. MURTAZA A. MANGUNGU]*

mnaliangalia katika mtazamo wa namna gani!

Waheshimiwa Wabunge wa Kusini wamezungumza; kipande cha barabara ya kutoka Ndundu hadi Somanga sasa hivi tuna zaidi ya miaka saba barabara ile haikamiliki. Hii yote inatuonesha ni jinsi gani ambavyo mnatunyanyapaa watu wa Kusini. Haiwezekani barabara na miradi mingine iwe inakamilika lakini kipande cha barabara hiki cha kilomita chini ya 60 hakikamiliki kwa miaka hii yote. Haiwezekani! Tumeanza ujenzi wa daraja la Malagalasi leo hii limeshakamilika na inamaliziwa barabara. Sisi tuna nini? Mbona hamtuambii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunazungumzia suala la kuongeza kina cha bandari, bandari ichimbwe na iongezwe. Kina cha bandari ya Kilwa *naturally* ni zaidi ya mita 14. Haya tunakwenda kuchimba mashimo, ya nini tunapoteza pesa chungu nzima wakati *natural port* ipo? Hakuna mpango wowote wa kuendeleza Bandari ya Kilwa, tunakuja hapa tunaelezana maneno tu ambayo hayafiki mwisho! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa gesi ambao umeingia nchini kwetu ni sekta mpya, lakini *DMI* haijashiriki kikamilifu kuweza ku-*train* watu wa Mikoa ya Kusini kuweza kushiriki katika uchumi huu. Tunahitaji *support* ya watu kwenda kufanya kazi katika maeneo hayo ya uchimbaji gesi. Wanatoka nchi za nje. Mradi wa ujenzi wa Chuo Kikuu cha *(DMI)* mpaka leo haijulikani na hata kwenye taarifa ya Kamati humu hamna. Sasa tunataka kutekeleza nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa nishati, najua Sera ya Gesi inaandaliwa, lakini kwa *draft* ambayo mimi nimeiona ya mara ya tatu, ni lazima tutenganishe *upstream, midstream* na *downstream*, haiwezekani tukaweka hivi vitu vyote katika eneo moja. Mheshimiwa Waziri, hili unalielewa vizuri, lakini tunaomba mlifanyie kazi ili mtenganishe katika utengenezaji wa sera.

Vilevile, nilitaka nizungumzie kuhusiana na miradi ya umeme ya *REA*. Tumepata orodha leo lakini hii orodha

*[MHE. MURTAZA A. MANGUNGU]*

ambayo imekuja, haioneshi utekelezaji umefikia wapi? Sisi tunatoa gesi na gesi ndiyo inayozalisha umeme na mara nyingine hizi taa zinazowaka humu ndani ni kutokana gesi inayotoka Songosongo. Lakini wananchi wanaozunguka katika yale maeneo, mbona wanapewa ahadi zisizotekelezeka? Kila siku miradi ya umeme itakuja, itakuwa; itakuja, itakuwa; mpaka lini? Watoto wanazaliwa, wanakua mpaka tunawaandikisha shule lakini bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka nilizungumzie ni kwamba kumekuwa na mchakato wa uongezaji wa *tariffs* za umeme. Mimi nakubaliana na hiyo lakini kwa sasa nasema siyo wakati muafaka. Kwanza, tuhakikishe tunazalisha umeme wa kutosha na tuingize umeme wa kutosha kwenye soko ndiyo tuongeze bei au tuangalie namna nyingine. *TANESCO* inajiendesha kwa hasara sasa hivi; kwa kipindi kirefu hatukufanya uwekezaji katika uzalishaji wa umeme; tuna miradi ya umeme ambayo tumeikumbatia na haijaanza; Mradi wa umeme Ngaka mpaka leo hatujui umefikia wapi na hakuna hata maelezo.

Kuna mradi wa umeme wa *Megawatts 400*, bahati nzuri tumepata maelezo ya Kinyerezi, tunajua utakwenda; lakini Mheshimiwa Waziri tuongeze kasi ya utekelezaji wa hii miradi. Wizara hii mmeipokea na mnaifanyia kazi vizuri sana, lazima tuwapongeze, kibinadamu mnafanya kazi vizuri. Lakini tunahitaji kasi zaidi. Tutakapokuwa tumeongeza upatikanaji wa umeme hapo ndiyo tutaangalia namna ambavyo tunaweza tukarekebisha *tariffs* za umeme.

Tumezungumzia suala la mazingira, Wabunge wote wanalalamikia hali ya mazingira, umeme haupatikani wa kutosha, lakini kuna tatizo la ukataji miti kwa ajili ya mkaa. Tuna Makaa ya Mawe, kwa nini hatuanzishi miradi ya kutengeneza *briquettes*? Badala ya kutumia makuni na kuhangaika na Mikaa hii ambayo watu wanahangaika nayo, kwa nini tusitengeneze *briquettes*?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho kabisa ambalo nataka nilizungumzie, ni tatizo la kivuko cha

Kigamboni. Hivi tunavyozungumza, kama kuna mtu ambaye ameangalia taarifa ya habari, lile boti wakati linavusha watu lilikwama katikati. Mamlaka ya Bandari ndiyo iliyotuma Tagu kwenda kuivusha. Wananchi wa Kigamboni wananyanyasika, ukienda pale baiskeli hazipewi kipaumbele, zinaachwa zaidi ya mara tatu, gari zinakwenda tu na ukiangalia kihesabu eneo ambalo gari inachukua na idadi ya baiskeli ambazo zinaingia pale ni bora hata mruhusu kupita baiskeli peke yake, magari yakazunguka maeneo ya Mbagala na maeneo mengine. Wananyanyasika.

Sasa hivi tunavyojua ni kwamba mradi wa utengenezaji wa mabasi ya kwenda kasi, lile eneo lote limeondolewa, watu wanakuja kupanda mabasi eneo la Posta. Mvua ikinyesha pale hakuna mtu ambaye anaweza akawatazama wananchi wanavyonyanyasika. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali mwangalie hili, ni namna gani tunaweza tukawasaidia wenzetu ambao wako kwenye adha kubwa kwa hivi sasa, tulitatue hili tatizo tuweze kuweka miundimbinu inayofa kwa matumizi ya watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nakushukuru Mheshimiwa Mangungu. Namwita Mheshimiwa Juma Njwayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Felix Mkosamali.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niungane na Wabunge wenzangu kuchangia hoja za Kamati hizi mbili.

Awali ya yote naomba kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati kwa mchango wao ulio nadhifu, lakini pia Wajumbe kwa ushiriki na kutuletea vitu vyenye afya vizuri kabisa hapa Bungeni leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuishauri Serikali katika maeneo yafuatayo:-

La kwanza, ni katika suala la ujenzi wa barabara.

*[MHE. JUMA A. NYWAYO]*
Uzoefu nilioupata hivi sasa ni kwamba barabara nyingi zinazotengenezwa hapa nchini baada ya miaka mitano mpaka nane zinaharibika. Lakini nimefanya utafiti usio wa kina sana, jambo ambalo nimekuja kulibaini ni kwamba barabara hizo zinatengenezwa kwa unene ile *thickness* ya sentimeta kama mbili hivi.

Kwa hiyo, naomba kuishauri Serikali kwamba sasa iangalie ni vizuri tuka-*invest* tukatumia gharama kubwa lakini tukajenga barabara ya unene wa sentimeta nne mpaka tano ili uweze kuhimili mizigo mikubwa inayopita kwenye barabara hiyo.

Ninayo mifano hapa; kama barabara ya kwetu kati ya Mnazi Mmoja Lindi hadi Masasi, barabara ile ilijengwa na *BENACO* miaka ya 1970 lakini ukarabati umefanywa mara chache chache sana na kwenye maeneo ambayo kwa kweli imeonekana kuna haja ya kufanya ukarabati au marekebisho kidogo. Lakini imekuwa ikiendelea kuwa imara pomoja na maafa ya mafuriko iliyowahi kupata, imekuwa ya kudumu na ya uhakika tofauti na barabara zinazojengwa sasa. *(Makofi)*

Barabara ya Pugu ilijengwa kabla ya uhuru, sasa ya Mwalimu Nyerere; kabla ya uhuru lakini iko imara, marekebisho yanayofanywa ni madogo. Lakini barabara tunazojenga sasa hata haijaisha kutoka Nangurukuru kwenda Mchinga, yaani marekebisho makubwa tu yamefanywa. Kwanza tulimwambia aanze tena Mkandarasi yule, ameanza tena; lakini ukipita leo bado kuna mashimo mashimo. Naiomba Serikali ibadilishe utaratibu angalau *thickness* ya barabara zetu iwe inayoendana na hali ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni reli ambalo Wabunge wengi waliochangia wameeleza sana. Reli ndiyo itakuwa ukombozi wa matatizo mengi ya kusafirisha mizigo nchini kwetu. Ndiyo njia pekee itakayosaidia kuinua uchumi wetu. Haiwezekani leo mafuta kupeleka Kigoma na Mwanza yapite kwenye barabara hiyo tu. Kama hili la kudumisha reli haliwezekani, basi tuone uwezekano wa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*



kujenga bomba la kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza ili iweze kusaidia maeneo hayo. *(Makofi)*

Vilevile napata shida kidogo, kaka yangu Mheshimiwa Mwakyembe, wewe kaka yangu ile ahadi ya reli kutoka Mtwara hadi Mbambabay, Liganga na Mchuchuma inakwenda legelege. Zipo ahadi kubwa za kubadilisha uwanja wa Mtwara kufanyiwa ukarabati mkubwa.

Bandari ya Mtwara tumeahidiwa hapa kwamba itarekebishwa, na kweli tunaona kuna maendeleo yanafanywa, wako *SHIROMBAG* na Makampuni mengine mengi yanafanya jambo la maana, dalili zinaonekana. Lakini wakati haya yanafanyika, lazima reli hiyo itengenezwe, ijengwe iende sambamba na hali ya Mtwara sasa. Tusifike mahali hiyo ikawa tatizo la kuendelea Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba kuchangia hivi leo ni suala la Makampuni ya Mafuta. Hivi karibuni kumetokea kutoelewana kidogo baadhi ya Watanzania wazawa na Serikali wakilaumu kwamba wazawa hawapewi kipaumbele kwenye sekta ya gesi.

Uzoefu ambao nimejaribu kuutafua kidogo, inaonekana nchi za wenzetu walitengeneza Makampuni yakawa na uwekezaji mkubwa wa Serikali kwamba mchango wa Serikali ulikuwa mkubwa, Makampuni hayo ni ya Serikali, lakini wadau wengine wa nchi hizo wakawekwa kidogo. Kwa mfano, ukienda Brazil kuna *Petrol.Bras*, ukienda India kuna *OG Company Limited,* ukienda Angola, kuna Sonango, kama nayataja vizuri.

Sasa wenzetu wale wamekuwa wakifanya kila aina ya utafiti, kuchimba na kufanya biashara ya mafuta na pia wamepanua mipaka, wanakwenda mpaka nchi nyingine. Kama *Petrol.Bras* iko hapa nchini. Sasa na sisi tutengeneze mazingira hayo, tuwe na Kampuni ya kizalendo itakayofanya mambo ya utafiti, uchambuzi na biashara ya mafuta. Tuipe 20% hivi wazawa waingie humo na sisi 80%. Hii itaondoa mambo ya makelele maana wazawa watajiona ni sehemu

*[MHE. JUMA A. NYWAYO]*
ya mchango mkubwa kwenye Sekta ya Nishati.

Hali iliyopo sasa inaleta manung'uniko yasiyo rasmi na ya yasiyo na sababu.

Pia *TPDC* ipo, mimi nilidhani jambo hili lingefanywa na *TPDC* ikawa rahisi tu. Lakini *TPDC* haijapewa *full mandate*, haijawa *empowered* wa kuweza kufanya haya mambo. Tunaipa nusunusu lakini tuipe sasa uwezo, haki na wajibu wake ili iweze kunusuru nchi yetu na tuondoe hii migogoro isiyo ya lazima kati ya Serikali na wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, pengine siku-*declare* tu *interest* mwanzoni na sasa niseme.

Nilitembelea *TPDC*, kuna chumba muhimu sana kwa tasnia ya madini na nishati kwa ujumla; lakini tuna chumba kimoja kinachotunza *data* za mitetemo na data za miamba na kumbukumbu muhimu za jiolojia ya miamba. Lakini cha ajabu chumba hicho kwanza ni kichafu, kinavuja, hakuna mpango. Kwenye vitu muhimu hivi vya kuendeleza raslimali ya Taifa vinaachwaje hivyo? Serikali iisaidie, Profesa Muhongo, hilo ni lako. Isaidie *TPDC*, kumbukumbu zilizopo na *data* zilizopo pale za kisayansi zitunzwe mahali pazuri ili kesho na keshokutwa watoto wetu wazitumie *data* hizo kwa ajili ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la bomba la gesi. Tumetembelea bomba la gesi kama Kamati, kazi inayofanyika ni kubwa na nzuri. Lakini pamoja na hali hiyo inayoendelea huko, kuna jambo kwamba wananchi bado hawajapata elimu ya kutosha ambayo inawapa mwanga kwamba bomba hilo ni lao na kwamba linachangia uchumi wa nchi yetu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*[MHE. JUMA A. NYWAYO]*

Tunatakiwa kuongeza jitihada ya kutengeneza mazingira; kwanza, Watanzania wajue kwamba bomba hilo ni kwa manufaa ya nchi, lakini pili lionekane tu kwamba bomba lenyewe hili ni mali ya Watanzania. *(Makofi)*

Sambamba na hilo, lile la wafanyakazi, lazima tuhakikishe kwamba kama mkataba ulivyo; wafanyakazi wa Madimba kwenye kiwanda cha kuchakata gesi yenyewe hakuna mtaalamu mzawa hata mmoja aliyeko pale! Waliopo wote ni wageni. Ingawaje kinachofanywa sasa ni kujenga sana majumba, lakini kazi yenyewe kubwa itakayofanana na uchakataji wa gesi bado, lakini tungeanza sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwenye bomba, wapo wale tuliowapa kazi, hakuna *professionals* wa mambo hayo waliopo. Wale wachache tulionao, mimi najua hatuna wataalamu wengi sana kwenye sekta hii, basi wale wachache waliopo tuwatumie ipasavyo wakae pale ili tukipata tatizo lolote wenyewe wawe ni watu wanaoweza kuokoa matatizo yaliyopo. Vinginevyo tutapata matatizo makubwa sana huko mbele ya safari.

Pia nataka kuishauri Serikali kwamba kule ambako tunategemea gesi iwe chanzo cha kusukuma uchumi wetu kutoka Mtwara kwenda kule, wala hazizidi kilomita 50. Kwa nini tusiwekeze kwa kuweka lami pale ili watu wanaokwenda kule iwe rahisi?

Leo tunakwenda kule na mvua zikishanyesha kunakwama, inakuwa aibu! Watu wengi wa nje wanakwenda kuangalia, wanakwenda pia kujifunza mambo mbalimbali ni vizuri tutengeneze urahisi wa mawasiliano ya kufika Madimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kwa sababu kuna Kamati mbili za Miundombinu, naomba Wizara ya Miundombinu, kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuweka lami Mtwara, Tandahimba, Newala hadi Masasi.

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Murtaza Mangungu, sidhani kama yupo na kwa sababu orodha yangu ni ndefu kwa mtu ambaye nikimtaja....

**MBUNGE FULANI:** Yupo.

**NAIBU SPIKA:** Yupo, ahsante sana. Mheshimiwa Murtaza Mangungu atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Njwayo.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninapenda kumweleza ndugu yangu Bwana Peter Serukamba na mzee wangu Mheshimiwa Mwambalaswa, uchumi wa nchi hii aidha kwenda mbele, kurudi nyuma au kukwama, inatokana na utendaji na utekelezaji wao. Hakuna maendeleo ya kiuchumi bila nishati, hakuna maendeleo ya kiuchumi bila kuwa na miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamechangia leo asubuhi wameeleza mambo mengi sana, lakini na mimi ningependa nichangie machache pamoja na kuwiana na mawazo ambayo wao wamekuwa wakiyatoa.

Kwanza, ninastaajabu sana mpango wa ufufuaji wa reli unasuasua, lakini kuna jambo ambalo nimejitahidi sana kufikiria na kufuatilia katika nchi mbalimbali sijapata kuona nimeona Tanzania peke yake; barabara za Tanzania ndiyo barabara pekee ambazo zikinyeshewa na mvua lami yote inatoka. Huu ni utafiti rahisi tu ambao unaweza ukaufanya, mvua ikinyesha barabara zetu za lami, lami zinatoka zinabaki kokoto tupu kesho mashimo yanaendelea! Sijui hili wenzetu mnaliangalia kwa mtazamo gani?

*[MHE. MURTAZA A. MANGUNGU]*

Waheshimiwa Wabunge wa Kusini wamezungumza, kipande cha barabara ya kutoka Ndundu hadi Somanga sasa hivi tuna zaidi ya miaka saba barabara haikamiliki na hii yote mnatuonesha ni jinsi gani ambavyo mnatunyanyapaa watu wa Kusini. Haiwezekani barabara na Miradi mingine iwe inakamilika lakini kipande cha barabara hiki cha kilomita chini ya 60 hakikamiliki kwa miaka yote! Tumeanza ujenzi wa Daraja la Malagarasi leo hii umeshakamilika na inamaliziwa barabara, sisi tuna nini mbona hamtuambii?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunazungumzia suala la kuongeza kina cha bandari, bandari ichimbwe na iongezwe. Kina cha Bandari ya Kilwa *naturally* ni zaidi ya mita 14, haya tunakwenda kuchimba mashimo ya nini tunapoteza pesa chungu nzima wakati *natural port* ipo, hakuna mpango wowote wa kuiendeleza Bandari ya Kilwa, tunakuja hapa tunaelezana maneno tu ambayo hayafiki mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa gesi ambao umeingia nchini kwetu ni sekta mpya, lakini *DMI* haijashiriki kikamilifu kuweza ku-*train* watu wa Mikoa ya Kusini kuweza kushiriki katika uchumi huu. Tunahitaji *support* ya watu kwenda kufanya kazi katika maeneo hayo ya uchimbaji gesi, wanatoka nchi za nje. Mradi wa Ujenzi wa Chuo Kikuu cha DMI mpaka leo haijulikani na hata kwenye Taarifa ya Kamati humu hamna. Sasa tunataka kutekeleza nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa nishati, najua Sera ya Gesi inaandaliwa, lakini kwa *draft* ambayo mimi nimeiona ya mara ya tatu ni lazima tutenganishe *upstream, midstream* na *downstream*, haiwezekani tukaweka hivi vitu vyote katika eneo moja. Mheshimiwa Waziri, hili unalielewa vizuri, lakini tunaomba mlifanyie kazi ili mtenganishe katika utengenezaji wa hii Sera.

Vilevile, nilitaka nizungumzie kuhusiana na Miradi ya Umeme ya *REA.* Tumepata orodha leo lakini hii orodha ambayo imekuja haioneshi utekelezaji umefikia wapi. Sisi

tunatoa gesi na gesi ndiyo inayozalisha umeme na mara nyingine hizi taa zinazowaka humu ndani ni kutokana gesi inayotoka Songosongo. Wananchi wanaozunguka katika yale maeneo mbona wanapewa ahadi zisizotekelezeka? Kila siku Miradi ya Umeme itakuja itakuwa, itakuja itakuwa, mpaka lini? Watoto wanazaliwa, wanakua mpaka tunawaandikisha shule lakini bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka nilizungumzie, kumekuwa na mchakato wa uongezaji wa *tariffs* za umeme. Mimi nakubaliana na hilo, lakini kwa sasa nasema siyo wakati mwafaka. Kwanza, tuhakikishe tunazalisha umeme wa kutosha na tuingize umeme wa kutosha kwenye soko ndiyo tuongeze bei au tuangalie namna nyingine. *TANESCO* inajiendesha kwa hasara sasa hivi kwa kipindi kirefu hatukufanya uwekezaji katika uzalishaji wa umeme. Tuna Miradi ya Umeme ambayo tumeikumbatia na haijaanza. Mradi wa Umeme Ngaka mpaka leo hatujui umefikia wapi na hakuna hata maelezo. Kuna Mradi wa Umeme wa *megawatts 400* bahati nzuri tumepata maelezo ya Kinyerezi tunajua utakwenda, lakini Mheshimiwa Waziri tuongeze kasi ya utekelezaji wa hii Miradi. Wizara hii mmeipokea na mmeifanyia kazi vizuri sana, lazima tuwapongeze kibinadamu mnafanya kazi vizuri lakini tunahitaji kasi zaidi. Tutakapokuwa tumeongeza upatikanaji wa umeme hapo ndiyo tutaangalia namna ambavyo tunaweza tukarekebisha *tariffs* za umeme.

Tumezungumzia suala la mazingira, Wabunge wote wanalalamikia hali ya mazingira, umeme haupatikani wa kutosha na ukataji mkaa. Tuna makaa ya mawe kwa nini hatuanzishi Miradi ya kutengeneza *briquettes*? Badala ya kutumia kuni na kuhangaika na mikaa hii ambayo watu wanahangaika nayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho kabisa ambalo nataka nilizungumzie ni tatizo la Kivuko cha Kigamboni. Hivi tunavyozungumza kama kuna mtu ameangalia taarifa ya habari, lile boti wakati linavusha watu lilikwama katikati. Mamlaka ya Bandari ndiyo iliyotuma

*[MHE. MURTAZA A. MANGUNGU]*

tagi kwenda kuivusha. Wananchi wa Kigamboni wananyanyasika, ukienda pale baiskeli hazipewi kipaumbele zinaachwa zaidi ya mara tatu, magari yanakwenda tu na ukiangalia kihesabu eneo ambalo gari linachukua na idadi ya baiskeli ambazo zinaingia pale ni bora hata mruhusu kupita baiskeli peke yake magari yakazunguka maeneo ya Mbagala na maeneo mengine.

Sasa hivi tunavyojua ni kwamba, Mradi wa Utengenezaji wa Mabasi ya kwenda kasi, lile eneo lote limeondolewa watu wanakuja kupanda mabasi eneo la Posta. Mvua ikinyesha hakuna mtu ambaye anaweza akawatazama Wananchi wa kule wanavyonyanyasika. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali liangalieni hili ni namna gani ambavyo tunaweza tukawasaidia wenzetu ambao wapo kwenye adha kubwa kwa hivi sasa. Tulitatue hili tatizo tuweze kuweka miundombinu inayofaa kwa matumizi ya watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mangungu. Mheshimiwa Juma Njwayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Felix Mkosamali!

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niungane na Wabunge wenzangu kuchangia hoja za Kamati hizi mbili.

Awali ya yote, naomba kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati kwa mchango wao ulio nadhifu, lakini pia wajumbe kwa ushiriki na kutuletea vitu vyenye afya, vizuri kabisa hapa Bungeni leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuishauri Serikali katika maeneo yafuatayo:-

La kwanza, ni katika suala la ujenzi wa barabara. Uzoefu nilioupata hivi sasa unaonesha kwamba, barabara

nyingi zinazotengenezwa hapa nchini, baada ya miaka mitano mpaka minane zinaharibika. Nimefanya utafiti usio wa kina sana, jambo ambalo nimelibaini ni kwamba, barabara hizo zinatengenezwa kwa unene ile *thickness* ya sentimeta kama mbili hivi. Kwa hiyo, naomba kuishauri Serikali kwamba, sasa iangalie, ni vizuri tuka-*invest* tukatumia gharama kubwa lakini tukajenga barabara ya unene wa sentimeta nne mpaka tano iweze kuhimili mizigo mikubwa inayopita kwenye barabara. Ninayo mifano, barabara ya kwetu kati ya Mnazi Mmoja Lindi hadi Masasi, barabara ile ilijengwa na *BENACO* miaka ya 70, ukarabati umefanywa mara chache sana na kwenye maeneo ambayo kuna haja ya kufanya ukarabati au marekebisho kidogo. Imeendelea kuwa imara pomoja na maafa ya mafuriko iliyowahi kupata barabara hiyo, lakini imekuwa ya kudumu na ya uhakika tofauti na barabara zinazojengwa sasa.

Barabara ya Pugu ambayo hivi sasa inaitwa Mwalimu Nyerere, ilijengwa kabla ya uhuru lakini ipo imara, marekebisho yanayofanywa ni madogomadogo. Barabara tunazojenga sasa hata haijaisha kutoka Nangurukuru kwenda Mchinga, marekebisho makubwa tu yamefanywa. Kwanza, tulimwambia aanze tena Mkandarasi yule, ameanza tena ukipita leo bado kuna mashimo mashimo. Naiomba Serikali ibadilishe utaratibu angalau *thickness* ya barabara zetu iwe inayoendana na hali ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba, Wabunge wengi waliochangia wameelezea sana suala la reli. Reli ndiyo itakuwa ukombozi wa matatizo mengi ya kusafirisha mizigo nchini kwetu, ndiyo njia pekee itakayosaidia kuinua uchumi wetu. Haiwezekani leo mafuta kupeleka Kigoma, Mwanza, yapite kwenye barabara hiyo tu. Kama hili la kudumisha reli haliwezekani, basi tuone uwezekano wa kujenga bomba la kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza ili liweze kusaidia maeneo hayo. *(Makofi)*

Vilevile ninapata shida kidogo, kaka yangu Mheshimiwa Mwakyembe, ile ahadi ya reli kutoka Mtwara

hadi Mbambabay, Liganga na Mchuchuma inakwenda legelege. Zipo ahadi kubwa za kubadilisha Uwanja wa Mtwara kufanyiwa ukarabati mkubwa, Bandari ya Mtwara tumeahidiwa hapa kwamba itarekebishwa na kweli tunaona kuna maendeleo yanafanywa wako SHULUMBAGA na makampuni mengine mengi yanafanya jambo la maana, dalili zinaonekana. Wakati haya yanafanyika, lazima reli hiyo itengenezwe na ijengwe iende sambamba na hali ya Mtwara, tusifike mahali hiyo ikawa tatizo la kuendelea kwa kule Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninaloomba kuchangia hivi leo ni suala la makampuni ya mafuta. Hivi karibuni kumetokea kutoelewana kidogo, baadhi ya Watanzania wazawa na Serikali wakilaumu wazawa hawapewi kipaumbele kwenye Sekta ya Gesi. Uzoefu ambao nimejaribu kuutafuta kidogo, inaonekana nchi za wenzetu walitengeneza makampuni yakawa na uwekezaji mkubwa wa Serikali, mchango wa Serikali ulikuwa mkubwa, makampuni hayo ni ya Serikali lakini wadau wengine wa nchi hizo wakawekwa kidogo. Kwa mfano, ukienda Brazil kuna *Petrobrass*, ukienda India kuna *OG Company Limited,* ukienda Angola kuna Sonango, kama nayataja vizuri.

Sasa wenzetu wamekuwa wakifanya kila aina ya utafiti, kuchimba na kufanya biashara ya mafuta na pia wamepanua mipaka wanakwenda mpaka nchi nyingine kama *Petrobrass* ipo hapa nchini. Sasa na sisi tutengeneze mazingira hayo, tuwe na kampuni ya kizalendo itakayofanya mambo ya utafiti, uchambuzi na biashara ya mafuta, tuipe 20% hivi wazawa waingie humo na sisi 80%. Hii itaondoa kelele maana wazawa watajiona ni sehemu ya mchango mkubwa kwenye Sekta ya Nishati. Hali iliyopo sasa inaleta manung'uniko yasiyo na sababu.

*TPDC* ipo, mimi nilidhani jambo hili lingefanywa na *TPDC* ikawa rahisi tu, lakini *TPDC* haijapewa *full mandate*, haijawa *empowered* kuweza kufanya haya mambo, tunaipa nusunusu. Tuipe sasa uwezo, haki na wajibu wake

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)


iweze kunusuru nchi yetu na tuondoe hii migogoro isiyo ya lazima kati ya Serikali na Wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, pengine siku-*declare* tu *interest* mwanzoni sasa niseme. Nilitembelea *TPDC*, kuna chumba muhimu sana kwa tasnia ya madini na nishati kwa ujumla, lakini tuna chumba kimoja kinachotunza *data* za mitetemo na *data* za miamba na kumbukumbu muhimu za jiolojia ya miamba. Cha ajabu chumba hicho kwanza ni kichafu, kinavuja, hakina mpango, kwenye vitu muhimu vya kuendeleza rasilimali ya Taifa vinaachwaje hivyo? Serikali iisaidie, Mheshimiwa Profesa Muhongo hilo ni lako, isaidie *TPDC*, kumbukumbu zilizopo na *data* zilizopo za kisayansi zitunzwe mahali pazuri ili kesho na keshokutwa watoto wetu wazitumie *data* hizo kwa ajili ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la bomba la gesi. Tumetembelea bomba la gesi kama Kamati, kazi inayofanyika ni kubwa na nzuri. Pamoja na hali hiyo inayoendelea huko, Wananchi bado hawajapata elimu ya kutosha ambayo inawapa mwanga kwamba bomba hilo ni lao na litachangia uchumi wa nchi yetu. Tunatakiwa kuongeza jitihada ya kutengeneza mazingira, kwanza, Watanzania wajue kwamba bomba hilo ni kwa manufaa ya nchi, lakini pili lionekane ni mali ya Watanzania.

Sambamba na hilo, lile la wafanyakazi lazima tuhakikishe kama mkataba ulivyo, wafanyakazi pale Madimba kwenye kiwanda cha kuchakata gesi yenyewe, hakuna mtaalamu mzawa hata mmoja aliyepo pale, waliopo wote ni wageni. Ingawa kinachofanywa sasa ni kujenga sana majumba, kazi yenyewe kubwa itakayofanana na uchakataji wa gesi bado, lakini tungeanza sasa. Hata kwenye bomba wapo wale tuliowapa kazi tu, hakuna *professionals* wa mambo hayo waliopo. Wale wachache tulionao, mimi najua hatuna wataalamu wengi sana kwenye sekta hii lakini basi wale wachache waliopo tuwatumie ipasavyo, wakae pale ili

*[MHE. JUMA A. NJWAYO]*

tukipata tatizo lolote waokoe matatizo yaliyopo; vinginevyo, tutapata matatizo makubwa sana huko mbele ya safari.

Nataka kuishauri Serikali kwamba, sasa kule ambako tunategemea gesi iwe chanzo cha kusukuma uchumi wetu kutoka Mtwara kwenda kule, wala hazizidi kilomita 50; kwa nini tusiwekeze kwa kuweka lami ili watu wanaokwenda kule iwe rahisi? Leo tunakwenda kule na mvua zikishanyesha unakwama, inakuwa aibu! Watu wengi wa nje wanakwenda kuangalia, wanakwenda pia kujifunza mambo mbalimbali, ni vizuri tutengeneze urahisi wa mawasiliano ya kufika Madimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kwa sababu kuna Kamati mbili za Miundombinu, naomba Wizara ya Miundombinu kuna ahadi ya Rais ya kuweka lami Mtwara, Tandahimba, Newala hadi Masasi. Tumetenga shilingi bilioni 3.2 kwenye bajeti iliyopita kwa ajili ya upembuzi yakinifu, lakini mambo yanaenda polepole, wapiga kura wetu wa maeneo yale wanatulalamikia sana jambo hili liende kwa haraka. Mheshimiwa Rais aliahidi alipokuwa Newala, alipokuwa Tandahimba na alipokuwa Nanyamba, tusimdhalilishe Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuzungumzia kidogo kuhusu *REA, REA* inafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Felix Mkosamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia hoja zilizowasilishwa na Wenyeviti wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki chache zilizopita tulisikia Waziri wa Ujenzi anasema kuna malori yanapita na

*[MHE. FELIX F. MKOSAMALI]*
mizigo mikubwa sana, baada ya muda mfupi yale malori yakaruhusiwa kuendelea kupita na aliyeyaruhusu ni Waziri Mkuu. Sasa tulitakiwa tufahamu, je, huyu Waziri wa Ujenzi alitoa kauli ile kwamba malori yanayopita yana uzito yanaharibu barabara zitaisha Waziri wake Mkuu akiwa hajui; na kama Waziri Mkuu wake alikuwa anajua, kwa nini ameruhusu malori haya yaendelee kupita?

Sisi tunamheshimu sana Mheshimiwa Magufuli, kwamba huwa ni mtu wa *principle.* Sasa kama ni mtu wa *principle* na anafahamu kabisa barabara zinaendelea kubonyea; kwa nini hakujiuzulu baada ya kupingwa hoja yake ambayo alikuwa anaisimamia kwamba barabara zinaisha baada ya muda mfupi? Sasa amekataliwa na bosi wake na malori yanaendelea kupita; kama kweli ni mtu wa *principle* ambaye amekuwa anasema wanaojenga kwenye barabara sijui hawatalipwa na nini na yeye afuate *principle* hiyo, amejibu amesimamia vizuri amesema magari yanayozidisha mizigo hayatapita, lakini amekataliwa yanapita! Sasa atuoneshe msimamo huo aliokuwa anatuonesha. Asipofanya hivyo, tutajiuliza huo ukali sasa ukoje, ni msimamo wa kweli ama ni kitu gani? Tutajua ni nguvu ya soda! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepewa hapa orodha ya Miradi ya Umeme Vijijini na wakati wa Bunge la Bajeti tulipewa pia orodha hii, lakini vijiji hivi hakuna ambacho kimefanyika. Kule kwetu mimi sijaona ambacho kimefanyika toka tumepitisha bajeti mwezi wa sita, sijaona vijiji ambavyo mlisema vitajengwa Kibondo hakuna ambacho kimefanyika, sijui hata nani anajibu hapa maana hii ni kuonesha orodha au ni vitendo vya namna gani?

Profesa tunakuheshimu, lakini twende kwenye utekelezaji, toka mwezi wa sita mpaka leo kitu gani kimefanyika Kibondo? Kwenye Taarifa hii inasema Miradi ya *Phase* ya Kwanza inaisha Desemba, 2013, lakini kuna maeneo watu wameomba kuunganishiwa umeme zaidi ya mwaka mzima hawajaunganishiwa. Hiyo Miradi itakamilika vipi wakati kila siku Wananchi wanalalamika hakuna nyaya,

*[MHE. FELIX F. MKOSAMALI]*

hakuna nguzo, hakuna nini na Miradi yenyewe ukitazama ramani mfano ni Mradi wa Kibondo, ukitazama ramani ambayo Kampuni ya NAMIS ilipaswa kujenga hawajafika maeneo yote. *(Makofi)*

Sasa Miradi hii inakamilika namna gani na hawa watu wa Makampuni ambao mnawapatia *tender* wameshazowea wanajua wana-*play* na ninyi kwamba si muda utaisha; kwa hiyo, kila Mwananchi akienda anaambiwa hakuna mita, hakuna nguzo, hakuna nini, sasa mtueleze mnaifunga vipi hii *project* wakati bado maeneo haya hayajakamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepitisha bajeti ya ujenzi wa barabara mwezi wa sita kutoka Nyakanazi kwenda Kigoma, tukaambiwa zitatumika na fedha pia zilizopitishwa mwaka jana, *tender* imetangazwa tarehe 23 Mei mpaka leo hakijafanyika kitu chochote. Sasa tuambiwe hizo fedha zipo wapi, *tender* inachukua muda gani kutangazwa na kufunguliwa na kukabidhiwa?

Tujulishwe, juzi tumemwuliza hili swali hapa Waziri Mkuu barabara ile vipi; amezunguka Mkoa mzima wa Kigoma Wananchi wanamwuliza vipi barabara hii ahadi ya toka mwaka tisini na ngapi sijui themanini sijui mwaka gani, vipi? Hatutaki kusema uongo tunataka vitendo. Mambo haya Mawaziri wa Wizara hizi wengi wanajitahidi sasa lazima tujiulize shida ni pesa au nini kwa sababu tunawaamini? Mawaziri wengi hawa tunawaamini wana uwezo wa kufanya kazi vizuri wote wa Wizara zote wanajitahidi, *what is the problem* kama ni Wizara ya Fedha Mheshimiwa Mwakyembe tuambie tunajua una uwezo, tuambie hapa mimi ningeweza kufanya hivi kwa muda fulani lakini shida ni pesa na zimekwenda wapi kwa nini hazipatikani, tujulishe.

La sivyo na wewe tutakuwajibisha tutasema huyu kama ambavyo wameanza watu kukuchana hapa na wewe utaingizwa huko, utaonekana na wewe hauna *principle.* Lazima tujue tatizo ni nini, wewe upo ndani ya

*Cabinet,* una-*collective responsibilities* mnazungumza na Waziri wa Fedha na wengine lakini kazi hazifanyiki, reli haifufuliwi, tatizo ni nini kama ni pesa tuambie nani ameshindwa kukusanya kodi? Aliyeshindwa achomoke atupishe sisi tuendeleze nchi yetu kuliko kufanya mambo ya ubabaishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Felix Mkosamali. Mheshimiwa Munde Tambwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Makilagi!

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia. Nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wote wanaohusika na mjadala huu na vilevile nawapongeza Wenyeviti wa Kamati wote waliowasilisha Taarifa zao hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara ya Miundombinu kwa kutupatia Uwanja wa Ndege Mkoa wa Tabora. Tulikuwa tuna matatizo sana, hatuna barabara, hatuna reli, hatuna uwanja wa ndege, *at least* hiyo ndege sasa hivi inatua Tabora; tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliambiwa kuna ukarabati wa vichwa vya treni unafanyika, kule kwetu Tabora tuna tatizo sana la usafiri, reli ni uti wetu wa mgongo sisi watu wa Tabora, Mpanda, Kigoma na kadhalika. Mheshimiwa Mwekyembe, Bunge lililopita alituambia vichwa vinakarabatiwa na kuna vichwa vipya vitakuja. Leo tena tumeona vinakarabatiwa. Namwomba Mheshimiwa Mwekyembe wakati anajibu tujue vichwa hivi vitakuja lini, mabehewa haya yanayokarabatiwa yatakuja lini, tuna uhaba mkubwa hali siyo nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Mkoa wa Tabora wana imani sana na Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, tuna imani na utendaji wake wa kazi ni mzuri,

*[MHE. MUNDE T. ABDALLAH]*

anafanya kazi vizuri, lakini tunaomba katika hili asituangushe. Tuna imani naye sana kwamba, tutapata hivi vichwa vya treni kwa wakati isipokuwa atuambie ni lini kwa sababu watu wana shida kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanakaa njiani mpaka siku nne kutoka Dar es Salaam kwenda Tabora, hawana uwezo wa kupanda mabasi, nauli ni kubwa. Hiki ni kipindi cha likizo, hawawezi kupanda mabasi wala ndege, wanategemea usafiri wa reli, wanakaa njiani siku nne na watoto wadogo, watu wanateseka sana, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo kwa umakini mkubwa sana, hali ni mbaya.

Mheshimwa Naibu Spika, niseme pia hata vifaa kwetu ni bei kubwa sana, unakuta *cement* mfuko mpaka shilingi 22,000 kwa sababu ya usafiri wa barabara. Tungekuwa na reli vifaa hivi vingeshuka bei sana, tunapata shida sana, tunaambiwa Tabora na Kigoma hakuna maendeleo tunapataje maendeleo wakati vifaa bei kubwa? Mtu anajenga Dar es Salaam kwa *cement* ya shilingi 12,000 kwa mfuko, mimi najenga kwa *cement* ya shilingi 22,000; vipi tutakuwa sawa? Tunaomba Serikali ituangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niongelee suala zima la barabara. Barabara kwetu siyo nzuri, tumehangaika sana, tumeahidiwa barabara ingekamilika mwaka 2012 haikukamilika, tukaambiwa itakamilika mwaka huu haijakamilika. Juzi tu barabara ilikuwa haipitiki, mvua imenyesha barabara ya Nzega - Tabora imekatika imejaa maji, nimetuma picha kwenye *WhatsApp,* utasikitika akina mama na watoto wameteremshwa kwenye mabasi wamekaa kwenye maji yanafika kiunoni, hali ni mbaya sana, tunaomba Serikali ituangalie kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wakandarasi walipwe pesa ambazo hawajalipwa waweze kujenga barabara. Naamini uwezo upo wa kuwalipa mbona Mikoa

*[MHE. MUNDE T. ABDALLAH]*
mingine barabara zinapitika, mbona Mikoa mingine wanasafiri kwa lami moja kwa moja na *baloon* mtu anatoka Mtwara mpaka Dar es Salaam, mtu anatoka Dar es Salaam mpaka Mwanza na *baloon* tu; sisi ni mpaka lini jamani? Tunaiomba Serikali ituangalie kwenye suala zima la barabara hali yetu siyo nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala zima la usafirishaji wa mizigo. Sisi pia tunasafirisha tumbaku lakini Kigoma wenzetu wanalima sana mazao ya chakula na mazao mengine, tunatumia magari gharama zinakuwa kubwa, kunufaika kwetu kunakuwa kudogo sana. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali iangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ni uchumi. Tumeona nchi nyingi zimeendelea kutokana na reli, India imeendelea sana kutokana na reli, South Africa imeendelea sana kutokana na reli. Naamini hata sisi Tanzania reli yetu itakapotengenezwa uchumi wetu utapanda kwa kiasi kikubwa. Tukumbuke Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, ameweka historia katika nchi hii, amejenga kilometa nyingi za lami kuliko Rais yeyote Tanzania. *(Makofi)*

Naomba niseme kuwa, itabakia kuwa historia kwa sababu hizi barabara zitaharibika zote, malori ni mazito sana, mizigo inapita kila siku. Tuangalie Waheshimiwa Wabunge kila siku tunaenda Dar es Salaam, Dodoma, kila siku barabara hiyo inatengenezwa ni lini haitengenezwi? Kila siku ile barabara lazima ikarabatiwe kwa sababu ya mizigo ni mikubwa. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iangalie suala zima la reli. Naomba Mheshimiwa Waiziri na Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu watakapokuja hapa kwenye Bajeti waje na hela nzuri itakayofaa kukarabati reli. Kila siku imekuwa ni hadithi tu ambazo hazifikii mwisho. Mheshimiwa Waziri nirudie, tuna imani sana na wewe, tunakufahamu ni mchapa kazi, kwa hiyo, katika hilo tunakuomba sana utusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sheria moja ya *road toll,* kila mtu anaponunua mafuta anakatwa asilimia fulani

inaenda kutengeneza barabara. Mimi nakubali lakini tuangalie hali ilivyo kwenye reli, hali ya reli ni mbaya sana, lakini bado tunakatwa hiyo asilimia inapelekwa kutengenezea barabara; nadhani siyo *fair,* hizi ni sheria siyo Bibilia, siyo Msahafu, zinabadilishika. Naomba sasa Serikali ije na Muswada, *otherwise,* sisi Wabunge tutakuja na hoja binafsi tukatae kukatwa hiyo *road toll* kwenye mafuta ya reli ila hizo hela za kukatwa kwenye mafuta ya reli zikakarabati reli, hali ni mbaya sana, watu wanalala njiani siku nne mpaka tano. Sisi tunachangia *road toll,* hela zetu za mafuta zinakatwa mamilioni ya pesa yanatoka kwenye reli yanapelekwa kwenye Mfuko wa Barabara, naomba Sheria hiyo kwa sasa irekebishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nirudi kwenye nishati na madini, niongelee suala la nishati. Mheshimiwa Naibu Waziri Simbachawene, alishawahi kuja kule Tabora Manispaa, nampongeza sana. Alitembelea kwenye vijiji vyetu ambavyo havina umeme, akatuahidi tutaletewa umeme. Vilevile bajeti iliyopita nimeona tumetengewa fedha kwa ajili ya kupata umeme huo kwenye vijiji vya Ifucha, Itonjanda, Misha, Kazima, Kakola, Inala na kadhalika, lakini mpaka leo umeme huo haujawaka. Cha kusikitisha zaidi, kuna vijiji vingine kama Kazima na Itonjanda nyaya za umeme zinapita pale, umeme mkubwa, lakini watu hawana umeme. Inasikisha sana, namuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* atuambie ule umeme kule Tabora utawaka lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala moja ambalo mimi binafsi kwa sababu hili Bunge lina heshima zake, naomba niongee kidogo tu kwa sababu sisi ni Wabunge. Naomba nichukue fursa binafsi kuongea na Wananchi wangu wa Tabora kwamba, mimi Munde niliambiwa nimejenga Zahanati kule Tabora, nimelipwa pesa nyingi kule Tabora, lakini nawaambia Wananchi wangu wa Tabora kwamba, sijajenga Zanati, sijalipwa hata senti tano, mwenye ushahidi wowote alete hapa Bungeni. Nawaomba watulie na hizo ni vuguvugu za siasa. Vilevle nawaambia kuwa mwaka 2015 nitagombea na kwa nguvu za Mwenyezi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Mungu, nitapata Ubunge. Kwa hiyo, hiyo ni siasa tu inaendelea hapa Bungeni, sijajenga na hamna ushahidi wowote wa kuthibitisha jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Munde Tambwe. Umetuambia utagombea lakini hujatuambia unagombea wapi; sijui unagombea Kongwa, maana Mtani wangu huyu anaweza akagombea hata Kongwa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nataka kuwataarifu kwamba, Mheshimiwa John Magufuli, Waziri wa Ujenzi, hayupo humu Bungeni, imemlazimu kurudi nyumbani amepatwa na msiba wa mama mkwe wake. Kwa hiyo, hayupo kwa sababu ya msiba ambao ameupata na si sababu nyingine. Ningeomba kuwataarifuni.

Tunaendelea na michango, Mheshimiwa Amina Makilagi!

**MHE. AMINA N. MAKILAGI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hii mada iliyoko mbele yetu na hizi Wizara nne kwa ajili ya maendeleo yetu na Uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nianze kuipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kazi nzuri sana na njema inayofanya ya kuweka miundombinu ya barabara. Nimetembea nchi nzima nimejionea mwenyewe, Serikali hii imefanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha Wananchi wa Tanzania wanapata miundombinu ya barabara ili wawe na maisha bora kwa kila Mtanzania. Vilevile naomba naipongeza Serikali kwa kuboresha sana huduma za umeme vijijini. Ni ukweli usiopingika kwamba, wale walio macho wameona na walio na masikio wamesikia, Serikali yetu ipo kazini inafanya kazi nzuri sana, pamoja na miundombinu ya mawasiliano,

uchukuzi, bandari na reli. Kwa kweli naomba niipongeze sana Serikali yetu ya CCM, hapa ninachoweza kusema Serikali iongeze bidii kwa sababu Wananchi wa Tanzania tuliwaahidi kupitia Ilani yetu ya CCM kwamba, wakichague Chama cha Mapinduzi na kufikia mwaka 2015 maisha bora ya Watanzania yatafikiwa kwa kuwawekea miundombinu ili waweze kuimarisha uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi naomba sasa nitoe ushauri kwa mambo machache niliyochagua kuyazungumzia na leo nitajikita katika Jimbo langu la Mkoa wa Mara, katika Jimbo langu la Mkoa wa Tabora na katika Jimbo langu Mkoa wa Ruvuma. Majimbo mengine yaliyobaki leo mtanisamehe nitaongea katika mada nyingine zitakazofuata siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na Mkoa wa Mara na hapa naanza kwa kuishukuru sana Serikali yetu ya CCM kwa kukarabati barabara yetu ya lami kutoka Mwanza mpaka Musoma kwa kiwango cha lami. Nilikuwepo huko juzi, kazi inaendelea vizuri sana, naomba kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Mara na Mwanza, kuishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri inayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu tangu, nilipokwenda Mkoa wa Mara mwezi wa tano na juzi kabla ya kuja Bungeni hapa nilikuwa Jimboni, nimekuta kipande cha kutokea pale Lamadi mpaka Bunda kipo kama nilivyokiacha mwezi wa tano. Ninapenda kujua Mheshimiwa Waziri akisimama hapa atuambie shida ni nini; kama shida ni mkandarasi aliyewekwa hana uwezo aondoke, kama ni fedha hazipo za kumlipa alipwe, kwa sababu ile barabara ya kutoka Mwanza mpaka Musoma ilikuwa ya kiwango cha lami. Serikali imebandua lami ile na kutuwekea lami mpya, sasa Wananchi wanapoendelea kuhangaika kupita katika vichochoro na mvua zinanyesha, wanahangaika wanataabika, mabasi yanayotoka mpaka Kenya maeneo mbalimbali ya nchi yetu tunateseka. Naomba leo Mheshimiwa Waziri atoe majibu na Wananchi wa Mwanza na Mara wasikie hii barabara itakamilika lini

na kwa sababu hiki kipande ni cha muda mrefu, naona juzi wamekiacha wamerukia tena Musoma Mjini na Musoma Mjini wameanza kuparua, sioni lami inaendelea kuwekwa; hapa shida ni nini? Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kazi nzuri sana inayofanywa ya kutupatia barabara ya lami kuanzia Makutano – Mugumu – Nyamuswa mpaka Loliondo; nimekuta kazi imeanza, wameanza kung'oa visiki na kusafisha barabara.

Kilichonishangaza pia, tangu nilipotoka mwezi Februari nimekuta wanang'oa visiki na juzi nimeenda nimekuta bado wanang'oa visiki. Sasa swali langu najiuliza; huyu Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete ameahidi ile barabara ikifika mwaka 2015 itakuwa imekamilika kwa kiwango cha lami; kama visiki vinang'olewa miezi tisa, hii barabara tutaipata lini? Ninamwomba Mheshimiwa Waziri akisimama hapa atupe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni kubwa, mkandarasi mmoja hawezi. Ninaomba wawekwe makandarasi wa kutosha, mmoja aanzie Makutano mpaka Nyamuswa kwa Mheshimiwa Wasira, mwingine aanzie Nyamuswa mpaka Serengeti kwa Mheshimiwa Kebwe na mwingine aanzie Longido mpaka Serengeti, barabara zikutane, kama walivyofanya katika maeneo mengine.

Mheshikiwa Naibu Spika, naizungumzia barabara hii kwa sababu wazo la kuijenga kwa kiwango cha lami ni la Baba wa Taifa. Baba wa Taifa hakuwa mbinafsi, aliangalia Watanzania wote. Sasa barabara zake zote wa Mkoa wa Mara hakuna lami, ukiachia moja inayotoka Mwanza kuelekea Kenya. Ninaomba Mheshimiwa Waziri akisimama atupe ukweli wa hii barabara na aiwekee mkakati na fedha tulizotengewa shilingi bilioni tatu hazitoshi. Itafutwe pesa popote, kama ni ya mkopo, kama ni ya kutoa wapi; hii fedha iongezwe na Barabara yetu ya Musoma mpaka Serengeti ijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara nyingine inayotoka Kisorya, kilomita 50, Kisorya mpaka Bunda nayo tumepewa shilingi bilioni mbili. Shilingi bilioni mbili haziwezi kujenga barabara, lakini hata ile barabara kasi yake imeshanitia mashaka, kwa sababu naona bado wanang'oa visiki, kazi haijaanza. Ombi langu, fedha ziongezwe na kasi iongezwe, ikiwezekana pia na makandarasi hapa waongezeke, badala ya kuwa mmoja wawe wawili na kama mkandarasi anadai, alipwe fedha zake kazi ianze na Wanamara nao wajivunie rasilimali za Taifa ambazo wamezivuna kabla hata ya Uhuru, nao walichangia sana kuleta Uhuru wa nchi yetu mpaka sasa tunaona matunda yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ya Mkoa wa Mara ni barabara ya kihistoria. Barabara ya kihitoria hii inayoitwa ni Barabara ya Musoma – Busekera, Baba wa Taifa aliwahi kwenda kujificha mafichoni huko Visiwani Kome, Visiwani Lukuba; kwenda kupanga mipango ya kuikomboa nchi yetu na Mataifa mengine. Ni barabara ambayo yeye mwenyewe alitoa wazo kwamba, inatuunganisha kiuchumi Wananchi wa Mkoa wa Mara na wengine kwa sababu kule kuna Ziwa. Ni barabara ni ya muda mrefu sana kabla ya Uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha ni kwamba, pamoja na kwamba ni wazo alilolitoa Baba wa Taifa la kuanzisha barabara ya lami, alikuja Mheshimiwa Rais Mkapa mwaka 1995 wakati wa Kampeni, alitoa ahadi kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami. Amekuja tena mwaka 2000 akihutubia mkutano pale Busekela, akaahidi kwamba barabara hii itajengwa kwa lami. Akaja tena mwaka 2005 Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, akihutubia Wananchi wa Mkoa wa Mara kupitia Mkutano wa Hadhara pale Musoma Mjini Nyakato, amerudia tena mwaka 2010, ahadi za Viongozi mara nne, anaahidi hii barabara itajengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu aliyonipa Mheshimiwa Dkt. Magufuli wakati akijibu swali langu katika

Bunge lililopita hayakunirisha. Maana alisema kwamba, hii barabara imetengewa kilometa tano kwa ajili ya barabara ya lami. Kilomita tano, haiwezi kwisha leo. Ombi langu nilikuwa nataka leo Wananchi wa Mkoa wa Mara wasikie barabara hii itajengwa lini kwa kiwango cha lami, kwa sababu ni mawazo ya Mwalimu, ni ahadi ya Mkapa, ni ahadi ya Kikwete? Wananchi wa Mara wote wananisikia na hasa Wananchi wa Busekela Musoma Vijijini wananisikiliza zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie Viwanja vya Ndege. Mkoa wa Mara ni mwanzilishi wa nchi yetu. Mkoa wa Mara ni Mkoa ambao inafanyika kazi nzuri, lakini kwenye suala la Kiwanja cha Ndege tumesahaulika. Mkoa wa Mara Kiwanja chake cha Musoma kipo katikati ya watu, kipo mjini. Hivi ninavyozungumza, hakuna ndege inayotua, uwanja umefungwa. Nikiwa binti mdogo tulitenga uwanja kule Nyasurura Musoma Vijijini, Wilaya ya Butiama, mpaka leo miaka 30 iliyopita, uwanja upo, Wananchi hawafanyi chochote, tunasubiri Uwanja wa Ndege. Leo nataka nipate majibu, huu Uwanja wa Musoma katika Mkoa wa Mara unajengwa kwa ajili ya Uchumi wa Taifa na hasa ukizingatia Mkoa wa Mara unazungukwa na Hifadhi ya Taifa, lakini pia tuna Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Uwanja wa Serengeti. Uwanja wa Wilaya ya Serengeti ni ahadi pia ya Mheshimiwa Rais na wawekezaji wetu wamekubali kutenga shilingi bilioni tano na zimeshatoka. Kinachosubiriwa hapa eti ni Wataalam wa kwenda kuangalia masuala ya mazingira, sijui uwanja ujengwe lini. Leo nataka nipate maelezo na Wananchi wa Serengeti wasikie maana ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na wapo tayari kwa ajili ya uchumi wao. Tujue kazi imeishia wapi, uwanja utajengwa lini kwa manufaa ya Watanzania na hasa kwa kufungua rasilimali ya Sekta ya Utalii. Kwa sababu tumekuwa tukipoteza rasilimali nyingi sana, Watalii hawatumii Uwanja huu, wanapitia Kenya, mwisho mapato yetu ya Taifa yanapotea. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie pia Bandari. Leo nimesema Jimbo la Mkoa wa Mara, ninalipa kipaumbele. Tumekubaliwa Mkoa wa Mara tutajengewa Bandari katika eneo la Nyasurura, Wilaya ya Butiama. Mpaka leo Wananchi wametoa maeneo yao, wameachia maeneo yao, hakuna anayelima. Sasa leo pia nataka nijue, hii Bandari itajengwa au haijengwi na kama inajengwa ni pale pale Nyasurura au pamehamishwa pale Musoma Vijijini? Naomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie Barabara ya Musoma kupitia kule kwa Mwanasheria Mkuu, Kyagata. Barabara hii pia ni ya kihistoria, imekuwa inawekewa kila siku changarawe hivi hii lami itafika lini katika hii barabara?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Kidumu Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Makilagi, tunakushukuru sana. Mheshimiwa Saleh Pamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Nassari!

**MHE. SALEH AHMED PAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia machache katika hoja zilizoko hapa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Wabunge wengine, kutoa pongezi kwa Kamati, kwa Wenyeviti na kwa Wajumbe wa Kamati hizi mbili. Taarifa zao zote nimezisoma, zimejaa maoni na mapendekezo mazuri sana. Napenda nichukue nafasi hii pia niwapongeze Mawaziri hawa, wanafanya kazi katika mazingira magumu, lakini wanajitahidi katika kutekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo manne ambayo ninataka kuyazungumzia kwa haraka haraka kwa sababu ya muda. Nataka kuzungumzia suala la mafuta na gesi, nishati, Shirika letu la TANESCO, madini na

*[MHE. SALEH AHMED PAMBA]*
wachimbaji wadogo wadogo na muda ukipatikana nitazungumzia juu ya usafiri wa anga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo katika magazeti na katika semina mbalimbali, malumbano ya hapa na pale hasa yanayohusu ushiriki wa Watanzania katika Sekta ya Gesi na Petroli. Moja ambalo nataka kulisema ambalo nchi zote nyingine duniani zinafanya ni kwamba, maliasili hizi ni maliasili za Watanzania. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile Watanzania wana haki ya kushiriki katika maliasili hizi za gesi na mafuta. Kinachotofautiana pale ni utaratibu tu kwamba, Wananchi walio na rasilimali hizi wanashiriki vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano imetolewa katika nchi za wenzetu, Miradi hii ni mikubwa na inahitaji mitaji mikubwa sana. Serikali kupitia Taasisi wanazoziunda ndizo ambazo zinashiriki katika sekta hii kwa ajili ya Wananchi wake. Mifano ipo mingi; nchi kama Norway, tunayo *State Oil,* nchi kama Uingereza, Kampuni ya BP ni Kampuni ya Wananchi wa Uingereza. Kikubwa kinachofanyika pale ni kuhakikisha Wananchi wanafaidi rasilimali ile kupitia kampuni zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wetu sisi Tanzania, napenda niipongeze sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tunao mkataba mzuri sana wa ku-*share resources* hizi. Mikataba hii ya Uchimbaji Mafuta na Gesi ambayo ni *PSA* ni mizuri kabisa. Inasema kwamba, asilimia 75 ya mapato, asilimia 75 ya *resources* zote zitamilikiwa na yule ambaye ameleta mtaji mkubwa na asilimia 25 zitamilikiwa na Wananchi. Suala ni kwamba, tunawamilikisha Wananchi wetu vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi tayari imeshaunda Kampuni kupitia *TPDC.* Zipo kampuni mbili; Kampuni ya *COPEC* ambayo ina-*deal* na mafuta na Kampuni ya *GASCO* ambayo ina-*deal* na mambo ya gesi. Kinachotakiwa kufanywa kwa upande wa Serikali, Kampuni hizi zisibaki tu majina kwa Msajili wa

Kampuni. Kampuni hizi zipate uendeshaji mzuri, zipate Mameneja wazuri na kubwa zaidi hizi kampuni lazima ziwe *capitalized.* Tuweke mitaji mikubwa ziweze kushiriki pamoja na Makampuni haya ambayo yamekuja hapa nchini. Kwa hiyo, hiyo ni changamoto kwa Serikali kuhakikisha kampuni hizi tunazipa mitaji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo nataka kulizungumzia ni suala la nishati, hasa linalohusu umeme pamoja na Shirika letu la *TANESCO*. Utaratibu unaotumika sasa ni kwamba, tunatumia utaratibu wa kupata umeme wa dharura na Serikali yetu inatumia fedha nyingi sana katika maeneo ya *capacity charges*. Kwa hiyo, tunachoiomba Serikali na nasema napenda nichukue nafasi hii niipongeze sana Serikali, kwa kuanzisha Miradi hii minne mikubwa; Kinyerezi I, Kinyerezi II, Kinyerezi III na Kinyerezi IV, huo ni mwelekeo mzuri wa kuondokana na utegemezi wa hawa *Independent Power Producers* ambao wanatu-*charge* fedha nyingi sana katika *capacity charges.* Kwa hiyo, nasema Miradi hii isimamiwe vizuri, tuendelee vizuri, tuipe *TANESCO* uwezo wa kumiliki mitambo yake na kama ni ziada basi itoke katika *Independent Power Producers.* Nadhani hilo ni eneo ambalo litatusaidia sana katika kuondokana na matatizo ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia kuhusu *TANESCO* ni jinsi na utaratibu gani ambao hili Shirika tutaliondoa katika hali iliyopo sasa. Kwa kihistoria, *TANESCO* ina matatizo kwa sababu zaidi ya kipindi cha miaka 15, hakuna uwekezaji mkubwa uliofanyika katika Shirika hili, kwa sababu tulikuwa katika utaratibu wa ubinafsishaji wa Benki ya Dunia. Sasa wakati umefika wa kuhakikisha Shirika hili tunalifanyia marekebisho, lakini tuwe waangalifu. Tuwe na marekebisho ambayo yatahakikisha Shirika linaendelea kufanya kazi, lakini *restructuring* yake inaenda kwa utaratibu mzuri bila kuathiri uzalishaji umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni wachimbaji wadogo wadogo. Naipongeza sana Wizara, wametenga fedha kwa ajili ya

wachimbaji wadogo wadogo. Tatizo lililopo ni kwamba, hawa kama jina lao linavyosema ni wachimbaji wadogo wadogo, hawana *collateral,* hawana kitu cha kuweka dhamana. Mmepeleka fedha Benki ya Rasilimali *(TIB),* kwa upande mmoja pale ndipo ambapo mmekosea, lazima mngeweka utaratibu wa kuweka Mfuko unaojizungusha wenyewe, kwa sababu wachimbaji wadogo hawa hawana *collateral,* hawana nyumba ya kuweka, hawana mashine za kuwekeza. *TIB* kuna masharti magumu ya Kibenki, kwa hiyo, lazima tuondoe utaratibu ule, tuutafute utaratibu mwingine ambao tutawasaidia wachimbaji wadogo wadogo waweze kupata *capital,* waweze kupata vifaa, bila kuingia kwenye masharti magumu ya Benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuongelea suala lingine moja kubwa. Upande wa madini, tunayo migodi ya dhahabu kama minne, mitatu, hivi. Ukiangalia nchi yetu na ukisoma ripoti zinazotoka kwa *GST,* nchi yetu ina madini mengi sana. Kwa hiyo, wakati umefika kuhakikisha tunapanua wigo wa uchimbaji wa madini. Inawezekana tatizo lipo, hatujaliona. Labda sheria zetu siyo *conducive* sana, labda sheria zetu haziwavutii sana. Kwa hiyo, ipo haja kwa Wizara kuangalia Sheria hizi za Uchimbaji wa Madini, Sheria za *Exploration,* tuhakikishe nchi yetu yote inakuwa na migodi, kwa sababu tunayo makaa ya mawe, tunacho chuma na tunayo *uranium.* Hata hapa Bahi tuna *uranium* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina madini mengi, inawezekana miundombinu au taratibu mbalimbali za uwekezaji zina kikwazo. Taratibu zilizowekwa mwaka 1996 zilizowaleta hawa BARRICK na ASHANTI, lazima tuziangalie ili tuwe na ASHANTI wengi waweze kufanya kazi na uchumi wetu ukue.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, nataka nizungumzie usafiri wa anga. Hapa Wabunge wengi wamezungumzia *Air Tanzania*. Usafiri wa Anga ni muhimu kwa nchi yoyote hasa nchi inayokuza utalii na biashara. Ni aibu hatujamaliza tatizo la *Air Tanzania* kwa zaidi ya miaka

15 au zaidi ya miaka 20. Wakati umefika tumalize tatizo la *Air Tanzania*. Tusafishe *balance sheet* yake, tuhakikishe *balance sheet* ni nzuri ili wawekezaji wake na biashara ... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SALEH AHMED PAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kamishna Saleh Pamba. Mheshimiwa Nassari, atafuatia Mheshimiwa Madabida!

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami kwa unyenyekevu nakushukuru kwa kunipa fursa hii niseme machache kuhusiana na Taarifa za Kamati zilizosomwa leo hapa. Nitazungumzia machache ya Jimboni kwangu na kama muda utaruhusu nitaongea na mengine vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la usambazaji wa umeme vijijini. Jana nilipata fursa ya kuuliza swali la nyongeza hapa na nikawa muungwana kweli kwa kuipongeza Wizara ya Mishati na Madini, kufuatia Miradi ambayo imekuwa ikitekelezwa kwenye Jimbo langu tangu nimekuwa Mbunge sasa. Vilevile nikaongelea upungufu ambao tumeu-*note* na nitaomba niuzungumzie tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Miradi ya Umeme kwenye Vijiji kama vya Mulala, Ngolekoli, Kata ya Ngwalusamba, Shela, Urisho, Kyuta, Mbala na maeneo mengine, imekwenda vizuri inakaribia kukamilika. Pamoja na imechelewa, tatizo ni kwamba, vijijini kwetu tunapeleka umeme maeneo ambayo hayako *surveyed.* Ukienda mjini, nguzo moja ya umeme inaweza ikahudumia hata nyumba nne au familia tano. Vijijini, ili familia moja iweze kuunganishwa umeme peke yake ina uwezo wa kutumia nguzo mpaka nne.

*[MHE. JOSHUA S. NASSARI]*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mkandarasi aliyepewa kazi kwenye Halmashauri yangu ya Meru, anayeitwa *Urban Enduro* alikuwa *slow* kweli. Ameleta nguzo nyingi zimelazwa chini, wamefikishiwa baadhi ya Wananchi wachache umeme. Tatizo lililokuwepo ni ule wizi niliouzungumza jana hapa wa zile Kamati zinazojiita Kamati za Umeme kwenye Vijiji, kuchangisha pesa kwa Wananchi. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema ule ni wizi. Ninafikiri nitamletea nyaraka ili aweze kujua Wizara ina-*deal* vipi na hao watu, kwa sababu kuna watu ambao walikataa kulipa hizo fedha, hawakuunganishiwa umeme na hawajawekwa kwenye *list* hata kama nguzo zipo nje ya nyumba zao.

La pili ni maeneo mengine ambayo yapo *expected* kuunganishwa na umeme kwa maana ya kwenye Mradi wa *REA Phase II* na juzi nimeona wataalam wakipita kuweka alama kule kwenye Kata yangu ya Ngarananyuki, ambayo haikupata umeme. Vilevile Kata ya Leguruki, maeneo mengine ya Vijiji vya Kaugoro, Kilinga na maeneo mengine mengi, nimeona tayari *procedure* zimeanza. Mimi naomba Wizara sasa iwe makini na mkandarasi aliyepewa kazi hii asije akachelewa kama yule wa *Urban Enduro.*

Lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la mgao wa umeme. Wabunge wengi hapa hawajalizungumza kwa sababu pengine umekuwa Wimbo wa Taifa kwa miaka mingi sasa. Waziri Muhongo alituambia hapa akasema kufikia Februari mwaka huu mgao wa umeme ungekuwa historia kwenye Taifa. Leo tunapozungumza, hata kule ninakotokea Jimboni kwangu hakuna umeme. Jana hapakuwa na umeme, juzi umeme umewaka kwa saa tatu; ninashindwa kuelewa mwezi Februari mpaka leo haujafika?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naongea kwa masikitiko makubwa. Tulikuwa tunaongea habari ya *industrialization* jana hapa. Sasa sijui tuna-*industrialize* vipi kama hatuna uhakika wa umeme? Viwanda vinafungwa, tuna-*cease* uchumi wa Wananchi. Watu wanaofanya kazi

za *saloon*, watu wanaofanya kazi za *welding,* wanashindwa kufanya kazi zao kwa sababu ya kutokuwa na uhakika wa umeme. Tunamwathiri mpaka Mwananchi wa chini kabisa. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri awe anatoa kauli ambazo tuna uhakika kwamba zinakwenda ku-*meet deadline* kwa mujibu wa taarifa ya Serikali na siyo kuwaambia mwezi Februari na leo ni Desemba bado tuna tatizo kubwa la umeme kwenye nchi; ni aibu.

Juzi kulikuwa kuna mgao wa umeme lakini tunashindwa kuambiwa ukweli, tunaambiwa mitambo ya Symbion haizalishi umeme lakini Wizara haituambii. Sisi tunapojaribu kuuliza wataalamu huko chini tunaambiwa bwana sisi siyo wasemaji wa *TANESCO* wala wa Wizara, hatuwezi kusema lakini ukweli ni huu kwamba, mitambo ya Symbion ndiyo ilikuwa haizalishi umeme na wanachodai ni tatizo la mafuta au kutokulipwa. Sasa naomba Wizara ijipambanue na iweke wazi nini hasa lilikuwa tatizo.

Nizungumzie habari ya uchukuzi kidogo. Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, mwalimu wangu aliniambia tangu mwaka jana hapa na tukazungumza kuhusu reli kutoka Moshi kupita KIA kwenda Arusha kwa maana ya *commuters* kwa maana ya reli ya abiria na aliniambia kufikia mwishoni mwa mwaka huu tayari mchakato mzima ungekuwa umeanza. Leo ni mwisho wa mwaka tunaongea, hatujaona kilichofanyika. Mheshimiwa Waziri aliniambia tena ukifika Jimboni kwako nendeni mkaangalie uzungumze na Wananchi ili ujue *stations* kabisa za kushusha na kupakia. Hilo tumelifanya, leo ni mwezi wa 12 naonekana mwongo Jimboni. Ningeomba mwalimu wangu Daktari Mwakyembe, nakuheshimu sana, ni vyema nalo ukaligusia ili Wananchi wa Arumeru wajue nini kinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nafikiri kuna umuhimu mkubwa wa kulizungumza hata kama halipo kwenye Taarifa; hili ni Bunge na hiki ndiyo kisima cha fikra cha Taifa letu. Wananchi wanakaa kwenye TV kuanzia asubuhi mpaka jioni kuangalia Wabunge wanafanya kitu gani, kuangalia Serikali inakwenda kuwafanyia nini

Wananchi wake, lakini badala yake tunaligeuza Bunge kuwa kijiwe cha mipasho, kuwa kijiwe cha kufanya *character assassination*, kuwa kijiwe cha kuharibu familia za watu na mimi sidhani kama ni sawa hata kidogo.

Mimi ni mdogo kuliko wote humu ndani, lakini naomba nisikilizwe kwa busara chache nilizonazo hizi. Kwamba, asubuhi imezungumzwa habari ya safari hapa ya Dominical Republic. Ningependa nizungumzie kidogo tu kwamba, wakati mwingine mnawapa Wabunge lawama ambazo siyo za kwao, hawastahili hata kidogo. Ofisi ya Bunge imepanga safari, Wabunge wanakwenda Dominical Republic, wamefika Dubai wamekaa siku tatu, kufika Dubai peke yake siku tatu, Dubai kwenda New York siku mbili, siku tano tayari hizo. Unakwenda Dominical Republic unafika Siku ya Jumamosi halafu Siku ya Jumapili kesho yake ile ni nchi ya Kikatoliki hakuna kazi na Jumatatu Wabunge wanarudi. Haya ni matumizi mabaya ya fedha za umma halafu tunakuja kubebesha Wabunge mizigo, tunajaribu kuunganisha matukio tunafanya *character assassination.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze vizuri hapo. Tukichukulia habari zote zinazoandikwa na kusemwa huko nje tukaja kuzisema humu ndani, hakuna atakayesalimika, hakuna atakayepona. Tumeona watu wakiandikwa wakipewa *scandal* huku mpaka za watoto wadogo, lakini tumekaa kimya kwa sababu tunavyoona siyo mahali pake hapa ni mahali pa kuzungumza mambo muhimu kwa ajili ya mustakabali wa Taifa letu. Tunafika kwenye Bunge watu wanaanza kutafuta visa, wanaangalia huyu kafanya, ndugu yangu naomba kuwashauri na kwa umri wangu mdogo nafikiri Bungeni ni sehemu njema ya kuzungumza. Nimeona kwenye magazeti na mimi nimeandikwa, naomba nizungumze hilo vilevile Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Keissy umesimama!

**TAARIFA**

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo tunayozungumza siyo nadharia au uongo. Ninaiomba Serikali, hii siyo mipasho, mtu anaiba ng'ombe akirudisha ng'ombe aachiwe! Sheria ya Bunge ndiyo Sheria ya Serikali. Wote walioiba hela za Serikali kupitia safari, hawakwenda safari, tumesema msamaha hakuna wapelekwe polisi, hamna mjadala hapa. Polisi ndiyo Wataamua, hakuna cha mipasho, hamna cha nini, wizi ni wizi, mwizi wa kuku anafungwa akirudisha kuku aachiwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, haya tuache siyo mipasho! Ndugu zangu tunakuja hapa tunaipigia Serikali ya CCM karaha. Tunaipigia kelele Serikali ya CCM haifanyi kazi, Serikali ya CCM haifanyi namna gani, kumbe sisi ndiyo wezi. Unapewa milioni sita unakaa Dar es Salaam, unapewa milioni tano unakaa Dar es Salaam! Itafuatiliwa ni wizi. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Keissy, Waheshimiwa Wabunge, ningependa kuchukua nafasi hii kuwaomba sana, ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Nassari, ambaye anaendelea kuchangia, hizi *topic* ziacheni tu, yaani anayebeba hizi *topic* analeta mkanganyiko ambao hatuuhitaji. Watu wengi ambao tunawagusa wana familia zao, wana heshima zao katika jamii na hawajahukumiwa na Mahakama yoyote, ni tuhuma ambazo hazijafanyiwa kazi kufika mahali popote. Kwa hiyo, siyo vizuri kila mmoja akianza kurudiarudia na kadhalika na sisi ni Wabunge tutafikishana mahali pabaya sana. Ningeliwaomba sana, hebu tuchangie mada zilizopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nassari endelea!

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Sijui kama Mheshimiwa Keissy alinipa taarifa au ni nini na nisingelipenda kumjibu sana kwa sababu sidhani kama mimi na yeye tunafanana hata kwenye uelewa wa mambo. Niendelee na mchango. *(Kicheko)*

*[MHE. JOSHUA S. NASSARI]*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa nakizungumza ndicho ulichokisema. Ume-*flow* kile nilichokuwa nakisema kwamba, Bunge ni sehemu ya kujadili mustakabali wa nchi, ni sehemu ya kujadili *issues*, siyo sehemu ya kujadili watu, siyo sehemu ya kujadili *personal life style* ya mtu, siyo sehemu ya kujadili huyu mtu huwa anakula nini au anakunywa nini, siyo sehemu ya kujadili mtu ana wake wangapi ana watoto wangapi, ni sehemu ya kujadili mambo muhimu kwa ajili ya Taifa letu. Ndiyo sababu mimi ni Mbunge wa Upinzani, lakini nimeanza kwa kuipongeza Wizara ya Nishati na Madini kwani naona wanastahili sifa kwa mambo wanayofanya ya usambazaji wa umeme vijijini. Haya ndiyo mambo ya kuzungumza hapa na pale wanapokosea tunawashauri. *(Makofi)*

Imekuwa *trend* ya miaka mingi ya hili Bunge kufanywa sehemu ya watu kujipatia sifa, watu waandikwe kwenye magazeti kesho. Mimi sijazungumza niandikwe kwenye gazeti. Niliandikwa sana kwa mwezi mzima wakati nagombea Ubunge ulinitosha na Mheshimiwa Keissy nikuombe tu kwamba, usitake uandikwe kila siku, uandikwe kwa *issues*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema hivi; nilichokuwa nakisema mwanzo ni kwamba, wakati mwingine watu wanabebeshwa mizigo ambayo siyo yao. Nilizungumzia *trip* ya siku sita hapa ambazo watu wako safarini halafu wanakuja kusemwa vibaya na hekima za kiongozi ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nassari, nilishatoa mwongozo kwamba, tujielekeze katika mada zilizopo mezani.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Basi Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee na mambo mengine. Nirudi kwa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, kuhusu suala la reli. Gharama za maisha zinapanda kila siku. Aliongea Mbunge mmoja jana hapa, nafikiri anatokea Geita kwamba, sementi Dar es Salaam inauzwa shilingi 15,000 ikifika Geita

inauzwa mpaka shilingi 25,000 mpaka 30,000 kwa sababu ya gharama za usafirishaji. Tutakuwa Taifa la ajabu sana kama tukiendelea kuwekeza kwenye Barabara na kuendelea kuwekeza kwenye kununua malori halafu tunasahau usafiri wa reli. Ama kwa hakika kama tunataka ku-*industrialize* lazima turudishe usafiri wa reli, lazima tukubali na kuhakikisha umeme wa uhakika unapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nizungumzie Viwanja vya Ndege na leo hii nimepata taarifa kwamba, pale Uwanja wa ndege wa Arusha, Ndege ya *Ethiopian Airlines* ilitua pale kwa dharura. Baada ya dharura ile kumalizika ilipaswa iondoke ili ikatue Kilimanjaro, lakini kwa sababu ya Uwanja mdogo wa ndege ule kwa sababu ya *runway* kuwa fupi, ndege ikapitiliza kwenye *runway* na matairi ya mbele yakaingia kwenye udongo, bahati watu wamepona wakaenda kushushwa na ngazi kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kuna umuhimu mkubwa wa kuangalia upya viwanja vyetu vya ndege, tuangalie usalama wa watu. Juzi kwenye Uwanja huo wa Ndege wa Arusha, Ndege ya *Precision Airways* imepasua matairi yote ya nyuma ikataka kuua watu na Mheshimiwa Lowassa alikuwepo ndani ya ndege ile, mlisikia kwa sababu habari iliandikwa vizuri kweli. Uwanja huo huo tena leo tunasikia *runway* imekuwa fupi na ndege imepitiliza kwenye *airstrip*. Habari hizi zinashitua kweli, nilikuwa nasikiliza redio hapa nikasikia baadhi ya redio mpaka zimeanza kuongea mambo mengine ambayo sidhani kama yalikuwa sahihi sana kwamba, ndege imeanguka kwenye Shamba la Kahawa la Bulka na nikalazimika kupiga simu kwenye Uwanja wa Arusha nikaambiwa siyo kwenye shamba la kahawa, lakini imepitiliza kwenye *runway*. Kwa hiyo, kuna haja ya kutazamwa upya usalama wa viwanja vyetu vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho hapo hapo ningependa kufahamu, hapo nyuma tumesikia baadhi ya Wafanyakazi wa Viwanja vya Ndege, ambao walisimamishwa kazi kama si kufukuzwa kufuatia uzembe

ambao ulionekana wa madawa ya kulevya kupita kwenye viwanja vyetu na mojawapo ya sakata kubwa ilikuwa ni sakata maarufu kama sakata la akina Masogange, ambapo watu walisimamishwa kazi, kwa sababu ya dawa ambazo zilipita kwenye uwanja. Baadaye wale akina dada waliposhikwa Afrika Kusini walikuja kuachiliwa na kusafirishwa na Serikali kwamba walikuwa hawajabeba madawa. Ningependa pia kufahamu wale wafanyakazi waliokuwa wamesimamishwa kazi hivi wamerudishwa kwenye nafasi zao baada ya kuthibitika kwamba yaliyopita hayakuwa madawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru na muda huu unatosha, ahsante sana. Nafikiri aliyenielewa amenielewa, ambaye hajanielewa hatanielewa mpaka siku ya mwisho. Naomba Bunge hili liwe sehemu ya kujadili masuala nyeti, masuala ya Taifa na siyo kujadili nani kavaa nini na nani anatoka na nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi!

**TAARIFA**

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe taarifa ili tusitoke hapa na picha tofauti kuhusu aliyoyasema Mheshimiwa Nassari ya Ndege ya *Ethiopian Airlines* iliyo-*land* Kiwanja cha Ndege cha Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haikuwa *scheduled flight* kuja Kiwanja cha Ndege cha Arusha. Ilikuwa ni *flight* kutoka Adis Ababa kuelekea Afrika ya Kusini, lakini Rubani ikabidi ashuke pale. Kile kiwanja hakiwezi kupokea ndege *Boeing 769* nafikiri, ni ndege kubwa nadhani ikiwa na abiria 213 na *crue* tisa. Sasa hatuwezi kusema kila kiwanja Tanzania kiwe na *runway* ya kutosheleza ndege kubwa kabisa ya *Airbus 38;* haiwezekani. Ilikuwa ni *emergency landing* na itakapoondoka pale ile ndege itabidi washuke abiria wote

wakasubiri *KIA* tupunguze mafuta, kwa hiyo, ndiyo mambo ambayo yatatakiwa kufanyika pale kwa sababu *otherwise runway* ni fupi. Nilitaka nitoe tu hiyo *clarification*.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mambo yaliyotokea asubuhi humu ndani ya Bunge, nilijikuta nimeongea kauli ambayo iliwakwaza wengi hasa ambao ni waadilifu katika ndoa zao. Siyo Wabunge wote wanafanya vitendo vya ufuska humu ndani, wengi ni waadilifu na wana ndoa zao na wana heshima zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifute ile kauli yangu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maryam Msabaha, kwa uungwana wako. Mheshimiwa Zarina Madabida; aah, kabla ya Mheshimiwa Zarina, Mheshimiwa Mama Anna Abdalah ulisimama? Tafadhali, samahani sana sikukuona mama yangu.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nachukua nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Maryam Msabaha. Jamani huo ndiyo uungwana. Huo ndiyo uungwana na ninaomba jambo hili liishe na limekwisha. Tusije tukaendeleza tena limekwisha. *(Makofi)*

Mimi nakushukuru sana Mheshimiwa Maryam Msabaha, umewaokoa akina mama wengi na akina baba wengi wanaopigiwa simu na wake zao na waume zao wanaulizwa wewe wa kwako yuko wapi! Nasema hili jambo limekwisha na ninakushukuru sana kwa uungwana huu. Ninafikiri hili jambo la afya kwa Bunge letu kama mtu akikosea aseme jamani naomba tu nafuta maneno yangu. Ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana mama yetu Mheshimiwa Anna Abdallah, kwa kutushauri na kutuongoza na ndiyo wajibu wako kwa kweli. Mheshimiwa Zarina Madabida, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kafumu!

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba niseme mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, kwa hiyo, ninaunga mkono yale yote ambayo Mwenyekiti wetu ameyawasilisha. Ninaona na mimi nichangie kidogo katika masuala mengine na hasa ninataka kuzungumzia kuhusu msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam umuhimu wake kila mtu anajua. Dar es Salaam ni mji mkuu wa biashara, Dar es Salaam inategemewa sana katika makusanyo ya nchi, inakusanya karibu asilimia 75, Dar es Salaam inategemewa sana kwa Bandari, lakini sasa hivi ya msongamano ni mbaya sana. Kutoka mahali pamoja kwenda mahali pengine, *distance* ndogo tu kutoka Kinondoni kwenda Mjini, inaweza ikakuchukua saa mbili. Kutoka Ubungo kwenda Mbezi inaweza kukuchukua saa tatu na hivyo watu wanatumia muda mwingi sana na hizo saa tatu ni safari moja tu. Kwa hiyo, kama saa mbili kwenda saa tatu kurudi, saa tano mtu anatumia njiani. Ukiyapigia hesabu ni fedha nyingi sana ambazo zinapotea njiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kwamba, Dar es Salaam ina umuhimu wake. Kumekuwa na matengenezo mbalimbali na kusema kweli ni lazima niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, kwa matengenezo mbalimbali ya barabara, ukarabati pamoja na barabara mpya za mabasi yaendayo kasi. Vilevile Manispaa imejenga barabara nyingi, lakini hii barabara ya mabasi yaendayo kasi imekuwa mwiba mkali sana na hatua za haraka zinahitajika, kama hazikuchukuliwa tunaweza katika kipindi tunachosubiri mpaka imalizike ambayo nimeambiwa ni mwezi Machi mwaka 2015, ni muda mrefu sana. Kwa hiyo, ninaomba Waziri mwenye dhamana tuangalie jinsi gani

tunaweza tukafanya kwa sababu huko nyuma tumekuwa na matengenezo ya barabara mbalimbali lakini hatukuwa na msongamano mbaya kama uliopo sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasiwasi kama hata barabara hizi zitakapomalizika kutakuwa na tahfifu ya msongamano. Huku nimelisema hili hata wakati tunachangia kwenye bajeti kwamba barabara za Manispaa nyingi sana zimetengenezwa. Kinondoni zimetengenezwa, Masaki zimetengenezwa, Mbezi zimetengenezwa, lakini makutano yetu yako Salander Bridge. Kila ninapozungumza sioni kama kuna mkakati wowote wa kutengeneza Salander Bridge kutanua daraja lile. Zinakuja *lane* nne zinaingia mbili, zinatoka huko *lane* nne zinarudi mbili, kwenda mjini na kurudi kutoka mjini. Kingine zaidi tuliambiwa kutakuwa na boti itakayotoka Feri inakwenda Bagamoyo. Mimi nikawa najiuliza hivi kweli siyo kiini macho hiki? Hii boti tunapanda kwenda wapi? Hii boti itabeba magari mangapi? Hizi boti zitakuwa ngapi kuweza ku-*service* na kuweza kuondoa msongamano huu?

Kwa hiyo, nilikuwa ninasema Mawaziri wanaohusika wawe *a bit more realistic* kwamba hii boti tunatoka wapi na kwenda wapi au ni kiini macho tu cha kututoa njiani! Hilo moja.

Barabara ya Kilwa vilevile na daraja hili nimeshalizungumza pia, Daraja la Gerezani. Pale tumeambiwa kutakuwa na *flyover* ambayo itakuwa inaelekea Tazara, lakini tumezungumza katika Kamati kwamba, *structure* ya Dar es Salaam jinsi ilivyo kila mtu anakwenda *City Centre*. Sasa utapotengeneza ya kwenda kule TAZARA, nani anakwenda TAZARA labda watakaokuwa wanakwenda *Airport,* lakini ama sivyo tunataka kufungua ili wanaotoka Kurasini waweze kwenda mjini na kurudi bila kuwa na foleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipango yetu ya maendeleo hakuna mtu ambaye hajui umuhimu wa Bandari ya Dar es Salaam na Reli ya Kati. Ninataka kusisitiza yale

maneno ambayo tumeyasema kwenye Kamati. Tumekuwa tunazungumza maneno mengi, hii Gati Namba 13 na 14 imezungumzwa kwa miaka minane na bado tunazungumza. Reli ya Kati tumezungumza kwa muda wa miaka saba na bado tunazungumza. Sasa nashangaa tutazungumza mpaka lini? *(Makofi)*

Tulipokuwa tunasafiri kwenda kwenye ziara hii ya mafunzo tukiwa ndani ya ndege nilikutana na gazeti moja *National News* la Kenya. Wakati sisi bado hatujaamua hata kuhusu hii Reli ya Kati wenzetu wanasema *high speed gauge railway construction set to begin,* hii ilikuwa Novemba. Wenzetu Novemba tayari na Mkandarasi ameshapatikana wa kujenga reli na anasema reli hii ita-*connect* Kenya, Uganda pamoja na Tanzania. Sisi tunazungumza, bado tunazungumza na wakati mwingine tunalumbana hatujui nini tunachotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana na hasa wale ambao wapo kwenye dhamana, hebu tuache kuzungumza, sasa hivi ifike mahala tuanze kutenda. Tutawalaumu wenzetu nchi za jirani wanatuacha, wanafanya hivi, lakini mchawi tunae sisi wenyewe. Wakati wenzetu wanatenda, wakipata *opportunity* kidogo wanaitumia, sisi tunaacha inapeperuka. *(Makofi)*

La mwisho, sijui utendaji kazi huu dhaifu wa Tanzania ni kutokana na *design* au *default,* kwa sababu sisi tumetembelea katika Idara mbalimbali, Bandari tumekuta karibu *the entire management wana-act,* kuanzia Mkurugenzi, sijui Mkurugenzi wa nini mpaka Mkurugenzi Mkuu ana-*act*. Tumeenda Kiwanja cha Ndege, Mkurugenzi Mkuu ana-*act,* yaani kila mtu ana-*act.* Sasa yule mtu anaye-*act* anatoa wapi tija ya kufanya kazi? Mimi naomba sana na nafikiri Waziri wa Utumishi yupo, kuna malumbano sijui *Board* ndiyo iamue nani wa kuteuliwa au sijui Tume ya Ajira, haya malumbano yanakuja ya nini *at the end of the day* tunao-*lose* ni sisi kwa sababu kazi haziendi! Sasa kazi haziendi, hatujui kama ni kwa ajili ya ku-*act*, hakuna *competent* wafanyakazi au ni kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana waliokuwa *responsible* wananisikia, wale wanao-*act* kama wapo *competent* wapewe, kama sivyo, watafutwe watu *competent* wakafanye kazi hiyo. Kuliko namna hii sisi kila siku tunasema, tunalumbana, tufanye kazi tuache maneno. Tumezungumzia kuhusu masuala ya kufanya *PP,* tumekwenda tumeona wenzetu jinsi *PP* inavyofanya kazi. Sisi kwetu hapa *PP* haifanyi kazi. Sasa sijui aliyeturonga amekufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, lakini ninaomba Watanzania tuache maneno twende kwenye vitendo. Nashukuru, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zarina Madabida, ahsante. Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu, atafuatiwa na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed!

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kama Wabunge wengine nichangie hoja zilizopo mbele yetu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na tumefanya kazi kwenye Kamati ile, kwa hiyo, nitazungumza kwa kifupi sana.

Nianze kwa kutoa pole tena kule Jimboni kwangu kuna maafa yaliyotokea, mvua ilinyesha, Wananchi nyumba zao zikaondolewa na wamepata matatizo, basi nawapa pole na baada ya Bunge nitaenda kuwaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba, Serikali inafanya vizuri sana katika kuendeleza Miradi ya Umeme. Ningependa nitoe pongezi sana kwa namna ambavyo Serikali inajenga miundombinu ya kusambaza umeme katika nchi yetu. Kuna Mradi mmoja unapeleka umeme wa msongo mkubwa kwenda Shinyanga kutoka Iringa. Mradi huu unapita kwenye Jimbo la Igunga. Utekelezaji wake umeleta matatizo kidogo kwa Wananchi wangu na ningependa nimwambie Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali, wajaribu kurekebisha hayo matatizo ili Mradi huu uweze kutekelezwa vizuri zaidi.

*[MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU]*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu umepita katika vijiji vinane ambavyo ni Mgongolo, Makomelo, Kijiji cha Mbutu, Kijiji cha Bukama, Imalanguzu, Mwamakona, Igurubi na Mwakwangu. Sasa katika harakati za kupita humo, Mradi huu umewapitia Wananchi na mashamba yao. Naishukuru sana *TANESCO* na Viongozi wa Mradi huo, walifanya e*valuation* ili Wananchi hawa waweze kulipwa. Walifanya vizuri na wakapeleka fedha Halmashauri ya Wilaya ya Igunga. Bahati mbaya watekelezaji wa kuweza kuwafidia watu hawa walifanya makosa kidogo, wamewapunja watu na wengine hawakuwafidia kabisa. Jambo hili nililifuatilia mpaka nikalifikisha Wizarani na Wizara ikachukua hatua, inaonekana kweli makosa yamefanywa na walipaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara leo ni kama miezi mitatu hivi bado jambo hili halijarekebishwa na tayari mkandarasi ameshafika kwenye eneo anataka kuanza kazi. Naiomba Wizara iwalipe hawa watu kwa wakati, msiwaondoe mpaka mtakapowalipa ili Mradi uende kufanyika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshazungumza na Naibu Waziri, nikamweleza tuwasaidie Wananchi hawa kwa sababu sasa hivi wanalalamika kwamba, tunataka kuondolewa na kilimo kimeanza. Mradi uende, naomba Mradi huu usikwamishwe kwa ajili ya Wananchi wa Igunga. Walipeni Wananchi ili Mradi uweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kidogo kuhusu Sekta ya Madini. Sekta ya Madini kwa Sheria inasimamiwa na Sheria ya Madini chini ya Kamishna wa Madini. Mimi nilikuwa Kamishna wa Madini, nilichukua nafasi ya mtangulizi wangu Mheshimiwa Mwakarukwa, ni Sekta yenye changamoto nyingi sana na ndiyo ina Sheria Maalum na mtu maalum wa kuisimamia. Bahati mbaya sana tangu nimeondoka, Kamishna hajateuliwa, miaka mitatu leo mtu ana-*act,* matokeo yake sasa Sekta haisimamiwi kila mtu ni Kamishna. Ukienda Wizarani mambo ya Kisheria yote ya Sheria ya Madini yanapelekwa kwa Katibu Mkuu,

*[MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU]*

yanapelekwa kwa Waziri. Sasa kila mtu ni Kamishna, huwezi ukasimamia Sekta namna hiyo. Ndiyo maana Sheria ilitengenezwa na mtu maalum wa kushughulikia jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kama Sheria ya Ardhi, Kamishna wa Ardhi ndiyo anayefanya shughuli hizo kwa Sheria. Kwenye Sekta ya Madini, Waziri ana nafasi yake ya kutoa leseni za uchimbaji mkubwa na mdogo, lakini leseni za utafuataji na mambo mengi ni shughuli ya Kamishna wa Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda leo Wizara ya Nishati na Madini, wasimamizi wa Sekta hiyo ni wengi, *TMAA* imechukua nafasi yote, kila kitu utasikia *TMAA, TMAA,* Kamishna wa Madini yupo wapi na Ofisi zake hizi? Ana Kanda nane katika nchi hii na ofisi nyingi kabisa, lakini hatumsikii kabisa, tunavunja Sheria. Naomba Serikali iteue Kamishna, mwachieni afanye kazi yake vizuri, msimuingilie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia kwenye Sekta ya Madini ni utafutaji wa madini ndiyo uti wa mgongo wa upatikanaji wa migodi baadaye. Kuna Mbunge hapa alisema, nadhani ni Mheshimiwa Saleh Pamba, ni vizuri tuhakikishe tunatafuta madini. Shughuli ya utafutaji madini tuwaalike watu wafanye hii kazi ili baadaye tuwe na migodi mingi tuweze kujenga uchumi. Tusipokuwa na migodi tukajenga uchumi hatutaweza kuendelea. Kwa hiyo, naomba shughuli ya kutafuta madini, tutengeneze mazingira mazuri zaidi. *(Makofi)*

Sasa hivi kuna mazingira siyo rafiki sana katika utafutaji wa madini. Utafutaji wa madini unafanywa na wachimbaji wadogo, unafanywa na kampuni ndogo za utafutaji madini, wanaita *junior companies,* hawa wakubwa wanakuja kuchukua *project* imeshaenea. Sasa wametengenezewa mazingira ambayo hawawezi kufanya utafutaji, wamepandishiwa kodi hizi za kawaida. Kwa hiyo,

wengi hawawezi ku-*maintain* leseni zao. Mwisho tutashindwa kupata migodi hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kengele ya kwanza imelia, nimalizie kwa kusema barabara ya kutoka Igurubi kwenda Igunga, Mheshimiwa Magufuli alituahidi kwamba itakuwa ya *TANROADS* na tumeshapeleka maombi kwake. Namwomba Mheshimiwa Magufuli, atupandishie hadhi barabara hii msimu ujao ianze kushughulikiwa na *TANROADS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu, nakushukuru sana. Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Raya Khamis. Mheshimiwa Rajab!

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Kamati hizi mbili ambazo zimewasilisha Ripoti zake leo hii. Kwanza, nawapongeza Wenyeviti wa Kamati hizi kwa namna ambavyo wameweza kuwasilisha Taarifa zao. Nawapongeza pia Wajumbe wa Kamati hizi kwa namna ambavyo wamewasaidia Wenyeviti wao kuweza kutuletea Taarifa ambazo zina mashiko na zinazotoa mwelekeo halisi wa nini kifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na Wizara ya Sayansi na Teknolojia kuhusiana na Mkongo wa Taifa. Sasa hivi kuna hujuma kubwa ambazo zinafanywa na baadhi ya Wananchi wasio waadilifu kwa kuhujumu Mkongo wa Taifa uliopo ardhini na ule uliopo baharini. Nataka niwaombe Wananchi kwamba, kuhujumu Mkongo huu wa Taifa ni kuhujumu maendeleo ya nchi. Naiomba Wizara ya Sayansi na Teknolojia, ijaribu kuendelea kutoa elimu zaidi kwa Wananchi ili waelewe umuhimu wa huu mkongo.

*[MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED]*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri zetu tuna tatizo la uwekaji wa kumbukumbu za mahesabu pamoja na utoaji wa taarifa za mahesabu. Kitu ambacho sasa hivi tunahisi kwamba kitatusaidia katika Halmashauri zetu ni huu mfumo ambao Serikali imeuanzisha wa *Epicor.* Kufanikiwa kwa mfumo wa *Epicor* kutatokana na kuwepo kwa huu Mkongo wa Taifa. Kwa hiyo, tunaomba Wizara ijaribu kuharakisha huu Mkongo wa Taifa uweze kuenea katika Halmashauri zetu zote ili sasa taarifa za fedha zijulikane na kuonekana kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kuhusu suala la minara ya simu. Bado katika nchi yetu Halmashauri nyingi zinakosa mapato yake kutoka katika minara ya simu. Hawa *services providers* bado hawajaweka kipaumbele kuzilipa Halmashauri zetu fedha ambazo zinatokana na minara ya simu. Nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba, hebu ajaribu kuingilia kati ili Halmashauri zetu ziweze kupata haki zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niende upande wa *TTCL.* Naomba Mheshimiwa Waziri kama atapata muda wakati wa kujumuisha hapa anieleze ni kwa nini hadi sasa Ofisi ya *TTCL* Pemba haijaanza kujengwa? Kitu ambacho tulikizungumza miaka mitatu nyuma baada ya kuona tumekuwa tunapiga kelele sana humu ndani, mlichokifanya ni kwenda kuzungusha uzio wa mabati katika eneo lile, lakini kazi yenyewe bado haijaanza. Atupe maelezo kamili, kitu gani kinakwamisha ujenzi wa Ofisi ile ya *TTCL* pale Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Shirika la Posta, limefanya vizuri kule Pemba na sasa hivi wameweza kuweka mambo ambayo yameleta uhai katika Shirika hili la Posta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa Gati 13 na 14, Wabunge wengi wamezungumzia, lakini na mimi nataka nimwambie Mheshimiwa Mwakyembe kwamba, Gati 13 na 14, ndicho chanzo ambacho kilifanya

Mheshimiwa Nundu kuondolewa katika hii Wizara. Wakati ule mimi nilikuwepo katika Kamati ya Miundombinu, ninalijua sakata lililokuwepo. Kitu kilichopelekea mpaka baadhi ya Mawaziri humu wakaondolewa katika Wizara hiyo. Sasa leo bado tunaendelea kusikiliza maneno tu kuhusu Gati 13 na 14. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikubaliane na Taarifa ya Kamati kwamba, muda wa maneno bila vitendo umekwisha. Watanzania sasa hivi wamechoka maneno yenu, wanataka kuona vitendo, Gati 13 na 14 wanataka waone. Kila kitu kilikuwa tayari mpaka fedha zilikuwa tayari, tulihakikishiwa humu ndani ya Bungeni, lakini leo mnaturudisha tena katika lugha zile zile. Hebu tuelezeni kitu gani hasa ambacho kinakwamisha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie sasa suala la madini, alizungumza vizuri hapa Mheshimiwa Kafumu kuhusiana na Kamisheni ya Madini kiasi kwamba akaomba kuundwe Kamisheni Maalum kwa ajili ya kushughulikia mambo haya ya madini. Ninataka niwakumbushe Serikali kwamba, huko nyuma kulikuwa na Kamati ya Jaji Bomani, Kamati ya Bomani ilitoa hili pendekezo; sijui kwa nini Serikali hamtaki kuifuatilia? Nakupongeza sana Mheshimiwa Kafumu kwa jinsi ulivyolieleza na nafikiri sasa Serikali itakuwa imesikia, itarudi kuona ile Kamati ilipendekeza nini katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka vilevile nichukue nafasi hii niupongeze Mgodi wa *Resolute Tanzania Limited* uliopo Tabora. Kwa kweli huu Mgodi umesaidia sana na umetoa fedha nyingi kiasi kwamba Wananchi wa Halmashauri ile wamefaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Betty Machangu alipokuwa Mkuu wa Wilaya na Mheshimiwa Selelii wakati ule alipokuwa Mbunge, fedha zile ziliwasaidia sana Wananchi. La ajabu ni kwamba, bahati mbaya Mheshimiwa Selelii hakurudi, pale kuna Mbunge msomi kafifiisha maendeleo ya Halmashauri ile kutokana na fedha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



zile. Bado kuna zaidi ya bilioni 2.3 ambazo zimetolewa hazijatumika. Niwape pole sana Wananchi wa Nzega kwa hilo lililowakuta na niseme tu kwamba, humu ndani tunasema kuna Mawaziri mizigo, lakini mimi naamini vilevile kuna Wabunge mizigo. Kuna haja ya kukaa tukajitathmini, tukaona nini mahitaji ya Wananchi. Naamini kwamba, Wananchi wa Halmashauri ile watakuwa wamesoma na wamepata funzo kamili. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimalizie kuhusu habari ya *TMAA.* Kwa kweli kazi wanayoifanya *TMAA* inafanana kabisa na kazi ambayo inafanywa na TRA. Sioni kwa namna gani *TMAA* inaleta manufaa katika Sekta hii ya Madini. Ni vyema sasa hii *TMAA* mkaiondoa mkaunda hii Kamisheni, naamini hii Kamisheni itaweza kufuatilia fedha hata zile za mirabaha ambazo zinapelekwa katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, ahsante sana. Kama nilivyosema Mheshimiwa Raya Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Desderius Mipata!

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza, ningependa kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati kwa Hotuba zao nzuri. Naamini Serikali itazichukua na kuzifanyia kazi pamoja na maoni ambayo tutayapendekeza Wajumbe na Wabunge wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ningependa ku-*declare interest,* mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini. Ningependa zaidi kuongelea japokuwa wengi tayari wamelisemea, suala la mabomba ya gesi kule Mtwara. Bomba la gesi kama Kamati tulipata nafasi ya kulitembelea tukaona jinsi ambavyo ujengaji wa lile bomba unavyokwenda na jinsi ambavyo watu wa Wizara

wamejitahidi na *speed* ambayo wanayo, wale watu wanastahili kupata pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na yote, tunasikitika kwamba, tulipokwenda Watanzania ambao tuliwaona pale ni vibarua tu, hakuna *engineers,* hakuna watu wa kutazama lile bomba pindi wale wajenzi wa China watakapoondoka sisi tutafanyaje *maintenance*, ina maana tutawaita tena Wachina waje wafanye *maintenance* wakati Watanzania wapo na nafasi zipo. Ninadhani bado nafasi ipo, Serikali iliangalie hili, Wizara iliangalie hili suala la kuchukua Watanzania wapelekwe China wakasome jinsi ya kuliendesha na kulisimamia bomba la gesi litakapokamilika na vilevile tusiwe na tabu ya kuhangaika, wazawa wapo lazima tutafute watu wa nje, kwa kweli ni kitu cha kujifunza kama Watanzania na Serikali kwa ujumla tuwe na wazawa ambao wataendesha suala hili la bomba kusaidia Serikali yao kwa jumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kuzungumzia suala zima la ugawaji wa vitalu vya gesi. Suala hili linazungumziwa sana lakini bado tunakuta linaleta mzozo jinsi gani na nani na ni wakati gani na mtu mwenye sifa zipi anatakiwa awe na umiliki wa vitalu vya gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoitaka Serikali na Wizara kwa ujumla, tunaiambia kwamba, Mtanzania yeyote, mzawa yeyote au Kampuni yoyote ya Kitanzania ya mzawa yeyote, ambayo ina fedha za kutosha za kuendesha vitalu hivi vya gesi na kuendesha Miradi hii, basi isisite kuwapa leseni kuendeleza suala hili. Kwa upande mwingine, ningependa jambo hili liangaliwe kwa umakini kwa sababu tunaona mfano mzuri katika ugawaji wa vitalu vya madini; kwa mfano, katika Mkoa wa Geita zaidi ya asilimia 70 ya vitalu vya madini vimechukuliwa na mzawa, Mtanzania, amevihodhi lakini haviendelezwi chochote. Kwa hiyo, tunakuta kunafanyika kazi ya udalali ambayo haina faida kwa Serikali, vile vitalu vimekaa haviendelezwi, ina maana tunakosa kodi kama Serikali, yaani kuna mgao ambao unatakiwa upatikane maeneo ya uchimbaji na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



mambo mengine ambayo yanaendelea katika maeneo hayo, lakini yamekaa tu *idle* hakuna ambacho Serikali tunakipata. Kwa hiyo, nadhani hiyo pia iwe somo na iangaliwe vizuri katika ugawaji wa vitalu vya gesi tusije tukapoteza pato la nchi yetu kwenye masuala mazima ya kupata kodi kutokana na vitalu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kuongelea suala zima la mgao wa umeme. Wabunge wengi wamelizungumzia, watu wengi wanalisemea ndani ya Bunge na nje ya Bunge kwamba kuna tatizo la umeme. Umeme unakuwa umegaiwa, lakini tunachoitaka kwa kuwa sasa tayari Mradi wa Kiwira wamepewa *STAMICO,* tunaitaka *STAMICO* kwa ujumla watafute wadau ama watafute mikopo kulishughulikia suala hili na kuondoa suala zima la ukatikaji wa umeme mara kwa mara. Kufanya hivyo kutasaidia kuondoa tatizo hili na kutasaidia kuwa na umeme wa uhakika vilevile, maana ukatikaji wa umeme mara kwa mara unapelekea watu wengi kupata hasara katika biashara zao, watu wengi kutokwenda makazini, yaani zaidi ya asilimia 35 ya Watanzania ama zaidi ya asilimia 50 wanafanya kazi kupitia umeme. Kwa hiyo, ina maana kukatika kwa umeme uzalishaji unapotea, watu wanakosa kwenda makazini, kwa hiyo, tunaitaka *STAMICO* waliangalie hili kwa undani, watafute wadau, watafute mikopo kokote ambapo wanaona inafaa, basi walifanyie haraka suala hili na kuhakikisha umeme unapatikana kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuongelea suala zima la kodi migodini. Tuna migodi mingi na baadhi ya migodi hiyo inakwepa ulipaji wa kodi. Kama Serikali kwa kweli yaani ni pengo kubwa kukosa kodi kupitia migodini. Baadhi ya migodi mfano Williamson Diamond, tulibahatika kwenda pale tukaona, vilevile tukataka kujua ulipaji wao wa kodi kwenye Serikali. Madai ni kwamba, wamenunua mitambo, mitambo ile inafanya kazi wataanza kulipa kodi pindi ambapo watakuwa tayari wamesharejesha fedha za mitambo yao. Nilitaka kujua ni lini fedha zao zitarejeshwa na ni muda gani watachukua kuanza kulipa kodi

*[MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS]*
kukamilisha deni lao la kununulia mitambo kuanza kulipa kodi kwa Serikali?

Pia ningependa kujua watakapokuwa tayari wamesharudisha deni lao wameshaanza kulipa kodi *whatever* itakavyokuwa, hili pengo ambalo limebaki hapa ni zaidi ya miaka 40 sasa, huu muda ambao hawajalipa kodi Serikali inapata fidia gani na inajilipa kivipi? Kwa hiyo, Waziri ama yeyote ambaye atahusika na hili, ningependa kupata maelezo sahihi kuhusiana na hili na jinsi ambavyo Serikali imepoteza kodi kupitia hili na jinsi ambavyo tutapata kodi zetu ama fidia kutokana na muda wote ambao migodi hii ama mgodi huu kwa ujumla haujalipa kodi kwa kipindi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamezungumzia suala la *REA*, nisingependa kupoteza muda kulizungumzia. Kwa msisitizo ningependa kusema, fedha zinazotolewa kwenda *REA* kuendeleza Miradi ya Umeme Vijijini tunakuta bado zinatolewa kwa kusuasua. Kama zinatolewa kwa kusuasua bado Wabunge wataendelea kulalamika, Wabunge wataendelea kupiga kelele humu ndani umeme vijijini hautafika. Kama fedha zitatolewa kwa wakati, zitatolewa zinavyotakiwa, naamini Mradi wa Umeme Vijijini *(REA),* utakwenda kwa wakati na sehemu zote watapata umeme. Kwa kuchelewa kufanya hivyo, tunaitia hasara Serikali yetu kwa kuwaacha Watanzania ambao wanaishi vijijini, Watanzania ambao hawana umeme kuendelea kuharibu misitu, kuendelea kufanya matumizi mabaya ya misitu, kuchoma na mambo mengine kwa ajili ya kupata mkaa na vilevile kuendelea kuwabebesha mzigo Watanzania ambao hawana umeme wanastahili kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri kulikuwa kuna *slogan* hapa ELIMU KWANZA. Katika *Big Results Now* nadhani na elimu ipo, lakini sasa elimu tunaangalia wale wa vijijini ni mtoto wa maskini. Mtoto huyu anahangaika, mtoto huyu inafika jioni anahitaji kusoma, anahitaji awe na mwangaza, anahitaji umeme asome lakini tunaona

*[MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS]*

anashindwa kusoma, anashindwa kufanya vizuri masomo yake, baadaye tunaanza kutafutana kulaumiana wakati Serikali haijaona umuhimu wa kutoa fedha kwa wakati, wa kutoa fedha zinavyotakiwa katika Mradi wa Umeme Vijijini. Kwa kufanya hivyo, itawasaidia hata wanafunzi ambao wanaishi vijijini hawana umeme, kupata muda mzuri, kusoma vizuri na vilevile kufanya *revision* vizuri ya masomo yao na kuwaondolea matatizo ya macho, maana unakuta sasa hivi tatizo la macho kadiri tunavyozidi kwenda linazidi kukua na hasa kwa wale ambao wanakuwa wanasoma na wanapata mazingira magumu katika kusoma. Tunawapa mazingira magumu watu ambao hawastahili. Kwa kweli ningependa kusisitiza maeneo hayo na nisingekuwa na mengi ya kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raya Khamis, tunakushukuru sana. Mheshimiwa Desderius Mipata, atafutiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii lakini pia namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati hizi mbili; Kamati ya Nishati na Madini na Kamati ya Miundombinu. Nawapongeza pia Wasimamizi Wakuu wa Wizara katika Wizara hizi mbili, wote wanafanya kazi nzuri sana. Niwe tofauti na wenzangu, kwa kweli Nishati na Madini, Miundombinu na Uchukuzi, Mawaziri hawa wanatutoa kimasomaso, wanajitahidi sana katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Wizara ya Nishati na Madini. *REA* katika taarifa tulizopokea ikiwa ni pamoja na taarifa tuliyokwishaijadili kwamba, *REA* wanatakiwa kusaidiwa, lakini wanakwamishwa na utoaji wa fedha unaocheleweshwa na Serikali na Hazina inatakiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



ibebeshwe mzigo, hatuisemi sana hapa. Hazina ndiyo wanachelewesha fedha, lazima tuwe na mkakati wa namna ya kutoa fedha haraka ili zikafanye kazi. Miradi hii tunayoiweka mbele yetu haitatekelezeka bila fedha kupatikana kwa wakati. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwe na utaratibu wa kutoa fedha haraka ili kazi ikafanyike. Kazi nzuri iliyofanyika katika Wizara hii ya Nishati na Madini ni pamoja na kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais kupeleka umeme Namanyere.

Changamoto ambayo tunayo hapa ni usambazaji umeme vijijini. Vijiji vyote vya Nkundi, Kantawa, Kasu, Vilundikwa, Chala na Kacheche vyote umeme haujasambazwa. Sasa hii ni changamoto, ingekuwa inafaa wakati tunakuwa na mipango ya kupeleka umeme kwenye vijiji vinavyohusika basi tuwe tunajiandaa vizuri pia kusambaza, kwa sababu Wananchi wanausubiri kwa hamu. Hii ni dhahiri itatusaidia utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la umeme vilevile tuone namna tunavyoweza kupeleka katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Ukanda wa Ziwa wa Tanganyika. Watu wa *REA* nawashukuru sana, wameshapita vijiji vyote kubaini namna ya kufanya na katika ziara zangu nimeona wamesaini vitabu katika vijiji vyote. Sasa ningeomba tufanye mipango ionekane kwenye karatasi hizi ni lini tunawapelekea umeme huko. Umeme ukifika Mwambao mwa Ziwa Tanganyika tutakuwa tumewakomboa Watanzania wengi wanaoishi kimaskini bila sababu, kwa kuwa eneo lile lina maliasili nyingi, lakini watu hawawezi kuishi kulingana na maliasili zinazowazunguka kiutajiri, kwa sababu hawana jinsi ya kutumia utajiri ule. Umeme ukiingia pale, biashara ya kupeleka samaki Zambia itakuwa imekwisha na tutatengeneza fedha sisi wenyewe na Halmashauri zetu zitatajirika. Kwa hiyo, naomba *REA* waweke mkazo zaidi ili njozi hizo ambazo wameshazionesha ziweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni katika mpango huu wa sasa hivi ambao *REA* wametupendekezea

watatupelekea umeme katika Vijiji vya Londokazi, Chonga, Katani, Chilatila, Miula, Ntalamila, Kalundi, Kate, Isale, Mtapenda, Namchuchi na Msihofu. Vijiji hivi ni muhimu sana katika uzalishaji. Umeme utakuwa mkombozi mkubwa, kinachotakiwa ni Serikali kutoa fedha, isiwe ni kauli tunaenda tunazungumza. Nimefanya ziara mara nyingi, nikienda nazungumza jambo hili hili, watu wanakinai na mwisho wanasema labda uongo Mbunge wetu hutuelezi vizuri. Kumbe ni mipango iliyoandaliwa na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi na tunatakiwa tukaieleze na tunaieleza kama ilivyo. Sasa tunaomba kasi katika utekelezaji ndiyo itafsiri mipango hii, utendaji ndiyo utafsiri mipango hii itaweza kutusaidia zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ahadi za Mheshimiwa Rais. Katika barabara, Mheshimiwa Rais alikwishaahidi katika Mkoa wetu wa Rukwa na Katavi kwamba, barabara ya lami itaunganika kutoka Mbeya kuja Sumbawanga na kwenda Mpanda. Kasi ya ujenzi wa barabara hii siyo nzuri hasa kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda na hii mnamwangusha Mheshimiwa Rais. Naomba Watendaji wa Wizara na juzi nilikuwa naongea na Mheshimiwa Magufuli, kwamba, aende kutembelea na mara nyingi akitembelea Miradi inaongezeka kasi, sasa sijaona kasi ile kama inasaidia sana.

Kazi inaenda taratibu mno na sehemu nyingine kama kutoka Namanyere kwenda Kibaoni hakuna kazi inayofanyika kabisa na huko ndiko Waziri Mkuu anatoka. Sasa kama hamuwezi kuogopa Miradi ambayo ipo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu sijui itakuwaje! Mimi naomba tujaribu kuona. Kasi ya barabara zingine tunaziona jinsi zinavyofanyika kwa haraka na watu tunashindwa kueleweka kwamba labda hatusimamii au hatusukumi vya kutosha. Kwa hiyo nawaomba pamoja na kutembelea miradi hii lakini kasi iongezeke kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji huo huo kuna mgogoro pale Chala. Huo mgogoro wa Chala tumekaa tumekutana kwenye Bodi ya Barabara, tumeunda

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*[MHE. DESDERIUS J. MIPATA]*

Tume ikaenda ikachunguza ikaleta mapendekezo Serikalini. Naomba mapendekezo yale yaheshimiwe, yatakuwa jibu la kumaliza mgogoro wa fidia Chala. Jambo hili tusipolisema kwa kasi litatuletea shida hasa katika vipindi vya uchaguzi. Naomba hilo la fidia ya Chala ni kero kwa Wananchi wa Chala, kwa sababu barabara yote ile watu wote wamefidiwa imebaki hapo. Mheshimiwa Rais niliweza kumfikishia habari hii alipokutana na Wabunge wa CCM na akaahidi, akamwambia Naibu Waziri wa Ujenzi kwamba, angalieni hili jambo lifanyike haraka. Nashangaa mpaka sasa hakuna kitu kinachoendelea. Sasa ni namna gani ni nani zaidi atakayezungumza kama Mbunge wao nimezungumza, Mheshimiwa Rais amemwambia Naibu Waziri, sasa nini tunachosubiri sasa hivi. Kwa hiyo, naomba utekelezaji wa haraka ili Wananchi wawe na imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo barabara zingine alizoahidi Mheshimiwa Rais katika uchaguzi uliopita. Barabara ya kutoka Kana kwenda Kala. Nawashukuru barabara hii tumepata fedha kidogo, shilingi 400,000,000, lakini bado haziwezi kutosha. Barabara ya kutoka Kitosi kwenda Wampembe, Mheshimiwa Rais pia alitoa ahadi kwamba ataiboresha, nashukuru nilipita pale Wizarani juzi tumepata shilingi 200,000,000 lakini bado hazitoshelezi. Barabara ya kutoka Ninde kwenda Namanyere hakuna hata shilingi moja iliyokwishatolewa na muda umekwisha na bado Rais atakuja kuwatembelea. Sasa tutamjibu nini? Naomba watekelezaji wote, nimewakumbusha mara kwa mara mhakikishe tunapata fedha hizo ili kunusuru heshima ya Viongozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme lingine, Ukanda wote wa Mwambao hautembelewi na Viongozi na wanashindwa kutembea kwa sababu barabara ni mbovu mno. Naomba na ni wito rasmi kwa Mheshimiwa Rais, naomba utakapokuja Mkoani Rukwa, ukubali kuja kwenye Jimbo langu tena uende Tarafa ya Wampembe. Nimeenda kule wananiambia kila mara wanasema hatujamwona Rais wetu, hatujamwona Kiongozi yeyote huku mkubwa. Kwa

hiyo, naomba utakapokuja uje uone changamoto hizi tunazozisema; hakuna umeme, hakuna barabara na wala mawasiliano ya simu watu wanakaa kwenye ukanda tajiri sana hawawezi kuvichakata, samaki hawawezi kupata, uchumi unaotakiwa kutokana na mazingira yanayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo kuhusu viwanja vya ndege. Rukwa ni Mkoa wa muda mrefu na unachangia sana katika Uchumi wa Taifa hili hasa kwa kutupatia chakula, lakini tumeusahau. Mpanda tumeanza, sasa hivi Katavi wana kiwanja cha ndege kizuri, Mbeya wana kiwanja cha ndege kizuri, sisi bado. Pamoja na ukarabati wa kiwanja kilichopo sasa hivi kuendelea, lakini tunatakiwa tuwe na kiwanja cha kisasa ambacho kitaweza kuvutia utalii katika eneo letu. Eneo letu ni tajiri sana. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuendeleza kiwanja chetu cha ndege cha kisasa zaidi kama kinavyofanana na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nizungumzie reli na meli na usafiri wa majini ni muhimu sana. Pale Wampembe, Wananchi wanapoenda kupanda meli yao wanapanda katika hali hatarishi sana. Tungependa kuona miundombinu inayojengwa katika maeneo mengine ijengwe na pale pamoja na Msamba. Msamba meli haitui lakini ni mahali muhimu sana, kuna mizigo ya kutosha na kuna wafanyabiashara wengi. Ninashangaa hata wanavyosema biashara haitoshelezi, nadhani ufuatiliaji uangaliwe. Suala la reli ningetoa mawazo katika kuangalia mtazamo mpana na baadaye katika nchi yetu ni lazima tuangalie maeneo yenye uzalishaji kama Rukwa. *(Makofi)*

Tuanze kuwa na mawazo ya kutoa reli kutoka Mpanda, tunapofanya maboresho ya reli ile isogee mpaka kwenye maghala ya Sumbawanga, ambao ni wazalishaji wakubwa wa nafaka nchini hapa, hakuna mahali pengine panapozalishwa kama huko. Tukishawasaidia kwa usafiri wa namna hiyo tutaweza kuwa tunasaidia Wananchi wale

katika uzalishaji mzuri, lakini na usambazaji kwa Serikali tutakuwa tumepunguza gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nirejee kusema kwamba, Viongozi hawa wanafanya kazi vizuri, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ijitahidi, bado tuna nafasi kubwa sana na tunaaminiwa na Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mipata, viswahili vingine vya kutoka Rukwa huko. Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Athumani Mfutakamba!

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia. Kwanza kabisa, nianze kuwapongeza Wenyeviti wote wa Kamati ambao wamewasilisha hapa Bungeni Ripoti zao na niwapongeze pia Mawaziri wote ambao wapo katika sekta hizo. Sitakuwa nimekitendea haki Chama changu cha Mapinduzi kama sitaipongeza Sekretarieti ya Chama cha Mapinduzi, kwa ziara zake ambazo wamekuwa wakizifanya kuhakikisha Ilani ya Chama cha Mapinduzi inatekelezeka. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro, ambaye ameteuliwa kuwa Mbunge mwenzetu katika Bunge hili, ambaye kwa kweli sisi wanawake wote tuna haki ya kujivuna kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naiomba Serikali yetu itoe kipaumbele katika Sekta hii ya Mlundombinu kwa sababu imekuwa mara nyingi sana haipewi kipaumbele na hasa Wizara ya Uchukuzi. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu toka kipindi kilichopita mpaka sasa hivi, lakini siku zote tumekuwa tukiilalamikia Serikali kwa kutoa fedha kidogo sana katika Wizara ya Uchukuzi.

*[MHE. RITTA E. KABATI]*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka karibu mara mbili tulitaka kugoma kupitisha Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa sababu imekuwa ikipewa pesa ndogo sana na pesa inayopewa haifiki kwa wakati, kwa hiyo, inasababisha kazi nyingi sana haziendi kama inavyotakiwa. Hata tukitenga pesa nyingi katika kutengeneza barabara zetu hizi nchini, tusipotoa kipaumbele kwenye Sekta hii, nafikiri tutakuwa hatujitendei haki wenyewe kwa sababu barabara nyingi sana zitakuwa zinaharibika hazifanyi kazi inavyotakiwa. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali sasa hivi itoe kipaumbele kwenye Sekta hii hasa Wizara ya Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuipongeza Serikali yetu kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikiifanya kuhakikisha barabara zote za Mikoa sasa hivi angalau zimeunganika. Tulitembea karibu Tanzania nzima tukaona kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanyika katika Sekta hii ya Barabara, niwapongeze pia hata Mawaziri waliopo kwenye Sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Iringa uchumi wake unategemea sana kilimo, misitu pamoja na Mbuga ya *Ruaha National Park*. Utaona barabara zinazozunguka katika maeneo hayo bado hazijapewa kipaumbele. Nakumbuka mwaka jana nilileta swali langu Bunge lililopita kuuliza kuhusu barabara inayokwenda *Ruaha National Park* lini itawekewa lami. Kwa sababu tunajua ile barabara ni ya kiuchumi, kama ingewekewa lami ingeweza kusaidia sana kipato katika Mkoa wetu na kuleta ajira kubwa sana. Kwa hiyo, ninaomba na niliambiwa upembuzi yakinifu unaendelea, toka mwaka jana mpaka mwaka huu, upembuzi yakinifu utakwisha lini? Kwa sababu hata katika barabara hizi za Mgololo zinazozunguka msitu, upembuzi yakinifu ndiyo tunaambiwa unaendelea. Hata hizi barabara za Kilolo bado upembuzi yakinifu unaendelea. Kilolo ni sehemu ambapo kuna kilimo unategemea kutusaidia katika Mikoa mingi sana ya Kilimo lakini barabara zake zote ni matatizo makubwa. Naomba Serikali sasa hivi itoe kipaumbele kutengeneza lami katika barabara ambazo ni

*[MHE. RITTA E. KABATI]*

za kiuchumi ili kuinua uchumi wa Mkoa wetu na Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee pia kuishukuru Serikali kwa kazi kubwa ambayo imekuwa ikiifanya katika ujenzi wa viwanja vya ndege. Kwa kweli tumetembea katika viwanja vyote vya ndege na tumeona kazi kubwa nzuri inayofanyika katika viwanja hivyo. Naendelea kuomba na mimi pia nimehudhuria sherehe nyingi sana za uzinduzi wa viwanja hivi kikiwemo cha Bukoba, Mafia, Tabora na kadhalika, kwa kweli Serikali yetu inafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Sisi Wananchi wa Iringa ni lini tutasherehekea kile kiwanja chetu cha Nduli kwasababu kila siku tunasherehekea vya wenzetu na kila siku tunaongea Kiwanja cha Nduli mbona hakijengwi? Wananchi wa Iringa kila siku wananisikia, naenda kuhudhuria sherehe za wenzangu; ni lini na wao watahudhuria kwenye sherehe yetu ili na sisi angalau tuweze kufaidika na kiwanja chetu cha Nduli? Unaona kiwanja hiki sasa hivi kwa sababu zinatua ndege ndogo tu hata gharama ya uendeshaji imekuwa kubwa, hakuna kituo cha mafuta. Tunajua kama kutakuwa na matengenezo, angalau zitatua ndege kubwa *Fastjet* tutaweza kutumia gharama ndogo sana kwa nauli. Kutokana na barabara mbaya tunajua sasa hivi kuna wagonjwa watatumia hicho kiwanja cha ndege.

Naomba Serikali hasa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, kaka yangu, kila siku hiki kiwanja tumeambiwa mipango inaendelea. Tumeambiwa tu mipango sasa mpaka lini; mbona sisi watu wa Iringa tunasahaulika na vitu vingi? Jamani na sisi tusikilizeni watu wa Iringa angalau mtutengenezee hizo barabara za kiuchumi na kiwanja chetu cha ndege ili tuweze na sisi kufurahi kwamba, tuna Wabunge wanatetea humu Bungeni. *(Makofi)*

Pamoja na utengenezaji wa viwanja hivi niungane na wale Wabunge wenzangu waliozungumzia Shirika letu la Ndege la *ATCL.* Nasikia uchungu sana nikiona hata nchi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)



ndogo zina ndege zao, lakini sisi mpaka leo hii ndege tumekuwa tukiizungumzia muda mrefu sasa imekuwa historia. Tunaomba sana Mheshimiwa Mwakyembe, tuambie tatizo ni nini ili tuweze kutatua hili tatizo? Tuna rasilimali nyingi sana katika nchi yetu sidhani kama tutashindwa, tuuze mgodi mmoja tu tununue hata ndege tano, kumi, ili kuhakikisha kwamba na sisi Tanzania tuna Shirika la Ndege lipo juu linaenda kila nchi tuweze kutangaza nchi yetu. Maana yule Twiga sasa hivi amekaa tu kwenye ndege lakini haeleweki popote. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu Shirika la *TAZARA.* Nasikia uchungu sana, wafanyakazi hawa wamekuwa wakiteseka kwa muda mrefu sana. Haya malipo toka sisi tupo katika Kamati hii na nilionana na Sekretariati ya Chama cha Mapinduzi ilienda kuongea nao. Sasa ifikie mwisho hawa wafanyakazi wana haki ya kupewa madai yao, wapeni madai yao. Hili Shirika mbona linadai madeni mengi, tuambieni sasa hawa wanaodaiwa nao wamefanyiwa nini? Najua wanadai madeni mengi sana *TAZARA*, lakini madeni hili Shirika litaweza kujiendesha. Kwa hiyo, ninaomba, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, kaka yangu, tuambie sasa haya madeni yamefikia wapi; kila siku tunasikia tu madeni na wao wanadai? *(Makofi)*

Niendelee kuzipongeza Sekta zetu hizi za Miundombinu, Sayansi na Teknolojia, pia niwapongeze Mawaziri wote, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Labda tu tuelezwe kuhusu Mkongo wa Taifa sasa umefikia wapi, kwa sababu huu Mkoa wetu wa Iringa kuna baadhi ya vijiji bado mawasiliano yake siyo mazuri sana. Huko Killolo, Iringa Vijijini kwa Mheshimiwa Lukuvi, Mufindi, bado kuna maeneo pia mawasiliano yake siyo mazuri, kwa hiyo, Serikali yetu ituambie huo Mkongo wa Taifa utaisha lini? Mwisho wa matatizo haya ni nini Wananchi waweze kujua Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya kazi? Tunajua hata Watendaji wa Chama cha Mapinduzi nao wanafuatilia utekelezeji na Ilani kuhakikisha sasa hakuna Chama chochote ambacho kitakitoa tena. Wanasema CCM ni ngumu kutoka madarakani. *(Makofi)*

Nizungumzie kuhusu Miradi ya Umeme; nakuomba Mheshimiwa Waziri, angalia umeme kwenye shule zetu za sekondari, nyingi sana hazina umeme. Tuliambiwa wangepewa kipaumbele katika zile shule na hospitali au zahanati ambazo zipo vijijini zipatiwe huu umeme wa *REA* haraka sana. Tutakuwa hatuwatendei haki watoto wetu, wanafanya mitihani bila kufanya *practice* katika fani zao. Kwa hiyo, naomba sana zipewe kipaumbele. Kuna Dabaga katika hospitali nyingi sana wamenipigia simu hata leo, nilipoambiwa nitachangia wakaniambia Hospitali ya Kidabaga, Merini, bado hakuna umeme mpaka sasa hivi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba sana angalieni vijiji. Huu Mradi wa *REA* uangalie bila kubagua na tupewe Ripoti ya *REA* kuonesha vijiji gani ambavyo vitapatiwa umeme kwa wakati huu na vijiji gani vitapatiwa umeme wakati mwingine ili tutakapokwenda kusema utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tujue kweli huu umeme utatekelezeka. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, nawapongeza sana Mawaziri wote na niseme kwamba, Serikali yetu ijitahidi kutoa pesa kwa wakati ili Mawaziri wetu wasitukanwe kwamba ni mizigo. Pengine wanasema mizigo kwa sababu pia hawaletewi pesa kwa wakati, kama vitu havitekelezeki wanaonekana hawafanyi kazi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Iringa. Mheshimiwa Athumani Mfutakamba, atafuatiwa na Mheshimiwa David Silinde!

**MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitoe shukurani kwa kunipa fursa ya kuchangia Taarifa hizi za Wizara mbili.

*[MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA]*

Kwanza, naipongeza Kampuni ya *ATCL,* ndege imeanza kwenda Bunjura kuanzia jana, ni jitihada nzuri. Naishukuru Wizara ya Nishati na Madini kwa Vijiji vya Igalula, Goweko, Kigwa A, Kigwa B, Imalakaseko na Nsololo, muda siyo mrefu sasa mkandarasi yuko kwenye *site* kuanza kufanya kazi hiyo; napongeza sana, huu ni utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Reli ya Kati, *standard gauge* hatuna *solution* kama hatuwezi kuwa na *standard gauge* na kuboresha Bandari ya Dar es Salaam kwa maana ya kujenga Gati 13 na 14. Hii haina mjadala wala mbadala. *Standard gauge* itatuongezea treni kwenda kwa haraka, lakini kupanua kwa bandari na kuongeza kina hasa Gati Namba 13 na 14 kutafanya meli kubwa, *Fourth Generation Ships,* kuweza kuja pale na kontena elfu kumi mpaka elfu kumi na tano. Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, wakati uliopita aliniarifu kwamba, Kampuni iliyopatikana ni *China Harbor Corporation (CHC)* na mkopo wa *Exim Bank* walikuwa mbioni kuupata, ulikuwa umepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatujengi Gati 13 na 14, hatupanui Reli ya Kati kwa kwenda kwa *standard gauge,* tutapitwa na sisi lazima tuende haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende Kiwanja cha Ndege cha Tabora. Ninashukuru sana hata Mheshimiwa Munde amekizungumzia. Tukiongeze urefu kwa sababu mkakati sasa hivi ni kuongeza mazao ya matunda pale, ndege kubwa ambazo ni *transport carriers* ziweze kuja pale kubeba matunda ya aina mbalimbali na kuuza masoko ya nje, hilo linawezekana kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Mkongo wa Taifa, sasa hivi nchi nyingi zinaenda kwenye *IT parks.* Mkongo wa Taifa huu utatuwezesha kupata ajira kwa vijana wote wanaojua masuala ya kompyuta hata vijijini kwa sababu upo kule mtu hahitaji kuja mjini. Tukiweza kufanya uchakataji wa biashara (*Business Processing),* yapo makampuni mengi yanaweza kuajiri vijana wetu, kama

*[MHE. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA]*

tukiwa na mkataba, Makampuni yapo Silicon pale New York, yanaweza kuja kutoa ajira hizo kwa vijana wetu bila kusafiri kwenda kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Taifa wa Akiba wa Gesi *(Sovereign Wealth Fund)*, naomba kujua; je, Mfuko huu ukianzishwa katika fedha nyingi tutakazopata kwenye gesi, nchi kama Katal, Norway, Abudhabi, Trinidad and Tobago, Algeria na Libya, wamefaidika sana kwa *Sovereign Wealth Fund*. Je, Mfuko huu wa kiuchumi na kimaendeleo unaweza kusaidia Mikoa ambayo ipo nyuma kwa sasa hivi kimaendeleo kama Tabora, Pwani, Lindi, Mtwara, Rukwa, Katavi, Singida na Shinyanga. Maana mapatano forodhani melini tunapakia, kwa hiyo, tuanze kujipanga mapema kuona huu Mfuko wa Gesi wa Akiba utasaidiaje. Je, ni Sera ya Gesi Asilia ya Mwaka 2013 inaangalia nini tunaweza kujifunza kwenye nchi ambazo zimefanya vibaya kwenye Mifuko kama hii kama Nigeria na Mexico? Naomba kama naweza kupata majibu hayo kutoka kwa wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Barabara ya Itigi – Tabora, ukitoka Kigoma mpaka Dar es Salaam hiki kipande ambacho hakina lami ni kilometa 89. Sasa najua Wizara ya Ujenzi iliweka bilioni mbili kwenye Bajeti, lakini ningeomba tuelewe sasa hivi tumefanya jitihada gani ili na hiki kipande kiwekwe lami kutoka Kigoma mpaka Dar es Salaam iwe lami tu. La sivyo, Wananchi wa Kata za Tura, Malongwe, Kigwa mpaka kufika Tabora, Kizenge, wana hamu sana ya kupata lami kwa sababu huu ni wakati Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, amefanya jitihada kubwa za kutuwekea lami. Ningependa sana katika kipindi hiki, Chaya mpaka Nyahuwa nasi pia tuwe na lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru lakini niseme kwenye masuala ya Mkongo wa Taifa lazima tuchukue utaratibu ambao tunaweza kuwa na e-biashara, e-wanyama pori na e-afya. Hizi zitatusaidia kutumia huu mkongo kuweza kutatua matatizo mengi ya kibiashara na ya kielimu tukitumia huu mkongo kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri niishie hapo lakini nawashukuru sana Wenyeviti wote waliotoa taarifa hizi, nafikiri zimetupa mwelekeo mzuri; Mheshimiwa Mwambalaswa na Mheshimiwa Peter Serukamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushuru sana, Mhandisi Mfutakamba. Kama nilivyosema awali, Mheshimiwa David Silinde ndiyo anafuata, Mheshimiwa Martha Mlata ajiandae!

**MHE. DAVID E. SILINDE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi ya kuchangia Kamati hizi za Nishati na Madini na ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo natakiwa ni-*declare,* mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, lakini nitachangia zaidi upande wa miundombinu hususan maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka yetu nchini, Mpaka wa Tunduma, Namanga, Sirali, Holili na mingine ni sehemu ambayo ndiyo inaweza kupelekea mapato mengi katika hili Taifa. Nasema haya kwa sababu kila siku ndani ya Bunge tunasema na bado Serikali haisikii ni namna gani wanaweza kutumia mipaka kama sehemu ya mapato. Tunayasema haya kwa mfano pale Tunduma, Jimboni kwangu, leo ukienda msongamano unaokutana nao wa Dar es Salaam haufikii, wa Dar es Salaam unatembea lakini wa Tunduma ni mgumu sana kutembea. Haya yote yanatokana na mfumo wa Serikali kushindwa kushirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Mamlaka ya Bandari Tanzania kupitia Wizara ya Uchukuzi, kupitia Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, walikubaliana kufanya kazi saa 24. Mamlaka ya Bandari *(TPA),* wanafanya kazi saa 24 wanapakuwa magari. Magari haya yote kwa mfano ni magari ya mizigo yanakwenda katika mipaka ambapo ndiyo kwenye ushuru wa forodha *(Custom);* kwa mfano,

*[MHE. DAVID E. SILINDE]*

Tunduma wapo watu wa *TRA* pale wanafanya kazi saa nane. Ukienda kwa utaratibu huu mmoja yupo Dar es Salaam anafanya kazi saa 24, mwingine yupo mpakani anafanya kazi saa nane. Hapa hakuna *ratio*, sasa unashangaa Serikali inafanya kazi namna gani! Matokeo yake ni nini? Badala ya msongamano wa magari sasa kuwa Bandarini msongamano wa magari ya mizigo unabaki kuwa mipakani ambapo ni hatari zaidi kwa usalama wa nchi tofauti na ilivyokuwa bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili tutataka kuliangalia upya. Mimi ninachotaka kusema hapa ni kwamba, kwa sababu *TRA* ndiyo wanaohusika sana katika maeneo ya mipaka na wao sasa wafanye kazi saa 24 kama tulivyokuwa tunapendekeza kila siku. Hapa maana yake Dar es Salaam watatoa magari saa 24 na mipakani *TRA* watafanya kazi saa 24, maana yake nchi muda wote itakuwa inafanya kazi. Huu mgongano hutokana na Mamlaka ya Mapato ipo chini ya Wizara ya Fedha na *TPA* ipo chini ya Mamlaka ya Bandari. Matokeo yake, Wizara ya Fedha ina misingi yao ya kazi na Mamlaka ya Bandari chini ya Wizara ya Uchukuzi wana misingi yao ya kazi. Sasa hatuwezi kuendelea na huu mfumo, kwa hiyo, lazima tukubaliane kuwa na mfumo mmoja wa kulisaidia hili Taifa hususan kuondoa hii misongamano. Kwa hiyo, nashauri lazima kuwe na ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ukienda hapo hapo Bandarini kuna wizi wa ajabu sana. Ningependa Serikali itolee majibu. Wizi wenyewe ni nini? Kuna watu wanaita *ICD* hawa wanahusika na masuala ya kuhifadhi magari wanafanya kazi saa nane, siku za Jumamosi na Jumapili hawafanyi kazi. Jumamosi na Jumapili hawafanyi kazi, lakini mtu akinunua gari anachajiwa siku saba. Gari likikaa mwezi mmoja maana yake na zile siku nane za *weekend* analipa mtu ambazo wao hawafanyi kazi analipia huu si wizi. Sasa Jumamosi na Jumapili *ICD* hawafanyi kazi, lakini hizo hizo siku mtu anapokwenda kulipa *storage* ya gari hizo siku mbili analipishwa; huu si wizi wa ndani na ulio wazi kabisa? *(Makofi)*

*[MHE. DAVID E. SILINDE]*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yapo chini ya Wizara ya Uchukuzi pamoja na kwamba, *ICD* ipo *privately owned*. Tungependa sasa Serikali nalo hili mjaribu kulizingatia. Kwa hiyo, kama wao hawafanyi kazi Jumapili na Jumamosi na kama wao vilevile wanafanya kazi saa nane, *charging* ya watu ya mizigo yao katika *storage* ilingane na muda wanaofanya kazi. Wasi-*charge* muda ambao hawafanyi kazi, ule ni wizi na tunawaibia sana Watanzania na Wafanyabiashara. Kwa hiyo, ningependa hili lizingatiwe. Hapa ni mfumo ubadilike kuanzia Wizara ya Fedha washirikiane na watu wa Uchukuzi angalau tukienda na huu mfumo hili Taifa tutasaidiana.

Ninapenda sana kutolea mfano, eneo la Tunduma peke yake, huwa linaliingizia Taifa kila mwezi kuanzia shilingi bilioni 1.8 mpaka bilioni mbili. Maana ni karibu shilingi bilioni 24 kwa mwezi. Sasa tukiruhusu mfumo wa saa 24 tukapunguza msongomano wa magari kwa kutengeneza *dual carriage way* kama tulivyopendekeza. Unapotengeneza dual carriage way tafsiri yake ni kwamba, kunakuwa na njia ya magari ya mizigo kwenda nchi za nje. Ukiingia watu wanaendelea na kazi zao kama kawaida *that's very simple* hapatakuwa na msongamano, kazi zitaendelea, tutarahisisha mwenendo. Serikali itapata mapato mara tatu ya inavyopata wakati uliopo. Haya yote mnashindwa kuyazingatia na ni mambo rahisi na yanaweza kutekelezeka. Ningeomba hili suala lifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine suala la *One Border Post* lisije likawa kitendawili kwa sababu mara nyingi kila siku tumekuwa tunaambiwa tutatengeneza. Tutakaporuhusu *One Border Post* kabla ya mwaka 2015 hata haya masuala ya kasungura kadogo yatatekelezeka. Sasa hivi itaendelea kubaki kuwa nadharia, *One Border Post* itajengwa itapita miaka mitano, sita, saba, lakini mwisho wa siku tutakuja kuwalaumu kwa kushindwa kutekeleza, jambo ambalo linawezekana kutekelezeka kwa sababu linarudisha. Hili ndilo tatizo kubwa la Serikali yetu kwamba, tumekuwa tukiweza katika Miradi isiyokuwa na manufaa tofauti na Miradi ambayo inaweza kuliingizia pato Taifa

*[MHE. DAVID E. SILINDE]*

kama ambavyo sisi tumekuwa tunapendekeza. Kwa hiyo, hili ningeomba lifanyike.

Kutokana na mikanganyiko ambayo inatokea Mipakani kama Tunduma, tulikuwa tunapendekeza kila siku, tunaomba manufaa ya Mipaka yetu, *service levy* ya *0.3 percent* tulipwe na sisi. Mkiweza kuwa mnatupatia kama tuna uwezo wa kuwaingizia pato la bilioni mbili kwa nini msitupile *service levy* ya shilingi angalau milioni 60 mpaka 70 kwa mwezi. Nina uhakika hii tunaweza tukabadilisha maendeleo ya pale kwa sababu sisi ndiyo tunaokabiliwa na changamoto za pale mpakani. Tupo katika hatari ya moto, ujambazi, lakini vilevile pana maambukizi makubwa sana ya UKIMWI kutokana na msongamano mkubwa uliopo lile eneo. Nimelisemea sana, ningeomba sasa Serikali mli-*consider* na lifanyiwe kazi mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni masuala ya barabara. Halmashauri nyingi nchini tumeomba kupandishiwa hadhi barabara zetu kwenda kupitia Wizara ya Ujenzi. Imekuwa ni muda mrefu, miaka miwili, watu wanasema unavyopeleka maombi watu wa Wizara kwenda kukagua barabara wanahitaji miaka miwili ili waipitie hiyo barabara waipandishe hadhi. Kibaya zaidi, barabara tunazoziombea zipandishwe hadhi kwa mfano sisi tumeomba barabara kutoka Kakozi - Kapele kwenda Namchinga mpaka Ilonga, kilomita 50.6. Tumeomba barabara kutoka Ntungwa - Chilulumo - Mkuluwe mpaka Namsamba, kilometa 51.1 zipandishwe hadhi, lakini miaka miwili sasa Serikali haijibu imekaa kimya inaingiza mapato.

Kibaya zaidi, sisi tupo vijijini na ndiyo tunaoingiza sana Pato hili Taifa, lakini cha ajabu ni kwamba, asilimia 80 ya Watanzania maskini wanaolipa kodi na kuzalisha, kwa maana ya mazao ya mahindi na mazao ya biashara, hatuzingatiwi na Serikali. Kwa hiyo, Miradi yote kwa mfano hata mapato niliyotolea katika mipaka yanatoka maeneo ya vijijini Tunduma yanakwenda Serikali Kuu yananufaisha zaidi Dar es Salaam na Mijini yanaacha maeneo ya vijijini. Sasa hatuwezi, lazima haya tunayoyapeleka ni maombi

*[MHE. DAVID E. SILINDE]*

yanayogusa Wananchi wengi na maskini, ningependa lizingatiwe.

Jambo la tatu, mimi nilitaka nizungumzie suala la umeme vijijini. Wananchi wa vijijini wameteseka sana, tangu dunia ianze hawajawahi kuona mwanga. Sasa hawa ndiyo walipa kodi, wanaonewa na ndiyo wapiga kura wakuu wa Chama cha Mapinduzi. Tofauti na maeneo ambayo sisi Upinzani tunayaongoza, maana kule tunapoongoza sisi Upinzani ndiyo kuna umeme, maji na barabara. Wale ambao wanawapigia kura kwa nini mnawanyanyasa hivyo? Hatuwezi kuendelea kutumia umaskini wao na unyonge wao, wakati wanalipa kodi wanazalisha. Kwa hiyo, ningewaomba Serikali ndani ya kipindi hiki kifupi hususan Wilaya yangu ya Mombo tulete umeme haiwezekani sisi Wilaya ya Mombo ukiondoa Halmashauri ya Mji wa Tunduma peke yake, miaka yote hata Kata moja hakuna umeme, jamani hamtuonei huruma. Kila siku naongea hamnionei huruma! Sizungumzi kwa manufaa yangu, nazungumza kwa manufaa ya Wananchi wa Mbozi wanaowapigia kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa David Silinde. Mheshimiwa Martha Mlata, atafuatiwa na Mheshimiwa Kamishna Zambi!

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

*(Hapa umeme ulikatika)*

*(Saa 1.25 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 19 Desemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*